# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 29 Mei, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa alize swali lake.

Na. 467

**Ujenzi wa Jengo la *OPD* Kituo cha Afya Kiloleli – Busega**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga jengo la *OPD* katika Kituo cha Afya cha Kata ya Kiloleli, Wilaya ya Busega?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Kiloleli ni miongoni mwa vituo vya afya 202 vikongwe na vyenye miundombinu pungufu ambavyo vinahitaji ukarabati mkubwa ili kuendana na mahitaji ya sasa ya utoaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali itavifanyia ukarabati na kujenga majengo muhimu katika vituo hivyo kwa awamu, kikiwemo Kituo cha Afya Kiloleli katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega ambacho kitajengewa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)*. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia fedha za ujenzi wa hospitali tatu mpya za Mkoa wa Simiyu na vituo vya afya 13 na vyote vinafanya kazi, ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Wilaya katika Mkoa wa Simiyu na vituo vya afya vina upungufu wa wafanyakazi. Je, ni lini Serikali itatuletea watumishi wa kutosha katika hospitali hizo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Hospitali ya Wilaya ya Itilima haina gari la kubeba wagonjwa, gari wanalotumia wanakwenda kuazima katika Kituo cha Afya Ikindiro. Je, ni lini Serikali itatuletea gari ya kubeba wagonjwa katika hospitali ya Wilaya ya Itilima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, amefuatilia kwa karibu sana suala la watumishi katika hospitali za halmashauri katika Mkoa wa Simiyu. Nimhakikishie tu kwamba katika ajira zote zilizopita miongoni mwa mikoa ambayo ilipewa kipaumbele cha kupewa watumishi wengi zaidi kwa sababu ya upungufu wa watumishi katika halmashauri hizo ni Halmashauri za Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kila kibali cha ajira kitakapojitokeza tutawaangalia. Hivi karibuni Mheshimiwa Rais ametoa kibali cha ajira zitatangazwa wakati wowote kuanzia sasa; tutahakikisha tunaupa kipaumbele Mkoa wa Simiyu pamoja na halmashauri zake ili hospitali za halmashauri zake ili hospitali za halmashauri ziwe na watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, pili kuhusiana na magari ya wagonjwa. Magari ya wagonjwa yanatolewa katika halmashauri zetu ili yatoe huduma kwenye vituo vyote pamoja na hospitali ya halmashauri. Si kila kituo cha afya kitakuwa na gari lake linalojitegemea la wagonjwa kwa sababu ya utaratibu wa *cascade supervision* pamoja na *referral system.* Kwa hiyo niwaombe tu halmashauri ya Itilima watumie hiyo gari ambayo ipo kwenye kituo cha afya kwa ajili ya rufaa pia katika ngazi ya halmashauri wakati Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kupeleka gari nyingine ya wagonjwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Mguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Twaha Mpembenwe kwa niaba ya Mheshimiwa Charles.

Na. 468

**Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE K.n.y. MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda katika Jimbo la Mwibara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya wa Mwaka 2015 unaelekeza kuwepo kwa hospitali moja kwa kila halmashauri. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda tayari imepatiwa shilingi bilioni 3.65 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya halmashauri. Ahsante.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Twaha ninaona ameketi. Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi kupata majengo ya wodi za wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Ubungo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imepewa zaidi ya bilioni 3.8 kwa ajili ya ujenzi wa majengo mbalimbali ya huduma. Kazi ya ujenzi inaendelea; nimefanya ziara pale tumeona kuna majengo ambayo hayajakamilika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mama Kisangi kwamba Serikali inatambua uhitaji wa fedha. Tayari tumekwishaiweka kwenye mpango wa hospitali za halmashauri ambazo zitaletewa fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo yaliyobaki.  Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, sasa aulize swali lake.

Na. 469

**Kupeleka Fedha ya Ujenzi wa Kituo cha Afya Maweni – Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Maweni - Ng'hoboko – Meatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali ilipeleka shilingi bilioni moja katika Halmashauri ya Wilaya

ya Meatu kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ilamba Ndogo na Mwasengela. Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye kata za kimkakati kote nchini. Aidha, Kata ya Ng'hoboko itajengewa kituo cha afya kwa kuzingatia mahitaji na vigezo vilivyoainishwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Swali la kwanza; je, Serikali haioni haja ya kupandisha hadhi Zahanati ya Mwabuzo kuwa kituo cha afya ili iweze kuhudumia kata nne zilizopo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kituo cha Afya Ilamba Ndogo na hospitali ya wilaya hazina *ambulance*. Je, Serikali haioni haja ya kuziletea *ambulance*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali imekuwa ikipandisha hadhi baadhi ya zahanati kuwa vituo vya afya kulingana na idadi ya wananchi wanaotibiwa katika maeneo hayo na pia idadi ya vijiji au kata ambazo zinategemea huduma kutoka katika zahanati hizo. Kwa hiyo naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge Leah Komanya kuhusiana na Zahanati ya Mwabuzo; kwamba tuifanyie tathmini ili kuona kama inakidhi vigezo vya kuwa kituo cha afya basi tutakwenda kufanya hivyo kwa kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na magari ya wagonjwa, Serikali imeendelea kupeleka magari na katika mwaka huu Mheshimiwa Rais amenunua magari zaidi ya 628 na halmashauri zote zimepata magari mapya ya wagonjwa ikiwemo Halmashauri ya Meatu. Ninafahamu kwamba Halmashauri ya Meatu ni kubwa bado inahitaji magari zaidi. Niombe waendelee kutumia magari yaliyopo kwa maana ya utaratibu wa *cascade* na *referral system* wakati tunasubiri magari mengine kwenda kuongeza nguvu katika vituo ambavyo amevitaja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itapeleka Kituo cha Afya katika Tarafa ya Msitu wa Tembo Wilaya ya Simanjiro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba Kata ya Msitu wa Tembo katika Halmashauri ya Simanjiro ni moja ya kata ambazo zimekwishaainishwa kama kata za kimkakati kwa sababu ya ukubwa wake pamoja na umbali kutoka kituo cha jirani zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Asia Halamga, amefuatilia mara kadhaa. Nimhakikishie kwamba Serikali tayari imekwishaweka mpango mkakati wa kwenda kujenga kituo cha afya katika kata hiyo na kata nyingine zote za kimkakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2008 Serikali ilijenga jengo la mama na mtoto, lakini halijakamilika mpaka leo pale Kata ya Msaada, je, lini sasa watamalizia jengo hilo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Utaratibu wa ujenzi wa miundombinu hii ya huduma za afya ni kwa kutumia mapato ya ndani ya halmashauri, lakini pia fedha ya Serikali Kuu. Kwa hiyo naomba kwanza nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chemba kwamba waone uwezekano wa kutenga fedha kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo hilo ambalo limekaa tangu mwaka 2008. Pili, walete Taarifa Rasmi Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuone kama

hawana uwezo wa kukamlisha kwa mapato ya ndani, basi Serikali Kuu tutafute fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunde Mjini, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

Na. 470

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Guta – Bunda Mjini**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. ROBERT C. MABOTO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Guta – Bunda Mjini.?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi 2023/2024, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 2.65 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa maboma katika vituo vya kutolea huduma za afya katika Halmashauri ya Mji wa Bunda.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye Kata za kimkakati kote nchini. Aidha, Kata ya Guta itajengewa kituo cha afya kwa kuzingatia mahitaji na vigezo vilivyoainishwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nataka kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwanza kwa kuwa Kituo cha Afya

Guta Mheshimiwa Mbunge amekuwa akikisemea hapa kwa mara nyingi sana kuhusu ujenzi wake. Je, ni lini hasa Serikali na kwa sababu walishatolea ahadi hapa ya kujenga vituo vya afya, itajenga kituo cha afya kwenye Kata hiyo ya Guta?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; niliahidiwa hapa mara nyingi sana kujenga kituo cha afya kwenye Kata ya Mihingo. Je, ni lini ahadi hiyo ya kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Mihingo itatimilizwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kata ya Guta katika halmashauri ya Mji wa Bunda, kwanza walishaleta maombi ya kujenga kituo cha afya, lakini kwa wakati huo miaka miwili iliyopita hakikukidhi vigezo, kwa maana ya idadi ya wananchi pamoja na ukubwa wa eneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuliwaelekeza kuendelea kuboresha vigezo ambavyo vitafanya Kata ya Guta kuwa na sifa ya kuwa kituo cha afya. Hata sasa tumemwagiza mkurugenzi na nisisitize hapa, wafanye maandalizi hayo na kutuletea taarifa rasmi ili tuone na kama inakidhi vigezo basi tuweze kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Guta.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kata ambayo Mheshimiwa Getere ameitaja katika jimbo lake nimhakikishie tu kwamba aliainisha kwenye vituo vya afya vya kimkakati na tayari tunatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga vituo hivyo vya afya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe sasa aulize swali lake.

Na. 471

## Ujenzi wa Vibanda vya Abiria katika Vivuko vya Bwisya, Bugolora na Kisorya

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa vibanda vya abiria katika vivuko vya Bwisya, Bugolora na Kisorya utaanza ikizingatiwa fedha yake ilitengwa katika bajeti ya mwaka 2023/2024?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *TEMESA* imekamilisha kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa majengo ya abiria na ofisi za vivuko vya Bwisya, Bugolora na Kisorya. Kwa sasa *TEMESA* inaendelea na taratibu za manunuzi ya kupata wakandarasi watakaotekeleza ujenzi wa miradi hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na jitihada ninatambua na mchakato unaoendelea, lakini wananchi wa Ukerewe wanataka kujua specific; je, ni lini ujenzi huo utaanza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kivuko cha Kayenze kwenda Bukimwi Jimboni Ukerewe upande wa Bukimwi miundombinu kwa ajili ya gati ni mibovu sana. Hakuna gati na mazingira yake kimsingi siyo mazuri. Je, ni lini Serikali itajenga gati pamoja na banda kwa ajili ya abiria kwenye eneo hilo la Bukimwi.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taratibu za manunuzi ndizo zinazotuongoza lini wataanza. Kwa kuwa tulikwishakamilisha na tumekwishatangaza kuwa tunatafuta wakandarasi maana yake ni kwamba taratibu zitakavyokamilika tutaanza ujenzi. Ndiyo maana tunasema kwamba sasa hivi tunatafuta wakandarasi na fedha tulishaitenga, kwa hiyo hakuna kitakachozuia. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Ukerewe kwamba taratibu za manunuzi zitakapokamilika mkandarasi ataanza kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, kwenye Kivuko ya Kayenze Bukimwi na hasa upande wa Bukimwi, naomba nimwagize Mtendaji Mkuu wa *TEMESA* pamoja na Mtendaji wa Kanda ya Ziwa watembelee kivuko hiki na hasa eneo la Bukimwi ili kuona uchakavu halafu walete mapendekezo. Ninaweza kuona namna gani Serikali inaweza kuboresha kivuko hicho na hasa eneo hili la Bukimwi ili wananchi waweze kupata huduma bora. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge wa Kilosa; Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma kwa niaba yake.

Na. 472

**Ujenzi wa Daraja Mji wa Kilosa**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA K.n.y MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga daraja katika Mji wa Kilosa kuvuka Mto Mkondoa ambalo limebomolewa na mafuriko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mto Mkondoa upo kwenye Barabara ya Dumila – Ludewa – Kilosa – Ulaya – Mikumi yenye urefu wa kilometa 142.3 katika eneo la Kilosa. Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS),* Mkoa wa Morogoro tarehe 15 Mei, 2024 imesaini mkataba na Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Mto Mkondoa. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, licha ya hivyo nina maswali mawili madogo. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itajenga Daraja la Mbuga – Mwaya ambalo limekatika kwa sababu ya mafuriko?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, ni lini Serikali itaimarisha na kuendelea kukamilisha ujenzi wa Madaraja ya Chakwale pamoja na Nguyami. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, madaraja aliyoyataja ya Mwaya ambayo yameharibika kwa sababu ya mafuriko sasa hivi Serikali tunatafuta fedha kwa ajili ya kurejesha miundombinu yote na

kipaumbele kitakuwa ni madaraja yote ambayo hasa ndiyo yameathirika, likiwemo hili daraja alilotaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Daraja la Chakwale na Nguyami, madaraja yameshakamilika kufanyiwa usanifu na tayari yako kwenye mpango wa kuanza kuyajenga. Kwa hiyo, muda wowote zabuni zitakuwa zimeshatangazwa kwa ajili ya kuyajenga hayo madaraja mawili ya Nguyami na Chakwale. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Barabara ya Orkesumet kwenda Ruvu Remit mpaka Hedaru mawasiliano yamekatika kabisa na maji yamejaa barabarani *Kalavati* limefunikwa. Je, ni lini sasa Serikali itakwenda kujenga daraja katika eneo la Gunge ili kurudisha mawasiliano? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri hilo daraja la Gunge nalifahamu kuna maji mengi kama alivyosema na hapa ni kwamba maeneo yote ambayo yaliharibika kwa sababu ya mvua tumerejesha lakini yale ambayo maji yamekuwepo na yameendelea kupita imekuwa ni vigumu sana kurejesha.

Mheshimiwa Spika, nimwagize Meneja wa Mkoa wa Manyara kwamba aweze kutembelea eneo hilo na kama mazingira yataruhusu kurejesha hayo mawasiliano afanye haraka na kama atakwama kwa ngazi yake ya mkoa basi awasiliane na *TANROADS* makao makuu ili waweze kuhakikisha kwamba mawasiliano yanarudishwa katika daraja hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tuna daraja kwenye Mto Ruwegu kwenye barabara inayotoka

Namtumbo, Mtonya, Mgombasi, ni daraja la muda mrefu jembamba la njia moja lakini mvua zilizonyesha mwaka huu zimeliathiri daraja hilo. Je, Serikali nayo imeliweka katika *list* ya kulikarabati na kulijenga upya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Meneja Mkoa wa Ruvuma na Mameneja wote walishapewa taarifa na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tuna madaraja yote ambayo yameathirika likiwepo na daraja hili la Ruwegu ambalo Serikali sasa inajipanga kuhakikisha kwamba kama nilivyosema tunarejesha mawasiliano yote katika madaraja, kama halikuathirika, basi ni kuliimarisha, kama limeondoka lote basi ni kulijenga hilo daraja upya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, Daraja la Maga na la masqaroda na Waziri anayafahamu hali yake ni mbaya na Mkandarasi amewekwa pale lakini hajengi. Je, lini wanapeleka fedha ili na madaraja yale yajengwe? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama mkandarasi yupo na hajengi labda kutakuwa na tatizo lingine, lakini kama kuna changamoto nyingine, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, baada ya hapa tuonane kwa sababu pia Meneja wa Mkoa wa Manyara yupo, tuweze kuona tatizo ni nini ili daraja hili liweze kujengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 473

**Tatizo la Mawasiliano – Mtwara Mjini**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, lini tatizo la mawasiliano ya simu katika baadhi ya Kata za Jimbo la Mtwara Mjini litaisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, *UCSAF* kwa ujumla wake inashughulikia upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo ya vijijini na baadhi ya maeneo ya mijini yaliyopo pembezoni yasiyo na mvuto wa kibiashara. Hivyo, *UCSAF* itakwenda kufanya tathmini kwa maeneo ya Mtwara Mjini yaliyopo pembezoni na yasiyo na mvuto wa kibiashara kuona kata zipi zenye changamoto ya mawasiliano ili ziweze kuwekwa katika mpango wa kufikishia mawasiliano katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; hilo Jimbo la Mtwara Mjini kuna Kata za Mitengo, Jangwani na Naliendele ni kata za mjini. Nataka kujua *exactly* ni lini Serikali inaenda kuwezesha mawasiliano kwa sababu wananchi wamekuwa wakipata shida?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; nini kauli ya Serikali kuhusu kupanda kwa vocha ya kukwangua iliyokuwa inauzwa shilingi 1,000 sasa hivi inauzwa shilingi 1,200, iliyokuwa inauzwa shilingi 500 sasa hivi inauzwa shilingi 600? Nataka kujua kwa sababu wananchi hawaelewi. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Malapo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hizi kata alizozitaja Mheshimiwa Malapo, ametaja kata ambazo ziko Mtwara Mjini pale, tutaendelea kufuatilia kwa nini mawasiliano yanakatika katika kwa sababu kazi kubwa imeshafanyika, hivyo, niwatoe hofu wananchi mawasiliano yatakwenda kuimarika hivi punde.

Mheshimiwa Spika, swali lake namba mbili, bei za vocha za kukwangua, hili limejitokeza katika maeneo mbalimbali ya nchi hata pale Mkoa wa Songwe, Tunduma, Mbozi limejitokeza, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakifuatilia na sisi tumefuatilia na tumeshawaagiza *TCRA* waweze kuhakikisha watoa huduma hawa hawapandishi hizi bei kiholela lazima wafuate utaratibu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Sanya *Station*, Mtakuja, Tindigani ndani ya Kata ya Kia havina mawasiliano na wananchi wanapata shida sana kufanya mawasiliano. Je, ni lini Serikali itajenga mawasiliano kwenye maeneo haya? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashishe Mafuwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge anafuatilia sana vijiji hivi, lakini nimhakikishie katika utaratibu wa *UCSAF* tayari tuna minara 758 ambayo inaendelea kujengwa nchini lakini tuna *bunch* nyingine ya zaidi ya minara 600. Kwa hiyo, hivi vijiji vyote tunatarajia kuvifikishia huduma ya mawasiliano. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, vijiji vingi vya Jimbo la Newala Vijijini vinakosa mawasiliano ya simu. Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano hayo ili kurahisisha utendaji katika vijiji hivyo? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mbunge wa Newala Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yapo katika mchakato wa kuhakikisha mwaka ujao wa fedha tunaweza kuyafikia na wananchi wanapata huduma ya mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'azi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake, kwa niaba yake...

*(Hapa Mhe. Tunza Malapo alisimama kutaka kuuliza swali kwa niaba ya Mhe. Mwanaisha Ulenge)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza umetoka kuuliza swali sasa hivi, hapana wamesimama wenzio, nilikuwa nasema ili wewe ukae wasimame wale ambao hawajapata nafasi ya kuuliza. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso.

Na. 474

**Programu ya Kuinua Elimu kwenye Mikoa iliyo nyuma Kielimu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO K.n.y. MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakuja na mpango maalum wa kuinua elimu kwenye mikoa iliyo nyuma kielimu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mipango na mikakati mbalimbali yenye lengo la kuboresha na kuinua viwango vya elimu na mafunzo nchini kwa ujumla ambayo inahusisha kuwekeza katika miundombinu ya elimu kama vile ujenzi na ukarabati wa shule na vyuo vya elimu, kutoa mafunzo na rasilimali mbalimbali kwa walimu ili kuboresha uwezo wao wa kufundisha, kukuza matumizi ya sayansi na teknolojia katika elimu pamoja na kuweka sera na mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa usawa na kwa wote.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kutekeleza mipango na mikakakati mbalimbali yenye lengo la kuboresha elimu na mafunzo katika maeneo yote nchini. Utekelezaji huo unafanyika kutokana na taarifa za tathmini ya ubora wa elimu zinazofanyika ili kubaini changamoto zinazoikabili Sekta ya Elimu Nchini. Aidha, Serikali inaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo ya elimu katika kuweka mipango ya kuboresha na kuinua ubora wa elimu pamoja na kuweka usawa wa utoaji wa elimu na mafunzo katika mikoa yote nchini kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; tunatambua sasa tuko kwenye sera mpya ya elimu ambayo imeanza utekelezaji wake

na sera hiyo ni pana imebeba mambo mengi. Ni kwa kiwango gani Serikali imejipanga kulingana na malengo waliyojiwekea kuhakikisha sera hiyo inatekelezwa kwa ufanisi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; suala la kuinua ubora wa elimu kwenye maeneo ya pembezoni na maeneo yote kwa ujumla ni pamoja na motisha kwa walimu. Nini mkakati wa Serikali kutoa motisha kwa walimu ili waendelee kufundisha vizuri na elimu iwe katika ubora unaotakiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la kwanza kuhusiana na suala la utekelezaji wa sera yetu mpya naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba sera hii tunaitekeleza kwa awamu ili katika kila hatua tuweze kuwa tunafanya tathmini. Kwa hiyo, utekelezaji wake utakuwa unakwenda kwa awamu ili kujenga uwezo kwanza kwa watekelezaji wa sera hii, lakini vile vile ili kuweza kupeleka vile vifaa vinavyohitajika wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulidhani tutakapofanya kwa awamu, taratibu taratibu na huku tukiendelea kufanya *monitoring and evaluation* na ile tathmini ya kina tunaweza tukatekeleza kwa ufanisi zaidi. Kwa hiyo, huo ndio mkakati wa Serikali ili kuweza kutekeleza sera hii kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la pili; upande wa motisha kwa walimu, naomba nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, Serikali imekuwa ikiendelea kutoa motisha kwa walimu hasa kwenye yale maeneo ya stahiki zao pale wanapostahili kupanda madaraja Serikali imekuwa ikifanya hivyo, lakini mwaka juzi baada ya zoezi la sensa Serikali imeweza kutoa vishikwambi kwa walimu hawa ili kuhakikisha kwamba wanakwenda kuvitumia kwenye utendaji wao wa kazi za kila siku na Serikali itakuwa inafanya hivyo kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujua Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia hasa walimu wanaopangwa mikoa ya pembezoni kama Kagera wakipangiwa kwenda tayari wameshavunjika moyo, *at least* kuwapatia posho ya mazingira magumu ili kuwatia moyo kufundisha watoto wetu? Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kikoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, walimu wamekuwa wakipangwa kwenye maeneo mbalimbali na maeneo mengine ni pembezoni. Kwa vile Mheshimiwa Kikoyo, anatoa ushauri kwa Serikali tunaomba tuchukue ushauri wake tukaufanyie tathmini ili kuweza kuona namna gani Serikali inaweza ikatekeleza utaratibu huu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ualimu cha Shinyanga maarufu *SHYCOM* ni chuo kikongwe sana na miundombinu imechakaa. Je, nini mpango wa Serikali kukiboresha na kukifanyia ukarabati chuo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mnzava, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali tulishaanza kufanya ukarabati wa chuo kile labda Mheshimiwa Mnzava hajaenda kwa siku nyingi, lakini ukienda pale tumefanya ukarabati mkubwa sana

kwenye hiki Chuo cha *SHYCOM* na tunaendelea kufanya hivyo kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Katika mwaka ujao wa fedha tumeweka bajeti kwa ajili ya ukarabati na kuongeza miundombinu sio kwenye hicho Chuo cha *SHYCOM* peke yake bali kwenye vyuo vyote vya ualimu pamoja na kuweka mkongo wa *internet* au mkongo wa Taifa kwa ajili ya *internet* kwenye vyuo hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Boniphace Butondo.

Na. 475

**Vituo vya Afya Kuunganishwa na Maji Kutoka Ziwa Victoria**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha Vituo vya Afya kwenye mtandao wa maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria Wilayani Nyang'hwale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha huduma ya majisafi, salama na ya kutosheleza inapatikana katika maeneo yote ikijumuisha taasisi za umma vikiwemo Vituo vya Afya, Zahanati na Shule. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imefikisha huduma ya majisafi na salama katika Vituo vya Afya na Zahanati

4,939 kati ya 6,134 kwa kutumia miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa maji wa Ziwa Victoria. Aidha, kipaumbele kinachotolewa cha kufikisha huduma ya maji kwenye taasisi za umma ikiwemo Shule, Zahanati na Vituo vya Afya kwa sanifu za miradi na utekelezaji wa miradi mbalimbali inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali inaandaa Mpango Maalum wa kufikisha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Zahanati, Vituo vya Afya na Shule zisizo na huduma hiyo ambapo maandalizi hayo yanatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024. Utekelezaji wa mpango huo unatarajiwa kuanza mara moja baada ya kukamilika utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitatu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali yaliyotolewa katika swali hili, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ipo miradi katika Wilaya ya Kishapu, mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria kutoka Igaga kwenda Mwamashele hadi Kata ya Lagana unaotekelezwa chini ya Kampuni ya *Emirates*, mradi huu ulitakiwa kukabidhiwa mwaka wa fedha uliopita lakini mpaka sasa haujakamilika. Ni lini sasa Serikali inaenda kuweka nguvu kubwa ili mradi kuhakikisha mradi huu mkubwa unakamilishwa na wananchi wanaondokana na adha kubwa ya maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; iko miradi mikubwa iliyofanikiwa sana katika Wilaya ya Kishapu hasa Miradi ya Maji ya Ziwa Victoria, lakini pia miradi ya visima virefu ipo yenye changamoto na hiyo iliyofanikiwa. Mheshimiwa Waziri, yuko tayari kuambatana nami ili mradi twende tukaone mafanikio na pale palipo na changamoto aweze kuzitatua? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na kwa dhati nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, lakini kubwa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie tumepata taarifa tumepokea bilioni 80 kwa ajili ya kulipa wakandarasi mbalimbali nchini. Nimwelekeze Katibu Mkuu Wizara ya Maji, fedha hizi zimeshaingia zilipwe mara moja kwa wakandarasi ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji maeneo mbalimbali ikiwemo Kishapu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni juu ya kwenda Kishapu, Nipo tayari tuweze kuongozana na kwenda kuangalia kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyotolewa mwaka 2021 ya kuwekeza kwenye Mradi wa Maji wa Kitongoji cha Masaninga na Nasaya Jimboni Kilwa Kaskazini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunayo magari na eneo hilo lina changamoto, nielekeze wakala wa uchimbaji visima achimbe kisima mara moja katika hilo eneo ili wananchi wale waweze kupata huduma ya majisafi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Serikali yetu ya Awamu ya Sita imeonesha uthubutu wa kutaka kuanza kutumia maji ya Mto Rufiji kujenga mradi mkubwa. Je, mpaka sasa hatua imefikia wapi kwa

ajili ya kuwezesha maeneo yaliyosalia ya Rufiji, Mkuranga na Kibiti kupata majisafi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali na maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kutumia rasilimali toshelevu tulizokuwa nazo mito pamoja na maziwa ili kutatua tatizo la maji kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge lako Tukufu na Bunge limeshatupitishia bajeti ni moja ya miradi ambayo sasa tunakwenda kuanza kufanya usanifu wa haraka ili utekelezaji wake uweze kuanza mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini sasa mna mpango wa kuweka mita za malipo kabla katika Jimbo letu la Temeke? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu,

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, huo ndio uelekeo wa Wizara na tumekwishaanza na niwaelekeze DAWASA kwa kuwa ni ombi maalum la Mheshimiwa Mbunge wao basi tuone namna ya haja ya haraka kuhakikisha eneo la Temeke nalo tunaianza hii kazi mara moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 476

**Kukamilika kwa Mradi wa Maji Ndaje – Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Ndaje unaopeleka maji katika Vijiji vya Mbesa Airport na Lijimbo utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika; naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji Mbesa-Ndaje katika Wilaya ya Tunduru Mkoani Ruvuma. Mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa miundombinu kutoka kwenye chanzo kwenda kwenye tanki lenye ujazo wa lita 100,000 na ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilometa 13.5 umekamilika. Aidha, awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo inaendelea na imefikia wastani wa 60% ambapo inahusisha ukarabati na ujenzi wa matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 200,000, ulazaji wa mabomba ya usambazaji umbali wa kilometa 32.1 pamoja na ujenzi wa vituo 25 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2024 na utanufaisha wananchi wapatao 12,500 waishio kwenye Vijiji vitatu vya Mbesa, Lijimbo na *Airport*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kuhusiana na mradi huu, ni kweli unaendelea vizuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Mradi wa Masuguru - Mchoteka ambao ulianza tangu mwaka 2022 umesimama kwa muda mrefu kwa sababu mkandarasi kakosa pesa za kuendeleza mradi huu na ana *certificate* ya shilingi milioni 79, hajalipwa tangu februari mwaka huu. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya

kukamilisha mradi huu ili kumpa Mkandarasi aweze kuendelea na kazi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mradi wa Msinji Serikali iliingia mkataba na *Trinity Enterprises* ya Dar es Salaam tangu mwaka jana Julai. Mpaka leo hajaanza kazi kwa kisingizio kwamba hajapata *advance payment* ya shilingi milioni 160. Je, ni lini Serikali itampa mkandarasi huyu fedha ili aanze kazi katika Mradi wa Msinji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mpakate kwa kazi ambayo anaifanya hasa katika Jimbolake la Tunduru. Kubwa kama nilivyoeleza tumekwishapokea shilingi bilioni 80 kwa ajili ya malipo ya wakandarasi, kwa hiyo hakuna kisingizio. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge saa saba tukutane, tuone haja ya kuharakisha hili jambo ili kazi zisilale katika Jimbo la Tunduru. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Igongwi ni mradi mkubwa sana unaopeleka maji kwenye kata tatu na zaidi ya vijiji nane. Ni lini mradi huo utakamilika kwa maana ya usambazaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Nakushukuru.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mradi wa Igongwi ni mradi wa kimkakati na ni mradi mkubwa, nafikiri ufike mwisho. Kwa hiyo, kikubwa ni kutoa fedha ili kuhakikisha mradi ule tunaukamilisha. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Mwenyekiti wetu sitokuwa kikwazo tutaulipa kwa haraka ili kuhakikisha mradi ule tunaukamilisha kwa wakati, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itachimba kisima cha maji *(borehole)*, Kijiji cha Alaililai Kata ya Gelai Lumbwa, Wilayani Longido, Mkoa wa Arusha ambapo pesa zilikwishakuja lakini zimekaa tu na wananchi wanapata tabu, kisima hakijachimbwa na mwaka wa fedha unaisha? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nilielekeze hili jambo lifanyike kwa haraka kwa sababu magari yapo hakuna kisingizio. Kwa hiyo, mtu anayehusika na uchimbaji wa kisima, hiyo kazi ifanyike na mimi mwenyewe nitalisimamia kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Mradi wa Visima vya *Kisarawe II* utakamilika na kusambaza maji katika kata za Jimbo la Mbagala? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeunda timu kwa ajili ya kwenda kufuatilia utekelezaji wa hivyo visima na tutapata ripoti hivi karibuni. Nia ni kuleta msukumo na kuhakikisha ile kazi inakamilika kwa wakati. Nataka nimhakikishie Mbunge, baada ya hii taarifa, nitafika mimi mwenyewe kusukuma ili kuhakikisha hii kazi inakamilika mara moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itafanya ukarabati katika Mradi wa Maji kutoka Ukwile, Wilaya ya Mbozi kuelekea Tunduma ambao unahudumia Kata ya Mpemba na Kata ya Katete hasa kwa kuwa miundombinu iliyopo imetengenezwa mwaka 1971, hivyo ni chakavu sana na inashindwa kutoa huduma inayokusudiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Eneo la Mbozi ni eneo ambalo linahitaji kuangaliwa kwa macho ya karibu sana na nimepokea hiyo *concern* na tutalifanyia kazi kwa haraka sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mbangara umekuwa ukitengewa pesa kwa muda wa takribani miaka miwili sasa, lakini hakuna hata senti moja iliyokwenda na mradi haujaanza. Nini maelezo ya Serikali kuhusiana na mradi huu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kutekeleza miradi ya maji na wananchi waweze kupata huduma. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge lako hili mida ya saa saba kwa kuwa nina kikao kingine naomba tukutane ili tuweze kujadiliana utekelezaji hasa juu ya mradi huu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Kalulu ina changamoto kubwa sana ya maji na Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokwenda kule kwenye uchaguzi mdogo mwaka 2017 aliahidi kuwachimbia kisima kirefu cha maji. Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa maji kule na kumtua mama ndoo kichwani na kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, malekezo ya Viongozi Wakuu sisi kwetu ni utekelezaji. Kwa hiyo, naomba nielekeze hili jambo lifanyike mara moja kuhakikisha hiki kisima kinachimbwa na

kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu ili wananchi wa eneo hilo waweze kupata maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ombi langu la karibu miaka mitatu sasa la kutembelea Dongo kwenye Bwawa la Dongo ni lini tunakwenda na Mheshimiwa Waziri? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nimwahidi wiki ijayo, naomba nifike Dongo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Tangu tarehe 5 Machi, 2023, miradi ya maji ilisainiwa Kata ya Ntobeye na Kumuyange, Kata ya Nyamiaga, Wilaya ya Ngara, lakini mpaka sasa mkandarasi hajaonekana *site*. Je, ni lini mkandarasi huyo ataanza kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji, lakini naomba hili nilipokee na niweze kulifuatilia kwa haraka lakini kwa kuwa mkandarasi amekwishakabidhiwa kazi ni lazima afanye kazi. Kama ameshindwa kazi tutamchukulia hatua na tuweke mkandarasi ambaye ataweza kuifanya hii kazi kwa haraka na kuhakikisha watu wanapata huduma muhimu sana ya maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Ilemela imejenga katika milima na kulikuwa na Mradi wa Serikali wa kuweka mtandao wa maji taka na maji safi, lakini mradi huo ulisimama. Ni lini mradi huo utaendelea ili watu

walioko milimani waweze kupata huduma hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mama Mabula kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika Jimbo la Ilemela. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge, hili nilipokee kwa ajili ya ufuatiliaji ili kuhakikisha kwamba tunaisukuma hii kazi mara moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 477

**Ujenzi wa Vituo vya Askari wa Wanyamapori - Arumeru**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Askari Wanyamapori katika Vijiji vya Olchorapus, Imbibia na Engalaoni-Arumeru?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu ikiwemo ujenzi wa vituo vya Askari Wanyamapori katika maeneo mbalimbali nchini yenye changamoto hiyo. Lengo ni kuwasogeza askari karibu na maeneo ya jamii kwa ajili ya kuwezesha udhibiti wa wanyamapori kwa wakati na kuepusha madhara kwa wananchi na mali zao.

Mathalan, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 Serikali ilijenga vituo 16 katika maeneo yenye changamoto hiyo na kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Serikali imepanga kujenga vituo vingine 16 katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga vituo hivyo katika maeneo mengine yenye changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu ikiwemo Wilaya ya Arumeru kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputi, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; je…

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, Mbunge anayezungumza yuko upande huo. Tafadhali rudi viti vya mbele kidogo ili amalize kuzungumza. Ahsante sana.

Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakati Wizara ikisubiri kupata fedha za kujenga kituo kikubwa katika Vijiji vya Engalaoni, Oljorobusi na Imbibya, Wizara haioni sasa ni wakati muhimu wa kujenga kituo kidogo cha dharura ili kunusuru wananchi wa vijiji hivyo na wanyama wakali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kumekuwepo na uharibifu wa mazao ya wananchi katika hivyo vijiji ambavyo nimevitaja vya Engalaoni, Imbibya na Oljorobusi na nimekuwa nikifuatilia fidia hiyo. Je, Serikali imefikia wapi katika kuwalipa wananchi hao fidia ya migomba yao na mazao mengine yaliyoharibiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti wanyamapori kwenye eno hili, taasisi yetu ya *TANAPA* ndiyo inasimamia zoezi hili na taasisi yetu ina kituo kule Olmotonyi. Vilevile, tunawatumia askari wa *VGS* kutoka Hifadhi ya Jamii ya *WMA* kule Enduimeti. Katika siku za karibuni tumeona kumekuwa na ongezeko la wanyamapori katika eneo hili. Ndani ya Wizara tumeshasema kwamba kufuatia ongezeko hili wenzetu wa *TANAPA* waangalie uwezekano wa kuweka kituo cha muda.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaagiza askari wetu wa uhifadhi wa *TANAPA*, waende kwenye eneo hilo kwa haraka waende uwezekano wa kuanzisha kituo cha muda.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiwasiliana nasi kuhusiana na fidia kwa madhara yanayopatikana kwa wananchi kwenye eneo hili. Takribani wananchi 130 hivi wamekwishafidiwa jumla ya shilingi milioni 32. Tunao wananchi wachache wamebakia. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge atupe fursa ili tuweze kuyashughulikia madai yao na tuweze kuwalipa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 478

**Ujenzi wa Soko la Remagwe – Sirari**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, lini Soko la Remagwe – Sirari litajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, inaendelea na taratibu za kukamilisha ujenzi wa soko la kimkakati lililokuwa chini ya Mradi wa *DASIP* lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Eneo la Sirari katika Kijiji cha Remagwe. Mwezi Desemba, 2023 zabuni kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa soko hilo ilitangazwa na mzabuni amekwishapatikana. Aidha, zabuni kwa ajili ya ujenzi wa soko hilo ipo katika hatua ya upekuzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa soko hilo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa soko hilo utawezesha kuendeleza biashara ya mazao ya mahindi na mchele katika maeneo ya mpakani hususani Nchi ya Kenya. Ahsante sana,

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Hili soko ni Mkombozi wa Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara na Kanda ya Ziwa. Ni la kimkakati, liko mpakani, mazao yetu yanapotea na ni hasara kwa wakulima. Swali la kwanza; ningependa kujua kwa nini Mheshimiwa Naibu Waziri hakutaja kiwango cha fedha ambacho zinatumika kujenga soko hili ili tuone ukubwa wa soko litakalojengwa kwa *scope* hiyo ambayo ameitaja hapo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; upekuzi umeanza kufanyika tangu Desemba, 2023 mpaka leo. Je, utaisha lini ili ujenzi wa soko uanze mara moja na watu wangu waweze kupata huduma ya mazao yao? Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, sababu ya kutokutaja gharama ni kwa sababu iko katika hatua ya upekuzi.

Kwa hiyo, wakishamaliza maana yake ndiyo tuta-*confirm*. Hatua ya upekuzi huwa inafanyika kati yetu pamoja na Ofisi ya *AG* ambao baada ya mkandarasi kupita tunapeleka kule kwa ajili ya mapitio. Kwa hiyo, wao wakishajiridhisha baada ya mikataba, *then* wanatuletea sisi na wakishaleta maana yake mkandarasi tunamkabidhi *site* aanze kazi. Kwa hiyo, jambo hilo tutalifanya mara baada ya kukamilisha hizo taratibu. Ninaamini lipo katika hatua za mwisho. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Soko maarufu kwa jina la *TASAF* katika Mji wa Ilula ndilo soko pekee la mazao ya mbogamboga katika Wilaya ya Kilolo, lakini miundombinu yake ni chakavu na ina hali mbaya. Je, Wizara iko tayari tulete pendekezo la gharama kwa ajili ya kuboresha soko hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa sababu siyo masoko yote yako chini ya Wizara ya Kilimo, masoko karibu yote yako chini ya halmashauri. Sisi kama Wizara jukumu letu ni kuzisaidia hizo halmashauri kuboresha hayo masoko ili yaweze kuwa bora na kufanya kazi kwa kisasa. Kwa hiyo, niseme tuko tayari tuletee, tutakaa na tutazungumza tuone wapi tunaweza kusaidia. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kuna mkakati gani kati ya Wizara ya Kilimo na TAMISEMI kuhakikisha Soko la Ndizi la Kiwira ambalo tayari limekwishafanyiwa mchakato mzima liweze kujengwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri eneo la soko hili nalifahamu na hata tulipokuwa katika ziara kule Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwishatolea maelekezo, kwamba Wizara ya Kilimo tushirikiane na TAMISEMI kuhakikisha soko hili linajengwa ili tuweze kuwasaidia wakulima wa eneo la Kiwira. Kwa hiyo, lipo katika mipango baada ya kupokea hayo maelekezo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumekwishafika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. sasa nitaleta Tangazo la wageni ndiyo nililonalo hapa mbele. Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Kwanza, ni wageni wa Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa ambaye ni Waziri wa Ujenzi. Tunaye Balozi Mhandisi Aisha Amour, Katibu Mkuu; Bwana Ludovick Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu; na Mheshimiwa Mary Chatanda, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania. Ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Pia wapo Mheshimiwa Zainab Telack, Mkuu wa Mkoa wa Lindi; Ndugu Paschal Rwamgata, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Karagwe; Mheshimiwa Julius Laizer, Mkuu wa Wilaya ya Karagwe; Mhandisi Amin Mcharo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS);* Dkt. Ombeni Swai, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Majengo *(TBA);* Dkt. Fatma Mohammed, Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Ujenzi *(NCC);* na Ndugu Octavian Mshiu, Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Barabara *(RFB)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo Mhandisi Deogratius Nyanda, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA);* Wakili Menye David Manga, Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili ya Wahandisi *(ERB);* Dkt. Ludigija Bulamile, Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi; Bwana Stephen Paschal Makigo, Mwenyekiti wa Chama cha Makandarasi; na Ndugu Bernard

Ndakidemi, Rais wa Chama cha Wakadiriaji Majenzi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Jeniffer Bashungwa, Mke wa Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Ndugu Betha Bashungwa, Dada yake; Ndugu Sankara Bashungwa na Ndugu Solana Bashungwa, hawa ni watoto wake. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao ndugu Subilaga Kasekenya, Mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ndugu Denis Kasekenya, Agness Kasekenya na Debora Kasekenya ambao ni watoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na matangazo ya Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wengine.

Wapo wageni 100 wa Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, ambao ni Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi ngazi ya Matawi, kutoka Chamwino – Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini, huyu ni Kaimu Afisa Taaluma kutoka Longido, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, ambaye ni Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, hawa ni wadogo zake kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, ambaye ni mtoto wake kutoka Igunga, jamani huyu mtoto amezaliwa akiwa shule ya msingi ama? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Cosato Chumi, mwanafunzi wa Chuo cha Diplomasia Kurasini. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Neema Mwandabila, ambaye ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi Taifa kutoka Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Nicodemas Maganga ambaye ni Mpiga kura wake kutoka Mbogwe. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni wapiga picha kutoka Moshi Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani ambao ni Viongozi wa Chama cha Ushirika kutoka Mbogwe, Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Shamsia Mtamba, ambaye ni mdogo wake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambao ni ndugu zake kutoka Bukoba Vijijini.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Hawa Mchafu ambao ni rafiki yake akiwa na familia yake kutoka Dar es Salaam.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, ambao ni Viongozi wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa, karibuni sana. Hawa ni Viongozi wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa au ni tangazo limekosewa? Mheshimiwa Hasunga usijekuwa umechukua vyeo vya watu, maana viongozi nilikuwa nawatazama sura hapa. Hawa ni wa kutoka Vwawa au Taifa lakini ngazi nyingine? Hebu sema vizuri.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, hawa ni Maafisa kutoka Umoja wa Vijana wa Taifa.

**SPIKA:** Ni Maafisa siyo viongozi, sawa acha nirudie tangazo.

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, ambao ni Maafisa kutoka Umoja wa Vijana wa Chama Cha

Mapinduzi, karibuni sana, maana Viongozi wasije wakaona wamepinduliwa huko. *(Makofi)*

Tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Biharamulo, Mkoa wa Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao Wageni mbalimbali ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Yupo Ndugu Augustino Ndabaha ambaye ni Afisa Biashara wa Kampuni ya Bima Mtawanyo ya *Grand Reinsurance* Tanzania *Limited*. Karibu sana. *(Makofi)*

wapo Wakadiriaji Majenzi watatu kutoka Taasisi ya Wakadiriaji Majenzi Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wajumbe wanne wa Chama Cha Msakuzi *Neighbors* kutoka Mbezi Wilaya ya Ubungo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 57 na Walimu wanne wa shule ya Awali na Msingi *Genius Kings*' kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 28 na walimu sita kutoka shule ya Sekondari *St*. Marks ya Jijni Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni tulionao hapa Bungeni asubuhi hii, wengine tutaendelea kuwatangaza kadri watakavyoingia hapa ndani. Sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimwite sasa Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Waziri wa Ujenzi, aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ninaliomba Bunge lako Tukufu liridhie kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama leo hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba hotuba yangu yote iingie katika Kumbukumbu za Bunge kama ilivyowekwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Hotuba nikiwa Waziri wa Ujenzi, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ujenzi tangu tarehe 30 Agosti, mwaka jana 2023.

Mheshimiwa Spika, ninamwahidi Mheshimiwa Rais kuwa, kupitia dhamana hii aliyonipa, nitafanya kazi kwa weledi, bidii, uaminifu na ubunifu kwa kushirikiana na watumishi wenzangu katika Wizara na wadau wa Sekta ya Ujenzi ili kuhakikisha kuwa sekta hii inakua na kuendelea kuwa kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge tupunguze sauti kidogo tumsikilize Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa namna ambavyo wanamsaidia Mheshimiwa Rais katika majukumu ya kuitumikia nchi yetu. Nawashukuru pia Viongozi hawa kwa miongozo na maelekezo mbalimbali wanayonipatia katika kuisimamia Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya uongozi wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki kwa maelekezo na ushauri wa Kamati ambao umekuwa chachu katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Naishukuru pia Kamati kwa kuchambua kwa kina taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kupitisha Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri, maelekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu yangu umekuwa rahisi kutokana na ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwa viongozi wenzangu katika Wizara. Nawashukuru sana Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya, Naibu Waziri; Balozi Mhandisi Aisha Salim Amour, Katibu Mkuu; pamoja na Ndugu Ludovick James Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu. Nawashukuru pia Wakuu wa Idara na Taasisi na Mameneja wa Mikoa wa *TANROADS* pamoja na watumishi wa Wizara na Taasisi zake kwa kujituma katika utekelezaji wa majukumu tuliyokasimiwa Wizarani. Tunamwahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania wote hatutawaangusha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya ni Naibu Waziri mnyenyekevu na mchapakazi, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kumwamini na tunaahidi kudumisha umoja na mshikamano wa Wizara hii kuendelea kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa *speed* na viwango. Ninawapongeza wananchi wa Jimbo la Ileje kwa kuchagua Mbunge makini na mchapakazi ninawasihi sana

wananchi wa Jimbo la Ileje wampe tena nafasi Bungeni mwakani kwa mitano tena Mheshimiwa Mhandisi Kasekenya ili kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Muungano wa Mabunge Duniani, imani hii uliyooneshwa kimataifa inaakisi uwezo mkubwa ulionao katika uongozi wa Bunge letu Tukufu pamoja na masuala ya kimataifa. Umeweza majukumu haya mazito yenye kuleta heshima kubwa kwa nchi yetu naomba wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini waendelee kuwa watulivu na wakupe mitano tena mwakani kwani wamepata bahati ya kukupata wewe kiongozi hodari na adimu kwa Mbeya, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika, kwa kuendelea kutekeleza vyema wajibu wake katika kukusaidia kusimamia na kuliongoza Bunge letu. Nampongeza Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga pamoja na Wenyeviti wapya wa Bunge waliochaguliwa hivi karibuni Dkt. Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, hongereni sana Waheshimiwa Wenyeviti.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Karagwe kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuwatumikia pamoja na kutekeleza jukumu la kuwawakilisha humu Bungeni. Ninawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu na maarifa yangu yote ili kuhakikisha Wilaya yetu ya Karagwe inapata maendeleo tunayopenda. Ahsanteni sana Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Karagwe mkiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Komredi Rwamgata kwa kuwa humu Bungeni leo kuwawakilisha wananchi wa Karagwe wenzetu kwenye bajeti ya Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia mke wangu mpendwa Jennifer *a.k.a* Mama Alaska, watoto wangu, Santo, Solana, Sankara na Samora, Mama yangu na wadogo zangu kwa namna

wanavyonitia moyo na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Serikali leo tunaye humu Bungeni kwa nafasi yangu ya mlezi wa madereva wote wa Serikali nchini, nitumie fursa hii kuwapongeza madereva wa Serikali kwa majukumu yao katika kuendesha na kutunza vyombo vya moto vya Serikali. Nitoe wito kwa madereva hawa kuendelea kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, ninawataka wale wachache wanaoharibu taswira nzuri ya madereva wa Serikali kwa vitendo vilivyo kinyume na maadili waache mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue fursa hii kuwapongeza Vijana wa Jangwani *(Young Africans)* kwa kuvishwa taji la ubingwa wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara, ninawapongeza pia kwa kuchukua ubingwa mara tatu mfululizo na kuweka historia kuchukua ubingwa mara 30 tangu kuanzishwa kwa ligi. Imekuwa timu ya pekee hapa nchini kuweka historia hii. Vilevile naomba niwapongeze Simba kwa kuwa Mabingwa wa Ligi ya Muungano, hongereni sana Simba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2024, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu alitimiza miaka mitatu toka ameingia madarakani. Katika kipindi hicho cha uongozi wake, mafanikio makubwa yamepatikana.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa Barabara, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani Machi, 2021, mtandao wa barabara za lami ulikuwa kilometa 10,830.2, hadi kufikia Machi, mwaka huu 2024, mtandao wa barabara za lami umeongezeka na kufikia kilometa 12,028.7 katika kipindi cha miaka mitatu ya Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa madarakani miradi ya barabara 25 zenye jumla ya kilometa 1,198.5 imekamilika kujengwa katika Mikoa mbalimbali nchini. Barabara hizo ni:

(i) Ujenzi wa Barabara ya Tabora (Usesula) – Koga – Mpanda; (*Lot two*): Komanga – Kasinde (kilometa 120) Mkoani Tabora;

(ii) Ujenzi wa Barabara ya Tabora (Usesula) – Koga – Mpanda; (*Lot three*): Kasinde – Mpanda (kilometa 118) Mkoani Katavi;

(iii) Ujenzi wa Barabara ya Tabora (Usesula) – Koga – Mpanda (*Lot one*): Usesula – Komanga (kilometa 115) Mkoani Tabora;

(iv) Ujenzi wa Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga *Port* (kilometa 107) Mkoani Rukwa;

(v) Ujenzi wa Barabara ya Nyahua – Chaya (kilometa 85.4) Mkoani Tabora;

(vi) Ujenzi wa Barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (kilometa 66) Mkoani Ruvuma.

(vii) Ujenzi wa Barabara ya Kidahwe – Kasulu (kilometa 63) Mkoani Kigoma;

(viii) Ujenzi wa Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba (kilometa 55) Mkoani Mara;

(ix) Ujenzi wa Barabara ya Njombe – Moronga (kilometa 53.9) Mkoani Njombe;

(x) Ujenzi wa Barabara ya Moronga – Makete (kilometa 53.5) Mkoani Njombe;

(xi) Ujenzi wa Barabara ya Mpemba – Isongole (kilometa 51.2) Mkoani Songwe;

(xii) Ujenzi wa Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu (sehemu ya Makutano – Sanzate (kilometa 50) Mkoani Mara;

(xiii) Ujenzi wa Barabara ya Lusitu – Mawengi (kilometa 50) mkoani Njombe;

(xiv) Ujenzi wa Barabara ya Nyakanazi – Kakonko (Kabingo - kilometa 50) Mkoani Kigoma;

(xv) Ujenzi wa Barabara ya Loliondo – Mto wa Mbu (sehemu ya Waso – Sale *Junction*) (kilometa 50) Mkoani Arusha;

(xvi) Ujenzi wa Barabara ya Chunya– Makongolosi (kilometa 39) Mkoani Mbeya;

(xvii) Ujenzi wa Barabara ya Rudewa – Kilosa (kilometa 24) Mkoani Morogoro;

(xviii) Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (kilometa 25.7) pamoja na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji Mkoani Dar es Salaam;

(xix) Ujenzi wa Barabara, sehemu ya Kusenyi – Suguti (kilometa 5) Mkoani Mara;

(xx) Ujenzi wa Barabara ya Ardhi – Makongo – Goba (Sehemu ya Ardhi – Makongo - kilometa 5) Mkoani Dar es Salaam;

(xxi) Upanuzi wa Barabara ya Morocco – Mwenge (kilometa 4.3) Mkoani Dar es Salaam;

(xxii) Ujenzi wa Barabara ya Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (Mbezi Mwisho); sehemu ya Wazo Hill – Madale (kilometa 4.2) Mkoani Dar es Salaam;

(xxiii) Ujenzi wa Barabara ya Tungi – Kibada (kilometa 3.8) Mkoani Dar es Salaam;

(xxiv) Ujenzi wa Barabara ya Banana - Kitunda - Kivule - Msongola, sehemu ya Kitunda – Kivule (kilometa 3.2) Mkoani Dar es Salaam; na

(xxv) Upanuzi wa Daraja la Gerezani na barabara ya maingiliano (kilometa 1.3) Mkoani Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho cha miaka mitatu tangu Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia madarakani jumla ya miradi ya barabara 74 zenye urefu wa kilometa 3,794.1 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kati ya miradi ya barabara hizo 74 utekelezaji wa miradi ya barabara 12 umefikia zaidi ya 70% au zaidi na miradi 62 utekelezaji wake upo chini ya 70%, miradi hiyo imeonyeshwa katika aya ya 17 ya kitabu cha hotuba ya Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa madaraja makubwa. Katika miaka mitatu ambayo tunaadhimisha Mheshimiwa Rais toka ameingia madarakani yamekamilika kujengwa madaraja nane:-

(i) Daraja la Wami, Mkoani Pwani;

(ii) Daraja la Tanzanite, Mkoani Dar es Salaam;

(iii) Daraja la Gerezani, Mkoani Dar es Salaam;

(iv) Daraja la Mpwapwa, Mkoani Dodoma;

(v) Daraja la Kiyegeya, Mkoani Morogoro;

(vi) Daraja la Ruhuhu, Mkoani Ruvuma;

(vii) Daraja la Kitengule, Mkoani Kagera na;

(viii) Daraja la Msingi, Mkoani Singida.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho ujenzi wa madaraja makubwa matano uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

(i) Daraja la J.P. Magufuli (Kigongo – Busisi) Mkoani Mwanza, uko asilimia 88 na tunalenga likamilike kufika mwaka huu Desemba 2024;

(ii) Daraja la Mbangala Mkoani Mtwara, liko 66%;

(iii) Daraja la Pangani Mkoani Tanga, liko 23%;

(iv) Daraja la Mbambe Mkoani Pwani, liko 25%; na

(v) Daraja la Simiyu Mkoani Mwanza, liko 15%.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Viwanja vya Ndege, Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vitatu (3) katika kipindi cha miaka mitatu ya Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa madarakani, ambavyo ni viwanja vya ndege vya Songea, Mtwara na Songwe. Katika kipindi hicho, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya viwanja vya ndege saba (7) ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Viwanja hivyo ni:-

(i) Msalato *Airport* tuko 56.9% kwa kazi za ujenzi wa miundombinu ya kutua na kurukia ndege na 22.56% kwa kazi za ujenzi wa jengo la abiria na majengo majengo mengine;

(ii) Musoma *Airport* tuko 55%;

(iii) Iringa *Airport* tuko 90%;

(iv) Kigoma *Airport* awamu ya tatu tuko asilimia 3.7;

(v) Sumbawanga *Airport* tuko asilimia 8.4;

(vi) Shinyanga *Airport* tuko 11%; na

(vii) Tabora *Airport* awamu ya tatu tuko 38%.

Mheshimiwa Spika, taarifa za manunuzi zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Lake Manyara, Iringa awamu ya pili na Kiwanja cha Ndege cha Tanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita kwa upande wa *TEMESA* imepata mafanikio makubwa katika utoaji wa

huduma za vivuko kupitia *TEMESA* katika kipindi cha kuanzia Machi, 2021 hadi Mei 2024, Wizara imeendelea na ujenzi wa vivuko vipya ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Serikali itahakikisha Mkandarasi *MS* Songoro *Marine* analipwa fedha zote ili akamilishe ujenzi wa vivuko hivi ndani ya mwaka huu. Kwa mwezi Mei pekee mkandarasi huyu amelipwa jumla ya shilingi bilioni 1.53.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji wa madeni ya *TBA;* katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, *TBA* iliingia na deni lenye jumla ya shilingi bilioni 14.35. Kutokana na jitihada kubwa zilizofanywa na Wizara kupitia *TBA* katika kipindi tajwa, *TBA* imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 4.3; hii ni sawa na 30% ya malimbikizo ya deni. Hivyo, deni liliobaki ni shilingi bilioni 10.05. Natoa wito kwa wapangaji wote kuhakikisha kuwa wanalipa kodi za pango kwa wakati kuepusha usumbufu kwao na kwa *TBA*. *TBA* inaendelea na jitihada za kufuatilia ulipaji wa madeni hayo kwa kutumia dalali wa Mahakama ili fedha hizo zitumike kukarabati nyumba zilizopo na kujenga mpya ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika ukusanyaji wa madeni ya *TBA,* kupitia zoezi hilo ambalo niliagiza kuna baadhi ya wadaiwa walikwazika. Ukusanyaji wa madeni hayo ni maelekezo ya Bunge lako Tukufu na *CAG*. Hivyo, tunawaomba mtuvumilie wakati wa utekelezaji wa zoezi hili kwani ni zoezi endelevu. Ni matarajio yangu kuwa baada ya kukamilika kwa zoezi hili *TBA* itaweza kuboresha huduma zake ili wapangaji wafurahie maisha bora ndani ya nyumba za *TBA* na kujenga majengo mengi zaidi kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kudhibiti uzito wa magari; kuzuia uharibifu wa miundombinu ya barabara ni jambo la lazima na zoezi endelevu kwa kuwa tabaka la lami la barabara hujengwa kwa gharama kubwa. Wizara ina mpango wa kufunga mizani yenye teknolojia inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo *(Weigh in Motion System)* katika vituo vyote vya mizani nchini ili kutatua changamoto ya msongamano wa magari katika vituo vya mizani.

Mheshimiwa Spika, nimeshaagiza ndani ya Wizara na tunaanza kutekeleza hii bajeti ninayoomba. Katika bajeti tunapanga kujenga mizani 32 kama *weigh in motion*. Lengo ni kuwa na jumla ya mizani 110 ifikapo mwaka 2026/2027. Mizani hii yenye teknolojia ya kisasa hufungwa barabarani ili kuchuja magari ambayo hayazidi uzito na kuyaruhusu kuendelea na safari. Hivyo, msafirishaji hatalazimika kuingia katika kituo cha mizani endapo gari lake halitabainika kuzidi uzito katika mizani ya *weigh in motion*. Hivi sasa tunakuta msongamano wa magari kwenye mizani hata magari ambayo hayajazidi uzito. Teknolojia hii itatusaidia kuondoa hiyo kero.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya marekebisho katika maeneo hatarishi yaliyopo Barabara kuu ya kwenda Zambia ili kupunguza ajali za barabarani hususan eneo la Mlima Kitonga lenye urefu wa kilomita 7.6 kwa kufanya upanuzi wa kona tano zenye urefu wa kilomita 1.6 na upana wa mita tano.

Mheshimiwa Spika, ujenzi utaendelea kwa awamu hadi Mlima wote wa Kitonga upitike bila shida yoyote. Ujenzi wa maeneo ya maegesho, barabara za dharura na barabara ya mchepuo yenye urefu wa kilometa 2.8 kwa kiwango cha lami umefanyika ili kutenganisha malori na magari mengine katika eneo la Inyala, Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Spika, hayo ni machache katika mengi mazuri ambayo Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeyafanya katika Sekta ya Ujenzi. Hakika Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mama na Rais mwenye maono, mwonesha njia na mchapakazi. Tunamwombea afya njema na maisha marefu ili aendelee kuiongoza Tanzania yetu kufikia mafanikio makubwa kijamii na kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uharibifu mkubwa wa miundombinu, barabara na madaraja kutokana na mvua za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya. Nchi yetu imeathirika na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameleta athari za kimazingira katika

maeneo mbalimbali dunia nzima. Athari hizo kwa Tanzania zimejidhihirisha kupitia mvua kubwa za *El-Nino* zilizonyesha kwa takribani miezi tisa mfululizo, kuanzia Septemba mwaka jana hadi hivi sasa mwezi huu wa Mei. Mvua hizo zimesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara na madaraja kote nchini.

Mheshimiwa Spika, Mikoa iliyoathiriwa zaidi ni Lindi, Ruvuma, Morogoro, Singida, Tabora, Dodoma, Kilimanjaro, Songwe, Simiyu, Mbeya, Rukwa, Mwanza, Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Njombe, Iringa, Mtwara, Shinyanga na Manyara. Vilevile, Kimbunga Hidaya kiliyakumba maeneo ya Pwani ya nchi yetu na kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani.

Mheshimiwa Spika, mvua kubwa zilizoambatana na kimbunga hiki zilisababisha kukatika kwa mawasiliano baina ya Mikoa ya Pwani na Lindi eneo la Mikeng'ende, Songas, Somanga na Matandu, Nangurukuru. Maeneo mengine yaliyoathirika kwa kiasi kikubwa ni katika Barabara ya Nangurukuru – Liwale, Daraja la Miguruwe, eneo la Zinga na eneo la Mlowoka; Kiranjeranje – Namichiga, Daraja la Mto Mbwemkuru na Daraja la Kigombo pamoja na Tingi – Kipatimu, eneo la Mto Liomanga na eneo la Mto Chumo.

Mheshimiwa Spika, wakati tuko *site* kule tukisimamia barabara kuna mamalishe walitusaidia kutupikia chakula, nimewakaribisha Bungeni; naamini baadaye watatambulishwa. Kuna makapteni walitusaidia kututoa Somanga kwenda Kilwa Masoko, makapteni vijana watatu tumewakaribisha; naamini baadaye watatambulishwa. Pia, kuna Mzee Kimbwembwe *a.k.a* Mzee wa Jogoo naye yuko pamoja nasi naamini baadaye wataingia humu kwa ridhaa yako ili tuweze kuwatambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla uharibifu uliotokea katika Barabara ya Mtwara – Lindi – Dar es Salaam ni mkubwa na hivyo barabara yote inatakiwa kujengwa upya. Tayari manunuzi kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa kipande cha

Barabara ya Mtwara - Mingoyo yapo katika hatua za mwisho. Ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Julai mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua hatua za haraka kuhakikisha kuwa mawasiliano katika maeneo yaliyoathirika yanarejea. Hadi Mei 2024, kiasi cha shilingi bilioni 72 zilitolewa kwa ajili ya kurejesha mawasiliano. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za dharura. Tathmini ya jumla iliyofanyika imeonesha kuwa mahitaji halisi kwa ajili ya miundombinu iliyoathirika na mvua za *El-Nino* Kimbunga Hidaya ni shilingi trilioni 1.07. Serikali inasubiri taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa *(TMA)* kuhusu kumalizika kwa msimu wa mvua kwa ajili ya kuendelea na ukarabati na matengenezo ya maeneo yaliyoathiriwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ushiriki wa wazawa *(local content)* kwa maana ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi. Sekta ya Ujenzi ni mojawapo ya Sekta muhimu zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa. Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu wastani wa mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa katika kipindi cha miaka kumi (2012 – 2022) ni 14%. Sekta hii imekuwa ikikua kwa wastani wa 12% kwa mwaka kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miradi hiyo hutekelezwa na wakandarasi kutoka ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, pamoja na kutengewa kiasi kikubwa cha fedha, uchambuzi wa taarifa za usajili wa miradi ya ujenzi kwa miaka 10 iliyopita (2013 – 2024) umebaini ushiriki mdogo wa wakandarasi wazawa katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Usajili wa Makandarasi *(CRB)* kati ya jumla ya miradi 36,839 wazawa walitekeleza miradi 35,351 sawa na 95.9% ya miradi hiyo katika kipindi cha miaka 10 niliyoitaja. Hata hivyo, miradi iliyotekelezwa na wazawa ni midogomidogo yenye thamani ya shilingi trilioni

23.749, sawa na 38.5% ya thamani ya miradi yote iliyosajiliwa na kutekelezwa katika kipindi cha miaka 10, ambayo ni shilingi trilioni 61.638. Hivyo, wakandarasi wa nje ambao ni takriban asilimia 4.1 pekee walitekeleza miradi michache lakini yenye thamani kubwa (61.5% ya keki ya thamani ya miradi yote).

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizi za wakandarasi wa ndani, Wizara imedhamiria kuwawezesha wakandarasi wazawa kushiriki kwenye kazi kubwa za ujenzi kuanzia usanifu, ununuzi, ujenzi, matengenezo na ukarabati. Uwezeshaji wa wazawa utaleta manufaa ikiwemo kukuza biashara za wazawa, kupunguza matumizi ya fedha za kigeni, kuongeza ajira na ujuzi kwa wataalam wa ndani pamoja na kujenga uwezo wa kampuni za ndani kuweza kushindana Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Novemba mwaka jana niliitisha mkutano wa ushauriano na wakandarasi pamoja na washauri elekezi wa ndani kutoka mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo la mkutano huo lilikuwa kupata maoni na ushauri kutoka kwa wakandarasi wenyewe kuhusu changamoto walizonazo na utayari wa Serikali kuzitafutia suluhu. Baada ya mkutano huo, niliunda timu ya wataalam ili wachambue changamoto hizo na kuandaa Mkakati wa Kuongeza Ushiriki wa Wazawa katika Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi *(Local Content Strategy)*.

Mheshimiwa Spika, timu hiyo tayari imekamilisha kazi hiyo na imeandaa mapendekezo ya kufanyiwa kazi ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu. Hadi Mei mwezi huu 2024 tayari Serikali imetekeleza mapendekezeo kwenye hiyo *(Local Content Strategy)* ambayo tumeikamilisha na maeneo yafuatayo tumeyaboresha: -

Mheshimiwa Spika, *TANROADS* kwa kushirikiana na *PPRA* wanaendelea na taratibu za kuboresha ama kurekebisha vipengele kwenye makabrasha ya zabuni vilivyokuwa vikwazo kwa wakandarasi wazawa. Vipengele vilivyoboreshwa ni pamoja na:-

(a) Kupunguza kiwango cha mapato ghafi *(Average Turnover);*

(b) Kutumiwa kwa *Tender* au *Bid Securing Declaration* badala ya *Tender* au *Bid security.*

(c) Kutumia *Performance Bonds* au *Performance Securing Declaration* badala ya *Performance Bank Guarantee;* na

(d) Kutambua uzoefu wa wataalam badala ya uzoefu wa kampuni kwa ajili ya kazi zinazofanana *(Specific experience in the similar projects).*

Mheshimiwa Spika, Wizara imetenga miradi maalum kuwajengea uwezo wakandarasi wa ndani na wakandarasi wanawake ambao viongozi wao pia tumewaalika wawe pamoja nasi katika hii bajeti. Wizara ya Fedha imerekebisha Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa kuongeza wigo wa thamani ya miradi ya kutekelezwa na wazawa peke yao. Imependekeza kiwango kipande kutoka shilingi bilioni 10 za sasa hadi shilingi bilioni 50.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Wizara ya Fedha anayoiongoza kwa ushirikiano wa karibu kwenye utekelezaji wa mikakati ya kuwezesha wazawa ambapo utekelezaji wake tumeanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuwajengea uwezo wakandarasi wazawa, Wizara ina mkakati wa kuwajengea uwezo wakandarasi wanawake na kuongeza ushiriki wao katika miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara. Hadi sasa Wizara imetenga jumla ya kilometa 20 za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa ajili ya wakandarasi wanawake pekee. Kazi hizi zitagawanywa katika sehemu za kilometa tano tano ambapo wakandarasi wanawake pekee yao ndio wataomba kazi hizo. Hivi sasa miradi hii ipo kwenye hatua ya manunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wakandarasi wazawa kufanya kazi kwa weledi na utaalamu ili mikakati iliyowekwa na

Serikali isitafsiriwe kama mteremko. Hii ni kwa kuwa baadhi ya wakandarasi wazawa waliopewa miradi ya upendeleo wameikatisha tamaa Serikali kwa kutokuwa waadilifu, usimamizi wa miradi usioridhisha na kutumia muda mrefu katika utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa wakandarasi wa ndani ni kushiriki kikamilifu kwa uzalendo na uadilifu mkubwa katika ujenzi wa Taifa letu. Vilevile, mjiepushe na vitendo vya rushwa, tekelezeni mradi kwa ubora uliotegemewa ili kutoangusha dhamira hii njema ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuwainua kiuchumi. Kazi kwenu wakandarasi wazawa.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze kwa dhati Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Taifa Mary Chatanda kwa ufuatiliaji wa karibu kuhusu fursa hizi kwa wakandarasi wanawake. Ahsante sana Mwenyekiti wetu Mary Chatanda kwa kuwa pamoja nasi kwenye bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kujenga uwezo wa ndani ya taasisi na wastaafu wabobezi katika usimamizi wa miradi; *TANROADS* inatumia Kitengo chake cha Ndani cha Ushauri wa Kihandisi *(TECU)* katika usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja. Lengo ni kujenga uwezo wa taasisi zetu kusimamia miradi badala ya kutegemea wataalam nje.

Mheshimiwa Spika, hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za usimamizi wa miradi pamoja na muda uliotumiwa katika uamuzi wa wahandisi washauri. *TECU* ndiyo imesimamia ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa njia nane ya Kimara – Kibaha kilomita 19.2, Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Geita na Kiwanda cha Sukari cha Mbigili.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara kupitia taasisi zake *ERB* na *TANROADS* inaandaa utaratibu wa kutumia wataalam wa ndani waliostaafu *(Retired but not tired)* katika ujenzi wa matengenezo ya Barabara. *TECU* inaendelea kuwatumia wahandisi wabobezi waliostaafu katika usanifu na usimamizi wa miradi. Hiii imesaidia

kwa kiasi kikubwa kupunguza utegemezi wa wahandisi washauri kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, jambo hili la kutumia wahandisi wastaafu pia linatoa fursa kwa wataalam waliochipukia na ngazi ya kati kujifunza kutoka kwa wastaafu wabobezi ambao wapo nyumbani wakati wa ujuzi wao na wakati ujuzi wao bado unahitajika katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi kwa utaratibu wa kushirikisha Sekta binafsi *(PPP);* ujenzi wa miradi wa mjiundombinu hasa barabara na madaraja inaigharimu Serikali kiasi kikubwa cha fedha. Ili kuipunguzia Serikali gharama kubwa za utekelezaji wa miradi hiyo, Wizara imeanza kuishirikisha Sekta Binafsi kwa utaratibu wa *PPP*.

Mheshimiwa Spika, lengo la kutumia utaratibu huu ni kujenga miundombiunu na inasaidia kutekeleza miradi kwa wakati. Katika miradi ya barabara Serikali inakusudia kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kibaha – Chalinze – Morogoro – Dodoma *(Express way)* yenye urefu wa kilomita 423.8 kwa mfumo wa kulipia *(Toll Road system)*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa *EPC+F;* Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiisubiri *EPC+F* kwa hamu sana. Serikali imepanga kutekeleza miradi saba ya ujenzi wa barabara zenye jumla ya urefu wa kilomita 2,035 zenye kugharimu shilingi trilioni 3.7 kwa utaratibu wa *Engineering Procurement construction and Finance (EPC+F).*

Mheshimiwa Spika, *EPC+F* ni mfumo wa utekelezaji kwa kutumia wakandarasi ambao wanahusika katika taratibu za kumpatia mgharamiaji wa mradi kwa njia ya mikopo. Mfumo huu kwa nchi yetu ni mpya na lengo la kutumia mfumo huu ni kupunguza utegemezi wa fedha za ndani katika ujenzi wa barabara zetu. Mfumo huu kwa nchi yetu ni mpya na lengo la kutumia mfumo huu ni kupunguza utegemezi wa fedha za ndani katika ujenzi wa barabara zetu. Miradi hiyo saba nimeionesha na

kwa sababu ya muda Waheshimiwa Wabunge mnaweza mkaipata kwenye Aya ya 40 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mazungumzo na wakandarasi kuhusu ugharamiaji wa miradi yote saba ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa dhamira ya Serikali ya kutekeleza miradi hii ya *EPC+F* bado ipo palepale. Sasa naomba nieleze kwa muhtasari utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya matumizi ya kawaida; katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Ujenzi ilitengewa jumla ya shilingi 48,395,392,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 43,958,274,000 zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi zake na shilingi 4,437,118,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na taasisi zake. Hadi Aprili, 2024 jumla ya shilingi 48,665,781,258.75 zilikuwa zimetolewa na Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za maendeleo; katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilitengewa shilingi 1,419,843,057,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,699,800,000 zilihamishiwa Wizara ya Uchukuzi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Viwanja vya Ndege. Hivyo, Wizara ya Ujenzi ilibakiwa na shilingi 1,417,143,257,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi Aprili, 2024 fedha zilizopokelewa ni shilingi 1,421,842,330,490.81 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya fedha kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya miradi ya maenedeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa upande wa miradi ya barabara na madaraja. Maelezo kuhusu utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja yameoneshwa katika aya ya 42 mpaka 129 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya barabara na madaraja iliyosainiwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; pamoja na

utekelezaji wa miradi inayoendelea Serikali imeamua kutekeleza miradi mipya ya ujenzi wa barabara ili kuhakikisha wananchi wanatumia miundombinu bora ya barabara. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, mikataba ya ujenzi, ukarabati, usanifu wa miradi 25 mipya ya barabara na madaraja na mizani ilisainiwa. Kwa sababu ya muda miradi yote hii 25 inapatikana kwenye hii hotuba ninayoisoma pamoja na kwenye kitabu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Wizara ya Ujenzi imeandaa Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa kuzingatia viapaumbele vifuatavyo: -

(a) Kufanya matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja iliyoharibiwa na mvua za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya. Serikali inaendelea na majadiliano na wadau wa maendeleo wakiwemo *World Bank* na *African Development Bank* ili kupata fedha za matengenezo kupitia dirisha la dharura la *Contingency Emergency Response Component*. Kipaumbele kitakuwa ni kurejesha miundombinu ya madaraja na ma-*culvert* katika maeneo yaliyoathiriwa nchi nzima.

(b) Kipaumbele kingine ni kuendelea na utekelezaji wa miradi inayoendelea ambayo ni pamoja na ujenzi wa barabara za kimkakati zenye kufungua fursa za kiuchumi kama utalii, kilimo, madini, bandari, viwanda, Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere.

(c) Kipaumbele kingine ni miradi kupunguza msongamano wa magari katika Miji mikubwa kama vile Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma.

(d) Kipaumbele kingine ni ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa na nchi jirani kwa kiwango cha lami pamoja na barabara za ulinzi.

(e) Usanifu wa barabara mpya hasa mijini kwa kuzingatia mahitaji ya watumiaji wote wa barabara ikiwemo

wanamichezo, watembea kwa miguu na wanaoendesha vyombo visivyo vya moto; hususan baiskeli kama Bunge mlivyotushauri;

(f) Miradi ya kimkakati ikiwemo kukamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vya Msalato, Geita, Kigoma, Tabora, Songwe, Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Musoma, Songea, Tanga na Lake Manyara;

(g) Miradi ya udhibiti wa uzito wa magari ikiwemo kujenga mizani ya *weigh in motion* ili kupunguza msongamano wa malori barabarani na kwenye mizani;

(h) Miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko kupitia *TEMESA*;

(i) Miradi ya nyumba na majengo kupitia *TBA*;

(j) Kuendelea na matengenezo ya barabara kuu za mikoa pamoja na madaraja kwa kutumia wakandarasi wa ndani kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara pamoja na kuhakikisha kuwa barabara zinapitika katika majira yote ya mwaka;

(k) Kuendelea kuwajengea uwezo wataalam wa ndani kupitia programu mbalimbali kwa lengo la kuongeza wataalam wabobezi wa ndani ili waweze kusimamia miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa nchini *(local content)* kama nilivyoeleza. Hii ni pamoja na kukijengea uwezo kitengo cha ushauri elekezi wa miradi cha *TANROADS* (*TECU*) ili kiendelee kusimamia miradi mikubwa ya kimkakati;

(l) Kufanya mapitio ya Sera ya Ujenzi ya Mwaka 2003 na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani ya Mwaka 2009 pamoja na kanuni na miongozo mbalimbali inayohusiana na sekta ya ujenzi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na tabianchi;

(m) Kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utendaji kazi;

(n) Kutumia teknolojia za gharama nafuu katika ujenzi wa barabara hususan katika maeneo korofi;

(o) Kutekeleza Mkakati wa Uimarishaji na Utendaji kazi wa TEMESA kwa maana ya mkakati tulioukamilisha wa *TEMESA Transformation Strategy* ya mwaka huu 2024 – 2034.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida; katika Mwaka wa Fedha2024/2025, Wizara ya Ujenzi imetengewa shilingi 81,407,438,000 ikiwa ni bajeti ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 76,588,233,000 ni bajeti ya mishahara na shilingi 4,819,205,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Bajeti ya maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi ni shilingi 1,687,888,714,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,141,803,989,000 ni fedha za ndani na shilingi 546,084,725,000 ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani, shilingi 599,756,467,800 ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni shilingi 542,047,521,200. Mgawanyiko wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika kiambatisho namba moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi hiyo, Wizara kupitia *TANROADS* itaanza utekelezaji wa mradi wa kimkakati wa Ujenzi wa Daraja la Jangwani ambao ni sehemu ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa maendelezo ya Bonde la Mto Msimbazi. Daraja litakalojengwa lina urefu wa mita 390 pamoja na barabara unganishi yenye urefu wa mita 710 na kina cha mita 15.5 kutoka usawa wa bahari. Daraja hili litakapokamilika litatatua changamoto ya kujaa kwa maji katika Barabara ya Dar es Salaam – Morogoro eneo la Jangwani wakati wa mvua na kusababisha kufungwa kwa barabara hiyo mara kwa mara.

Tathmini ya zabuni ili kumpata mkandarasi na mhandisi mshauri zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ambayo inalenga kuondoa kero za msongamano wa magari katika majiji. Naomba niitaje. Miradi hiyo ni pamoja na upanuzi wa Barabara ya Mwanza – Usagara – Daraja la JPM kuwa njia nne, ina urefu wa kilomita 37, tutaanza na sehemu ya Mwanza – Usagara yenye urefu wa kilomita 22. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *BRT* awamu ya tatu; mradi huu unahusisha barabara ya Nyerere kuanzia makutano ya Barabara ya Kivukoni na Mtaa wa Azikiwe hadi Gongo la Mboto, yenye urefu wa kilomita 23.33. *BRT* awamu ya nne, kilomita 30.12; mradi huu unahusisha Barabara ya Ali Hassan Mwinyi – Morocco – Mwenge – Tegeta na kipande cha Mwenge – Ubungo. BRT awamu ya tano kilomita 27.6; mradi huu unahusisha Barabara ya Mandela kuanzia makutano ya Ubungo mpaka Bandarini. Makutano ya Mandela na Tabata, kuelekea Tabata Segerea na Tabata Kigogo.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe, kilomita 3.8, likiwemo Daraja la Mzinga ili kupunguza ajali na kero kubwa ya foleni katika eneo hili. Pia upanuzi wa Barabara ya Mwai Kibaki kuanzia Morocco – Shoppers Plaza – Kwa Nyerere – Kawe Roundabout – Kawe chini – Africana, jumla ya kilomita 11.6. Upanuzi wa barabara ya Uyole – Ifisi – Songwe – Airport jijini Mbeya yenye urefu wa kilomita 36 kutoka njia mbili kuwa njia nne na kazi inaendelea, tutaongeza *speed*.

Mheshimiwa Spika, vilevile ukamilishaji wa ujenzi wa Barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma unaohusisha ujenzi kwa kiwango cha lami, barabara ya mzunguko wa nje, wenye jumla ya urefu wa kilometa 112.92. Barabara hizi ni mbili; kuna kipande cha kuanzia *Ihumwa Dry port* karibu na mji wa Serikali; Matumbulu Nala, kipande hiki kina kilomita 60.62 na kipande kingine ni cha kuanzia Nala, njia ya Singida, uelekeo wa Iringa

Road kupitia Veyula – Mtumba – *Ihumwa Dry port* kina urefu wa kilomita 52.3.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya mzunguko wa ndani hapa Dodoma kuanzia *Bahi Roundabout – Image Roundabout – Ntyuka Roundabout – Makulu Roundabout* ina kilomita 6.3.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya mzunguko wa kati hapa Dodoma kuanzia Nanenane – Miyuji – Mnadani Sekondari – Mkonze – Ntyuka – Nanenane ina kilomita 47.2. Vile vile, pale Morogoro ukiwa unatoka Dar es Salaam, Morogoro Mjini tumeona kuna uhitaji wa kufanya upanuzi wa barabara kuja huku Dodoma eneo la…

*(Hapa Mheshimiwa Waziri alirekebisha maelezo ya hotuba yake)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kumradhi, hapa Dodoma nje ya Bunge tunapanga kupanua barabara kuelekea Morogoro eneo la kuanzia hapa Bunge hadi Mji wa Serikali Mtumba ili kupunguza foleni na usumbufu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ujenzi wa barabara za mchepuo za Singida eneo la Kisaki, Kititomo, Mtipa, Manga; upande wa Iringa tunapanga upande wa stendi ya Igumbilo – Kihesa Kilolo, kilomita saba. Upande wa Kilimanjaro, Kwa Sadala, Mheshimiwa Saashisha naona na Mheshimiwa Jesca naye anapiga makofi, upande wa Iringa tumejipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Songea eneo la Namanditi – Changarawe kilomita 14.4. Ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano Mkoa wa Morogoro, eneo la Msamvu – Kingolwira kilomita saba na Msamvu – Kihonda kilomita tano na Msamvu – Mafiga kilomita tatu ili kufungua mji wa Dodoma kwa wale ambao wanaelekea Iringa, Mbeya na wanaokuja Dodoma kupunguza muda mwingi ambao tunaupoteza na watumiaji wa magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirikishwaji wa sekta binafsi. Miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege, vivuko na majengo vinagharimu fedha nyingi na hivyo kuhitaji uwekezaji mkubwa. Ni dhahiri kuwa Serikali pekee haitakuwa na uwezo wa kutekeleza miradi hii yote kwa wakati kutokana na ufinyu wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuipunguzia Serikali gharama kubwa za utekelezaji wa miradi hiyo sambamba na kupunguza muda mrefu unaotumika katika kutekeleza miradi, Wizara inakaribisha ushiriki wa sekta binafsi kwa utaratibu wa *PPP*. Serikali imefanya maboresho makubwa katika Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Sura 103 kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu. Maboresho haya yatasaidia kuhakikisha kuwa mazingira ya uwekezaji yanakuwa rafiki zaidi kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Barabara, kama nilivyosema, tunakusudia barabara Kibaha – Chalinze – Morogoro – Dodoma kujenga *Expressway* kwa *toll system* kwa utaratibu wa *PPP*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaandaa andiko la ujenzi wa Barabara ya *TANZAM* kwa maana ya Dar es Salaam – Morogoro – Iringa – Mbeya – Songwe – Tunduma kwa *toll system* ya utaratibu wa *PPP*. Kuanzia Morogoro – Iringa – Mbeya – Tunduma kwa sababu kipande kingine cha Kibaha – Dodoma kitakuwa tayari kiko kwenye utaratibu huo. Kwa hiyo, kutoka Morogoro – Iringa – Mbeya – Tunduma na sehemu ya Igawa – Mbeya – Tunduma ambayo kwa kiasi kikubwa itasaidia kupunguza msongamano wa magari katika mpaka wetu na Zambia pale Tunduma na pia msongamano wa magari katika jiji la Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi mingine iliyoainishwa na Wizara ambayo inawezekana kutekelezwa kwa utaratibu wa *PPP* ni Barabara ya Mzunguko wa Dar es Salaam, *outer ring road*, kuanzia Bunju – Kibamba – Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma Kigamboni, kilomita 61 na *middle ring road* kuanzia Mbezi Mwisho – Kifuru – Banana – Kipara – Kigamboni kilomita 49. Pia daraja la pili la Kigamboni, pale ambako kivuko kinapita, tumeshapata

wawekezaji tunajadiliana nao. Wanaweza kujenga daraja kwa utaratibu ambao meli kubwa ya aina yoyote inaweza ikapita chini lakini bado kukawa kuna mawasiliano ya daraja ambapo maandalizi ya kufanya upembuzi yakinifu ya awali yanaendelea; na Barabara ya Himo – Moshi – Arusha Tengeru kilomita 78. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara inawakaribisha wawekezaji wenye nia kushiriki katika utekelezaji wa miradi hii na mingine itakayoibuliwa kwa ajili ya kutekelezwa kwa njia ya ubia. Wizara imepanga kufanya mkutano mkubwa wa wawekezaji kwa lengo la kutangaza hizi *package* na kujadiliana kuhusu namna bora ya kutekeleza miradi hii kwa utaratibu wa *PPP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkutano huo umepangwa kufanyika mwezi Julai, Waheshimiwa Wabunge tutawakaribisha ili tuweze kushiriki katika mkutano huu wa ku-*promote*, *PPP Conference*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miradi ya Vivuko kuna fursa mbalimbali katika uendeshaji wa vivuko hususan katika eneo la Kigamboni Kivukoni. Kwa sasa, eneo la Kigamboni lina wakazi zaidi ya 300,000 ambapo wanaotumia usafiri wa kivuko ni wastani wa watu 60,000 kila siku. Hata hivyo, kuna changamoto ya uchakavu wa vivuko vinavyohudumia katika eneo hilo ambapo kwa sasa kivuko cha *MV* Kazi pekee ndicho kinafanya kazi kwa uhakika. Aidha, Kivuko cha *MV* Magogoni kinaendelea kufanyiwa ukarabati mkubwa, Kivuko cha *MV* Kigamboni pia kipo katika matayarisho ya kufanyiwa ukarabati mkubwa; hivyo Serikali imeamua kushirikiana na sekta binafsi katika utoaji wa huduma za vivuko katika eneo hilo. Kwa sasa *TEMESA* inashirikiana na *Azam Marine Company Limited* kwenye utoaji wa huduma ya kivuko hapo Magogoni Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuangalia utaratibu bora zaidi wa ushirikiano huo ili kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na tija kwa pande zote mbili. Matarajio ya Wizara ni kuwa ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za vivuko katika eneo la

Kigamboni utaondoa kero kwa wananchi wanaotumia huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa wawekezaji wengine wenye nia ya kushirikiana na *TEMESA* katika utoaji wa huduma, si kwa vivuko pekee hata kwenye magari. Tunawakaribisha wawekezaji kuingia ubia *(joint venture)* na *TEMESA* katika matengenezo ya magari na ukodishaji wa mitambo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukemea taarifa za kupotosha zinazotolewa na vyombo vya habari kuhusu vivuko vya Kigamboni na kuzua taharuki kwa wananchi wa eneo hilo. Serikali ipo kazini na haiwezi kuhatarisha usalama wa raia wake kwa namna yoyote ile. Hivyo, niwaombe wananchi wa Kigamboni kuwa watulivu wakati Serikali inaendelea kuboresha huduma za vivuko pale Kigamboni sambamba na maboresho ya Barabara ya Kibada – Mwasonga *Junction* na Songani *Junction*, Kijata *Junction* yanayolenga kuifanya Kigamboni kuwa mji bora.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti ubora wa barabara. Katika kukabiliana na changamoto za kuharibika kwa barabara kabla ya muda wake, Wizara imepanga kuanza kutumia mitambo maalum ya kupima ubora wa barabara *(road scanners)*. Matumizi ya teknolojia hii yatatuwezesha kupima ubora wa barabara kama *x-ray* inavyopima mwili wa binadamu. Wizara imeamua kutumia teknolojia hii ya kisasa ili kuondoa kabisa matumizi ya vifaa visivyostahili katika upimaji wa ubora wa barabara vinavyotumika kwa sasa. Hivyo, sululu sasa basi. Matumizi ya mitambo hii yatadhibiti wakandarasi wasio waaminifu wanaocheza na viwango vya ubora wa barabara wanazojenga.

Mheshimiwa Spika, mitambo iliyonunuliwa ina thamani ya shilingi bilioni 5.1. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha hizi. Nikushukuru sana Mheshimiwa Spika, juzi ulitufungulia maonyesho na Waheshimiwa Wabunge nawashukuru mmeshiriki. Mitambo hii na magari haya ya kisasa yanaenda kutusaidia kuwadhibiti wakandarasi ambao walikuwa wanachakachua. Sasa muda wa wakandarasi hao

umekwisha, wakiendelea ku-*tamper* na ubora wa barabara, jela inawasubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ya kuwajengea uwezo makundi maalum hususan wanawake na vijana ili kuongeza ushiriki wao katika kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara kupitia *ERB*, *CRB* na *AQRB* itaandaa mpango mahususi wa kuwajengea uwezo vijana kwa nyenzo na ujuzi ili waanzishe kampuni za ujenzi na ushauri elekezi zitakazoshiriki katika ujenzi wa miundombinu kama tulivyobainisha kwenye *local content* niliyoitaja.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina mpango unaofanana na katika sekta nyingine, ambapo tumeona vijana wakiwekwa katika programu maalum. Sisi upande wa Wizara ya Ujenzi tunaangalia hawa vijana *graduate engineers* ambao kupitia programu ya *SEAP* wanaenda kusimamia ujenzi kwa kipindi cha miaka mitatu, wanapata *hands on experience* na wakitoka huko sasa kupitia hii *local content* wanaweza wakajiunga katika kikundi cha wachache, wakaandikishwa, wakaanza *class* ndogo ndogo za ujenzi huku tukiwajengea uwezo kupitia taasisi ambazo ziko chini ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, mikakati mingine inayotekelezwa na Wizara ni pamoja na kuendesha programu ya *SEAP* na *EAPP* kupitia *ERB* na *AQRB*. Programu hizi zinalenga kuwapatia ujuzi na uzoefu wahandisi wahitimu pamoja na wabunifu majengo na wakadiriaji ujenzi ili waweze kusajiliwa kama wataalam *(professionals)*.

Mheshimiwa Spika, vile vile Wizara kupitia *ICoT* inaendesha mafunzo ya muda mrefu katika fani za ujenzi umeme na mitambo katika ngazi za astashahada na stashahada ili kuzalisha wataalam watakaotumia Sekta ya Ujenzi. Mafunzi hawa ni muhimu sana katika utekelezaji wa kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, vile vile *ICoT* inaendesha mafunzo maalum ya muda mfupi kwa makundi maalum ya vijana

wanawake, wazee na wasiojiweza ili kuwajengea uwezo wa kushiriki katika kazi za matengenezo ya barabara zinazotolewa na *TANROADS* na *TARURA*. Lengo la mafunzo yote ni kuongeza ushiriki wa makundi hayo muhimu katika shughuli za ujenzi wa barabara. Wahitimu wa mafunzo haya huweza kuunda kandarasi kama nilivyosema kupitia *CRB* na hivyo kukidhi vigezo vya kupatiwa kazi za matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, katika hili UWT inaongozwa na mama yetu Mama Mary Chatanda kupitia umoja wa wakandarasi wanawake tumeshakaa; na kwa vile taasisi zetu wenyewe kama vile Baraza la Wajenzi na *ICoT* zina uwezo wa kuwafundisha vijana na akinamama hawa basi hata wakandarasi akinamama wajipange katika kusimamia kazi. Taasisi hizi zitakuwa zinawajengea uwezo ili waweze kujiamini na kusimamia shughuli za ujenzi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa makundi ya vijana na wanawake kurasimisha na kuingiza sokoni kazi zao ili kuchangamkia fursa hii adimu inayotolewa na Wizara. Wizara inaahidi kuwasimamia kwa kuzingatia taaluma zenu na kuwalea hadi kuwa kampuni kubwa zenye uwezo wa kushindana katika soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata nchi ambazo tumeona zimekua na zimekuwa na wakandarasi wakubwa walikuwa na mpango maalum wa kuziwezesha. Kwa hiyo, hata sisi kupitia hii *local content strategy* tukiamua kama Watanzania, *political* will ipo, Mheshimiwa Rais zile takwimu za keki kubwa kwenda kwa wakandarasi wa nje, alituelekeza tuje na mkakati; mkakati tumeukamilisha. Nimeshakaa na *multilateral organizations*, *World Bank*, *African Development Bank* na wahisani wote wa maendeleo. Tumewasilisha mkakati huu na wao wako tayari kushirikiana na sisi ili tuweze kuokoa fedha za kigeni; ambapo tunakopa fedha nyingi kwa ajili ya kujenga Barabara, lakini zikifika hapa hizo fedha za kigeni zinarudi huko ambako wakandarsi wa nje wanatoka na matokeo yake tunapoteza ajira, tunadumaza vipaji na *profession* hizi. Hivyo, kupitia mkakati huu tutaleta mageuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia hadhira hii, naomba kuwatambua na kuwashukuru, lakini kwa sababu muda wangu bado upo; nilikuwa nime-*skip* barabara ambazo tumeziweka kwenye mapendekezo nikarejea, kwa vile muda upo labda nizitaje hapa ili iwe …

**SPIKA:** Sijajua muda wako umebaki kiasi gani, kwa hiyo unaweza ukaanza kuzitaja ukaishia njiani.

Naambiwa hapa zimebaki dakika saba, kama zinatosha haya, kama hazitoshi basi elekea kumalizia, zimebaki dakika saba.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Basi niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwa vile zimebaki dakika saba niendelee na ile rejea ambayo niliitaja, lakini tumejipanga kwenye hiyo *package* ambayo nimeitaja.

Mheshimiwa Spika, kupitia hadhira hii naomba kuwatambua na kuwashukuru washirika mbalimbali wa maendeleo pamoja na wadau wote ambao wameshirikiana nasi kwa namna moja au nyingine katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru wafuatao; Benki ya Maendeleo ya Afrika *(African Development Bank), World Bank, JICA, OPEC Fund, KOICA,* Abu Dhabi *Fund*, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(EIB)*, *Kuwait Fund*, *Barick*, *EACOP*, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za *SADC*, Japan, China, Norway, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *NSSF* na *PSSSF*, Taasisi za fedha za *CRDB*, *NMB*, *NBC* na *TCB* na asasi mbalimbali zisizokuwa za Serikali, Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wengi tunawashukuru.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wadau hawa kipekee kwa kukubali kwa kauli moja kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa mkakati wa kuongeza ushiriki wa wazawa katika miradi ya ujenzi. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa tena shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwanza kwa ushirikiano ambao mmeendelea kutupa Wizara ya Ujenzi, lakini kwa usikivu wenu kwa bajeti hii ambayo ninahitimisha.

Mheshimiwa Spika, maombi ya Fedha za Wizara ya Ujenzi katika Mwaka Wa Fedha 2024/2025. Fedha ninazoziomba pamoja na masuala mengine, zitatumika kutekeleza kazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunaomba fedha hizi kukamilisha miradi ya barabara 12 ambayo utekelezaji wake umefikia 70% au zaidi, kama ilivyooneshwa katika Aya ya 17 ya Kitabu cha Hotuba yangu. Waheshimiwa Wabunge tunaomba mtuwezeshe ili hata mwakani wakati tunaenda kule, barabara hizi kwa vile ziko juu ya 70%, ziwe zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, kuendelea na miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja 62 ambayo utekelezaji wake uko chini ya 70%, lakini kazi inaendelea. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, wakituwezesha ina maana tunaenda kuongeza spidi ili barabara hizi na zenyewe ziweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kutekeleza miradi ya majengo ya Serikali; upande wa *TBA* kuna *shortage* kubwa sana ya nyumba hata kwa Waheshimiwa Wabunge hapa Dodoma. Kupitia bajeti na Sheria ya *TBA* ambayo tumeihuisha ya kuweza kushirikiana na sekta binafsi kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi, lakini kujenga nyumba kwa ajili ya mauzo. Bajeti hii tumejipanga kupunguza upungufu wa uhitaji wa nyumba kwa watumishi pamoja na kujenga kwa mujibu wa mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, Vivuko, Karakana na Viwanja vya Ndege. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,769,296,152,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 81,407,438,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara na taasisi na shilingi 1,687,888,714,000.00 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya

kawaida, shilingi 76,588,233,000.00 ni za mishahara ya watumishi na shilingi 4,819,205,000.00 ni za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inajumuisha fedha za ndani shilingi 1,141,803,989,000.00 na fedha za nje ni shilingi 546,084,725,000.00. Fedha za ndani zinajumuisha shilingi 599,756,467,800.00 kutoka Mfuko wa Barabara na shilingi 542,047,521,200.00 ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatisha mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa na Wizara katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 katika (Kiambatisho Na.1 – 5). Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa fursa hii, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

**HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, MHE. INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**A. UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja kwamba, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka wa fedha 2023/24, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2023/24. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu liridhie kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha

kusimama leo hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako kuwasilisha Hotuba nikiwa Waziri wa Ujenzi, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini, na kuniteua kuwa Waziri wa Ujenzi tangu tarehe 30 Agosti, 2023. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais kuwa, kupitia dhamana hii aliyonipa, nitafanya kazi kwa weledi, bidii, uaminifu na ubunifu kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Ujenzi ili kuhakikisha kuwa sekta hii inakua na kuendelea kuwa kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile naungana na Bunge lako Tukufu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Hakika sote tunajionea namna ambavyo Mheshimiwa Rais amefanikiwa kusimamia kwa dhati na kwa umakini mkubwa utekelezaji wa mipango na mikakati ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030). Uongozi wake mahiri, umekuwa chachu kwa viongozi wote tulio chini yake katika kusimamia maeneo tunayoyaongoza na kwa maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo wanamsaidia Mheshimiwa Rais katika uongozi wa nchi yetu. Nawashukuru pia Viongozi hawa kwa miongozo na maelekezo mbalimbali wanayonipatia ambayo yamekuwa dira yangu katika kuisimamia Wizara ya Ujenzi.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais

wa Muungano wa Mabunge Duniani. Imani hii uliyooneshwa kimataifa inaakisi uwezo mkubwa ulionao katika uongozi wa Bunge letu Tukufu. Aidha, nampongeza pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika, kwa kuendelea kutekeleza vyema wajibu wake katika kumsaidia Mheshimiwa Spika kusimamia na kuliongoza Bunge letu. Aidha, nawapongeza Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), pamoja na Wenyeviti wapya wa Bunge waliochaguliwa hivi karibuni Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb) na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.). Hongereni sana.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya uongozi wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso (Mb.) na Anne Kilango Malecela (Mb.) kwa maelekezo na ushauri wao ambao umekuwa chachu katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Naishukuru pia Kamati kwa kuchambua kwa kina Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/24 na kupitisha kwa kauli moja Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/25. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri, maelekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kutoa mkono wa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na wananchi wote kwa ujumla kufuatia vifo vya viongozi wetu wakuu wastaafu, Hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, aliyekuwa Waziri Mkuu katika Serikali ya Awamu ya Nne. Tutaendelea kuyaenzi mema yote waliyotuachia kupitia uongozi wao na tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, Amina.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika mwaka wa fedha 2023/24, Bunge lako Tukufu lilipata pigo kubwa kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu, Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali aliyefariki dunia tarehe 01 Julai, 2023 na Ahmed Yahya Abdulwakil, aliyekuwa Mbunge wa Kwahani

aliyefariki dunia tarehe 08 Aprili, 2024. Namuomba Mwenyezi Mungu awape wapendwa wetu hawa pumziko la amani.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote walioathirika kwa namna moja au nyingine kutokana na ajali za barabarani zilizotokea hapa nchini. Kipekee nitoe pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa watoto nane (8) wa Shule ya Msingi Ghati Memorial ya Jijini Arusha, ambao walifariki kutokana na basi lao kusombwa na maji walipokuwa wakienda shuleni. Nitoe wito kwa watumiaji wa barabara, na hasa madereva wa vyombo vya moto kuongeza umakini, hususan katika msimu wa mvua, ili kuepusha ajali za barabarani ambazo zingeweza kuepukika.

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutumia fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote walioathirika na mvua kubwa zilizoambatana na kimbunga Hidaya katika maeneo ya pwani ya nchi yetu na kusababisha vifo, majeruhi na upotevu wa mali. Kipekee nitoe pole kwa usumbufu mkubwa uliowapata watumiaji wa barabara zilizoathirika na kimbunga hiki hususan barabara ya Dar es Salaam - Lindi na kusababisha mawasiliano baina ya mikoa hiyo na mikoa mingine kukatika. Serikali ilichukua hatua za haraka za matengenezo ya barabara hiyo usiku na mchana na hivyo kurejesha mawasiliano ndani ya muda mfupi. Nichukue fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maelekezo na miongozo yake iliyotuwezesha kushughulikia changamoto hii kwa wakati.

**11.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, mnamo tarehe 03 Disemba, 2023 katika mji wa Katesh Wilaya ya Hanang', yalitokea maporomoko ya tope, magogo na mawe kutoka Mlima Hanang' hali iliyosababisha miundombinu mingi ya barabara, madaraja na makazi ya wananchi kuathirika. Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na TAMISEMI ilifanya tathmini ya uharibifu uliojitokeza katika miundombinu hiyo ambapo tahmini ilibainisha uharibifu katika barabara kuu ya Babati – Singida kilometa 1, mfereji wa barabara kuu na hifadhi ya barabara. Kwa upande wa barabara za Wilaya ya Hanang', jumla ya kilometa 19.70 ziliathirika katika mji wa Katesh.

**12.** ***Mheshimiwa Spika***, hatua za haraka zilichukuliwa na Serikali katika mpango wa muda mfupi ili kurejesha mawasiliano pamoja na kuondoa tope katika nyumba za wananchi zilizoathirika na maporomoko hayo. Kazi zilizofanyika ni pamoja na uondoaji wa mawe, tope na magogo katika barabara kuu na barabara za mitaa zilizoathirika na kurejesha mto katika njia yake ya asili ili kufungua barabara hizo. Nitumie fursa hii kutoa pongezi kwa timu za TANROADS na TARURA kwa kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha kuwa miundombinu ya barabara inapitika. Vilevile, ninaushukuru uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Manyara kwa ushirikiano wao wakati wote shughuli za kurejesha mawasiliano zilipokuwa zikifanyika.

**13.** ***Mheshimiwa Spika***, Mpango wa Muda Mrefu unaotekelezwa na TANROADS unahusisha kurejesha miundombinu katika hali yake ya awali kwenye barabara kuu ikiwa ni pamoja na kupendezesha mji wa Katesh. Kazi zilizoendelea kufanyika ni uwekaji tabaka la juu la lami (Overlay) kilometa mbili (2), ujenzi wa mtaro wa mawe na zege kilometa moja (1), usimikaji wa taa za barabarani 80 katika barabara yenye urefu wa kilometa mbili (2), ujenzi wa *paving blocks* mita za mraba 8,500 katika hifadhi ya barabara sehemu zenye maduka, ujenzi wa makalavati ya maji na ujenzi wa vivuko vya waenda kwa miguu katika mtaro wa maji.

## B. MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi, 2024, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitimiza miaka mitatu madarakani. Katika kipindi hicho cha uongozi wake, mafanikio makubwa yamepatikana katika nyanja takriban zote. Naomba uniruhusu japo kwa muhtasari nielezee mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka mitatu yanayohusu Sekta ya Ujenzi.

### Utekelezaji wa Miradi ya Barabara na Madaraja

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Machi, 2021 hadi Machi, 2024, Serikali ya Awamu ya Sita imepata mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja kama ifuatavyo:

**Ujenzi wa Barabara**

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi kupitia TANROADS inasimamia mtandao wa barabara wenye jumla ya kilometa **37,225.71** pamoja na jumla ya madaraja **9,563**. Mtandao wa barabara unahusisha Barabara Kuu zenye jumla ya kilometa **12,336.02** na Barabara za Mikoa zenye jumla ya kilometa **24,889.69**. Mtandao huu wa barabara una thamani (Asset Value) ya zaidi ya Shilingi Trillioni 32 kwa kuzingatia Tabaka la Juu. Barabara hizo zinahudumia takribani asilimia 70 ya magari yote nchini, na asilimia 85 ya mizigo na abiria nchini.

**17.** ***Mheshimiwa Spika*** Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilipoingia madarakani Machi, 2021, mtandao wa barabara za lami ulikuwa kilometa **10,830.2.** Hadi kufikia Machi, 2024, mtandao wa barabara za lami umeongezeka na kufikia kilometa **12,028.7** ikiwa ni ongezeko la kilometa **1,198.50** za lami. Ongezeko hili linatokana na kukamilika kwa miradi ya barabara **25** zenye jumla ya **kilometa 1,198.50**. Kukamilika kwa barabara hizi kumechangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha mawasiliano, kuimarisha biashara pamoja na kukuza uchumi wa maeneo husika. Barabara hizo ni:

i. *Ujenzi wa barabara ya Tabora (Usesula) – Koga – Mpanda; (Lot 2): Komanga – Kasinde (km 120) mkoani Tabora;*

ii. *Ujenzi wa barabara ya Tabora (Usesula) – Koga – Mpanda; (Lot 3): Kasinde – Mpanda (km 118) mkoani Katavi;*

iii. *Ujenzi wa barabara ya Tabora (Usesula) – Koga – Mpanda (Lot 1): Usesula – Komanga (km 115) mkoani Tabora;*

iv. *Ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107) mkoani Rukwa;*

v. *Ujenzi wa barabara ya Nyahua – Chaya (km 85.4) mkoani Tabora;*

vi. *Ujenzi wa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) mkoani Ruvuma;*

vii. *Ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Kasulu (km 63) mkoani Kigoma;*

viii. *Ujenzi wa barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 55) mkoani Mara;*

ix. *Ujenzi wa barabara ya Njombe – Moronga (km 53.9) mkoani Njombe;*

x. *Ujenzi wa barabara ya Moronga – Makete (km 53.5) mkoani Njombe;*

xi. *Ujenzi wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2) mkoani Songwe;*

xii. *Ujenzi wa barabara ya Makutano – Natta – Mugumu (sehemu ya Makutano – Sanzate (km 50) mkoani Mara;*

xiii. *Ujenzi wa barabara ya Lusitu – Mawengi (km 50) mkoani Njombe;*

xiv. *Ujenzi wa barabara ya Nyakanazi – Kakonko (Kabingo - km 50) mkoani Kigoma;*

xv. *Ujenzi wa barabara ya Loliondo – Mto wa Mbu (sehemu ya Waso – Sale Jct) (km 50) mkoani Arusha;*

xvi. *Ujenzi wa barabara ya Chunya– Makongolosi (km 39) mkoani Mbeya;*

xvii. *Ujenzi wa barabara ya Rudewa – Kilosa (km 24) mkoani Morogoro;*

xviii. *Upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) pamoja na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji mkoani Dar es Salaam;*

xix. *Ujenzi wa barabara, sehemu ya Kusenyi – Suguti (km 5) mkoani Mara;*

xx. *Ujenzi wa barabara ya Ardhi – Makongo – Goba (Sehemu ya Ardhi – Makongo -km 5) mkoani Dar es Salaam;*

xxi. *Upanuzi wa barabara ya Morocco – Mwenge (km 4.3) mkoani Dar es Salaam;*

xxii. *Ujenzi wa barabara ya Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (Mbezi Mwisho); sehemu ya Wazo Hill – Madale (km 4.2) mkoani Dar es Salaam;*

xxiii. *Ujenzi wa barabara ya Tungi – Kibada (km 3.8) mkoani Dar es Salaam;*

xxiv. *Ujenzi wa barabara ya Banana - Kitunda - Kivule - Msongola, sehemu ya Kitunda – Kivule (km 3.2) mkoani Dar es Salaam; na*

xxv. *Upanuzi wa daraja la Gerezani na barabara ya maingilio (km 1.3) mkoani Dar es Salaam.*

Aidha, katika kipindi hicho jumla ya miradi ya barabara **74** zenye urefu wa **kilometa 3,794.11** ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kati ya miradi hiyo, utekelezaji wa miradi ya barabara 12 umefikia asilimia zaidi ya 70. Barabara hizo ni:

i. *Tanga – Pangani (km 50);*

ii. *Muheza – Amani (km 4);*

iii. *Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3);*

iv. *Kanyani Jct – Mvugwe (70.5);*

v. *Mvugwe – Nduta Jct (km 59.35);*

vi. *Kibondo Jct – Kabingo (km 62.5);*

vii. *Noranga – Itigi (Mlongoji) (km 25);*

viii. *Itigi Township roads (km10.0);*

ix. *BRT I – Improvement (km 20.3);*

x. *BRT II (km 20.3);*

xi. *Nanganga – Ruangwa – Nachingwea: Lot 2: Nanganga – Ruangwa (km 53.2);*

xii. *Kidatu – Ifakara (km 66.9).*

Miradi mingine iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni:

i. *Ntendo – Muze – Kilyamatundu : sehemu ya Ntendo – Kizungu (km 25);*
ii. *Matai – Kasesya Road: Lot 1: Matai – Tatanda (km 25);*
iii. *Isyonje – Makete Road (sehemu ya Kitulo – Iniho (km 36.3);*
iv. *Itoni – Lusitu (km 50);*
v. *Mogabiri – Nyamongo (km 25);*
vi. *Uvinza – Malagarasi (km 51.1);*
vii. *Kumunazi – Kasulo – Bugene – Kyaka – Mutukula: Lot 2: Bugene – Burigi Chato National Park (km 60);*
viii. *Mnivata – Mitesa (km 100);*
ix. *Mitesa – Masasi (km 60);*

x. *TAMCO – Mapinga (km 13.59);*
xi. *Iringa (Ipogolo) – Kilolo (km 33.61);*
xii. *Kagera Sugar Jct – Kakunyu (km 25);*
xiii. *Tarime – Mogabiri (km 61.09);*
xiv. *Sabasaba – Sepuka – Ndago (km 77.4);*
xv. *Amanimakoro – Ruanda (km 35);*
xvi. *Tungamaa – Mkange (km 95.2);*
xvii. *Mianzini – Ngaramtoni (km 18);*
xviii. *Ifakara – Mbingu (km 62.5);* xix. *Mbulu – Garbabi (km 25);*
xix. *Labay – Haydom (km 25);*
xx. *Lusahunga – Rusumo (km 92);*
xxi. *Utete – Nyamwage (km 33.7);*
xxii. *Kasulu – Manyovu & Kasulu Town Links (km 68.67);*
xxiii. *Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60);*
xxiv. *Kikombo Jct – Chololo – Mapinduzi (JWTZ HQ) & Ntyuka Jct – Mvumi – Makulu (km 25);*
xxv. *Sanzate – Natta (km 40);*
xxvi. *Vikonge – Luhafwe (km 25);*
xxvii. *Luhafwe – Mishamo ( km 37.35);*
xxviii. *Nduta Jct – Kibondo Town – Kibondo Jct (km 25.9);*
xxix. *Kibondo – Mbamba (km 47.925);*
xxx. *Kibaoni – Mlele Jct (km 50);*
xxxi. *Itigi (Mlongoji) – Mkiwa (km 31.6);*
xxxii. *Handeni – Mafuleta (km 20.0);*
xxxiii. *Iringa Bypass (km 7.3);*
xxxiv. *Uyole – Ifisi (km 29);*
xxxv. *BRT III (km 23.33);*
xxxvi. *BRT IV (km 30.12);*
xxxvii. *Sengerema – Nyehunge (km 54.5);*
xxxviii. *Rehab. Ibanda – Kajunjumele, Kajunjumele – Kiwira Port & Reha. Kajunjumele-Itungi Port (km 32);*
xxxix. *Kizota – Zuzu SGR (km14);*
xl. *Maneromango – Kisarawe (km 3.125);*
xli. *Goba – Matosa – Temboni (km 3.0);*
xlii. *Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi (km 6.73);*
xliii. *Chanika – Mbande (km 3.8);*
xliv. *Morogoro (Bigwa) Mvuha (78);*
xlv. *Nachingwea – Ruangwa (km 57.6);*

xlvi. *Kibada - Mwasonga Jct (26.7);*
xlvii. *Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.6);*
xlviii. *Ruanda - Ndumbi Port (km 50);*
xlix. *Mbingu- Chita Jkt (km 37.5);*
l. *Kizengi Weighbridge (Tabora - Nyahua - Chaya);*
li. *Kongwa Jct - Ngambi – Mpwapwa (32.0);*
lii. *Kagwira – Kasekese (km 54.14);*
liii. *Kasekese- Ikola (km 56.91);*
liv. *Ndungu – Mkomazi (km 36);*
lv. *Isongole II – Ndembo (km 46.5);*
lvi. *Katumba– Lupaso (35.3);*
lvii. *Mbaka – Kibanja (km 20.7);*
lviii. *Kyerwa - Omurushaka (km 50);*
lix. *Ntyuka – Mvumi Hospital – Kikombo (km 53);*
lx. *Tatanda – Kasesya (km 25); na*
lxi. *Kahama – Bulyanhulu Jct – Kakola (km 73)*.

**Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Machi, 2021 hadi Machi, 2024, madaraja makubwa nane (8) yamekamilika kujengwa. Madaraja hayo ni:

i. Daraja la Tanzanite (km 1.03) mkoani Dar es Salaam;

ii. Daraja la Wami yenye urefu wa zaidi ya mita 510 mkoani Pwani;

iii. Daraja la Kitengule (m 140) mkoani Kagera;

iv. Daraja la Msingi (m 100 )mkoani Singida;

v. Daraja la Ruhuhu (m 98 ) mkoani Ruvuma;

vi. Daraja la Mpwapwa (m 60) mkoani Dodoma;

vii. Daraja la Gerezani (m 40) mkoani Dar es Salaam; na

viii. Daraja la Kiyegeya (m 25) mkoani Morogoro;

Aidha, hadi Aprili, 2024, ujenzi wa madaraja makubwa matano (5) upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:

i. Daraja la J.P. Magufuli (Kigongo – Busisi) yenye urefu wa kilomita 3.0 mkoani Mwanza, asilimia 88;

ii. Daraja la Pangani (m 525) mkoani Tanga, asilimia 23;

iii. Daraja la Simiyu (m 150) mkoani Mwanza, asilimia 15;

iv. Daraja la Mbangala (m 120)mkoani Mtwara, asilimia 66; na

v. Daraja la Mbambe (m 81) mkoani Pwani, asilimia 25;

**Miradi ya Kimkakati**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati ya barabara na madaraja kwa lengo la kuibua na kuchochea fursa za kiuchumi. Miradi mikubwa ya kimkakati inayoendelea ni pamoja na:

*i.* ***Mradi wa Ujenzi wa Daraja la J.P Magufuli (Kigongo – Busisi)*** lenye urefu wa kilometa tatu (3) unaohusisha ujenzi wa daraja linalounganisha maeneo ya Kigongo na Busisi na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 1.66. Mradi unatarajiwa kukamilika Disemba, 2024. Hadi mwezi Aprili, 2024 ujenzi ulifikia asilimia 88.

*ii.* ***Miradi ya Kupunguza Msongamano wa Magari Barabarani katika Jiji la Dar es Salaam***

Katika kukabiliana na changamoto ya msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, Serikali inatekeleza miradi ya ujenzi wa barabara za juu (Flyovers) ambapo ujenzi katika

makutano ya TAZARA, Ubungo, Uhasibu na Chang'ombe umekamilika.

Aidha, mazungumzo na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la JICA yanaendelea kwa ajili ya ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Mwenge na Moroco. Vilevile, ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya I kutoka Ubungo hadi Kivukoni umekamilika na awamu ya pili kutoka *City Center* – Mbagala unaendelea na umefikia Asilimia 99. Awamu ya tatu kutoka *City Center* – Gongo la Mboto umefikia Asilimia 26.55, awamu ya nne kutoka *City Center* – Tegeta kazi zimeanza na awamu ya tano kutoka Ubungo – Bandarini na Segerea – Tabata – Kigogo, zipo katika hatua za mwisho za manunuzi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali itaanza upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki na Mbagala – Vikindu.

***iii. Kupunguza Msongamano wa Magari katika Jiji la Dodoma***

Serikali inaendelea na mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma unaohusisha ujenzi kwa kiwango cha lami, barabara ya mzunguko wa nje yenye jumla ya urefu wa kilometa 112.3. Lengo la mradi huu ni kupunguza msongamano wa magari katikati ya Jiji la Dodoma ambapo, magari ambayo hayahitaji kupita katikati ya mji yatatumia barabara hiyo. Mradi huu unatekelezwa kwa sehemu mbili, ambapo hadi Aprili, 2024 utekelezaji wa sehemu ya kwanza ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Bandari Kavu (km 52.3) umefikia asilimia 75.53 na sehemu ya pili ya Ihumwa Bandari Kavu – Matumbulu – Nala (km 60) utekelezaji wake umefikia asilimia 61.

Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na Benki ya Dunia kwa ajili ya ufadhili wa upanuzi wa barabara zinazoingia na kutoka katika Jiji la Dodoma kuelekea Mbande (km 70) katika barabara ya Morogoro, kuelekea Msolwa (km 50) katika barabara ya Iringa, kuelekea Bahi (km 50) katika barabara ya Singida na kuelekea Zamahero (km 50) katika barabara ya Arusha kupitia mradi wa *Dodoma Integrated and Sustainable Transport* (DIST).

***iv. Kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Mbeya***

Serikali inaendelea na Upanuzi wa Barabara ya Uyole – Ifisi - Songwe Airport Jijini Mbeya yenye urefu wa kilometa 36 kutoka njia mbili kuwa njia nne. Lengo la mradi huu ni kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Mbeya ambapo hadi Aprili, 2024 utekelezaji ulikuwa umefikia asilimia 14.

***v. Kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Mwanza***

Katika Jiji la Mwanza, Serikali imepanga kufanya upanuzi wa barabara ya Mwanza - Usagara - JPM Bridge kwa njia nne (km 37); Sehemu ya Mwanza – Usagara (km 22).

***vi. Kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Arusha na Kilimanjaro***

Kwa upande wa mikoa ya Kilimanjaro na Arusha mradi utahusisha upanuzi wa barabara ya Tengeru – USA River, ujenzi wa mchepuo wa Kwa Sadala pamoja na daraja la Kikafu, Kibosho Shine hadi Kiboriloni katika mji wa Moshi, ambapo kazi ya Usanifu inaendelea.

***vii. Kupunguza msongamano wa magari katika Mji wa Iringa***

Kwa mkoa wa Iringa mradi utahusisha ujenzi wa barabara za mchepuo ya Iringa ambayo mkataba wake tayari umesainiwa.

***viii. Kupunguza msongamano wa magari katika Mji wa Songea***

Kwa Mkoa wa Ruvuma mradi utahusisha ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Songea ambayo ipo kwenye hatua ya manunuzi. Aidha, kazi ya  kupitia upya mahitaji ya barabara za michepuo nchi nzima kwa ajili ya kufanyiwa usanifu inaendelea.

**Miradi ya Viwanja vya Ndege**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vitatu (3) katika kipindi cha miaka mitatu ambavyo ni viwanja vya ndege vya Songea, Mtwara na Songwe.

Aidha, katika kipindi hicho, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya viwanja vya ndege saba (7) ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Viwanja hivyo ni Msalato (Asilimia 56.9 Package I - Miundombinu na Asilimia 22.56 Package II - Majengo); Musoma (Asilimia 55); Iringa (Asilimia 93); Kigoma (Awamu ya III Asilimia 3.7); Sumbawanga (Asilimia 10); Shinyanga (Asilimia 16); na Tabora (Awamu III Asilimia 45).

Vilevile, taratibu za manunuzi zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Lake Manyara, Iringa (Awamu ya II) na Kiwanja cha Ndege cha Tanga.

**Miradi ya Vivuko**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imepata mafanikio makubwa katika utoaji wa huduma za vivuko kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA). Katika kipindi cha kuanzia Machi, 2021 hadi Machi, 2024 Wizara imeendelea na ujenzi wa vivuko vipya nane (08) ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Vivuko hivyo vikikamilika vitatoa huduma katika maeneo ya Bwiro – Bukondo, Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangala, Nyakaliro – Kome, Buyagu – Mbalika, Mafia – Nyamisati na Magogoni – Kigamboni.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ***ukarabati wa vivuko***, Serikali kupitia TEMESA imekamilisha ukarabati wa vivuko 20 vinavyofanya kazi katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali imeendelea na ***ujenzi wa maegesho*** 12 pamoja na kuendelea na ***ujenzi wa miundombinu ya majengo*** katika maeneo ya kutolea huduma za vivuko.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendana na kasi ya mabadiliko katika ukuaji wa teknolojia, Wizara kupitia TEMESA imeendelea

kuboresha miundombinu wezeshi katika maeneo ya kutolea huduma za vivuko. Kazi zilizofanyika ni pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Mapato katika vivuko vyote; Mfumo wa Nishati ya Umeme Jua katika eneo la Ilagala-Kajeje pamoja na Mfumo wa Kamera na Mfumo wa Matumizi ya Kadi katika mageti ya kuingia katika kivuko cha MagogoniKigamboni. Vilevile TEMESA imefanikiwa kuboresha Mfumo wa Tiketi za Kielektroniki katika kituo cha Kigongo – Busisi. Kazi ya kusimika Mfumo wa Usimamizi wa Matumizi ya Mafuta inaendelea katika vivuko vyote.

**Miradi ya Nyumba na Majengo ya Serikali**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali kupitia Wakala wa Majengo Tanzania. Mafanikio hayo ni pamoja na:

i. Kukamilisha miradi ya kimkakati kama vile ujenzi wa Ikulu ya Chamwino, Ubunifu wa majengo ya Mji wa Serikali awamu ya pili na kuendelea kusimamia ujenzi wa majengo hayo;

ii. Kusimamia mradi wa ujenzi wa vihenge vya kisasa katika mikoa nane (8) nchini;

iii. Kukamilisha Awamu ya I ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa wakaazi 644 wa Magomeni Kota, Dar es Salaam na kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya II ya mradi huo ambapo jengo moja kati ya matano (5) lenye sakafu nane limekamilika;

iv. Kuendelea kusimamia ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Forodha katika eneo la Kasumulu wilayani Kyela kwenye mpaka wa Tanzania na Malawi;

v. Kukamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba 150 za Awamu ya I na kuanza ujenzi wa nyumba 150 za Awamu ya II kwenye mradi wa ujenzi wa nyumba 3,500 za makazi katika eneo la Nzuguni jijini Dodoma;

vi. Kukamilisha ujenzi wa nyumba 20 za viongozi katika eneo la Kisasa, Dodoma;

vii. Kukamilisha ujenzi wa jengo la makazi la sakafu 11 eneo la Sekei, jijini Arusha na ujenzi wa jengo moja la sakafu saba (7) katika eneo la Canadian Village Masaki Jijini Dar es Salaam;

viii. Kukamilisha miradi 107 ya Washitiri na kuendelea na utekelezaji wa miradi mingine 125. Kati ya miradi iliyokamilika, miradi 61 ni ya ushauri, 27 ni ya Buni-Jenga (Design and Build) na 19 ni ya ujenzi; na

ix. Kuhuishwa kwa sheria iliyoanzisha Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ili kuruhusu TBA kushirikiana na sekta binafsi katika kuendeleza miliki nchini. Sheria hiyo imehuishwa kupitia Tangazo la Serikali GN namba 595 la Agosti 25, 2023.

**Udhibiti Uzito wa Magari na Masuala ya Usalama Barabarani**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha miundombinu ya barabara zinaenda sambamba na uimarishaji wa miundombinu ya usalama barabarani. Lengo ni kuhakikisha usalama wa watumiaji wote wa barabara, ikiwa ni pamoja na kuzuia uharibifu wa miundombinu ya barabara ambayo hujengwa kwa gharama kubwa. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitatu katika masuala ya usalama barabarani ni pamoja na:

i. Wizara kupitia TANROADS, imefanikiwa kujenga mizani 12 ya kudumu ambayo ni mizani ya Usagara West (Mwanza), Rubana (Mara - 2), Matundasi (Mbeya), Mingoyo North (Lindi), Mikumi South (Morogoro), Kamsisi (Katavi), Mdori West (Manyara Igagala (Njombe), Nyantare (Mara) na Mkolye (Tabora - 2). Aidha mizani saba (7) inayopima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion) imejengwa Mikumi (2) mkoani Morogoro, Kemokouwa (Arusha -2), Mikese North (Morogoro) na Rubana (Mara – 2). Kupitia mizani hiyo, uzidishaji wa uzito unaoruhusiwa kisheria umeshuka kutoka

asilimia 0.48 kwa mwaka wa fedha 2021/22 hadi asilimia 0.26 kwa mwaka wa fedha 2023/24.

ii. Wizara ya Ujenzi kupitia TANROADS ilianzisha na kutekeleza utaratibu wa magari ya mafuta (fuel tankers) na makasha yenye rakili (sealed containers) kupima uzito katika vituo vitatu (3) tu vya mizani katika kila ushoroba. Vituo hivyo kwa kila shoroba ni kama ifuatavyo:

a. Ushoroba wa Kati

- Vigwaza, Njuki na Tinde (Dar es Salaam – Mwanza/Mara);
- Vigwaza, Njuki na Mwendakulima (Dar es Salaam – Rusumo/Kabanga);
- Vigwaza, Itigi, Ilolanguru (Dar es Salaam-Tabora/Kigoma);
- Vigwaza, Njuki na Mutukula (Dar es Salaam – Uganda)
- Vigwaza, Njuki na Nyakahura (Dar es Salaam - Rwanda/Burundi).

b. Ushoroba wa TANZAM

- Vigwaza, Wenda na Luhimba (Dar es Salaam – Ruvuma);
- Vigwaza, Wenda na Nkangamo (Dar es Salaam – Tunduma/Katavi);
- Vigwaza, Wenda na Uyole (Dar es Salaam – Kasumulu);
- Vigwaza, Wenda na Mpemba (Dar es Salaam – Tunduma).

c. Ushoroba wa Kusini

• Mkuranga, Mingoyo na Ndumbwe (Dar es Salaam – Mtwara);

• Mkuranga, Mingoyo na Sisi kwa Sisi (Dar es Salaam – Songea);

• Ndumbwe, Mingoyo na Sisi kwa Sisi (Mtwara - Songea).

d. Ushoroba wa Kaskazini

• Kunduchi, Msata na Himo (Dar es Salaam – Kilimanjaro);

• Kunduchi, Msata na Pongwe (Dar es Salaam – Tanga).

e. Barabara kuu ya Tanga – Rusumo/Kabanga/Mutukula

• Pongwe, Njuki na Nyakahura (Tanga – Burundi/Rwanda)

• Pongwe, Njuki na Mutukula (Tanga – Uganda)

Utaratibu huu umesaidia kupunguza muda wa safari pamoja na msongamano wa magari katika vituo vya mizani.

iii. Wizara imefanya marekebisho katika maeneo hatarishi (blackspot areas) yaliyopo barabara ya TANZAM kwa kuweka alama zote muhimu za barabarani, michoro ya barabarani, kufunga taa za usalama barabarani (street lights), kupanua makutano ya barabara pamoja na kujenga njia na vivuko vya waenda kwa miguu. Maeneo hatarishi yaliyofanyiwa marekebisho ni pamoja na Inyala Mkoani Mbeya; Kingolwira, Milima ya Iyovi, Mbuga ya wanyama ya Mikumi na Kijiji cha Mikumi Mkoani Morogoro; Picha ya Ndege, Kwa Mathias, Kongowe, Vigwaza na Chalinze

Mkoani Pwani pamoja na mlima Kitonga Mkoani Iringa. Aidha, ujenzi wa madaraja mapya ya Wami na Kibamba ambapo ajali nyingi zilikuwa zikitokea umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ajali za barabarani.

iv. Wizara imefanikiwa kukamilisha ufungaji wa taa za kuongoza watembea kwa miguu wanaovuka barabara katika maeneo ya shule ili kupunguza au kuondoa ajali za barabarani katika Shule za Msingi za Kinyerezi, Kifuru, Liwiti, Tabata JICA – Polisi, Kibasila na DUCE Gate 1.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** hayo ni machache kati ya mengi mazuri ambayo Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeyafanya katika Sekta ya Ujenzi. Hakika, Mama anaupiga mwingi. Tunamuombea afya njema na hekima zaidi ili aendelee kuiongoza Tanzania yetu kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi yanayojumuisha mafanikio yaliyopatikana katika awamu ya sita, naomba sasa nitoe taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2023/24 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

28. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/24 ni kama ifuatavyo:-

### C.1 FEDHA ZILIZOTENGWA NA KUTOLEWA

#### Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

29. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Ujenzi ilitengewa jumla ya **Shilingi 48,395,392,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 43,958,274,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi

wa Wizara na Taasisi zake na **Shilingi 4,437,118,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zake.

Hadi Aprili, 2024 jumla ya **Shilingi 48,665,781,258.75** zilikuwa zimetolewa na HAZINA kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 46,307,923,275.52** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 2,357,857,983.23** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zake.

**Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ilitengewa Shilingi **1,419,843,057,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kati ya fedha hizo, Shilingi **2,699,800,000.00** zilihamishiwa Wizara ya Uchukuzi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Viwanja vya Ndege. Hivyo, Wizara ya Ujenzi ilibakiwa na Shilingi **1,417,143,257,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni Shilingi **1,081,966,569,000.00** na Shilingi **335,176,688,000.00** ni fedha za nje. Fedha za ndani zilijumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali Shilingi **482,210,099,000.00** na fedha za Mfuko wa Barabara Shilingi **599,756,470,000.00.**

31. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 1,421,842,330,490.81**. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 1,085,172,671,145.57** ni fedha za ndani na **Shilingi 336,669,659,345.24** ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani zilizopokelewa, **Shilingi 583,486,514,233.61** ni kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 501,686,156,911.97** ni za Mfuko wa Barabara.

## C.2 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

### Miradi ya Barabara na Madaraja

32. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa tathmini ya mwaka 2023, mtandao wa Barabara Kuu na za Mikoa unaosimamiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ni **kilometa 37,225.71** kati ya hizo kilometa **12,336.02** ni barabara kuu na kilometa 24,889.69 ni barabara za mikoa.

Miradi ya Barabara Kuu iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/24 ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 350** pamoja na ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 25.** Kwa upande wa madaraja, mpango ulikuwa ni kuendelea na ujenzi wa madaraja **13,** kuanza ukarabati wa daraja moja (1), kuanza maandalizi ya ujenzi wa madaraja 11 pamoja na kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa daraja moja (1).

33. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 201.58** umekamilika na ujenzi wa **kilometa 148.42** unaendelea.

Kwa upande wa madaraja, ujenzi wa madaraja ya Mbangala (Mtwara) umefikia asilimia 66 na Mbambe (Pwani) umefikia asilimia 25. Vilevile, Makandarasi wa ujenzi wa Madaraja sita (6) ya Mirumba (Katavi), Mpiji Chini (Dar es Salaam), Simiyu (Mwanza), Sukuma (Mwanza), Kibakwe (Dodoma), Kerema Maziwa (Dodoma) wanaendelea na maandalizi ya ujenzi. Taratibu za manunuzi ya Makandarasi wa ujenzi wa madaraja nane (8) ya Sanza (Singida), Mkenda na Mitomoni (Ruvuma), Godegode na Nzali (Dodoma), Doma, Chakwale na Nguyami (Morogoro) zinaendelea. Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa madaraja ya Malagarasi Chini (Kigoma) na Munguli (Dodoma) unaendelea. Aidha, ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara) utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja ya Mtera Dam (Dodoma), Kinyerezi (Dar es Salaam), Kisorya – Ukerewe (Mwanza/Mara) na Suguti (Mara).

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 miradi ya barabara za mikoa iliyopangwa kutekelezwa ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 84** zinazohusisha **kilometa 50** kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 34** kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Vilevile, TANROADS ilipanga kufanya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara zenye urefu wa **kilometa 844.** Kati ya hizo, **kilometa 545** ni kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa

Serikali na **kilometa 299** ni kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Kazi nyingine ni kujenga na kufanya ukarabati wa madaraja/makalavati **59** kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **44** kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 jumla ya kilometa **30.45** za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya **kilometa 275.8** zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Aidha, ujenzi/ukarabati wa madaraja madogo **12** kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **13** kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na utekelezaji wa miradi inayoendelea, Serikali inaendelea kutekeleza miradi mipya ya ujenzi wa barabara ili kuhakikisha wananchi wanatumia miundombinu bora ya barabara. Katika mwaka wa fedha 2023/24, mikataba ya ujenzi/ukarabati wa miradi **24** mipya ya barabara na madaraja ilisainiwa. Miradi hiyo ni:

i. *Maboresho ya miundombinu ya mabasi yaendayo haraka iliyojengwa katika Awamu ya Kwanza; Ukarabati wa sehemu ya Obama Drive pamoja na barabara iendayo Stendi ya mabasi ya Kivukoni na barabara ya Msimbazi;*

ii. *Ujenzi wa daraja la Simiyu (m 150) na barabara unganishi kilometa 3.0 kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa usanifu na ujenzi;*

iii. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tarime - Mugumu (km 86); Sehemu ya Tarime – Mogabiri (km 9.3), Nyamongo – Mugumu (km 48.15) pamoja na barabara ya kuelekea Mugumu Roundabout (km 3.6);*

iv. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78) pamoja na ujenzi wa daraja la Ruvu (m 64) na daraja la Mvuha (m 60);*

v. *Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Nachingwea – Ruangwa – Nanganga (km 106); sehemu ya Nachingwea – Ruangwa (km 57.6);*

vi. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (km 41); sehemu ya Kibada – Mwasonga (km 26.7) na Songani Jct – Kijata Jct;*

vii. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ubena Zomozi - Ngerengere (km 11.6);*

viii. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitai – Lituhi (km 84.5); sehemu ya Ruanda – Ndumbi Port (km 50) kwa kiwango cha lami;*

ix. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ifakara – Kihansi (km 124); Sehemu ya Mbingu – Chita JKT (km 37.5);*

x. *Ujenzi wa Mizani ya Kizengi pamoja na uwekaji taa za barabarani katika barabara ya Tabora - Nyahua – Chaya;*

xi. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Iringa (Ipogolo) - Kilolo (km 33.61);*

xii. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Kongwa Jct – Ngambi – Mpwapwa (km 32) na Mpwapwa - Gulwe - Kibakwe (km 46.9);*

xiii. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kagwira – Ikola – Karema Port (km 112); Sehemu ya Kagwira – Kasekese (km 54.15);*

xiv. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kagwira – Ikola – Karema Port (km 112); Sehemu ya Kasekese - Ikola (km 56.91)*

xv. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Same - Kisiwani - Mkomazi (km 100.5); sehemu ya Lot 2: Ndungu – Mkomazi (km 36);*

xvi. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Isongole II – Kasumulu – Ipyana – Katumbasongwe (km 114.3) ikijumuisha barabara ya Ndembo – Isoko Spur Road (km 5.92) na sehemu ya Muungano – Ipyana (km 0.66); Lot 1: Isongole II – Ndembo (km 46) na Ndembo Spur Road (km 6);*

xvii. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Katumba – Mbambo - Tukuyu (km 79.4); sehemu ya Lot 3: Katumba– Lupaso (km 35.3);*

xviii. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Katumba – Mbambo – Tukuyu (km 79.4); sehemu ya Lot 4: Mbaka – Kibanja (km 20.7);*

xix. *Usanifu na ujenzi kwa kiwango cha lami (Design and Build) wa barabara ya Kyerwa - Omurushaka (km 50);*

xx. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Ntyuka Jct - Mvumi - Kikombo Jct (km 76) na Chololo - Mapinduzi (TPDF HQ) (km 5); sehemu ya Ntyuka – Mvumi Hospital - Kikombo (km 53);*

xxi. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Kahama – Bulyanhulu Jct – Kakola (km 73);*

xxii. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50.6); sehemu ya Tatanda – Kasesya (km 25);*

xxiii. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Dareda – Dongobesh (km 60); sehemu ya Dareda Mjini – Dareda Mission (km 8); na*

xxiv. *Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Sungusila – Nzera – Nkome Port (km 20.36).*

Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Miradi ya Matengenezo ya Barabara na Madaraja kwa kutumia Fedha za Mfuko wa Barabara (Roads Fund)**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, mpango wa matengenezo katika Barabara Kuu na Barabara za Mikoa ulihusisha matengenezo ya kawaida **kilometa 34,383.67,** matengenezo ya muda maalum **kilometa 3,612.59,** matengenezo ya sehemu korofi **kilometa 402.65** pamoja na matengenezo ya madaraja **3,129**.

Hadi kufikia Aprili, 2024, kazi zilizofanyika katika Barabara Kuu na Barabara za Mikoa ni matengenezo ya kawaida **kilometa 23,985.72,** matengenezo ya muda maalum **kilometa 2,166.46** matengenezo ya sehemu korofi **kilometa 287.83** pamoja na matengenezo ya madaraja **2,011.** Kwa ujumla, mpango wa matengenezo katika Barabara Kuu na za Mikoa ulikuwa umekamilika kwa asilimia **69.**

38. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara ilipanga kuendelea na udhibiti wa uzito wa magari na eneo la hifadhi ya barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 jumla ya magari **8,110,211** yalikuwa yamepimwa katika mizani **77** iliyopo nchini ambapo kati ya hayo, magari **21,124** sawa na asilimia **0.26** yalikuwa yamezidisha uzito zaidi ya asilimia 5 ya uzito unaoruhusiwa kisheria. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.702** zilikusanywa kutokana na tozo ya uharibifu wa barabara. Wizara imefanikiwa kudhibiti uzito wa magari unaoruhusiwa kisheria kutoka asilimia 0.48 kwa mwaka 2022/2023 hadi asilimia 0.26 kwa mwaka (2023/24). Aidha, vibali **46,437** vya kusafirisha mizigo isiyokuwa ya kawaida (Abnormal Load Permits) vilitolewa na jumla ya **Shilingi**

**bilioni 15.579** zilikusanywa kutokana na tozo ya vibali hivyo vya usafirishaji wa mizigo isiyokuwa ya kawaida.

**Utekelezaji wa Miradi kwa Utaratibu wa EPC+F**

40. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imepanga kutekeleza miradi 7 ya ujenzi wa barabara zenye jumla ya urefu wa kilometa 2,035 kwa utaratibu wa *Engineering, Procurement, Construction and Finance (EPC+F)*. Miradi hiyo ni Mafinga - Mtwango – Mgololo (km 81), Igawa - Songwe – Tunduma (km 218) pamoja na barabara ya mchepuo ya Uyole – Songwe (km 48.9), Masasi – Nachingwea - Liwale (km 175), Arusha – Kibaya – Kongwa Jct (km 453.42), Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo – Lumecha/Songea (km 435), Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (Simiyu) (km 339) na Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboroti – Mrijochini - Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 374.24).

Serikali inaendelea na mazungumzo na wafadhili ili kupata fedha za utekelezaji wa miradi hiyo.. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa dhamira ya Serikali ya kutekeleza miradi hii ya EPC+F bado ipo palepale.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** muhtasari wa utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja kwa mwaka 2023/24 hadi kufikia Aprili, 2024 ni kama ifuatavyo:

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Barabara ya **Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 30)** taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii zinaendelea.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Barabara ya **Mtwara – Newala – Masasi (km 210)**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za **Mnivata – Mitesa (km 100) na Mitesa – Masasi (km 60)** umeanza. Aidha, taratibu za manunuzi za kuwapata Makandarasi wa ujenzi wa barabara za **Mangamba – Madimba - Msimbati (km 35)** na **Namichiga – Ruangwa (km 20.6)** zinaendelea.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa barabara ya **Likuyufusi – Mkenda (km 122.50)**, taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Likuyufusi – Mhukuru (km 60)*** zimekamilika na maandalizi ya kusaini Mkataba na Mkandarasi aliyeshinda zabuni zinaendelea

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11),** Mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii umesainiwa tarehe 7 Februari, 2024 na Mkandarasi yuko katika hatua za maandalizi ya kuanza ujenzi.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24),** unafanyika kwa awamu ambapo ujenzi wa kilometa 4.7 umekamilika na ujenzi wa kilometa 3.6 unaendelea na umefikia asilimia 50. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Pangani – Mapinga (km 13.59)*** kwa kiwango cha lami anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami **barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7)**.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara ya **Musoma – Makojo – Busekela** (km 92), taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya **Musoma – Kusenyi (km 40**) kwa kiwango cha lami zinaendelea.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98)** unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2024, ujenzi wa sehemu ya ***Mpwapwa – Idilo (km 3)*** ulikuwa umekamilika. Aidha, Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya ***Kongwa Jct – Ngambi – Mpwapwa (km 32)*** umesainiwa tarehe 21 Februari, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Vilevile, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 46.9)*** zinaendelea.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54)** kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2024, mradi huu unaendelea ambapo

kilometa 43.55 zimekamilika. Aidha, ujenzi wa sehemu za ***Kamachumu – Lutenge (km 1)*** na ***Nshamba – Mlela (km 3)*** kwa kiwango cha lami unaendelea.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Iringa – Ruaha National Park (km 104**), taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zinaendelea. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya **Iringa (Ipogolo) – Kilolo (km 33.2**) kwa kiwango cha lami anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Muheza – Amani (km 36)** kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2024, ujenzi wa sehemu ya Kwemhosi – Bombani (km 4) unaendelea na umefikia asilimia 91.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ukarabati kwa kiwango cha lami wa **barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200.51),** taratibu za ununuzi wa kuwapata Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za *Mtwara – Mingoyo (km 82.27*) na *Mingoyo – Nanganga – Masasi (km 118.24)* zinaendelea.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara ya **Kibaoni – Majimoto – Muze – Kilyamatundu (km 189),** hadi kufikia Aprili, 2024, ujenzi wa sehemu ya ***Ntendo – Kizungu (km 25)*** kwa kiwango cha lami unaendelea na umefikia asilimia 43. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Kizungu – Muze (km 12)*** na barabara ya ***Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152)***.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Daraja la J.P. Magufuli (Kigongo – Busisi) na barabara Unganishi** unaendelea na umefikia asilimia 88. Ujenzi wa barabara ya ***Kagera Sugar Jct – Kakunyu; Sehemu ya Kagera Sugar Jct – Kitengule Jct (km 25)*** unaendelea. Taratibu za ununuzi wa kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa daraja la **Mzinga (Dar es Salaam)** ikihusisha upanuzi wa barabara ya ***Mbagala Rangi Tatu - Kongowe (km 3.8)*** zinaendelea. Aidha,

Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa daraja la **Ugalla (Katavi)**.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya **Morogoro – Dodoma pamoja na Daraja la Mkundi** ipo katika hatua za mwisho. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya ***SUA Main Gate – Mzinga Factory Gate (km 11)*** kwa kiwango cha lami. Aidha, katika barabara ya ***Njombe – Makete – Isyonje (km 157.4)***, ujenzi wa sehemu ya ***Isyonje – Makete (km 50)*** *sehemu ya* ***Kitulo – Iniho (km 36.3)*** unaendelea na umefikia asilimia 5.9. Vilevile, ujenzi wa sehemu ya ***Njombe – Njombe Referral Hospital (km 3)*** unaendelea kwa awamu.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105),** hadi kufikia Aprili, 2024 taratibu za ununuzi wa kuwapata Makandarasi wa ujenzi sehemu za ***Businde – Murongo (km 53.4)*** na ***Omugakorongo – Businde (km 51.6****)* zinaendelea baada ya kutangazwa upya.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa barabara ya **Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 145)**, hadi kufikia Aprili, 2024 ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Nanganga – Ruangwa (km 53.2)*** unaendelea na umefikia asilimia 77. Aidha, Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya ***Ruangwa – Nachingwea (km 55.7)*** umesainiwa tarehe 5 Februari, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi**.** Kwa sehemu ya ***Nangurukuru – Liwale (km 210),*** taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya ***Choya – Liwale (km 10)*** zinaendelea.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024, katika barabara ya **Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.1),** mkataba wa ujenzi wa sehemu ya ***Isongole II – Ndembo (km 46) na Ndembo Spur Road (km 6)*** umesainiwa tarehe 13 Februari, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Upembuzi – Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Barabara ya ***Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21),*** na ***Chang'ombe – Mkwajuni –***

***Makongolosi (km 61)*** umekamilika ambapo Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya ***Mlowo – Kamsamba*** *sehemu ya km 10* na ujenzi wa ***Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (Iboya OSIS)*** zinaendelea.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024, Upembuzi – Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa **barabara ya Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama (km 54)** umekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa jili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa **barabara ya Sengerema – Nyehunge (km 54),** mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 23 Aprili, 2023 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Hata hivyo, Serikali inaendelea na taratibu za kusitisha mkataba na Mkandarasi huyu kutokana na utendaji kazi usioridhisha. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya ***Kamanga – Katunguru – Sengerema (km 35)*** kwa kiwango cha lami.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara ya **Omurushaka – Nkwenda – Murongo (km 125),** mkataba wa ujenzi wa sehemu ya ***Kyerwa – Chonyonyo (km 50***) umesainiwa tarehe 19 Februari, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Aidha, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa sehemu iliyobaki ya kilometa 75 zinaendelea.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Upanuzi wa barabara Kuu zinazoingia katikati ya Jiji la Dodoma (Widening up of Dodoma Outer Roads Sections km 220),** kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya upanuzi wa barabara hizo zinazoingia katikati ya Jiji la Dodoma (km 220) zinazohusisha barabara za ***Dodoma – Morogoro (km 70), Dodoma – Iringa (km 50), Dodoma – Singida (km 50)*** na ***Dodoma – Arusha (km 50)***

zilikuwa zinaendelea ambapo Wahandisi Washauri wamewasilisha rasimu ya usanifu wa kina. Vilevile, Serikali inaendelea na majadiliano na Benki ya Dunia ili kupata fedha za mkopo wenye masharti nafuu kwa ajili ya upanuzi wa barabara hizi kwa kuanzia sehemu za ndani ya mji wa Dodoma chini ya mradi wa *Dodoma Intergrated and Sustainable Transport project* (DIST).

63. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Jct (km 76.07)** hadi Aprili, 2024 ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Ntyuka Jct – Ntyuka (km 8)*** na ***Kikombo Jct – Mapinduzi (km 16.4)***, unaendelea na umefikia asilimia 49. Aidha, Mkataba wa Ujenzi wa barabara ya ***Ntyuka – Mvumi Hospital - Kikombo (km 53)*** umesainiwa tarehe 13 Machi, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Vilevile, Usanifu wa Kina wa barababa za **Ihumwa – Hombolo (km 60)** na **Barabara ya kuingia Hospitali ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) Msalato (km 5.5**) unaendelea.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa barabara ya **Tarime – Mugumu (km 86)** kwa kiwango cha lami, sehemu ya ***Mogabiri – Nyamongo (km 25)*** unaendelea na umefikia asilimia 49. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu za ***Tarime – Mogabiri (km 9.3), Nyamongo – Mugumu (km 48.15) na Barabara unganishi ya Mugumu Roundabout (km 3.6)*** kwa kiwango cha lami anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Kwa upande wa barabara ya **Mika – Utegi – Shirati – Kirongwe (km 56.8),** taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Utegi – Shirati (km 27)*** zinaendelea.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Shelui – Nzega (km 110)** inaendelea. Aidha, taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Shelui – Sekenke – Tulya – Tyegelo (km 61.1); sehemu ya Shelui – Sekenke – Ntwike (km 20)*** zinaendelea.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Nzega – Kagongwa (km 65),** kazi za ujenzi wa sehemu ya Kagongwa – Sojo (km 18) kwa kiwango cha changarawe zinaendelea na zimefikia asilimia 90. Mhandisi Mshauri amewasilisha makisio ya gharama za kukamilisha kazi ya matabaka ya lami yaliyosalia ili kukamilisha ujenzi wa sehemu hii kwa kiwango cha lami. Aidha, taratibu za manunuzi ya Mkandarasi wa ujenzi wa Barabara ya **Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 50);** sehemu ya ***Isabdula – Bukwimba Station (km 10)*** kwa kiwango cha lami zinaendelea. Vilevile, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (km 136);** sehemu ya km 3 kutoka Mwanangwa unaendelea na umefikia asilimia 5.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya **Nyololo – Mtwango (km 40.4)** umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Singida – Sepuka – Ndago (km 75.0**), Mkataba wa ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umesainiwa tarehe 7 Agosti, 2023 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Kitai – Lituhi (km 90.0) pamoja na daraja la Mnywamaji,** ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Amanimakoro – Ruanda (km 35)*** unaendelea na umefikia asilimia 26. Aidha, Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya ***Ruanda – Ndumbi Port (km 50)*** kwa kiwango cha lami umesainiwa tarehe 13 Machi, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **barabara za Kuelekea Katika Vituo vya Reli ya Kisasa ya SGR (km 87.6),** taratibu za kusaini Mikataba na Mkandarasi wa ujenzi wa barabara za Morogoro – Kihonda SGR Station (km 10) na Rudewa – Kilosa SGR Station (km 3) zinaendelea. Aidha, ujenzi wa barabara ya Kizota – Zuzu SGR Station (km 14) unaendelea na umefikia asilimia 15. Taratibu za manunuzi katika barabara za Gulwe – Gulwe SGR

Station (km 2), Igandu – Igandu SGR Station (km 27), Ihumwa – Ihumwa Marshalling Yard (km 5.50), Bahi – Bahi SGR Station (km 4) na barabara za ndani za kituo cha SGR cha Dodoma (Access Roads to Dodoma SGR Station) zinaendelea. Katika barabara ya Mlandizi – Ruvu SGR Station (km 22) taratibu za kusaini Mkataba na Mkandarasi zinaendelea.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Tanga – Pangani – Makurunge (km 174.5),** ujenzi wa sehemu ya ***Tanga – Pangani (km 50)*** unaendelea na umefikia asilimia 75. Ujenzi wa sehemu ya ***Pangani – Mkange (km 124.5)*** sehemu ya Tungamaa – Mkange (km 95.2) umefikia asilimia 33 na ujenzi wa ***daraja la Pangani*** umefikia asilimia 25. Aidha, taratibu za manunuzi ya Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya **Mkata – Kwa Msisi (km 36)** zinaendelea.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Kisarawe – Maneromango – Mloka (km 150.46)** sehemu ya ***Kisarawe - Maneromango (km 54)*** kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2024 kilometa 24.25 sehemu ya ***Kisarawe – Sungwi*** zimekamilika na ujenzi wa mita 200 za sehemu ya ***Sungwi – Kisanga (km 3.4)*** umekamilika na ujenzi wa sehemu iliyobaki (km 3.125) unaendelea. Aidha, kwa Sehemu ya ***Sungwi – Masaki (km 2.1)*** taratibu za manunuzi ya Mkandarasi zinaendelea.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 120),** hadi kufikia Aprili, 2024 Mkataba wa ujenzi sehemu ya ***Kahama - Bulyanhulu Jct – Kakola (km 73)*** umesainiwa tarehe 16 Machi, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi. Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya BARRICK. Aidha, taratibu za manunuzi ya kuwapata Makandarasi na Wahandisi Washauri kwa ajili ya ujenzi wa barabara za **Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3), Nyikonga – Kashelo (km 10.5), Kashelo – Ilolangulu (km 15)** na **Ushirombo – Kilimahewa – Nanda (km 15.7)** kwa kiwango cha lami zinaendelea.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Nyamirembe Port – Katoke (km 50)** ujenzi wa km 1.7 kwa kiwango cha lami

unaendelea na umefikia asilimia 25. Kwa sehemu ya ***SIDO – Chato Zonal Hospital (km 5.3***) Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi na ***Chato Ginery – Bwina (km 8.1)*** ujenzi wa km 3 kwa kiwango cha lami umekamilika. Aidha, katika **Barabara ya Geita – Nzera - Nkome (km 54);** sehemu ya ***Sungusila - Nzera – Nkome (km 20.364)*** taratibu za kusaini Mkataba na Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zinaendelea.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 199.51)**, hadi kufikia Aprili, 2024, ujenzi wa barabara ya ***Kijenge – Usa River (Nelson Mandela AIST - km 20)*** umekamilika na kwa barabara ya ***Mianzini – Ngaramtoni (km 18)*** ujenzi kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 44. Aidha, Mkataba na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kazi ya Usanifu wa Kina wa barabara ya ***Tengeru – USA River (km 9.3), Daraja Jipya la Kikafu (m 560)*** pamoja na ***Barabara Unganishi (km 4.06), Barabara za Moshi Mjini (km 8.4)*** umesainiwa tarehe 13 Machi, 2024. Mhandisi Mshauri anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi ya Usanifu wa Kina.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa **barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji,** hadi Aprili, 2024, Mkataba wa ujenzi wa barabara ya ***Bigwa – Matombo – Mvuha – Kisaki (km 78)*** kwa kiwango cha lami umesainiwa tarehe 5 Februari, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya ujenzi. Katika barabara ya ***Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11),*** Mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami umesainiwa tarehe 7 Februari, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya ujenzi.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za ***Ubena Zomozi – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 178);*** *sehemu ya* ***Ngerengere – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 166.4)*** kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea. Vilevile, taratibu za manunuzi ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya ***Chalinze – Utete (km 354.9)*** zinaendelea. Aidha, kazi za matengenezo ya barabara za ***Maneromango – Vikumburu***

***– Mloka (km 100)*** na ***Kibiti – Mloka – Mtemele – Rufiji JNHHP (km 203)*** kwa kiwango cha changarawe zinaendelea.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi za ukarabati (overlay) wa sehemu ya ***Mlandizi – Chalinze (km 44.24)*** zinaendelea. Vilevile, ujenzi wa barabara ya ***Kwa Mathias (Morogoro Road) – Msangani (km 8.3***) kwa kiwango cha lami umekamilika. Ukarabati kwenye ***Barabara ya Msoga – Msolwa (km 10.2) (Chalinze Bypass)*** sehemu ya **km 7** unaendelea na umefikia asilimia 60. Aidha, sehemu ya ***Kibaha – TAMCO (km 4.5)*** maandalizi ya kutafuta Mkandarasi wa upanuzi wa sehemu hii kwa kiwango cha lami yanaendelea.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara ya **Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 118.10),** ukarabati na upanuzi wa sehemu ya ***Tegeta/Kibaoni – DAWASA/Basihaya (km 2.9)*** unatekelezwa kupitia mradi wa ujenzi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Nne (BRT IV). Serikali inaendelea kutafuta fedha za ukarabati na upanuzi wa sehemu ya ***DAWASA/Basihaya – Bagamoyo (km 47).***

80. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika barabara za ***Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel (km 141)*** kwa sehemu za ***Rulenge – Kabanga Nickel (km 32), Kumubuga – Rulenge – Murusagamba (km 75)*** na ***Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba (km 34),*** Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami**.**

81. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 ujenzi wa sehemu ya ***Kazilambwa – Chagu (km 36) na Urambo Roundabout*** kwa kiwango cha lami umekamilika. Aidha, ujenzi wa sehemu ya ***Uvinza – Malagarasi (km 51.1)*** umefikia asilimia 53.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke – Kibena (km 346.43),** Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya ***Ifakara – Mbingu (km 62.5)*** anaendelea na maandalizi ya ujenzi. Vilevile, Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya ***Mbingu – Chita JKT (km 37.5)*** kwa kiwango cha lami umesainiwa tarehe 13 Machi, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Katika Barabara ya

***Njombe (Kibena) – Lupembe – Madeke (km 126); Sehemu ya Kibena – Kidegembye (km 42)*** taratibu za manunuzi ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea**.** Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu ya ***Kihansi – Mlimba – Madeke (km 95.26)*** kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) zinaendelea baada ya kutangazwa upya.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389**), kazi za ujenzi wa sehemu ya ***Mbulu – Garbabi (km 25***) zinaendelea na zimefikia asilimia 28. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya ***Labay – Haydom (km 25)*** anaendelea na maandalizi ya ujenzi. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Mogitu – Haydom (km 68).***

84. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga /Bomang'ombe – Sanya Juu (km 105.16),** sehemu ya ***Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16)*** Mkandarasi wa ujenzi wa ***daraja la Kikafu Juu (m 25)*** na barabara unganishi (m 400) anaendelea na maandalizi ya ujenzi**.** Kwa upande wa barabara ya ***Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8)*** ujenzi unaendelea na jumla ya km 6 sehemu ya ***Kiboroloni - Kiharara*** zimekamilika. Aidha, taratibu za kusaini Mkataba na Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Sanya Juu – Kamwanga (Elerai – Kamwanga: km 44)*** zinaendelea. Taratibu za manunuzi ya Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Tarakea – Holili (km 53); sehemu ya Munga – Kitangara Mrere (km 10)*** zinaendelea. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu ya ***Bomang'ombe – Sanya Juu (km 25).***

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 60.6),** hadi Aprili, 2024 ujenzi wa sehemu za ***Bujesi – Mbambo (km 10) na Kibanja – Tukuyu (km 7)*** zimekamilika. Mikataba kwa ajili ya ujenzi wa sehemu za ***Katumba – Lupaso (km 35.3)*** na ***Mbaka – Kibanja (km 20.7)*** zimesainiwa tarehe 13 Februari, 2024 na Makandarasi wanaendelea na

maandalizi ya ujenzi**.** Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Mbambo – Ipinda (km 19.7)***.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa barabara ya **Dodoma – Manyoni (km 127) na Barabara ya Kuingia Manyoni Mjini (km 4.8)** umekamilika. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa ***Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni).*** Mkataba wa awali wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa ***OSIS*** umesitishwa kutokana na changamoto za kimkataba ambapo utekelezaji wake ulikuwa umefikia asilimia 50. Ujenzi utaendelea baada ya kufikia makubaliano ya stahiki za pande zote mbili.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Tabora – Mambali – Bukene – Itobo (km 114)** unafanyika kwa awamu, ambapo ujenzi wa sehemu ya km 1 kutoka kijiji cha Uduka unaendelea. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa **Barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8)** kwa kiwango cha lami.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Dumila – Kilosa – Mikumi (km 141),** ujenzi wa sehemu ya ***Rudewa–Kilosa (km 24)*** umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 72)*** kwa kiwango cha lami.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107)**, ujenzi wa barabara ya ***Matai – Kasesya (km 50)*** sehemu ya ***Matai – Tatanda (km 25)*** unaendelea na umefikia asilimia 37.6 na Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya ***Tatanda – Kasesya (km 25***) umesainiwa tarehe 26 Machi, 2024. Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya ujenzi.

90. ***Mheshimiwa Spika***, katika mradi wa **Ujenzi wa Madaraja Makubwa** hadi Aprili, 2024, ujenzi wa barabara unganishi katika Daraja la Sibiti (Singida) unaendelea na umefikia asilimia 5. Aidha, ujenzi wa madaraja ya Mbambe (Pwani)

umefikia asilimia 25 na Mbangala (Mtwara) asilimia 66. Vilevile, Makandarasi wa ujenzi wa Madaraja ya Mirumba (Katavi), Mpiji Chini (Dar es Salaam), Simiyu na Sukuma (Mwanza), Kibakwe na Kerema Maziwa (Dodoma) wanaendelea na maandalizi ya ujenzi. Taratibu za manunuzi ya Makandarasi wa ujenzi wa madaraja ya Sanza (Singida), Mkenda na Mitomoni (Ruvuma), Godegode na Nzali (Dodoma), Doma, Chakwale na Nguyami (Morogoro) zinaendelea. Usanifu wa kina wa madaraja ya Malagarasi Chini (Kigoma) na Munguli (Dodoma) unaendelea. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara) na ujenzi wa madaraja ya Mtera Dam (Dodoma), Kinyerezi (Dar es Salaam) na Suguti (Mara).

91. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Kyaka – Bugene – Kasulo** (**km 183.10**)**,** ujenzi wa sehemu ya ***Bugene – Kasulo –Kumunazi & Kyaka – Mutukula (km 124)*** sehemu ya ***Bugene – Burigi Chato National Park (km 60)*** unaendelea na umefikia asilimia 35.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa barabara ya **Isaka – Lusahunga (km 242),** kazi za ukarabati wa sehemu ya ***Lusahunga – Rusumo (km 92)*** zinaendelea na zimefikia asilimia 5. Kwa upande wa ujenzi wa ***Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Nyakanazi,*** mkataba wa awali umesitishwa kutokana na changamoto za kimkataba. Ujenzi utaendelea baada ya ya kufikia makubaliano ya stahiki za pande zote mbili. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Nyakasanza – Kobero (km 58***).

93. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya **Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102)** kwa kiwango cha lami.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa ajili ya miradi ya **Barabara za Mikoa** ni ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa kilometa **545**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa **50** na ujenzi wa madaraja/makalavati **59.** Hadi kufikia Aprili, 2024, kilometa **169.25** za barabara za mikoa zilikuwa zimekarabatiwa kwa kiwango cha

changarawe na kilometa **10.85** zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa madaraja/makalavati **12** uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam**, Ujenzi wa barabara ya ***Goba – Matosa – Temboni (*****km 6)** unaendelea kufanyika kwa awamu ambapo kilometa moja (1) imekamilika na ujenzi wa kilometa tatu (3) unaendelea. Aidha, upanuzi wa barabara ya ***Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry (km 25.1)*** unaendelea kwa km 1.4, ujenzi wa barabara za ***Kipata (m 700), Livingstone (m 350), Msikitini – Sharif Shamba (km 1), Kibamba Shule – Mpiji Magoe (km 9.2);*** *sehemu ya* ***km 1.4, Chanika – Mbande (km 3.8), Mbezi Msakuzi – Makabe Jct (km 8.36); sehemu ya m 500*** *na* ***Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi (km 6.73)*** unaendelea.

96. ***Mheshimiwa Spika***, taratibu za manunuzi ya Makandarasi wa ujenzi wa barabara za ***Mji Mwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 27);*** sehemu ya km 10 na ***Mbezi Victoria – Magoe Mpiji (km 9.55);*** sehemu ya km 6.55 zinaendelea. Aidha, taratibu za manunuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya upanuzi wa ***Barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1)*** zinaendelea.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya **Kolandoto – Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 122*)*** kwa awamu.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa barabara ya **Ndundu – *Somanga* (km 60),** ujenzi wa barabara ya ***Utete – Nyamwage (km 33.7)*** unaendelea na umefikia asilimia 2 na ujenzi wa ***daraja la Mbambe (m 81)*** katika ***barabara ya Ikwiriri – Mkongo (km 95)*** umefikia asilimia 25. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu za ***Kongowe – Malendego (km 160.65)*** na ***Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95)***.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Barabara ya ***Kasulu – Manyovu pamoja na***

***barabara za kuingia Kasulu Mjini (km 68)*** unaendelea na umefikia asilimia 64.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mradi wa **barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2 - km 112.3),** hadi Aprili, 2024 ujenzi wa sehemu ya ***Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3)*** unaendelea na umefikia asilimia 75.53 na ujenzi wa sehemu ya ***Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60)*** umefikia asilimia 60.62.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa ***barabara ya Mzunguko wa Ndani katika Jiji la Dodoma: Bahi R/About – Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu R/About (km 6.3),*** majadiliano na Serikali ya Japan kuhusu kukamilisha mkopo kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii yanaendelea. Aidha, kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa ***Dodoma City Middle Ring Road*** inayoanzia ***Nanenane – Miyuji – Mnadani Sekondari – Mkonze – Ntyuka – Nanenane (km 47.2)*** inaendelea na taarifa ya mwisho ya Usanifu wa Kina itawasilishwa Mwezi Juni, 2024. Vilevile kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya ***Msalato – Mtumba – Chamwino IKULU (km 30)*** unaendelea.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara ya **Kidatu–Ifakara–Lupiro–Malinyi–Londo–Lumecha/ Songea (km 499),** kazi za ujenzi kwa sehemu ya ***Kidatu – Ifakara (km 66.9)*** zinaendelea na zimefikia asilimia 88. Aidha, ujenzi wa barabara za kuelekea ***mashamba ya wakulima wa miwa ya Mbigiri (km 50)*** umefikia asilimia 90. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Chalinze– Magindu – Lukenge– Seregete B – Kabwe Jct – Mkulazi (km 77.50).***

103. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya **Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 365.36)** umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Mpanda Airport – Kasimba Jct (km 3)***. Katika barabara ya ***Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 185)***, hadi Aprili, 2024, kazi za ujenzi wa sehemu ya ***Sanzate –***

***Natta (km 40)*** ujenzi umefikia asilimia 41. Aidha, taratibu za manunuzi ya kuwapata Makandarasi wa ujenzi wa barabara za ***Wasso – Loliondo (km 10)***, ***Mto wa Mbu – Selela (km 20) na Ngaresero – Engaruka (km 39)*** kwa kiwango cha lami yanaendelea. Vilevile, maandalizi ya ujenzi wa barabara ya ***Natta – Mugumu (km 35)*** yanaendelea.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Ibanda – Itungi Port/Kajunjumele – Kiwira Port (km 32),** kazi za ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi ***(OSBP)*** cha ***Kasumulu/Songwe (Tanzania/Malawi Border)*** unaendelea na umefikia asilimia 93. Aidha, ukarabati wa barabara ya ***Ibanda – Itungi Port (km 26) na Kajunjumele (Iponjola) – Kiwira Port (km 6)*** umefikia asilimia 2 na Serikali inaendelea na taratibu za kusitisha mkataba na Mkandarasi kutokana na utendaji usioridhisha.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 803.6),** ujenzi wa barabara ya ***Mpanda – Mishamo – Uvinza; Sehemu ya Vikonge – Uvinza (km 159)*** kazi za ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Vikonge – Luhafwe (km 25)*** zinaendelea na zimefikia asilimia 58.74 na ujenzi wa sehemu ya ***Luhafwe – Mishamo/Bulamata Jct (km 37.35)*** unaendelea na umefikia asilimia 2. Kwa barabara ya ***Kibaoni – Sitalike (km 71)*** sehemu ya ***Kibaoni – Mlele Jct (km 50)*** ujenzi umefikia asilimia 14.73 na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Sitalike – Mlele Jct (km 21)*** zinaendelea. Kwa barabara ya ***Kagwira – Ikola – Karema Port (km 112),*** Mikataba ya ujenzi wa sehemu za ***Kagwira – Kasekese (km 54.14) na Kasekese – Ikola (km 56.91)*** imesainiwa tarehe 24 Januari, 2024 na Makandarasi wanaendelea na maandalizi ya ujenzi. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu za ***Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86) na Lyazumbi – Kabwe (km 65).***

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Nyanguge – Musoma/ Mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 202.25)**, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa Barabara ya ***Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4)***. 107. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Magole – Mziha – Handeni (km 152.8),**

sehemu ya ***Handeni – Kang'ata (km 30),*** taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa sehemu hii kwa kiwango cha lami zinaendelea.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini DSM na Barabara Unganishi,** Usanifu wa Kina wa maboresho ya ***Makutano ya barabara kwenye maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/ Mandela, Fire, Selander (Ali Hassan Mwinyi/ UN Roads JCT), Buguruni na Morocco*** umekamilika, Serikali inaendelea na majadiliano na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) kwa ajili ya ujenzi wa makutano ya barabara kwenye maeneo ya Morocco na Mwenge. Aidha, maboresho ya makutano ya Tabata/ Mandela yamejumuishwa katika mradi wa BRT V. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya maboresho ya makutano yaliyosalia.

109. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 181.8),** ujenzi wa barabara ya ***Mchepuo wa Maswa (km 11*****)** umekamilika. Kwa upande wa **Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (*Sehemu ya Ipole – Rungwa (km 172),*** *ujenzi wa* ***daraja la Msula (m 10) na barabara unganishi m 600*** unaendelea. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25),** Ujenzi wa sehemu ya ***Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5)*** umefikia asilimia 80, ***Mvugwe – Nduta Junction (km 59.35)*** umefikia asilimia 88, ***Kibondo Junction – Kabingo (km 62.5)*** umefikia asilimia 98 *na* ***Nduta Junction – Kibondo (km 25.9)*** umefikia asilimia 65. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Kibondo – Mabamba (km 48)*** unaendelea na umefikia asilimia 15.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya ***Kilindoni – Ras Mkumbi (km 54.4)*** taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi wa Barabara hii kwa kiwango cha lami zinaendelea.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi wa **Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Barabara Unganishi (km 46.3),** Mkataba wa ujenzi wa barabara ya ***Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (Km 41)*** kwa kiwango cha lami umesainiwa tarehe 13 Februari, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya ujenzi.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 215.8)** sehemu ya ***Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7)*** taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya **km 10** zinaendelea. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 112), sehemu ya Muhutwe – Kagoma*** zinaendelea. Vilevile Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Bukoba – Busimbe – Maluku – Kanyangereko – Ngongo (km 19.1)*** unaendelea.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa upanuzi wa barabara ya **Kimara – Kibaha (km 19.2) ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**, umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa **Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (Km 119)** kwa kiwango cha lami.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara ya **Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**, kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za ***Bunju – Kibamba – Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma – Kigamboni (km 61.0)*** na ***Mbezi – Mbezi Mwisho – Kifuru – Banana – Kipara – Kigamboni (km 49.0)*** zinaendelea.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Singida – Shelui (km 110)** unaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa ***Barabara ya Ulemo – Kinampanda – Gumanga (Singida) – Mkalama (km 46)*** kwa kiwango cha lami baada ya

kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara hii kukamilika.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road),** taratibu za manunuzi za kumpata Mkandarasi na Mhandisi mshauri kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa sehemu ya ***Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8)*** zinaendelea.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 535.25),** Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152.0)*** kwa kiwango cha lami. Kuhusu barabara ya ***Morogoro – Iringa (Tumbaku Jct. Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi) (km 158.45)*** taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii ziko kwenye hatua za mwisho.

119. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Same – Mkumbara – Korogwe (km 147.5),** Maandalizi ya kusaini mkataba wa ujenzi wa sehemu ya ***Same – Kisiwani – Mroyo (km 56.83)*** unaendelea. Aidha, Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya ***Ndungu – Mkomazi (km 36)*** umesainiwa tarehe 24 Januari, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya ujenzi (Mobilization). Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ukarabati kwa kiwango cha lami kwa barabara za ***Same – Himo (km 76), Mombo – Lushoto (km 32)*** na ujenzi wa barabara ya ***Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5).***

120. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa barabara ya **Mbeya – Makongolosi (km 267.9),** ujenzi wa sehemu ya ***Noranga – Itigi – Mkiwa (km 56.9)*** *sehemu ya* ***Noranga – Itigi (Mlongoji) km 25*** umefikia asilimia 73, ujenzi wa ***barabara za Itigi Mjini (km 10)*** umefikia asilimia 97, ujenzi wa sehemu ya ***Noranga – Doroto (km 6)*** na ***Itigi – Mkiwa (km 25.6)*** unaendelea na umefikia asilimia 4. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za ***Makongolosi – Rungwa – Noranga (km 356)*** na ***Mbalizi – Makongolosi (km 50)***.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Itoni – Ludewa – Manda (km 211),** hadi kufikia Aprili, 2024, ujenzi wa sehemu ya ***Itoni – Lusitu (km 50)*** kwa kiwango cha zege umefikia asilimia 22.4.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Handeni – Kibirashi – Kibaya – Njoro – Goima - Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 424.24)**, hadi kufikia Aprili, 2024 ujenzi wa sehemu ya ***Handeni – Mafuleta (km 20)*** umefikia asilimia 42 na Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Mafuleta – Kileguru (km 30)*** anaendelea na taratibu za kuwasilisha hati za dhamana ili akabidhiwe eneo la Mradi.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Makambako – Songea na Barabara ya Mzunguko ya Songea (km 295)**, hadi kufikia Aprili, 2024, taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Lutukila – Songea (km 95)*** na ***Mchepuo wa Songea (km 11)*** zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Ramadhani – Ilembula Hospital – Iyayi (km 75)*** na ukarabati wa barabara ya ***Makambako–Lutukila (km 200)*** kwa kiwango cha lami.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi wa barabara ya **Dodoma – Iringa (km 260),** ujenzi kwa kiwango cha lami wa mita 450 za ***Barabara ya Mchepuo wa Iringa (km 7.3)*** na ujenzi wa madaraja madogo 7 umekamilika, taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu iliyobaki ya ***Igumbilo – Tumaini Jct (km 6.85)*** kwa kiwango cha lami zinaendelea. Aidha, kazi za uimarishaji wa matabaka ya barabara katika barabara ya ***Iringa – Dodoma (km 264)*** zinaendelea kwa awamu ambapo hadi Aprili, 2024 jumla ya km 21.3 zimekamilika na uimarishaji wa sehemu ya km 4 zinaendelea. Vilevile, taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya ***Iringa – Pawaga (km 71.93);*** sehemu ya ***Pawaga Jct – Ikonongo (km 5) na Itundu – Ilolo Mpya (km 20)*** kwa kiwango cha lami zinaendelea.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa barabara ya **Dodoma – Babati (km 263.4)** umekamilika. Aidha, Mkataba wa

ujenzi wa barabara ya ***Dareda – Dongobesh (km 60)*** sehemu ya ***Dareda Mjini – Dareda Mission (km 8)*** umesainiwa tarehe 6 Aprili, 2024 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Vilevile, ujenzi wa barabara ya ***Miteremko ya Magara (Magara Escarpment - km 15)*** kwa kiwango cha zege unaendelea, hadi Aprili, 2024 jumla ya **km 4** zimekamilika na ujenzi wa sehemu ya **km 3** unaendelea. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Mchepuo wa Babati (km 27.5)***.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa barabara za **Chuo cha Uongozi (Uongozi Institute (km 8.8),** Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Barabara za Igawa – Songwe – Tunduma na Mchepuo wa Mbeya (km 266.9),** hadi kufikia Aprili, 2024, upanuzi wa sehemu ya ***Uyole – Ifisi – Songwe Airport (km 36)*** unaendelea na umefikia asilimia 14. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Iwambi – Mbalizi Bypass (km 6.5)*** kwa kiwango cha lami.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi wa **Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili hadi Tano (km 69.8),** kazi za ujenzi wa barabara ya ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili*** (CBD – Mbagala, km 20.3) zimefikia asilimia 98 na ujenzi wa miundombinu ya ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu*** (CBD – Gongolamboto km 23.33) zimefikia asilimia 45. Makandarasi wa ujenzi wa Barabara za ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Nne (Ali Hassan Mwinyi – Morocco – Mwenge - Ubungo (km 13.5)***, ***Mwenge – Tegeta/Basihaya (km 15.6)*** *na ujenzi wa* ***Miundombinu ya Majengo*** *ya* ***Mbuyuni, Simu 2000 na Kivukoni*** wanaendelea na maandalizi ya ujenzi.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu maboresho ya miundombinu ya **Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza,** mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi za maboresho. Aidha, taratibu za manunuzi za kuwapata makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ***Daraja la Jangwani (m 390)***

***pamoja na barabara unganishi (m 710)*** na barabara za ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano,*** unaohusisha ujenzi wa barabara ya Nelson Mandela kuanzia ***Ubungo hadi daraja la Mwalimu Nyerere*** pamoja na barabara ya Tabata kutoka Segerea kupitia Tabata Dampo hadi Mzunguko wa Kigogo katika barabara ya ***Kawawa (km 27.6)*** zinaendelea.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 katika mradi wa **Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT),** ujenzi wa jengo jipya la Taaluma na Utawala ICoT Morogoro unaendelea na umefikia asilimia 11. Aidha, **Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS),** umefikia asilimia 61. TANROADS imeajiri Mkandarasi mwingine kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizosalia ambazo zinatarajiwa kukamilika Aprili, 2025. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

131. ***Mheshimiwa Spika***, fedha za Mfuko wa Barabara zinatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara nchini. Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2023/24 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara katika Barabara Kuu ni pamoja na kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa kilometa **7,284.74** za barabara.

Hadi Aprili, 2024 Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa miradi **26** yenye jumla ya **km 1,523.43** umekamilika na miradi mingine **67** ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ambapo miradi **29** yenye jumla ya **km 1,772.18** ipo katika hatua ya Usanifu wa Kina, na miradi **38** yenye jumla ya **km 3,989.13** ipo katika hatua ya manunuzi kama ifuatavyo:-

***a.* Miradi ambayo Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina umekamilika:**

*i. Barabara ya Masonga – Kirongwe (TZ/Kenya Mpakani) (km 48.73);*

ii. *Barabara ya Kibaoni - Majimoto - Inyonga (km 152 );*

iii. *Barabara ya Mbalizi - Mkwajuni (Sehemu ya Galula – Mkwajuni – Makongolosi, km 61);*

iv. *Barabara ya Kagwira - Ikola – Karema (km 112);*

v. *Barabara ya Mkalama - Gumanga - Nduguti - Iguguno Shamba (km 89);*

vi. *Barabara ya Nanenane - Miyuji - Mnadani Sekondari - Ntyuka Jct – Nanenane (km 47.2);*

vii. *Barabara za Maingilio za TISS (km 3.5);*

viii. *Barabara ya Singida Urban - Ilongero - Haydom (km 93);*

ix. *Barabara ya Mbamba Bay - Lituhi (km 113);*

x. *Barabara ya Babati (Dareda) – Dongobesh (km 60);*

xi. *Barabara ya Omurushaka – Murongo (km 125);*

xii. *Barabara ya Mwanza – Nyanguge (km 25); xiii. Daraja la Bujonde – Mbeya;*

xiii. *Madaraja ya Chakwale (m 100), Nguyami (m 75) na Mjonga (m 60) - Morogoro;*

xiv. *Barabara ya Utete – Nyamwage (km 34);*

xv. *Barabara ya Nangurukuru – Liwale (km 210);*

xvi. *Barabara ya mzunguko wa mji wa Singida (km 46) ;*

xvii. *Barabara ya Magu – Bukwimba – Ngudu – Hungumalwa (km 64);*

xviii. *Barabara ya Airport – Igombe – Nyanguge (km 46);*

xix. *Barabara ya Old Bagamoyo (km 43.7);*

xx. *Barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 65);*

xxi. *Barabara ya Nyakato – VETA – Buswelu (km 3);*

xxii. *Barabara ya Mkuyuni – Nyakato (km 10);*

xxiii. *Barabara ya Ndulamo - Nkenja – Kitulo (km 42);*

xxiv. *Barabara ya Ushirombo – Nyikonga – Geita (Katoro) (km 59); na*

xxv. *Barabara za Makabe Junction/Mbezi Mwisho, Goba Jct – Msakuzi na Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi (km 15).*

***b.* Miradi ambayo Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina unaendelea:**

i. *Barabara ya Ulemo – Kinampanda – Gumanga – Mkalama (km 49);*

ii. *Barabara ya Mpwapwa – Gulwe – Rudi – Chipogoro ; Sehemu ya Kibakwe – Chipogoro (km 75.84);*

iii. *Barabara ya Simanjiro (Orkesumet) – KIA – Mererani (Sehemu ya Kongwa Ranch – Kiteto – Simanjiro – KIA (km 60);*

iv. *Barabara ya Morogoro (Msamvu Roundabout) – Morogoro Centre – Bigwa Junction (km 10);*

v. *Mteremko wa Mlima Kitonga (km 10);*

vi. *Upanuzi wa Barabara ya Arusha – Kisongo (km 8.8);*

vii. *Madaraja ya Kyabakoba na Kamashango na Barabara unganishi katika barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba;*

viii. *Barabara ya Kimotorok – Sukuro – Terati/Rotiana (km 128);*

ix. *Barabara ya Old Korogwe – Kwamndolwa – Magoma – Mabokweni (km 127.4);*

x. *Barabara ya Tengeru – Mererani (km 28);*

xi. *Barabara ya Geita - Nzera - Nkome Port (km 58.3);*

xii. *Barabara ya Bungu – Nyamisati (km 40.2);*

xiii. *Barabara ya Kuruya – Kinesi Junction (km 18.42);*

xiv. *Barabara ya Nyankanga - Rung'abure (km 91);*

xv. *Barabara ya Geita Town Section (Mtakuja - Buhalahala) iliyo sehemu ya Nyamuhama - Bwanga - Ibanda (km 24);*

xvi. *Barabara ya Mkuranga - Kisiju (km 39);*

xvii. *Barabara ya Kiluvya - Mpuyani (km 19.8);*

xviii. *Barabara ya Mkongo 2 - Ikwiriri (km 24.74);*

xix. *Barabara ya Katumba - Kafwafwa - Kyimo (km 21.98);*

xx. *Barabara ya Mbalizi - Shigamba (km 52);*

xxi. *Barabara ya Ihumwa - Hombolo - Mayamaya (km 55);*

xxii. *Barabara ya Sanya Juu (Nyumba Moja) - Tingatinga - Longido (km 65);*

xxiii. *Barabara ya Katumba Songwe - Kasumulu - Ngana - Ileje (Ndembo) (km 60);*

xxiv. *Barabara ya Ulemo – Kinampanda – Gumanga – Mkalama (km 49);*

xxv. *Barabara ya Ntendo - Muze - Kilyamatundu (km 200);*

xxvi. *Barabara ya Mbulu - Magugu (Mbuyu wa Mjerumani, km 63);*

xxvii. *Barabara ya Puge – Ndala – Ziba – Choma (km 109);*

xxviii. *Barabara ya Nyakahanga - Nyabiyonza – Nyakakika (km 96); na*

xxix. *Barabara ya Ngopito – Kimotorok – Singe (Babati) km 145.*

***c*. Miradi ambayo ipo katika taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina :**

*i.* *Barabara ya Mpanda – Ugalla – Kaliua – Ulyankulu – Kahama (km 457);*

ii. *Barabara ya Morogoro (Tumbaku Roundabout) – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi (km 156.45) na Daraja la Doma;*

iii. *Barabara ya Kibaha - Mlandizi – Chalinze (km 75);*

iv. *Barabara ya Bariadi – Salama - Ng'haya - Magu (km 76);*

v. *Barabara ya Chalinze – Manga ambayo ni sehemu ya Chalinze - Segera (km 93);*

vi. *Barabara ya Katesh – Haydom (km 63);*

vii. *Barabara ya Nyankumbu - Kharumwa - Nyang'holongo - Kahama (km 149);*

viii. *Barabara ya Bariadi - Kisesa - Mwandoya - Ngh'oboko (km 102);*

ix. *Daraja la Sanga;*

x. *Uandaaji wa 'Master Plan' ya Barabara zinazosimamiwa na TANROADS.*

xi. *Barabara ya Chaliigongo (Singida/Dodoma Brd) - Kipanga - Kidiho - Bihawana (km 68);*

xii. *Barabara ya Mandera – Mkange - Saadani (km 63);*

xiii. *Barabara ya Laela - Mwimbi - Kizombwe (km 98);*

xiv. *Barabara ya Kalambanzite - Ilemba (km 26);*

xv. *Barabara ya Ngogo – Mandawa – Chukuani (km 85);*

xvi. *Barabara ya Mtama – Mkwiti – Newala (km 74);*

xvii. *Barabara ya Mwandiga - Chankele - Mwangogo - Kagunga (km 60);*

xviii. *Barabara ya Kisarawe - Bwawa la Mwalimu Nyerere (km 187);*

xix. *Barabara ya Fulo – Nyambiti – Mallya (km 73);*

xx. *Barabara ya Manyoni - Heka - Ikasi – Chaliingongo (Singida/Dodoma Mpakani) (km 124);*

xxi. *Barabara ya Singida (Magereza) - Mtunduru - Iyumbu (km113);*

xxii. *Barabara ya Chimala - Matamba – Kitulo (km 51);*

xxiii. *Barabara ya Nachingwea - Liwale - Ilonga - Mwaya - Mahenge (km 345);*

xxiv. *Barabara ya Mambali – Bukumbi - Ishilimulwa – Shitage – Kahama (km105);*

xxv. *Barabara ya Simbo - Ilagala – Kyala (234km);*

xxvi. *Barabara ya Ikungi (Singida) - Londoni - Kilimatinde (Solya)(km117.9);*

xxvii. *Barabara ya Longido - Kitumbeine - Oldonyolengai (km 98);*

xxviii. *Barabara ya Makutano (Zerozero) - Sirari (km 83) na Barabara unganishi ya Tarime (km 5.4);*

xxix. *Barabara ya Gairo – Nongwe (km 55.54);*

xxx. *Barabara ya Miyombo - Lumuma – Kidete (km 71);*

xxxi. *Barabara ya Usagara – Kigongo na Busisi – Sengerema (km 56);*

xxxii. *Barabara ya Busisi – Nyang'wale (km 55);*

xxxiii. *Barabara ya Mabokweni – Maramba – Bombo Mtoni – Umba - Same (km 278): Sehemu ya Bombomtoni – Umba Junction (km 46.33);*

xxxiv. *Barabara ya Mabokweni – Maramba – Bombo Mtoni – Umba - Same (km 278): Sehemu ya Umba Junction - Mkomazi (km 82.24);*

xxxv. *Barabara ya Katoma - Kanyigo - Bukwali (km 38.83);*

xxxvi. *Barabara ya Newala - Makong'onda - Mbuyuni (km 42);*

xxxvii. *Barabara ya Maneromango - Vikumburu - Mloka - Mtemela Gate (km105); na*

xxxviii. *Barabara ya Inyonga – Ilunda – Kishelo Kitunda (km 163).*

132. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, kazi ya kuimarisha uwezo wa maabara ya vifaa vya ujenzi na mafunzo mbalimbali kwa ajili ya utumiaji wa Mwongozo wa uchanganyaji wa lami zinaendelea kupitia mradi wa ***Kuimarisha Uwezo wa Kitengo cha Utafiti (Research Development Unit - RDU) Katika Kupima Vifaa vya Ujenzi na Kuanzisha Teknolojia ya Kisasa ya (Asphalt Mix Design).***

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

133. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi ya ***ujenzi na ukarabati wa maegesho ya vivuko*** katika mwaka wa fedha 2023/24, kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ni kama ifuatavyo: Hadi Aprili, 2024, miradi iliyokamilika ni ujenzi wa maegesho ya Bugolora – Ukara na Iramba – Majita (Upande wa Majita), ujenzi wa miundombinu ya kivuko cha Chato na Musoma – Kinesi (eneo la Mwigobero), usimikaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mapato (Point of Sale – PoS Management System) katika vivuko vyote umefungwa na unafanya kazi. Kazi nyingine ni kukamilisha usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa kukatia tiketi (N-Cards System) katika kituo cha Magogoni – Kigamboni na maboresho ya mfumo wa kielektroniki wa kukatisha tiketi katika kituo cha Kigongo – Busisi.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi inayoendelea ni upanuzi wa eneo la maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni awamu ya pili ambapo zoezi la uthamini kwa ajili ya kulipa fidia kwa watakaopisha mradi limekamilika, kinachosubiriwa ni ulipaji fidia. Usimikaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mafuta unaendelea katika vivuko 19 vya MV Kazi, MV Kigamboni, MV Kilindoni, MV Misungwi, MV Sengerema, MV Mwanza, MV Sabasaba, MV Ilemela, MV Mara, MV Chato II,

MV Tegemeo, MV TEMESA, MV Kome II, MV Musoma, MV Ujenzi, MV Tanga, MV Pangani II, MV Kilambo na MV Mafanikio.

Aidha, ujenzi wa maegesho ya Mayenzi – Kanyinya (Ngara) umefikia asilimia 80, Ijinga - Kahangala (Magu) umefikia asilimia 48, Zumacheli (Chato – Nkome) umefikia asilimia 95, Mlimba – Malinyi upande wa Mlimba umefikia asilimia 40 na upande wa Malinyi umefikia asilimia 85 pamoja na maegesho ya Bwiro – Bukondo (Ukerewe). Kazi nyingine zinazoendelea ni ujenzi wa maegesho katika kituo cha Mwaya – Kajunjumele (Itungi Port) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95. Hata hivyo, utekelezaji umesimama kutokana na changamoto ya ongezeko la kina cha maji. Mapitio ya usanifu yamefanyika na hivyo ujenzi utaendelea baada ya taratibu za marekebisho ya Mkataba kukamilika. Aidha, mikataba ya ujenzi wa maegesho ya Kisorya – Rugezi, Kahunda – Maisome na Ilunda - Luchelele imesainiwa na ipo katika hatua za awali za kuanza utekelezaji.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zinazoendelea ni Upembuzi Yakinifu na Usanifu katika miradi ya ujenzi wa maegesho ya vituo vya Utete – Mkongo, Kasharu – Buganguzi na Muleba – Ikuza. Vilevile, ujenzi wa maegesho ya Nyakaliro – Kome, Buyagu – Mbalika, Bezi - Bukimwi pamoja na Iramba – Majita upande wa Iramba upo katika hatua za manunuzi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa maegesho ya Rusumo - Nyakiziba na Ilagala – Kajeje pamoja na miundombinu ya kivuko cha Muleba - Ikuza.

136. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu miradi ya ***ununuzi/ujenzi wa vivuko,*** hadi Aprili, 2024, ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Kisorya - Rugezi (Ukerewe) umefikia asilimia 81. Miradi mingine ni ujenzi wa vivuko vya Ijinga – Kahangala (Magu) asilimia 84; Bwiro – Bukondo (Ukerewe) asilimia 85; Nyakarilo – Kome (Buchosa) asilimia 60 na Buyagu – Mbalika (Sengerema) asilimia 45. Aidha, ujenzi wa kivuko kipya cha pili kitakachotoa huduma kati ya Nyamisati – Mafia (Pwani) umefikia asilimia 10 na ujenzi wa vivuko viwili vidogo (Sea Tax Ferries) katika kituo cha Magogoni – Kigamboni upo katika hatua za awali za utekelezaji.

Vilevile, ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma upo katika hatua ya manunuzi.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miradi ya ***Ukarabati wa Vivuko***, hadi Aprili, 2024, ukarabati mkubwa wa vivuko vya MV Ujenzi, MV Mara, MV Misungwi, MV Kyanyabasa, MV Tanga na MV Kitunda umekamilika. Aidha, ukarabati mkubwa wa kivuko MV Nyerere umefikia asilimia 81, MV Kilombero II ambacho kitahamishiwa Mlimba – Malinyi umefikia asilimia 79, MV Magogoni umefikia asilimia 55.2 na MV Ukara I umefikia asilimia 10. Vilevile, Ukarabati mkubwa wa kivuko MV Malagarasi, MV Ukara II, MV Sabasaba, MV Pangani II na MV Mafanikio upo katika hatua ya manunuzi. Ukarabati wa kivuko MV Kome II unasubiri upatikanaji wa kivuko mbadala na ukarabati wa kivuko MV Mwanza na MV Kigamboni bado haujaanza.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

138. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali.

139. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2024, Awamu ya I ya ujenzi wa nyumba 150 za watumishi jijini Dodoma imekamilika na utekelezaji wa Awamu ya II umefikia asilimia 15. Ujenzi wa Ghorofa za Watumishi wa Umma katika eneo la Magomeni Kota Awamu ya II "Block B" umefikia asilimia 96. Aidha, ujenzi wa Ghorofa za Watumishi wa Umma za Temeke Kota Jijini Dar es Salaam umefikia asilimia 33 na Ghana kota "Block II", Jijini Mwanza umefikia asilimia 7. Vilevile, ujenzi wa jengo la Ofisi za Wizara za Ujenzi na Uchukuzi katika Mji wa Serikali - Mtumba jijini Dodoma umefikia asilimia 73.

140. ***Mheshimiwa Spika***, katika mradi wa ukarabati wa nyumba 40 za Viongozi jijini Dodoma uliohusisha nyumba tano (5), utekelezaji unaendelea na hadi Aprili, 2024 nyumba mbili (2) zimekarabatiwa kikamilifu na tatu (3) zinaendelea kukarabatiwa.

Mradi wa ukarabati wa nyumba 30 za Viongozi mikoani, utekelezaji unaendelea na hadi Aprili, 2024 ukarabati wa nyumba moja (1) umekamilika na nyumba tatu (3) unaendelea. Aidha, ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI katika mikoa 20 zilizohamishiwa TBA utekelezaji ulianza kwa nyumba tisa (9) zilizopo mkoani Singida ambapo hadi Aprili, 2024 ukarabati umefikia asilimia 85.

141. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi mwingine unaotekelezwa ni ***Ujenzi na Ukarabati wa Karakana za TEMESA na TBA.*** Hadi Aprili, 2024, Ukarabati wa karakana sita (6) za TBA katika Mikoa ya Arusha, Mwanza, Morogoro, Tabora, Dar es Salaam na Mbeya upo katika hatua za awali.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya karakana za TEMESA iliyokamilika ni ujenzi wa karakana za TEMESA katika Mkoa wa Simiyu Awamu ya I na II pamoja na ukarabati mkubwa wa karakana ya Mbeya Awamu ya I. Aidha, ukarabati mkubwa wa karakana za TEMESA unaendelea katika mikoa ya Tabora, asilimia 85; Mwanza, asilimia 75; Kigoma, asilimia 75; Arusha, asilimia 60; Mara, asilimia 25; na Mtwara asilimia 15. Ukarabati wa karakana ya Ruvuma upo katika hatua za awali za utekelezaji. Vilevile, mikataba kwa ajili ya ukarabati wa karakana za Mkoa wa Pwani na Dodoma imesainiwa. Tathmini ya zabuni ili kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya ukarabati wa karakana za Tanga na Kagera pamoja na Karakana ya Mitambo (Heavy Plant) - Morogoro itakayotumika kama karakana ya Mkoa wa Morogoro inaendelea. Miradi ya ujenzi wa karakana mpya katika mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe, Katavi na karakana mpya ya kisasa jijini Dodoma ipo katika hatua za usanifu. Aidha, ukarabati mkubwa wa karakana ya MT Depot Awamu ya III upo katika hatua ya usanifu.

Mradi wa kusanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Matengenezo ya Magari, Umeme na Elektroniki umekamilika na kwa sasa unaendelea kufanyiwa marekebisho ili kukidhi vigezo vya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

**Udhibiti Uzito wa Magari, Masuala ya Usalama Barabarani na Mazingira**

143. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kuhakikisha kuwa barabara zetu zinakuwa salama kwa watumiaji. Wizara kupitia TANROADS imefunga mizani ya kisasa yenye uwezo wa kupima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (Weighing in Motion System - WIMS). Mizani hii ya kisasa hutumika kubaini magari ambayo hayajazidi uzito unaokubalika kisheria na kuyaruhusu kuendelea na safari na hivyo kupunguza msongamano wa magari katika vituo vya mizani. Hadi kufikia Aprili, 2024, Wizara imefunga mizani mitano (05) ya aina hiyo katika vituo vya mizani vya Mikese (1), Mikumi (2) na Rubana (2) hivyo kufikisha jumla ya mizani 20 inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea na zoezi la kudhibiti uzito wa magari barabarani na hivyo kuzilinda barabara, Wizara kupitia TANROADS imejenga mizani mipya minane (08) ambayo ni Mikumi South (Morogoro), Matundasi (Mbeya), Mdori East (Manyara), Uvinza (Kigoma), Nyantare na Rubana (Mara), Igagala (Njombe) na Mingoyo North (Lindi). Maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Mizani ya Kizengi (Tabora) yanaendelea. Aidha, Mizani ya Mikese North (Morogoro) na Uyole (Mbeya) imeboreshwa kutoka mizani inayopima uzito wa magari kwa ekseli moja na kuwa mizani inayopima uzito wa magari kwa kundi la ekseli.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kupitia TANROADS inaendelea na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mshauri Elekezi atakayefunga mfumo wa Kamera za CCTV na taarifa za vipimo vya uzito wa magari (*CCTV Camera and Data Management System*) katika mizani 56. Hadi sasa mfumo wa aina hiyo umefungwa katika mizani 13 ambao unasaidia utendaji kazi wa uwazi na hivyo kupunguza au kuondoa mianya ya rushwa. Mizani iliyofungwa mfumo huo ni Vigwaza North na South (Pwani), Mikumi, Mikese North na South (Morogoro), Nala (Dodoma), Njuki (Singida), Mpemba (Songwe), Mingoyo (Lindi), Himo 2

(Kilimanjaro), Mutukula (Kagera), Usagara (Mwanza) na Makuyuni (Arusha).

Vile vile, Wizara kupitia TANROADS imefanikiwa kuunganisha mfumo wa upimaji uzito wa magari (T-Load System) na mifumo mingine ya Mamlaka ya Mapato (TRA), Benki Kuu ya Tanzania (BOT) na mfumo wa malipo ya Serikali (GePG) katika mizani ya mfano ya Kimokouwa iliyopo mkoani Arusha ili kurahisisha wasafirishaji kupata moja kwa moja namba za malipo (Control Number) baada ya gari kubainika kuzidi uzito na hivyo kuondoa changamoto kwa wasafirishaji kutumia muda mrefu kwenye vituo vya mizani.

146. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **usalama barabarani,** kazi zilizotekelezwa hadi kufikia Aprili, 2024 ni pamoja na ufuatiliaji utendaji kazi wa vifaa vya kisasa vya upimaji uzito wa magari (Digital Load Cell) katika mizani kumi (10) ambayo ni Mikumi, Mutukula, Himo 2, Mingoyo, *Mikese North*, *Mikese South,* Njuki*,* Nala*,* Makuyuni na Mpemba. Aidha, uthamini kwa ajili ya kulipa fidia ili kupisha ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja cha Iboya (Songwe) umekamilika. Vilevile, Kampuni ya *M/s Ambicon Engineering Limited* inakamilisha maandalizi ya ripoti ya mwisho ya utafiti wa athari zinazotokana na uzidishaji wa uzito wa gari katika barabara.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha usalama barabarani Wizara kupitia TANROADS imeweka alama muhimu za barabarani, michoro ya barabarani, kufunga taa za kuongoza magari katika makutano ya barabara na taa za usalama barabarani katika maeneo ya miji, kupanua makutano ya barabara, kujenga njia na vivuko vya waenda kwa miguu. Hadi kufikia Aprili, 2024 maeneo hatarishi yaliyofanyiwa marekebisho ni pamoja na:-

i. Ujenzi wa barabara ya mchepuo (km 2.8) kwa kiwango cha lami ili kutenganisha malori na magari mengine, ujenzi wa maeneo ya maegesho, kuweka alama zote muhimu, ujenzi wa barabara za dharura/kujiokolea katika eneo la Inyala Mkoani Mbeya;

ii. Upanuzi wa kona tano (05) zenye urefu wa km 1.6 na upana wa mita 5 katika mlima Kitonga ili kupunguza ajali za barabarani, pamoja na kuweka vioo kwenye kona 16 katika mlima huo ambavyo vitasaidia uono mzuri kwa madereva na hivyo kupunguza ajali za barabarani mkoani Iringa.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni kuchapisha Mwongozo wa Ukaguzi wa Usalama wa Barabara (A Guide to Road Safety Audit) na Mwongozo wa Alama za Usalama Barabarani (A Guide to Traffic Signing) na kusambaza kwa Mameneja wote wa mikoa wa TANROADS ili kusaidia uwekaji wa alama na michoro barabarani inayozingatia miongozo hii. Aidha, Wizara kupitia TANROADS imetoa elimu ya usalama barabarani kwa wananchi 633 waliopo katika mitaa na maeneo ya shule za msingi na sekondari zilizopo katika Wilaya ya Temeke, Ilala na Kinondoni na wananchi 522 waliopo katika kata za Nzuguni, Mbalawala, Ihumwa, Nala, Matumbulu, Ng'ong'ona, Makutupora, Mbabala na Zuzu katika Jiji la Dodoma.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **menejimenti ya usimamizi wa mazingira** una lengo la kuelimisha na kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 katika Sekta ya Ujenzi. Hadi kufikia Aprili 2024, Hadidu za Rejea kwa ajili ya kuandaa Mkakati wa Kukabili Majanga kwa Sekta ya Ujenzi (Works Sector Disaster Management Strategy) zimekamilika, Maandalizi kwa ajili ya kufanya mafunzo kwa Wahandisi na Mafundi Sanifu kuhusu kuhimili mabadiliko ya tabianchi yanaendelea. Aidha, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Dubai tarehe 30 Novemba hadi 13 Disemba, 2023 ambapo, mojawapo ya maamuzi muhimu yaliyofikiwa ni kuanza utekelezaji wa majukumu ya Mfuko wa Kufidia Hasara na Uharibifu unaotokana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (Loss and Damage Fund). Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) ilitoa mafunzo ya kukabili madhara ya mvua za Elnino kwa Kamati za Maafa katika mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** katika uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 katika Sekta ya Ujenzi, miradi ya ujenzi wa barabara inafanyiwa tathmini za athari kwa mazingira. Hadi kufikia Aprili, 2024 miradi mitatu (3) imefanyiwa tathmini hiyo na miradi 11 imesajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini za athari kwa mazingira.

**Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Viwanja vya Ndege**

151. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa viwanja vya Ndege vya Geita na Msalato. Aidha, Wizara ilipanga kufanya ukarabati, upanuzi na uboreshaji wa jumla ya viwanja vya Ndege 11 nchini ambavyo ni pamoja na Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Tabora, Songwe, Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Musoma, Songea, Tanga, Lake Manyara, pamoja na ulipaji wa madeni kwa miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege vilivyokamilika vya Mwanza na JNIA.

152. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato,** hadi Aprili, 2024 utekelezaji wa *Package I* unaohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege (runway), barabara ya viungio (taxiway), maegesho ya ndege (apron) pamoja na usimikaji wa taa za usalama na kuongozea ndege umefikia asilimia 56.90. Aidha, utekelezaji wa *Package II* unaohusisha ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, Kituo cha Zimamoto, Kituo cha Hali ya Hewa na vituo vidogo nane (8) vya kufua umeme unaendelea na umefikia asilimia 22.56. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

153. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Kiwanja cha Ndege cha Kigoma,** kazi za ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na miundombinu yake, ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa uzio wa usalama, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa zinaendelea na utekelezaji umefikia

asilimia 3.7. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank - EIB).

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Kiwanja cha Ndege cha Tabora,** kazi za ujenzi wa Jengo la Abiria na miundombinu yake, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa kwa ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya zinaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 45.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi za ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege pamoja na eneo la usalama, usimikaji wa taa za usalama na taa za kuongozea ndege na umaliziaji wa jengo la abiria katika **Kiwanja cha Ndege cha Songwe** zimekamilika na kwa sasa mradi upo katika kipindi cha uangalizi.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji na ukarabati wa **Viwanja vya Ndege vya Sumbawanga na Shinyanga** unaohusisha kazi za ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege unatekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya. Hadi kufikia Aprili, 2024 utekelezaji wa miradi hii umefikia asilimia 10 na 16 mtawalia.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **kiwanja cha Ndege cha Musoma,** kazi ya upanuzi na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege, maegesho ya ndege, barabara ya kiungio na uzio wa usalama inaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 55.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **kiwanja cha Ndege cha Iringa,** ukarabati na upanuzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, maegesho ya ndege, mitambo na taa za kuongozea ndege, barabara ya kiungio na uzio wa usalama (Awamu ya Kwanza) umefikia asilimia 93. Kwa upande wa **Kiwanja cha Ndege cha Geita,** kazi ya ujenzi wa uzio wa usalama na barabara ya mzunguko, inaendelea na imefikia asilimia 70.

159. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi wote watakaopisha mradi wa ukarabati na upanuzi wa **Viwanja vya Ndege vya Tanga, Lake Manyara na Iringa (Awamu ya II)** na kwa sasa taratibu za manunuzi kwa ajili ya kupata Makandarasi na Washauri Elekezi wa miradi hii zinaendelea.

## C.3 UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA UJENZI

160. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yanayosimamiwa na Wizara hutekelezwa na taasisi zilizo chini ya Wizara zinazojumuisha Wakala tatu (Wakala wa Barabara Tanzania – TANROADS, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania – TEMESA na Wakala wa Majengo Tanzania – TBA); Bodi za Usajili tatu (Bodi ya Usajili wa Wahandisi – ERB, Bodi ya Usajili wa Makandarasi – CRB na Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi - AQRB); Bodi ya Mfuko wa Barabara – RFB; Baraza la Taifa la Ujenzi – NCC na Taasisi ya Mafunzo ya Teknolojia ya Ujenzi – ICoT. Utekelezaji wa taasisi hizo ni kama ifuatavyo:

### Bodi ya Mfuko wa Barabara

161. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Bodi ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **856,794,954,000.00** Kati ya fedha hizo, Shilingi **534,662,653,430** ni kwa ajili ya kugharamia kazi za barabara za Kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) ambazo husimamiwa na Wizara ya Ujenzi. Aidha, kiasi cha Shilingi **254,601,263,538** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia kazi za barabara za Wilaya ambazo husimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mgawanyo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo: Wizara ya Ujenzi Shilingi **59,406,961,492;** TANROADS Shilingi **534,662,653,430;** Ofisi ya Rais – TAMISEMI Shilingi **25,460,126,354,** TARURA Shilingi **229,141,137,184** na Shilingi **8,124,075,539** ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji wa Mfuko wa Barabara.

Hadi Aprili, 2024, Bodi imekusanya jumla ya Shilingi **662,508,672,160** sawa na asilimia **77** ya bajeti ya mwaka.

Mgawanyo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo: Wizara ya Ujenzi Shilingi **45,525,579,919.24;** TANROADS Shilingi **409,730,219,274.68**; Ofisi ya Rais – TAMISEMI Shilingi **20,097,100,765.99,** TARURA Shilingi **180,873,906,892.30** na Shilingi **6,281,865,308.23** kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji wa Mfuko wa Barabara.

162. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi inaendelea kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara kwa kutumia wataalam wa ndani na nje ya taasisi ili kupata thamani halisi ya fedha katika miradi inayotekelezwa. Jumla ya miradi 562 ilifanyiwa ukaguzi kwa kutumia wataalam washauri na miradi 28 kwa kutumia wataalam wa ndani kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi pia imeendelea kutoa elimu ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Kutoa Taarifa ya Hali ya Barabara kwa njia ya redio, runinga, mitandao ya kijamii, maonesho na mikusanyiko mbalimbali ambapo kumekuwa na mwitikio mkubwa wa watumiaji wa barabara kutoa taarifa. Vilevile, Bodi imeendelea kuratibu na kutekeleza zoezi la kuchukua takwimu na taarifa za hali ya barabara (road inventory and condition survey) kwa lengo la kuzitumia katika kuandaa mipango kazi na utekelezaji wa kazi za barabara.

**Wakala wa Majengo Tanzania**

164. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Wakala wa Majengo Tanzania ulipanga kutekeleza majukumu yake yanayohusisha ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali. Miradi hii ilitekelezwa kwa kutumia fedha za Ruzuku ya Serikali pamoja fedha za mapato ya ndani ya Wakala. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kutoa huduma za ushauri kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali, kujenga majengo ya Washitiri mbalimbali; kuuza nyumba zinazojengwa na TBA kwa Watumishi wa Umma; kupangisha nyumba za Serikali kwa Watumishi wa Umma na kupangisha baadhi ya majengo ya Serikali kwa wasio watumishi wa Umma ili kuongeza uwezo wa Wakala kujiendesha.

165. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi iliyotekelezwa kwa kutumia ***fedha za ruzuku*** ni kama inavyoonekana katika **Aya. 140 - 144**.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi inayotekelezwa kwa kutumia ***fedha za ndani za Wakala*** ni pamoja na ujenzi wa jengo la ghorofa kwa watumishi wa Umma eneo la Canadian Village, Dar es Salaam ''Block II" na III ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65, Ujenzi wa ofisi ya TBA Mkoa wa Geita umefikia asilimia 60 na ujenzi wa Ghorofa za Watumishi wa Umma za Ghana Kota ''Block I" jijini Mwanza ambao umefikia asilimia 50. Miradi mingine ni ukarabati wa Majengo mbalimbali nchini ambao unaendelea katika mikoa ya Dar es salaam, Dodoma, Arusha na Kagera, utekelezaji wake umefikia asilimia 15.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umetekeleza miradi 119 ya ***Washitiri***. Miradi hiyo ni pamoja na miradi 07 ya Buni Jenga (Design and Build) ambayo ni; ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Bariadi awamu ya II ambao umekamilika asilimia 100, Ujenzi wa jengo la ofisi ya kanda ya Sekretarieti ya Maadili ya Umma jijini Dodoma umefikia asilimia 95, Ujenzi wa jengo la ofisi ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi Mkoani Simiyu umefikia asilimia 97, Ujenzi wa nyumba ya Makazi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita umefikia asilimia 80 na Ujenzi wa wodi na jengo la Mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Burigi Chato awamu ya II umefikia asilimia 89.2.

***Mheshimiwa Spika,*** Wakala umeendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika ***Mji wa Serikali*** eneo la Mtumba Dodoma ikiwemo ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora awamu ya pili ambao umefikia asilimia 98. Wakala pia umeendelea kutoa huduma ya ushauri katika miradi ya ujenzi wa majengo ya Wizara 13 na Taasisi nne (4) ambapo utekelezaji wa miradi hii upo katika hatua mbalimbali.

168. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakala umetekeleza miradi 66 ya ***Ushauri (Consultancy***). Miradi hiyo ni pamoja na Ukarabati wa Kituo cha mafuta GPSA mkoani Katavi na Ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Kwimba, Mkoani Mwanza ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ujenzi wa uzio wa Ikulu ndogo

Arusha ambao umefikia asilimia 90, Ujenzi wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliyoko Sanawari, jijini Arusha ambao umefikia asilimia 25, Ujenzi wa mahakama ya Mwanzo iliyopo Kabanga, Ngara ambao umefikia asilimia 92 na Ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Moshi iliyopo Msaranga Kilimanjaro ambao umefikia asilimia 30.

169. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala vilevile umetekeleza miradi 27 ya ***Ujenzi na Ukarabati***. Miradi ya ujenzi na ukarabati iliyotekelezwa inajumuisha: Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Arusha ambao umefikia asilimia 96, ukarabati wa majengo kumi na tano katika Taasisi ya Mafunzo ya Kilimo ya Maruku, Kagera ambao umefikia asilimia 97 na ujenzi wa Jengo la uchunguzi na mionzi katika Hospitali ya Magonjwa ambukizi Kibong'oto mkoani Kilimanjaro Awamu I ambao umefikia asilimia 87 na awamu ya pili umefikia asilimia 50.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia ulitekeleza miradi miwili (2) ya ***Usimamizi (Project Management).*** Mradi wa kwanza ni kusimamia Mifumo ya joto, hewa na viyoyozi; Mifumo ya umeme; Mifumo ya vitambua moto na vitoa sauti; Mifumo ya majisafi na majitaka; Mitambo ya kangavuke (generators) na transfoma pamoja na usimamizi wa samani katika Ukumbi wa Bunge Dodoma. Vilevile, TBA ilitekeleza mradi wa usimamizi wa ujenzi wa majengo ya Kituo cha Pamoja cha Forodha Mipakani cha Kasumulu ambao umefikia asilimia 93.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, Wakala umeendelea kukabiliwa na changamoto ya malimbikizo ya madai ya kodi ya pango kwa wadaiwa sugu kwa Taasisi na Viongozi wa Serikali.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) uliingia na deni lenye jumla ya Shilingi 14,349,183,478.64. Aidha, katika mwaka huo wa fedha, Wakala ulipanga kukusanya kodi ya pango kiasi cha Shilingi 8,452,097,946.40. Kutokana na jitihada kubwa zilizofanywa na Wizara kupitia TBA, katika kipindi tajwa, Wakala umefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi 9,698,004,629.38. Kati ya hizo, Shilingi

5,394,956,136.00 ni kodi ya pango na Shilingi 4,303,048,493.38 malimbikizo ya deni.

Wakala unaendelea na jitihada za kufuatilia ulipaji wa madeni hayo kwa kutumia Dalali wa Mahakama ili fedha hizo zitumike kukarabati nyumba zilizopo na kujenga nyumba mpya ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kudhibiti ulimbikizaji wa kodi za pango, TBA imeanza na kutumia vitasa janja (smartlocks) na kufunga mfumo wa kisasa wa PAYLESS uliounganishwa na mfumo wa GRMS (Government Real Estate Managenent System) katika majengo mapya. Mfumo huo unakusanya kodi ya pango kupitia ankara za umeme na maji na kwa kuanzia, Mfumo huu umefungwa jengo jipya lililopo Magomeni Kota. Kupitia Mfumo huu, endapo mpangaji hatolipa kodi ya pango atakosa huduma ya umeme na maji, hivyo huduma hizo zitarejeshwa pindi atakapolipa kodi anayodaiwa. Baada ya kujiridhisha na utendaji wake, Mfumo huu utafungwa katika nyumba zote mpya za Serikali zinazopangishwa.

**Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania**

174. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2023/24, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ulipanga kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; kusimika na kufanya matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, majokofu na viyoyozi kwenye majengo ya Serikali na kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba ya Serikali. Kazi nyingine ni kuendesha shughuli za usafiri wa Vivuko vya Serikali zinazohusisha ujenzi na ukarabati wa vivuko, maegesho na miundombinu ya vivuko (majengo na uzio).

175. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024, utekelezaji wa miradi ya ***maegesho ya vivuko***, ***Ukarabati wa Vivuko, Ujenzi wa Vivuko Vipya*** na ***Ujenzi na Ukarabati wa Karakana*** kwa kutumia fedha za ruzuku ni kama inavyooneshwa katika **Aya 135 – 139.**

176. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia ulipanga kutekeleza ***Miradi ya Washitiri na Ushauri*** iliyohusisha kufanya matengenezo ya magari **31,581**, matengenezo na usimikaji wa mifumo **267** ya umeme, **665** ya majokofu na viyoyozi na mifumo 23 ya elektroniki. Aidha, Wakala ulipanga kutoa ushauri wa Kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo **90** ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu na kusimamia mifumo hiyo inayofikia 50. Wakala pia ulipanga kuendelea na usimamizi wa vivuko vya Serikali 33 ambavyo vinatarajiwa kutoa huduma kwa abiria wapatao 42,618,348; magari 1,542,691 na tani za mizigo 557,220 kwa mwaka. Vilevile, Wakala utaendelea na ukodishaji wa mitambo ya ujenzi wa barabara.

177. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024, Wakala umefanya matengenezo ya magari **21,413** umesimika mifumo ya umeme **55**, elektroniki **10,** viyoyozi na majokofu **45**. Aidha, miradi ya usanifu ya umeme, mitambo na electroniki 20 imetekelezwa. Aidha, Wakala unaendelea na usimamizi na uendeshaji wa vivuko vya Serikali 32 pamoja na ukodishaji mitambo.

**Bodi ya Usajili wa Wahandisi**

178. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) iliweka malengo ya kusajili wahandisi 3,136, mafundi sanifu 300, Kampuni za Ushauri wa Kihandisi 21, kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wataalam na wahandisi washauri (CPD), kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu (SEAP) 3,461 pamoja na kukagua shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa wenye kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024, Bodi imesajili wahandisi **1,337** mafundi sanifu **179** na makampuni ya ushauri wa kihandisi **13** na kufikisha jumla ya wahandisi waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali kuwa **37,345** na makampuni ya ushauri wa kihandisi kuwa **357**. Kati ya jumla ya wahandisi waliosajiliwa **34,303** ni wa ndani ya Nchi, na **3,042** ni wageni. Makampuni ya ushauri wa kihandisi ya Nchini ni **241** na ya kigeni ni 116.

Katika kipindi hicho, Bodi ilifuta usajili kwa wahandisi watalaamu **540.** Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya miradi **144** ilikaguliwa. Aidha, Bodi imesajili miradi **691** kati ya miradi **600** iliyojipangia mwaka huu na pia imekagua viwanda na Majengo 177 kati ya 135 iliyojipangia.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi pia iliandaa mafunzo elekezi mawili (2), kwa wahandisi wahitimu, na kwa Mafundi Sanifu. Vilevile, Bodi iliendelea kuwaapisha Wahandisi Wataalam Kiapo cha Utii kwa Taaluma (Professional Oath) ambapo jumla ya wahandisi 4,940 hadi sasa wamekwishaapishwa. Aidha, Bodi iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu 2,731. Jumla ya wahandisi wahitimu 12,186 wameshapitia Mpango huu tangu uanzishwe mwaka 2003.

Bodi vilevile iliandaa na kuadhimisha Siku ya Wahandisi 2023 (Annual Engineers' Day 2023) ambayo ilihudhuriwa na wahandisi zaidi ya 5,463. Mada iliyojadiliwa katika siku ya wahandisi ilikuwa ni "Ushiriki wa Watanzania kwenye miradi ya Kihandisi pamoja na usimamizi wa Ujuzi katika sekta ya Uhandsi, kuipeleka kada ya uhandisi katika viwango vya juu" (Local Content and Skill Management in the Engineering Sector; Taking Engineering Practitioners to the next level).

**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

181. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu makuu ya Bodi hii ni kusajili, kusimamia na kuratibu mwenendo wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi pamoja na Kampuni zao za Ushauri. Aidha, Bodi ina jukumu la kukagua sehemu zinakofanyika shughuli za ujenzi ili kuhakikisha ubunifu na usimamizi wa ujenzi unafanywa na wataalam waliosajiliwa.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, hadi Aprili, 2024 jumla ya wataalamu **135** wamesajiliwa na Bodi, ikiwa ni asilimia 86 ya lengo na kampuni **27** zimesajiliwa ikiwa ni

asilimia 112 ya lengo. Aidha, hadi Aprili, 2024 wahitimu **221** wamepatiwa mafunzo ikiwa ni asilimia 98 ya malengo yaliyopangwa. Vilevile, kufikia Aprili, 2024 miradi ya ujenzi **1,063** ilikuwa imesajiliwa ambayo ni asilimia 76 ya malengo yaliyopangwa.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, miradi ya ujenzi **3,518** imekaguliwa ikiwa ni asilimia 123 ya lengo. Miradi ambayo ilikutwa na kasoro, wataalam au waendelezaji wake walichukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ikiwemo, kutozwa faini au kufunguliwa mashtaka mahakamani.

Bodi pia ilifanikiwa kuendesha mitihani ya kitaalamu kwa wahitimu 87 katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Ubunifu wa Ndani ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Usanifu Teknolojia ya Majengo, Utathmini Majengo, Usimamizi Ujenzi na Usimamizi Miradi ambayo ni asilimia 32 ya lengo. Vilevile, kufikia Aprili 2024 Bodi imefanya mikutano 8 na wanafunzi wa shule za sekondari nchini.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

184. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Bodi ilipanga kusajili jumla ya Makandarasi wapya **1,200** na kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **3,200.** Aidha, Bodi ilipanga kuendesha kozi sita (**6**) za mafunzo katika vituo vitano **(5)** katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Iringa na kuendesha warsha moja **(1)** ya mafunzo ya ushirikiano wa ubia (Joint Venture) katika mkoa wa Mtwara.

Aidha, Bodi ilipanga kuendeleza Mfuko Maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia Makandarasi wa ndani (Contractor's Assistance Fund – CAF) pamoja na kuendelea na jitihada za kuhamasisha Makandarasi wazalendo kujiunga ili kuomba zabuni kwa mfumo wa ubia.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024**,** Bodi imesajili jumla ya Makandarasi **1,573** na kukagua jumla ya miradi **2,878**. Aidha, Bodi imeendesha kozi nne (**4**) za mafunzo katika vituo

vitatu (3) katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Mwanza na iliweza kuendesha warsha moja **(1)** ya mafunzo ya ushirikiano wa ubia (Joint Venture) katika mkoa wa Mtwara. Bodi pia iliendelea kuendesha Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (CAF) unaotoa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa Makandarasi wa Ndani ili kuwawezesha kushiriki katika zabuni na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Mtaji wa Mfuko huu umekua hadi kufikia Shilingi Bilioni **4.12** huku ukiwa na jumla ya wanachama **1,416** mwaka 2023/24. Aidha, Bodi iliweza kutoa dhamana kiasi cha Shilingi bilioni **6.6** ya malipo ya awali kwa makandarasi **113.**

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

186. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Baraza lilipanga kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ujenzi nchini. Hadi kufikia Aprili, 2024 Baraza limekamilisha kazi ya kuandaa mapendekezo ya rasimu ya Sheria ya Majengo (Building Act), kuendelea kuandaa rasimu ya Taratibu za Majengo (Building Codes) na rasimu ya viwango msawazo vya ujenzi wa majengo na samani za Serikali.

Baraza pia limetoa ushauri wa kiufundi na kitaalam kwa wadau wa sekta ya ujenzi ikiwa ni pamoja na NSSF, NHC, TANROADS, PPRA na BOT, kuchapisha taarifa ya utendaji wa Sekta ya Ujenzi pamoja na kuratibu utatuzi wa migogoro 61 iliyotokea katika miradi ya ujenzi.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Baraza limefanya ukaguzi wa kiufundi katika miradi mitano (5) ya TRA na kuendesha kozi tano (5) za mafunzo ya kujenga uwezo wa wadau 187 wa Sekta ya Ujenzi nchini. Kazi nyingine zilizofanyika ni kukusanya na kuchapisha takwimu za mwenendo wa bei za bidhaa na huduma za ujenzi kwa kipindi cha Julai, 2023 – Aprili, 2024, kuanzisha kanzidata ya taarifa za Sekta ya Ujenzi inayowezesha wadau kupata taarifa muhimu za Sekta ya Ujenzi pamoja na kushiriki katika uandaaji mikakati ya kuongeza ushiriki wa wazawa katika kutekeleza miradi ya ujenzi.

**Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)**

188. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo hiki kina jukumu la msingi la kuimarisha/kuboresha Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kutumia mbinu ya ukusanyaji na usambazaji wa teknolojia kwa Wadau kutoka ndani na nje ya nchi. Mkazo mkubwa umewekwa katika matumizi ya tekinolojia mpya katika ujenzi na mtengenezo ya barabara.

189. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Kituo kimeendelea kushirikiana na Kitengo cha Utafiti na Maendeleo *Research Development Unit* (RDU) cha Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kufanya tathmini na ufuatiliaji wa teknolojia mbalimbali mpya na mbadala katika ujenzi na matengenezo ya barabara nje na ndani ya nchi ili kuwezesha Wizara kupata teknolojia stahiki zenye ufanisi na gharama nafuu kwenye utekelezaji wa miradi. Aidha, Kituo kinaendelea na jitihada za kufufua na kuboresha Maktaba Mtandao yake kupitia ICoT ili kuendeleza jukumu lake la kutoa huduma za kusambaza teknolojia kwa njia ya maktaba. Maandalizi ya Hadidu za Rejea (ToR) na mahitaji yatakayomwezesha Mshauri Elekezi kubuni na kuendeleza Mfumo wa Maktaba mtandao (e-library) ya TanT2 na ICoT na Maandalizi ya Andiko (Concept Note) ya kubuni na kuendeleza Mfumo wa Maktaba hiyo yanaendelea. Kituo vilevile kimeshiriki kuandaa na kuhariri Jarida Na. 2 la Shirikisho la Barabara la nchi za Kusini mwa Afrika (ASANRA) ambalo limesambazwa kwa wadau wote wa SADC.

Vilevile, Kituo kilishiriki katika mkutano wa Kamati ya Kujenga Uwezo ya SADC (Regional Technology Transfer and Capacity Building Committee) kwenye masuala yanayohusu usambazaji wa teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji cha ASANRA kilichofanyika kuanzia tarehe 20 – 24 Novemba, 2023 jijini Pretoria, Afrika Kusini pamoja na kuwezesha ushiriki wa Wahandisi watano kutoka Idara ya Barabara kushiriki katika Mkutano wa 32 wa Taifa wa Wahandisi (IET) uliofanyika katika ukumbi wa AICC - Arusha kuanzia tarehe 30 Novemba, 2023 hadi tarehe 2 Desemba, 2023.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kushirikiana na TARA, ERB, CRB, EIT, Wizara ya Madini na National Economic Empowernment Council- NEEC katika kuandaa na kuendesha Semina kuhusu kujenga uwezo wa ushirikishwaji wa wazawa kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Sekta ya Ujenzi hapa nchini iliyofanyika tarehe 30 hadi 31 Januari, 2024 jijini Dar es Salaam pamoja na kuandaa na kuchapisha Nakala 300 za Jarida la Kituo Na. 8 lenye mada mbalimbali zinazohusu teknolojia, usalama barabarani, taarifa za miradi ya kimkakati na agenda za Serikali katika kuimarisha miundombinu ya usafirishaji; na kuratibu shughuli mbalimbali za Shirikisho la Barabara Duniani (PIARC) ili kushiriki kikamilifu katika Kamati za Kiufundi na vikosi kazi kwa mzunguko wa mwaka 2024 – 27.

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi**

191. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT) ina Kampasi mbili; Morogoro na Mbeya. Taasisi ina jukumu la kutoa mafunzo ya muda mrefu katika fani za ujenzi, umeme na mitambo katika ngazi za Astashahada na Stashahada ili kuzalisha wataalam watakaohudumia Sekta ya Ujenzi; kuendesha mafunzo maalum kwa wahitimu wa fani za kihandisi ili kuwajengea uwezo wahitimu pamoja na kuendesha mafunzo ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika kazi za ujenzi na matengenezo na ukarabati wa barabara. Majukumu mengine ni kufanya utafiti wa teknolojia mbalimbali katika Sekta ya Ujenzi, kuandaa, kuchapisha na kusambaza majarida yahusuyo teknolojia hizo, kufanya tathmini ya mafunzo yanayotolewa kulingana na mahitaji ya wakati husika ili kupunguza pengo lililopo katika masuala ya maarifa, ujuzi na teknolojia.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024 Mafunzo ya Stashahada yalitolewa kwa Wanafunzi **21** na kwa Wanafunzi **189** katika ngazi ya Elimu ya Ufundi Stadi VET II. Taasisi ilikamilisha udahili wa jumla ya Wanafunzi wapya **107** waliosajiliwa na

kujiunga na masomo katika ngazi za *NTA level* 4-6 na kudahili wanafunzi wapya wa Elimu ya Ufundi Stadi (VET) 153.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi inaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 209 wa Stashahada katika fani za Uhandisi Umeme, Mitambo na Ujenzi. Kati yao, wanafunzi wa mwaka wa kwanza (NTA level 4) ni 96, mwaka wa pili (NTA level 5) ni 68 na wa mwaka wa tatu (NTA level 6) ni 45. Vilevile, Taasisi inaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 364 wa daraja la I,II na III katika mafunzo ya Elimu ya Ufundi Stadi (VET).

194. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeandaa kozi fupi tatu (3) kwa washiriki 418 katika kozi ya udereva wa awali, udereva wa magari ya abiria na kozi ya maopareta wa mitambo ya Ujenzi. Hatua nyingine iliyofikiwa ni Taasisi kukamilisha utaratibu na kufanikiwa kupata kibali cha kutoa mafunzo ya Elimu ya ufundi Stadi daraja la tatu (VET level III), ambapo hadi sasa kuna wanafunzi 28 wanaoendelea na mafunzo.

195. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Taasisi imeendelea kusimamia kwa karibu ujenzi wa jengo jipya la Utawala na Taaluma, hadi Aprili, 2024 maendeleo ya ujenzi yamefikia asilimia 11.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi pia imetangaza kazi zake kwa njia ya maonesho katika mikutano ya mwaka ya wahandisi iliyoandaliwa na ERB na IET. Vilevile, Taasisi imekamilisha Upatikanaji wa Hati Miliki ya Taasisi katika Makao Makuu ya ICoT yaliyopo Morogoro.

197. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Kampasi ya Mbeya majukumu yafuatayo yalitekelezwa:- Taasisi iliandaa na kutoa Mafunzo ya kozi fupi kuhusu matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara ambapo kozi tatu (3) zimekamilika na jumla ya wahitimu 55 wamepatiwa mafunzo.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi vilevile imefanya uhamasishaji wa matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi

katika Halmashauri za Mikoa ya Mbeya, Njombe na Ruvuma. Aidha, Taasisi inaendelea kufanya matengenezo ya magari na mitambo na imefanikiwa kununua vipuri vya magari na mitambo; Ukarabati wa jengo la darasa na ofisi ya maktaba ambapo hadi sasa umefikia asilimia 80. Aidha, upimaji wa eneo la Taasisi na uwekaji wa alama za mipaka umekamilika ambapo Taasisi imepatiwa Hati Miliki katika Kampasi ya Mbeya.

**D. UHARIBIFU MKUBWA WA MIUNDOMBINU YA BARABARA NA MADARAJA KUTOKANA NA MVUA ZA EL-NINO NA KIMBUNGA HIDAYA**

200. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imeathirika na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yameleta athari za kimazingira katika maeneo mbalimbali dunia nzima. Athari hizo kwa Tanzania zimejidhihirisha kupitia mvua kubwa za El – Nino zilizonyesha kwa takriban miezi tisa (9) mfululizo kuanzia Septemba, 2023. Mvua hizo zimesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara na madaraja nchi nzima.

201. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini iliyofanyika mwezi Aprili, 2024 imeonesha kuwa mahitaji halisi kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu iliyoathirika na mvua za El – Nino ni Shilingi bilioni 986. Hadi Mei, 2024, jumla ya Shilingi bilioni 72 zilitolewa na HAZINA kwa ajili ya kazi za matengenezo ya dharura. Serikali inasubiri taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kuhusu kumalizika kwa msimu wa mvua ili itoe fedha zaidi na kutangaza zabuni za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya maeneo yote yaliyoathiriwa.

202. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, kimbunga cha kitropiki chenye upepo wa kilometa 119 kwa saa kilichojulikana kama **Hidaya** kiliyakumba maeneo ya pwani ya nchi yetu na kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu uliodhihirika katika mikoa ya Lindi, Mtwara, pamoja na kisiwa cha Mafia. Mvua kubwa zilizoambatana na kimbunga hiki, zilisababisha kukatika kwa mawasiliano baina ya mikoa ya Pwani na Lindi eneo la Mikereng’ende, Songas, Somanga na Matandu – Nangurukuru. Maeneo mengine yaliyoathirika kwa kiasi kikubwa ni katika

barabara ya Nangurukuru – Liwale (daraja la Miguruwe, eneo la Zinga na eneo la Mlowoka); Kiranjeranje – Namichiga (daraja la mto Mbwemkuru na daraja la Kigombo) pamoja na Tingi – Kipatimu (eneo la mto Liomanga na eneo la mto Chumo).

Kwa ujumla, uharibifu uliotokea katika barabara ya Mtwara – Lindi – Dar es Salaam ni mkubwa na hivyo barabara yote inatakiwa kujengwa upya. Tayari manunuzi kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa kipande cha barabara ya Mtwara - Mingoyo yapo katika hatua za mwisho. 203. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilichukua hatua za haraka kuhakikisha kuwa mawasiliano katika maeneo hayo yanarejea. Tathmini ya gharama za kurudisha mawasiliano ya barabara yaliyoathirika iliyofanyika ilionesha kuwa, mahitaji halisi kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo ni Shilingi bilioni 84.135. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za dharura ili kurejesha miundombinu iliyoathirika.

## E. MASUALA MTAMBUKA

### Ushiriki wa Wazawa (Local Content) katika Utekelezaji wa Miradi Mikubwa ya Ujenzi

204. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Ujenzi ni mojawapo ya Sekta muhimu zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, wastani wa mchango wa Sekta hiyo katika Pato la Taifa katika kipindi cha miaka kumi (2012 – 2022) ni asilimia 14. Aidha, Sekta hii imekuwa ikikua kwa wastani wa asilimia 12 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita. Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miradi hiyo hutekelezwa na Makandarasi kutoka ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, pamoja na kutengewa kiasi kikubwa cha fedha, uchambuzi wa taarifa za usajili wa miradi ya ujenzi kwa miaka kumi, (2013 – 2023) umebaini ushiriki mdogo wa makandarasi wazawa katika miradi hiyo.

205. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Usajili wa Makandarasi ambayo ina jukumu la kusajili miradi

inayotekelezwa na makandarasi nchini, kati ya jumla ya miradi 36,839, Wazawa walitekeleza miradi 35,351 sawa na asilimia 95.9 ya miradi hiyo. Hata hivyo, miradi iliyotekelezwa na wazawa ni midogomidogo yenye thamani ya Shilingi trilioni 23.749, sawa na asilimia 38.5 ya thamani ya miradi yote iliyosajiliwa na kutekelezwa katika kipindi hicho, ambayo ni Shilingi trilioni 61.638. Hivyo, makandarasi wa nje ambao ni takriban asilimia 4.1 walitekeleza miradi michache yenye thamani kubwa (asilimia 61.5 ya thamani ya miradi yote). Hii inaonesha kuwa asilimia kubwa ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inawanufaisha wageni kutoka nje ya nchi kuliko Wazawa. Sababu kubwa inayochangia hali hii ni uwezo mdogo wa makandarasi wa ndani wa kifedha, mitambo na wataalam hivyo inakuwa vigumu kwao kushindana kwenye zabuni za kazi na Makandarasi kutoka nje hasa Kampuni za Kichina.

206. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni za ndani za Makandarasi ni 14,800, za Ushauri wa Wahandisi ni 252 na Kampuni za Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ni 461. Kwa muda mrefu Makandarasi na Wahandisi washauri wa ndani wamekuwa na kilio cha ushiriki mdogo katika kazi kubwa za ujenzi. Sababu kubwa zinazochangia kuwepo kwa hali hiyo ni uwezo mdogo wa makandarasi hawa wa kifedha, mitambo na wataalam ikilinganishwa na kampuni za nje.

207. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na changamoto hizi za makandarasi wa ndani, Wizara imedhamiria kuwawezesha makandarasi wazawa kushiriki kwenye kazi kubwa za ujenzi katika hatua na taratibu zote kuanzia mipango, usanifu, ununuzi, ujenzi, matengenezo, ukarabati na ubomoaji. Uwezeshaji wa wazawa utaleta manufaa ikiwemo faida inayopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi kubaki nchini na kutumika kukuza biashara za wazawa; kupunguza matumizi ya fedha za kigeni; Kuongeza ajira na ujuzi kwa wataalam wa ndani pamoja na kujenga uwezo wa Kampuni za ndani kuweza kushindana kimataifa.

208. ***Mheshimiwa Spika,*** mnamo tarehe 21 Novemba, 2023 Wizara iliandaa mkutano wa mashauriano na makandarasi pamoja na washauri elekezi wa ndani kutoka mikoa yote

Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo la mkutano huo lilikuwa kupata maoni na ushauri kutoka kwa makandarasi wenyewe kuhusu changamoto walizonazo na utayari wa Serikali kuzitafutia suluhu. Baada ya mkutano huo, niliunda timu ya wataalam ili wachambue changamoto hizo na kuandaa Mkakati wa Kuongeza Ushiriki wa Wazawa katika Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi (Local Content Strategy).

209. ***Mheshimiwa Spika,*** Timu hiyo tayari imekamilisha kazi hiyo na imeandaa mapendekezo ya kufanyiwa kazi ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu. Mapendekezo hayo ni pamoja na:

i. Kurekebisha vipengele kwenye makabrasha ya zabuni ambavyo vina masharti magumu bila sababu za msingi na kufanya wazawa washindwe kuvitimiza wakati wa kuomba zabuni na hivyo kuondolewa kwenye mchakato wa zabuni;

ii. Serikali kuanzisha mpango maalum wa kuwajengea uwezo na kuwaendeleza makandarasi na wataalam wa ndani. Lengo ni kuwawezesha wakue na wawe na uwezo wa kushindana na wa nje na hata kuwa na uwezo wa kuomba kazi nje ya nchi na hivyo kupanua wigo wa ajira kwa watanzania; Aidha, Serikali kupitia Wizara kutenga asilimia kumi (10) ya bajeti ya kila mwaka ya maendeleo kwa ajili ya Miradi ya mafunzo kwa vitendo kwa Makandarasi Wazawa ili kuwajengea uwezo. Katika mafunzo hayo Makandarasi wazawa watapewa elimu ya maandalizi ya zabuni ikiwemo kuandaa bei halisi za kazi husika, tafsiri ya vifungu vya nyaraka za zabuni na mikataba, usimamizi wa rasilimali kama vile fedha, mitambo/vifaa na raslimali watu katika utekelezaji wa miradi;

iii. Sheria ya Manunuzi ya Umma kuboreshwa ili iongeze kiasi cha fedha kwa miradi ya kutekelezwa na wazawa peke yao kutoka kiasi cha Shilingi bilioni 10 cha sasa hadi Shilingi bilioni 50;

iv. Kutenga angalau asilimia 30 ya bajeti ya maendeleo ya upendeleo kwa wazawa (local exclusivity) ambapo Serikali

kupitia Wizara ya Ujenzi itandaa mwongozo wa namna ya kutekeleza miradi ya kujenga uwezo kwa wazawa. Mwongozo huu ni muhimu kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kutenga miradi, namna ya kuitekeleza na masuala ya ufuatiliaji na tathmini;

v. Kutenga angalau asilimia tano (5) ya bajeti ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya makundi maalum kama Wanawake;

vi. Miradi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina na ile ya Usimamizi (Supervision) inayotumia fedha za ndani ya nchi kutekelezwa na makampuni ya Washauri elekezi wa ndani na ile inayotumia fedha za mikopo na misaada itatekelezwa kwa ushirikiano kati Washauri Elekezi wazawa na wale wa nje; na

vii. Kazi za matengenezo ya barabara na madaraja kutekelezwa na Makandarasi Wazawa na kusimamiwa na Washauri Elekezi Wazawa pekee.

210. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 tayari Serikali imetekeleza mapendekezo hayo kwa kufanya yafuatayo:

i. TANROADS kwa kushirikiana na PPRA wanaendelea na taratibu za kuboresha/ kurekebisha vipengele kwenye makabrasha ya zabuni vilivyokuwa vikwazo kwa Wakandarasi wazawa.
   Vipengele vilivyoboreshwa ni pamoja na:

   a) Kupunguza kiwango cha mapato ghafi (Average Annual Turnover);

   b) Kutumiwa kwa Tender/ Bid Securing Declaration badala ya dhamana ya zabuni (Tender/ Bid security);

   c) Kutumia Performance Bonds/Performance Securing Declaration badala ya Dhamana ya Utekelezaji (Performance Bank Guarantee);

d) Kutambua uzoefu wa wataalam badala ya uzoefu wa kampuni kwa ajili ya kazi zinazofanana (specific experience in the similar projects).

ii. Wizara imetenga miradi maalum ya kuwajengea uwezo makandarasi wa ndani na makandarasi Wanawake; na

iii. Wizara ya Fedha imerekebisha Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa kuongeza wigo wa thamani ya miradi ya kutekelezwa na wazawa peke yao. Imependekeza kiwango kipande kutoka Shilingi bilioni 10 za sasa hadi Shilingi bilioni 50.

211. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na kuwajengea uwezo Makandarasi Wazawa, Wizara ina mkakati wa kuwajengea uwezo Makandarasi wanawake kwa kuongeza ushiriki wao katika miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara. Hadi sasa Wizara imetenga jumla ya kilometa 20 za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa ajili ya Makandarasi wanawake pekee. Kazi hizi zitagawanywa katika sehemu za kilometa tano tano ambapo Makandarasi wanawake pekee yao ndio wataomba kazi hizo. Hivi sasa miradi hii ipo kwenye hatua ya ununuzi.

**Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika Miradi ya Ujenzi**

212. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu inapoendelea kukua kiuchumi na kijamii, uhitaji wa miundombinu imara na ya kisasa unaongezeka. Miradi ya ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji ikiwemo barabara na viwanja vya ndege inagharimu fedha nyingi na hivyo kuhitaji uwekezaji mkubwa. Ni dhahiri kuwa, Serikali pekee haitakuwa na uwezo wa kutekeleza miradi hii yote kwa wakati kutokana na ufinyu wa bajeti.

213. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na miundombinu ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege, Wizara ya Ujenzi

inasimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali, vivuko pamoja na karakana za matengenezo ya magari. Hata katika maeneo haya, bado utekelezaji upo chini ikilinganishwa na fursa lukuki za uwekezaji zilizopo katika miradi hii.

214. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuipunguzia Serikali gharama kubwa za utekelezaji wa miradi hiyo sambamba na kupunguza muda mrefu unaotumika katika kutekeleza miradi, kuna haja ya kushirikisha sekta binafsi kwa utaratibu wa PPP. Kwa kutambua mchango wa Sekta Binafsi, Serikali imefanya maboresho makubwa kwenye Sheria ya PPP kwa lengo la kuvutia uwekezaji wenye tija na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu. Maboresho muhimu yaliyofanyika katika sheria hiyo ni pamoja na:

i. Kuruhusu taratibu mbadala za utatuzi wa migogoro, ikiwa ni pamoja na upatanishi na usuluhishi, pamoja na mashauri ya uwekezaji kusikilizwa kwa kutumia mahakama zitakazokubalika baina ya pande zote mbili badala ya mashauri hayo kusikilizwa katika mahakama za ndani;

ii. Kuweka takwa la miradi yote ya PPP kutekelezwa kupitia kampuni maalum ya kusimamia mradi husika, (Special Purpose Vehicle) ambapo ushiriki wa sekta ya umma katika kampuni hiyo hautakiwi kuzidi asilimia 25;

iii. Kutoa nguvu kwa Waziri mwenye dhamana ya PPP kuruhusu miradi (solicited projects) yenye sifa maalum kutopitishwa kwenye mchakato wa ushindani chini ya masharti maalum. Lengo ni kuharakisha utekelezaji wa miradi ya hiyo kwa kutoa nafasi ya kujadiliana moja kwa moja na sekta binafsi bila kupitia taratibu zilizozoeleka za ushindani.

Maboresho haya yatasaidia kuhakikisha kuwa mazingira ya uwekezaji yanakuwa rafiki zaidi, yenye uwazi na yenye ufanisi mkubwa kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa.

215. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya barabara, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Kibaha – Chalinze – Morogoro – Dodoma Expressway yenye urefu wa kilometa 531.8, kwa utaratibu wa PPP kama ifuatavyo:

i. Sehemu ya Kibaha – Chalinze (km 78.9), kazi inayoendelea ni uchambuzi wa *Proposals* (Evaluation of Technical & Financial Proposals) wa Makandarasi/ Wawekezaji waliofaulu Vigezo vya kupatiwa Nyaraka za Zabuni (Request for Proposals) ya kutekeleza mradi huu.

ii. Kwa sehemu ya Chalinze – Morogoro yenye urefu wa kilometa 84.9, Mshauri Elekezi yupo katika hatua za mwisho kukamilisha kazi ya Upembuzi Yakinifu.

iii. Kwa sehemu ya Morogoro – Dodoma (km 260) usanifu wa kina wa kawaida (Conventional Design) uko katika hatua za mwisho kukamilika. Usanifu utatumika kujenga maono (Concept) ya Mradi wa PPP.

Aidha, Serikali inaandaa andiko la ujenzi wa Barabara ya TANZAM kuanzia Morogoro – Iringa – Mbeya hadi Tunduma kwa kuanzia na sehemu ya Igawa – Mbeya hadi Tunduma ambayo kwa kiasi kikubwa itasaidia kupunguza msongamano wa magari katika mpaka wetu na Zambia pale Tunduma na pia msongamano wa magari katika Jiji la Mbeya ili kuijenga kwa utaratibu wa PPP.

216. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine iliyoainishwa na Wizara kwa ajili ya kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP ni:

i. Barabara za Pete Dar es Salaam (Outer Ring Road - km 78.63 na Middle Ring Road - km 53.31);

ii. Daraja la Pili la Kigamboni (Magogoni – Kivukoni); na

iii. Barabara ya Himo – Moshi – Arusha (Tengeru – km 78).

Wizara inawakaribisha wawekezaji wenye nia kushiriki katika utekelezaji wa miradi hii na mingine itakayoibuliwa kwa ajili ya kutekelezwa kwa njia ya ubia.

217. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miradi ya vivuko, kuna fursa mbalimbali katika uendeshaji wa vivuko hususan katika eneo la Kigamboni – Kivukoni. Kwa sasa, Kigamboni ina wakazi zaidi ya 300,000 ambapo wanaotumia usafiri wa vivuko ni wastan wa watu 60,000 kwa siku. Katika kuweza kuhudumia idadi hii kubwa ya watumiaji kwa vivuko, TEMESA inashirikiana na Azam Marine Company Ltd kwenye utoaji wa huduma kivukoni hapo. Aidha, Wizara inaendelea kuangalia utaratibu mzuri wa ushirikiano huo ili kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na tija kwa pande zote mbili. Aidha, Wizara inaendelea kuangalia utaratibu mzuri wa ushirikiano huo ili kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na tija kwa pande zote mbili. Matarajio ya Wizara ni kuwa ifikapo Agosti, 2024 Azam Marine watatoa huduma masaa 24 kwa siku sambamba na TEMESA.

Nitoe wito kwa wawekezaji wengine wenye nia kushirikiana na TEMESA katika utoaji wa huduma za vivuko katika maeneo mengine nchini. Aidha, tunawakaribisha wawekezaji kuingia ubia (Joint Venture) na TEMESA katika matengenezo ya magari na ukodishaji wa mitambo.

218. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya nyumba, TBA ina jumla ya nyumba na majengo 7,116 Tanzania Bara. Licha ya uwepo wa nyumba hizi, bado uhitaji wa nyumba kwa Watumishi wa umma na wananchi wengine ni mkubwa ambapo inakadiriwa mahitaji halisi ni takriban nyumba milioni 3. Ili kuongeza kasi ya uwekezaji katika nyumba, TBA imeweka mikakati mbalimbali ya kuongeza vyanzo vya fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi yake, ikiwa pamoja na kuboresha ushirikiano na sekta binafsi katika uendelezaji wa Milki nchini kama ifuatavyo:

i. Kuhuisha Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kupitia GN 595 ya August 2023. Uhuishwaji huu umeleta mabadiliko kwenye majukumu ya Wakala ikiwemo kuweza kuuza nyumba kwa watu binafsi. Hali hii itaiwezesha

TBA kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuendeleza Milki Nchini na kutafuta vyanzo vya Fedha kama Mikopo kwani miradi yote ambayo itaendelezwa kibiashara itaweza kupangishwa au kuuzwa kwa watu wote kulingana na hali ya soko;

ii. Kuendelea kutekeleza miradi ya uwekezaji wa ujenzi wa makazi na maeneo ya kibiashara kwa utaratibu wa kuingia ubia na wawekezaji binafsi;

iii. Kuendeleza viwanja vitatu (3) vya Wakala jijini Dar es Salaam kwa njia ya ubia na wawekezaji binafsi. Viwanja hivyo ni kiwanja namba 45 na 46 eneo la Chimara na kiwanja namba 266 eneo la Chole Oysterbay;

iv. TBA imehuisha Sera yake ya Ubia ya Mwaka 2006 ili kuendana na Soko la sasa na Mabadiliko. Sera hii mpya inatoa wigo mkubwa kwa Sekta Binafsi kufanya kazi na kushirikiana TBA katika uendelezaji wa milki kuu;

v. TBA imeanza kushirikiana na Taasisi za Kifedha katika kutafuta Mikopo ya Miradi yake mbalimbali ya kibiashara ikiwemo Canadian, Masaki ambapo mabenki mengi nchini yameonesha nia ya kutoa mkopo wa ujenzi lakini pia mkopo kwa wananunzi wa nyumba "Mortgage Financing" katika mfumo wa "Pre – Sale"; na

vi. TBA inatarajia kujenga jumla ya nyumba 1,056 katika Mkoa wa Dar es Salaam (440 Magomeni Kota, Nyumba 408 mradi wa Canadian Village na Nyumba 1008 Temeke Kota). Aidha, Wakala umeshaandaa list ya maeneo yaliyoiva kwa uwekezaji katika mikoa ya Dodoma, Arusha, Mwanza, Kahama na Geita na kuyatangaza kwa umma kwa ajili ya miradi ya ubia.

219. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe wito kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa, taasisi za kifedha, na wadau wa maendeleo kuchangamkia fursa hizi adhimu zilizopo katika sekta

ya ujenzi ili pande zote mbili, yaani Serikali na Wawekezaji Binafsi wafaidike.

**Kujenga Uwezo wa Ndani ya Taasisi Katika Usimamizi wa Miradi**

220. ***Mheshimiwa Spika,*** TANROADS ilisajili Kitengo chake cha ndani cha Ushauri wa Kihandisi (TECU) ili kukabiliana na changamoto ya kutegemea huduma za Usanifu na Usimamizi wa miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja kutoka kwa makampuni ya Kihandisi ya ndani na nje ya nchi. Kitengo hiki kilisajiliwa mwaka 2014 kwa ajili ya kufanya kazi za Usanifu na Usimamizi wa miradi ya barabara na madaraja. Faida za kuwa na Kitengo hiki ni kujenga uwezo wa wataalam wa ndani kusimamia miradi mikubwa ambao watakuwa na Mhandisi Mkazi (Resident Engineer) kwenye miradi ya usimamizi na pia kwenye nafasi muhimu za; barabara, madaraja, materials, n.k ambayo kwa kiasi kikubwa Usanifu na Usimamizi hufanywa na makampuni ya nje kwa sababu makampuni ya ndani hukosa utaalam na uzoefu wa kutosha kuwezesha kushindana kwenye zabuni.

Aidha, mara nyingi miradi ya ujenzi huanza huku Kampuni ya usimamizi ikiwa bado haijapatikana kutokana na taratibu za manunuzi kutokamilika kwa wakati na kulazimu TANROADS kuchukua jukumu la usimamizi hadi pale kampuni ya usimamizi itakapopatikana.

221. ***Mheshimiwa Spika,*** uwepo wa TECU umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za usimamizi wa miradi pamoja na muda unaotumiwa katika ununuzi wa Wahandisi Washauri. Aidha, TECU imeshiriki kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi kadhaa ya Kimkakati ikiwemo Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere (JNHPP), Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Njia Nane ya Kimara – Kibaha (km19.2), Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Geita na ujenzi wa kiwanda cha sukari cha Mbigiri.

222. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza miradi inayosimamiwa na TECU, TANROADS inaboresha Miongozo

(Guidelines) iliyopo ili kuendana na hali ya sasa ya usimamizi wa miradi iliyoongezeka. Mkakati huo wa kuboresha Miongozo utahusisha kuwajengea Wahandisi wake uwezo katika masuala kadhaa ikiwemo Usimamizi wa Mikataba (Contract Management), Usimamizi wa Matumizi ya Fedha (Financial Management) na uzoefu wa jumla wa usimamizi wa miradi mikubwa.

223. ***Mheshimiwa Spika,*** Mkakati mwingine ni kufanya TECU kuwa shindani na kuweza kutekeleza miradi sio tu ndani ya TANROADS, bali hata nje ya Wakala kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika usimamizi wa Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere na ujenzi wa kiwanda cha sukari cha Mbigiri.

Vilevile, TECU imeendelea kuwatumia Wahandisi mahiri waliostaafu ambao wamedhihirisha kuwa na uwezo wa kusimamia miradi kwa mfano usimamizi wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Kidatu – Ifakara (km 66.9) kwa kiwango cha lami.

Hatua hizi zimelenga kufanya Kitengo hiki kuwa shindani na kuweza kutekeleza miradi ndani na nje ya TANROADS kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika miradi iliyosimamiwa na Wakala.

**Matumizi ya Teknolojia Mpya katika Ujenzi na Matengenezo ya Barabara**

224. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na matumizi ya Teknolojia mbalimbali katika ujenzi na matengenezo ya barabara ambazo zinafanya zidumu kwa muda mrefu. Lengo ni kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa *materials* hasa changarawe zenye ubora unaotakiwa.

Teknolojia zinazotumika kwa sasa kiujumla zimegawanyika katika makundi manne ambayo ni *geo-polymer* (sementi mbadala), *ecoroads* (chemical stabilizers), *armaseal* (lami) na *ecozyme* (chemical stabilizers). Katika mwaka wa fedha 2023/24,

teknolojia hizo zimetumika na kuonesha ufanisi kwenye maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

i. Teknolojia ya sementi mbadala (geopolymer) imetumika katika barabara ya Chamwino IKULU – Dabalo (Sehemu ya km 1.5) Jijini Dodoma.

ii. Teknolojia ya *ecoroads* imetumika katika maeneo yafuatayo; Jijini Dodoma (km 1.0) utekelezaji umekamilika, Wilaya ya Chamwino (km 6.95) utekelezaji umekamilika na Wilaya ya Mufindi (km 10) utekelezaji umefikia asilimia 55. Aidha, kilometa 50 za teknolojia hii zitawekwa katika Barabara ya Nangurukuru – Liwale.

iii. Teknolojia ya *Amarseal* imetumika katika Barabara ya Mkata – Handeni.

iv. Teknolojia ya *ecozyme* imetumika katika barabara ya Itilima Oil – Ikindilio (km 5.2) (Simiyu) na utekelezaji umefikia asilimia 15.

225. ***Mheshimiwa Spika,*** Teknolojia nyingine iliyotumika ni ya matumizi ya *Water – Based RESIN Primer* ambayo tayari imetumika hapa nchini kwa upande wa Tanzania Visiwani. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI inafuatilia kwa karibu ufanisi wa Teknolojia hii ili ianze kutumika katika ujenzi na matengenezo ya barabara.

226. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto ya kuharibika kwa barabara kabla ya muda wake (premature failure), Wizara imepanga kuanza kutumia mtambo maalum wa kupima ubora wa barabara (Road Scanner). Matumizi ya teknolojia hii yatatuwezesha kupima barabara kama X-ray inavyopima mwili wa binadamu. Matumizi ya mtambo huu yatadhibiti makandarasi wasio waaminifu wanaocheza na viwango vya ubora.

**Upatikanaji wa Malighafi za Ujenzi**

227. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu upatikanaji wa malighafi za ujenzi, ikiwemo changarawe, mchanga, na kokoto, Wizara ya Ujenzi inaendelea na mazungumzo na Wizara ya Madini. Mazungumzo hayo yanalenga kupata namna bora ya kutatua changamoto kubwa ya upatikanaji wa malighafi hizo. Changamoto kubwa uwepo wa vishoka wanaoshikilia maeneo yenye malighafi za ujenzi na kutoza fedha nyingi. Serikali haitasita kuwachukulia hatua kali wale wote watakao bainika kujihusisha na mchezo huo mchafu. Dhamira ya Wizara ni kuwa kwa kadiri inavyowezekana maeneo hayo yamilikishwe TANROADS ili kupunguza gharama za ujenzi. Nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Antony Mavunde, Waziri wa Madini kwa ushirikiano anaotupatia katika kuhakikisha changamoto hii inatatuliwa.

**Ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

228. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira ya kuwa na ushirikiano wa karibu na taasisi zinazofanya shughuli zinazoshabihiana baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Kupitia ushirikiano huo, mwezi Novemba, 2023, taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi (ERB, AQRB, TANROADS, TEMESA na TBA) zilisaini Hati za Makubaliano ya Ushirikiano baina yao na Taasisi zenye majukumu yanayoshabihiana zilizopo SMZ. Lengo ni kubadilishana uzoefu, teknolojia na utaalam ili kudumisha Muungano wetu adhimu ambao umetimiza miaka 60 mwaka huu.

**Matumizi ya TEHAMA**

229. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kutoa huduma kwa wakati na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi. Ujenzi wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ambao utawezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kufanya ufuatiliaji na tathmini za

miradi yote chini ya Wizara umekamilika na Mfumo huo umeanza kutumika.

Vilevile, Wizara imeendelea kutumia mitandao ya kijamii kama vile *Instagram* na *X* katika kufikisha habari na matukio ya Wizara kwa wananchi kwa haraka zaidi.

## E. CHANGAMOTO ZILIZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA

230. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, zipo changamoto kadhaa ambazo zimechangia kutokufikiwa malengo kwa ufanisi uliokusudiwa. Changamoto hizo na mikakati ya kukabiliana nazo ni pamoja na:

### a) Mahitaji Makubwa ya Rasilimali Fedha

Mahitaji makubwa ya rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ikilinganishwa na mahitaji halisi yamesababisha malimbikizo ya madeni ya miradi ya maendeleo hususan, miradi ya barabara inayohusisha madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri.

***Mkakati***

Serikali imeweka mkakati wa kuhakikisha madai ya Makandarasi yanalipwa kwa wakati. Aidha, Serikali imeendelea na jitihada za kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi mbalimbali, ambapo umewekwa mkakati wa kulipa Shilingi bilioni 70 kila mwezi. Kati ya hizo Shilingi bilioni 50 ni maalum kwa ajili ya makandarasi wazawa.

### b) Mahitaji Makubwa ya Fedha za Matengenezo ya Barabara

Mfuko wa Barabara una uwezo mdogo wa kukidhi mahitaji ya matengenezo ya barabara. Kwa sasa Mfuko una uwezo wa

kugharamia asilimia 40.8 pekee ya mahitaji halisi ya matengenezo ya barabara Tanzania Bara.

***Mkakati***

Wizara kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mfuko ili kuongeza vyanzo vipya vya Mfuko.

**c) Uvamizi wa maeneo ya Hifadhi ya Barabara**

Wananchi wamekuwa wakivamia na kujenga katika maeneo ambayo TANROADS haijaweka alama za mwisho wa hifadhi ya barabara (Road Reserve). Hali hii husababisha usumbufu na gharama kubwa katika ujenzi wa barabara kutokana na Serikali kutakiwa kulipa fidia kubwa.

***Mkakati***

Wizara kupitia TANROADS imeendelea kuweka alama na kuzuia uendelezaji katika hifadhi za barabara. Aidha, Wizara imeendelea kuelimisha Umma kwa njia ya vyombo vya habari, vipeperushi, mikutano na semina ili waweze kufahamu vyema Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007.

## F. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

231. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Ujenzi inatarajia kutekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Mpango Mkakati wa Wizara (2021/22 – 2025/26); Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25. Aidha, Wizara imeandaa Makadirio ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

a) Kufanya matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja iliyoharibiwa na mvua za El Nino na Kimbunga Hidaya.

b) Kuendelea na utekelezaji wa miradi inayoendelea ambayo ni pamoja na:

i. Ujenzi wa barabara za kimkakati zenye kufungua fursa za kiuchumi kama utalii, kilimo, madini, bandari, viwanda, Bwawa la Kufua Umeme la Nyerere;

ii. Miradi ya kupunguza msongamano katika miji mikubwa kama vile Jiji la Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma;

iii. Ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, zinazounganisha na nchi jirani kwa kiwango cha lami pamoja na barabara za ulinzi;

iv. Usanifu wa barabara mpya hasa mijini kwa kuzingatia mahitaji ya watumiaji wote wa barabara ikiwemo wanamichezo, watembea kwa miguu na wanaoendesha vyombo visivyo vya moto;

v. Miradi ya kimkakati ikiwemo kukamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vya Msalato, Geita, Kigoma, Tabora, Songwe, Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Musoma, Songea, Tanga na Lake Manyara;

vi. Miradi ya usalama barabarani ikiwemo kujenga mizani, barabara za michepuo na njia za waenda kwa miguu na watumiaji wengine wa barabara;

vii. Miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko; na

viii. Miradi ya nyumba na majengo ya Serikali.

c) Kuendelea na matengenezo ya barabara na madaraja kwa kutumia Makandarasi wa ndani kwa asilimia 100 pamoja na kuhakikisha kuwa barabara zinapitika katika majira yote ya mwaka;

d) Kuendelea kukijengea uwezo Kitengo cha Ushauri Elekezi wa Miradi cha TANROADS (TANROADS Engineering Consulting Unit - TECU) ili kiendelee kusimamia miradi mikubwa ya kimkakati;

e) Kufanya mapitio ya Sera ya Ujenzi (2003) na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani (2009) pamoja na kanuni na miongozo mbalimbali inayohusiana na Sekta ya Ujenzi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na tabianchi;

f) Kuendelea kuwajengea uwezo wataalam wa ndani kupitia programu mbalimbali kwa lengo la kuongeza wataalam wabobezi wa ndani ili waweze kusimamia miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa nchini (Local content);

g) Kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utendaji kazi;

h) Kutumia teknolojia za gharama nafuu katika ujenzi wa barabara hususan katika maeneo korofi; na

i) Kutekeleza Mkakati wa Uimarishaji wa Utendaji kazi wa TEMESA (TEMESA Transformation Strategy 2024 – 2034).

**F.1 FEDHA ZILIZOTENGWA**

**Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

232. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Ujenzi imetengewa **Shilingi 81,407,438,000.00** ikiwa ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 76,588,233,000.00** ni Bajeti ya Mishahara na **Shilingi 4,819,205,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

233. ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi ni **Shilingi 1,687,888,714,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,141,803,989,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 546,084,725,000.00** ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani, **Shilingi 599,756,467,800.00** ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 542,047,521,200.00.**

Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika ***Kiambatisho Na. 1.***

**F. 2 MIRADI YA MAENDELEO**

**Miradi ya Barabara na Madaraja**

234. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepanga kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya barabara na madaraja katika mwaka wa fedha 2024/25.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na miradi hiyo, Wizara kupitia TANROADS itaanza utekelezaji wa mradi wa kimkakati wa ***Ujenzi wa Daraja la Jangwani*** ambao ni sehemu ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa maendelezo ya Bonde la Mto Msimbazi. Daraja litakalojengwa lina urefu wa mita 390 pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa mita 710 na kina cha mita 15.5 kutoka usawa wa bahari. Daraja hili litakapokamilika litatatua changamoto ya kujaa kwa maji katika barabara ya Morogoro eneo la Jangwani wakati wa mvua na kusababisha kufungwa kwa barabara hiyo mara kwa mara. Tathmini ya zabuni ili kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri zinaendelea.

236. ***Mheshimiwa Spika***, maelezo kuhusu miradi ya barabara na madaraja itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/25 ni kama ifuatavyo:

**Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74)**

237. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,200.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, sehemu za Soni – Bumbuli – Funta (km 30) na Kwameta – Kwashemshi (km 10). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Old Korogwe - Kwamndolwa – Magoma – Mashewa – Bombomtoni – Mabokweni (km 127.69), sehemu ya Maramba – Mabokweni (km 10) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (km 210)**

238. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 46,968.78** zinazojumuisha **Shilingi milioni 3,610.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 43,358.78** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi: sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) na kuendelea na ujenzi wa sehemu za Mnivata – Mitesa (km 100) na Mitesa – Masasi (km 60) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Namichiga – Ruangwa (km 20.3), Magamba – Madimba – Msimbati (km 35) na Mtama – Tandahimba (km 5) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.50)**

239. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,200.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2024/25, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Likuyufusi – Mkenda, sehemu ya Likuyufusi – Mhukuru (km 60) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nachingwea - Liwale (km 130)**

240. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 50.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2024/25, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.6)**

241. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.6) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24)**

242. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7)**

243. ***Mheshimiwa Spika,*** barabara ya Makofia – Mlandizi imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 660.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92)**

244. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,510.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Musoma – Kusenyi (km 40) kwa kiwango cha lami na kulipa deni la Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Suguti – Kusenyi (km 5).

**Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98)**

245. ***Mheshimiwa Spika,*** barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,500.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kongwa Jct – Ngambi – Mpwapwa (km 32) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa sehemu ya Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 46.9) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54)**

246. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Iringa – Ruaha National Park (km 104)**

247. ***Mheshimiwa Spika,*** barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 29,265.12** zinazojumuisha Shilingi **milioni 550.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 28,715.12** fedha za nje kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Iringa – Ruaha National Park (km 104). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Iringa (Ipogolo) – Kilolo (km 33.2) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muheza – Amani (km 36)**

248. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 880.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200.51)**

249. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 56,616.69** zinazojumuisha **Shilingi milioni 500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 56,116.69** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ukarabati wa sehemu za Mtwara – Mingoyo (km 82.27) na Mingoyo – Nanganga – Masasi (km 118.24) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kibaoni – Majimoto – Muze – Kilyamatundu (km 189)**

250. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,800.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu; sehemu ya Ntendo – Kizungu (km 25) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152); sehemu ya Kibaoni – Usevya (km 5) kwa kiwango cha lami. Kazi

nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kizungu – Muze (km 12) kwa kiwango cha lami.

**Daraja la Kigongo – Busisi (J.P. Magufuli) na Barabara Unganishi**

251. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 71,936.24** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa daraja hili na barabara unganishi.

**Daraja la Mzinga**

252. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 275.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Daraja la Mzinga katika Barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe Jijini Dar es Salaam.

**Daraja la Ugalla**

253. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 550.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa daraja hili lililopo katika mkoa wa Katavi.

**Daraja la Kitengule na Barabara Unganishi**

254. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,010.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kagera Sugar Jct – Kakunyu; sehemu ya Kagera Sugar Jct – Kitengule Jct (km 25) na kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja la Kitengule pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 18.

**Barabara ya Morogoro – Dodoma (km 260) pamoja na Daraja la Mkundi**

255. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,750.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Morogoro – Dodoma (km 260) pamoja na Daraja la Mkundi kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya SUA Main Gate – Mzinga Factory Gate (km 11.0) kwa kiwango cha lami.

**Daraja Jipya la Wami**

256. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja Jipya la Wami lililopo katika barabara ya Chalinze – Segera.

**Barabara ya Njombe – Makete – Isyonje (km 157.4)**

257. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,320.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Isyonje – Makete; sehemu ya Kitulo – Iniho (km 36.3), Mzani wa Igagala na barabara ya Njombe – Njombe Referral Hospital (km 3) kwa kiwango cha lami na kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara ya Njombe – Makete – Isyonje, sehemu za Njombe – Moronga (km 53.90) na Moronga – Makete (km 53.50). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Bulongwa - Iyoka - Madihani - Kidope (km 22), Madihani -Lufilyo (km 15.1), Kitulo - Matamba - Chimala (km 41) na Matamba - Mfumbi (km 33).

**Barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105)**

258. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Businde – Murongo (km 53.4) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Omugakorongo – Businde (km 51.6) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 108.9)**

259. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,805.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Nanganga – Ruangwa (km 53.2), Nachingwea – Ruangwa (km 55.7) na kuanza ujenzi wa barabara ya Nangurukuru – Liwale (km 228); Sehemu ya Choya – Liwale (km 10) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi

wa barabara ya Masasi – Nachingwea (km 45) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mpemba – Isongole (km 50.3)**

260. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,659.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za Mlowo – Kamsamba (km 10), Chang'ombe – Mkwajuni – Makongolosi (km 5) kwa kiwango cha lami na ujenzi wa kituo cha pamoja cha ukaguzi cha Iboya (One Stop Inspection Station – OSIS). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Utambalila - Chitete (km 17) kwa kiwango cha lami na kulipa madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 50.3).

**Barabara ya Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21)**

261. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.10)**

262. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,200.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Isongole II – Ndembo (km 52) na barabara ya kuingia Mji wa Ndembo (Ndembo Spur Road) kwa kiwango cha lami na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ndembo (km 44.10) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama (km 54)**

263. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,050.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Sengerema – Nyehunge - Kahunda (km 89)**

264. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Sengerema – Nyehunge (km 54). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Kamanga – Katunguru – Sengerema (km 35) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Omurushaka – Nkwenda – Murongo (km 125)**

265. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,200.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii sehemu ya Kyerwa – Chonyonyo (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Upanuzi wa Barabara Kuu Zinazoingia Katikati ya Jiji la Dodoma (km 220)**

266. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya upanuzi wa barabara kuu zinazoingia katika Jiji la Dodoma (km 220) zinazohusisha barabara ya Dodoma – Morogoro (km 70), Dodoma – Iringa (km 50), Dodoma – Singida (km 50) na Dodoma – Arusha (km 50).

**Barabara ya Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Jct. (km 76.07**)

267. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Jct (km 76.07); sehemu za Ntyuka Jct – Ntyuka (km 8), Kikombo Jct – Mapinduzi (km 16.4) na Ntyuka – Mvumi Hospital - Kikombo (km 53) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya kuingia Hospitali ya JWTZ Msalato (km 5.5). Kazi nyingine ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Ihumwa – Hombolo (km 60) ili kuijenga kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Tarime – Mugumu (km 86.05)**

268. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,200.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Mogabiri – Nyamongo (km 25) na Tarime – Mogabiri (km 9.3), Nyamongo – Mugumu (km 48.15) pamoja na barabara ya kuelekea Mugumu Roundabout (km 3.6). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Mika – Utegi – Shirati – Kirongwe (km 56.8); Sehemu ya Mika – Utegi – Shirati (km 27).

**Barabara ya Shelui – Nzega (km 110)**

269. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,550.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Shelui – Nzega (km 110). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Shelui – Sekenke – Tulya – Tyegelo (km 62); sehemu ya Shelui - Sekenke - Ntwike (km 20); kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65**)

270. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,492.67** zinazojumuisha **Shilingi milioni 550.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 1,942.67** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65); sehemu ya Kagongwa – Bukooba (km 18) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 50)**

271. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 10) na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (km 136); sehemu ya km 3 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mafinga - Mgololo (km 78)**

272. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 55.00** zimetengwa kwa ajili kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nyololo – Mtwango (km 40.4)**

273. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 550.00** zimetengwa kwa ajili kuanza ujenzi wa barabara ya Nyololo – Mtwango (km 40.4); sehemu ya Nyololo Jct – Nyololo (km 5) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kongwa – Kibaya- Arusha (km 430)**

274. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 55.00** zimetengwa kwa ajili kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Singida – Sepuka – Ndago - Kizaga (km 77)**

275. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Singida – Sepuka – Ndago (km 77) kwa kiwango cha lami na kuanza ujenzi wa barabara ya Sepuka – Mlandala – Urugu – Mtoa – Shelui (km 97.6).

**Barabara ya Kitai – Lituhi pamoja na Daraja la Mnywamaji (km 90)**

276. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) pamoja na daraja la Mnywamaji; sehemu za Amanimakoro – Ruanda (km 35) na Ruanda – Ndumbi Port (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Barabara za Kuelekea Katika Vituo vya Reli ya Kisasa ya SGR (km 87.6)**

277. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 8,890.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kizota – Zuzu SGR Station (km 14). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za kuelekea katika vituo vya reli ya kisasa (SGR) ambazo ni Morogoro – Kihonda SGR Station (km 10), Rudewa – Kilosa SGR Station (km 3), Gulwe – Gulwe SGR Station (km 2), Igandu – Igandu SGR Station (km 27), Ihumwa – Ihumwa Marshalling Yard (km 5.5), Bahi – Bahi SGR Station (km 4), Mlandizi – Ruvu SGR Station (km 22), barabara za ndani za kituo cha SGR cha Dodoma (Access Roads to Dodoma SGR Station -m100) na barabara ya Pugu – Kiltex (km 6.7).

**Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (km 174.5)**

278. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 35,236.90** zinazojumuisha **Shilingi milioni 3,500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 31,736.90** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Tanga – Pangani (km 50), Pangani (Tungamaa) – Mkange (km 95) kwa kiwango cha lami na daraja la Pangani (m 525). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mkata – Kwa Msisi (km 36).

**Barabara ya Kisarawe – Maneromango – Mloka (km 150.46)**

279. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kisarawe - Maneromango (km 54) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 215)**

280. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 40,339.46** zinazojumuisha **Shilingi milioni 4,185.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 36,154.46** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Kahama – Bulyanhulu Jct – Kakola (km 73.9) na kuanza ujenzi wa barabara za Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3), Nyikonga – Kashelo

(km 10.5), Kashelo – Ilolangulu (km 15), Ushirombo – Kilimahewa – Nanda (km 15.7). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Katoro – Nyikonga – Ushirombo (km 47):sehemu ya Ushirombo – Nyikonga (km 22.5), Masumbwe – Kashelo (km 60) na Kahama - Tulole - Muhulidede - Bukumbi - Mambali - Tabora (km 152.27): sehemu ya Kahama - Tulole (km 20) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)**

281. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,400.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Chato Ginery – Bwina (km 8.1) na SIDO – Chato Zonal Hospital (km 5.3) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50).

**Barabara ya Geita – Nzera – Nkome (km 54)**

282. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,800.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Geita – Nzera – Nkome (km 54); sehemu ya Nzera – Nkome (km 20.36).

**Barabara ya Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 199.51)**

283. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,010.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mianzini – Ngaramtoni (km 18) na kuanza upanuzi wa sehemu ya Tengeru – USA River (km 9.3), daraja jipya la Kikafu (m 560) pamoja na barabara unganishi (km 4.06) na barabara za Moshi Mjini (km 8.4). Kazi nyingine ni kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Sakina – Tengeru, barabara ya mchepuo ya Arusha (Arusha Bypass) na Kijenge – Usa River (km 20).

**Barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji (Access Roads To Rufiji Hydropower Project) - km 760.9**

284. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,800.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78) pamoja na ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara za Maneromango – Vikumburu – Mloka (km 100) na Kibiti – Mloka – Mtemele – Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (km 50). Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za Chalinze – Utete (km 354.9) na Ubena Zomozi – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 178); sehemu ya Ngerengere – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 166.4) ikiwa ni mandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro - Dodoma Expressway (km 531.8)**

285. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,540.00** fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ukarabati (overlay) wa barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24) na Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass km 10) na maandalizi ya upanuzi wa barabara ya Kibaha – TAMCO (km 4.5), kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kibaha – Mlandizi – Chalinze – Morogoro - Dodoma Expressway (km 465) kwa utaratibu wa PPP; sehemu za Kibaha – Mlandizi - Chalinze (km 78.9), Chalinze – Morogoro (km 126.1) na Morogoro – Dodoma (km 260). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Kwa - Mathiasi (Morogoro Road) – Msangani (km 8.3) pamoja na Mkandarasi aliyefanya kazi ya kuboresha maeneo hatarishi (Assorted Accident Blackspots) ya barabara ya Dar es Salaam – Morogoro na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Vigwaza.

**Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 118.1)**

286. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya kuanza ukarabati na upanuzi wa barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (sehemu ya Tegeta/DAWASA – Bagamoyo (km 46.9).

**Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 110)**

287. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Makandarasi kwa sehemu za Uyovu – Bwanga (km 43) na Bwanga – Biharamulo (km 67).

**Barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel Road (km 141)**

288. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba (km 34), Kumubuga – Rulenge – Murugarama (km 75) na Rulenge – Kabanga Nickel (km 32).

**Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 265)**

289. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 27,146.34** zinazojumuisha **Shilingi milioni 450.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 26,696.34** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Uvinza – Malagarasi (km 51.1) na Kazilambwa – Chagu (km 36) na barabara ya kuingia mji wa Usinge. Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi waliojenga barabara za Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 52), Kaliua – Kazilambwa (km 56), Urambo – Kaliua (km 28) na Urambo Roundabout.

**Barabara ya Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke – Kibena (Njombe) (km 346.43)**

290. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,585.05** zinazojumuisha **Shilingi milioni 5,260.50** fedha za ndani na **Shilingi milioni 1,324.55** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ifakara – Kihansi (km 124); sehemu za Ifakara – Mbingu (km 62.5) na Mbingu – Chita (km 37.5) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibena – Lupembe – Madeke (km 126); sehemu ya Kibena – Kidegyembe (km 42) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu ya Chita - Kihansi – Mlimba – Madeke - Kidegembye (km 95.26) ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389)**

291. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,550.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389): sehemu za Mbulu – Garbabi (km 25), Labay – Haydom (km 25) na Karatu – Mbulu, Garbabi – Labay & Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa kwa kiwango cha lami. Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mogitu – Hydom (km 68).

**Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga /Bomang'ombe – Sanya Juu (km 105.16)**

292. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,830.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16) na Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8). Kuanza ujenzi wa barabara za Sanya Juu – Kamwanga; sehemu ya Elerai – Kamwanga (km 39.5) na Tarakea – Holili (km 53); sehemu ya Munga - Kiwanda (km 10). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Marangu – Rombo Mkuu – Tarakea (km 64), Sanya Juu – Kamwanga (sehemu ya Sanya Juu – Elerai, km 32) na KIA – Mererani (km 26). Mradi huu

utahusisha pia kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Bomang'ombe – Sanya Juu (km 25).

**Barabara ya Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 60.6)**

293. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,110.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Katumba – Lupaso (km 35.3), Mbaka – Kibanja (km 20.7) pamoja na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mbambo – Ipinda (km 18.3). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Bujesi – Mbambo (km 10).

**Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127)**

294. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 50.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni).

**Barabara ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo (km 114)**

295. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tabora – Mambali – Bukene (km 114).

**Barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8)**

296. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8); sehemu ya Namanyere – Mfili II Bridge (km 20) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi (km 141)**

297. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,020.00** kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu za Dumila – Rudewa (km 45) na Rudewa – Kilosa (km 24). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 72) kwa kiwango cha lami; sehemu ya Ulaya (km 2).

**Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107)**

298. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,010.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50); sehemu za Matai – Tatanda (km 25) na Tatanda – Kasesya (km 25). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107). Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Laela – Mwimbi – Kizombwe (km 93) kwa kiwango cha lami.

**Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

299. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 21,680.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi katika daraja la Sibiti (Singida), ujenzi wa madaraja ya Mbambe (Pwani), Mbangala (Mtwara), Mirumba na Kavuu (Katavi), Mpiji Chini (Dar es Salaam), Simiyu na Sukuma (Mwanza) pamoja na Kibakwe na Kerema Maziwa (Dodoma). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa madaraja ya Sanza (Singida), Mkenda na Mitomoni (Ruvuma), Godegode na Nzali (Dodoma), Doma, Chakwale na Nguyami (Morogoro) pamoja na ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara). Aidha, mradi huu utahusisha kuanza maandalizi ya ujenzi wa Madaraja ya Mtera, Kondoa, Pahi, Mnenia, Mjonga, Suguta na Mwanjiri (Dodoma), Kisorya/Ukerewe (Mara/ Mwanza), Suguti (Mara), Mkili (Ruvuma) na Kalebe (Kagera). Kazi nyingine kuanza Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa daraja la Muhuwesi (Ruvuma) pamoja na kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa daraja la Munguli (Dodoma) na Malagarasi Chini (Kigoma); kununua vipuri vya madaraja ya dharura na kulipa sehemu ya madeni ya

Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa madaraja ya Magufuli na Kiyegeya (Morogoro), Ruhuhu (Ruvuma), Momba (Rukwa), Mara (Mara), Magara (Manyara), Msingi (Singida) na Mpwapwa (Dodoma).

**Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta (km 17.2)**

300. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Morocco – Mwenge (km 4.3).

**Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.1)**

301. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,010.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kumunazi – Kasulo – Bugene (km 133); sehemu ya Bugene – Burigi Chato National Park (km 60) pamoja na kuanza ujenzi wa sehemu za Burigi Chato – Kimisi (km 15) na Nyakahanga - Nyabiyonza - Nyakakika (km 96); sehemu ya Nyakahanga – Nyabiyonza - Chabalisa (km 22.5). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi wa sehemu ya Kyaka – Bugene (km 59.1).

**Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 392)**

302. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 15,704.46** zinazojumuisha **Shilingi milioni 1,060.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 14,644.46** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi – OSIS cha Nyakanazi pamoja na ukarabati wa sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 92). Mradi huu utahusisha pia maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nyakasanza – Kobero (km 58) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110).

**Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.75)**

303. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 9,552.21** zinazojumuisha **Shilingi milioni 130.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 9,422.21** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35), Nyahua – Chaya (km 85.4) na Tabora – Nyahua (km 85). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa Mizani ya Kizengi.

**Barabara za Mikoa (km 734.59)**

304. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, jumla ya **Shilingi milioni 61,585.00** zimetengwa kwa ajili ya barabara za mikoa na madaraja katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya kilometa **600** kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometa **60** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa Madaraja/ Makalavati **70.** Aidha, kati ya fedha hizi, **Shilingi milioni 726.00** zitatumika kwa ajili ya programu ya mafunzo kwa vitendo (Structured Engineers Apprentinceship Programme – SEAP) kwa wahandisi wahitimu. Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102)**

305. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102) pamoja na kuanza upanuzi wa barabara ya Mwanza - Usagara - JPM Bridge kwa njia nne (km 37); Sehemu ya Mwanza – Usagara (km 22).

**Mradi wa Kupunguza Msongamano Barabara za Dar es Salaam (km 165.16)**

306. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,781.49** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Goba – Matosa – Temboni (km 6), kuanza ujenzi wa barabara za Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66), Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry (One Lane Widening: km 25.1), kuanza upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 16.4) pamoja na kuanza ujenzi wa barabara za Mji Mwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 10), Kipata (m 700), Livingstone (m 170), Msikitini – Sharif Shamba (m 540), Kibamba Shule – Mpiji Magoe (km 9.2), Mbezi Victoria – Mpiji Magoe – Bunju (km 11), Chanika – Mbande (km 3), Mbezi Msakuzi – Makabe Jct (km 7) na Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi (km 7).

Fedha hizi pia zitatumika kulipa madeni ya Makandarasi wa barabara za Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14), Mbezi Mwisho – Goba (km 7), Tangi Bovu – Goba (km 9), Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6), Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7): sehemu ya Kitunda – Kivule (km 3.2), Ardhi – Makongo – Goba: sehemu ya Goba – Makongo (km 4), Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (Mbezi Mwisho); sehemu za Madale – Goba (km 5) na Wazo Hill – Madale (km 6) pamoja na Ardhi – Makongo – Goba; sehemu ya Ardhi – Makongo (km 5).

**Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 107.4)**

307. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 520.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nansio – Lugezi (km 6.0). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa sehemu za Kisorya – Bulamba (km 51) na Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4).

**Barabara ya Kolandoto – Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 122)**

308. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kolandoto – Kishapu – Lalago (km 64); Sehemu ya Kolandoto – Kola Bridge (km 10) na Iguguno Shamba –

Nduguti – Mkalama (km 89); Sehemu ya Iguguno Shamba - Mnolo (km 10).

**Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)**

309. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,210.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Utete – Nyamwage (km 33.7), kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa barabara za Kongowe – Malendego (km 160.50) na Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ikwiriri – Mkongo (km 27.74) na kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga (km 60).

**Barabara ya Kasulu – Manyovu (km 68)**

310. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 26,640.73** zinazojumuisha **Shilingi milioni 550.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 26,090.73** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68) na kuanza ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Manyovu/Mugina.

**Barabara ya Dodoma *City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2* (km 112.3)**

311. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 48,539.06** zinazojumuisha **Shilingi milioni 4,500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 44,039.06** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa Nje katika Jiji la Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road) sehemu za Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3) na Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60), Kikombo Jct – Chololo – Mapinduzi (JWTZ HQ) ) (km 16.40) na Ntyuka Jctn – Mvumi – Makulo (km 8.6). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Msalato – Mtumba – Chamwino IKULU (km 30) kwa kiwango cha lami pamoja na kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Mzunguko wa Ndani katika Jiji la Dodoma (Dodoma Inner Ring Road) kwa

sehemu ya Bahi R/About – Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu R/About (km 6.3) na Mzunguko wa Kati katika Jiji la Dodoma (Dodoma City Middle Ring Road) inayoanzia Nanenane – Miyuji – Mnadani Sekondari – Mkonze – Ntyuka – Nanenane (km 47.2).

**Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499)**

312. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,550.00** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 66.9) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Chalinze – Magindu – Lukenge – Seregete B – Kabwe Jct – Mkulazi (km 77.5). Mradi huu utahusisha pia kuendelea na ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara ya Dakawa Jct – Mbigiri (km 7) na barabara zenye jumla ya kilometa 50 kuelekea mashamba ya wakulima wa miwa ya Mbigiri. Aidha, mradi huu utahusisha ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (Forest – Londo – Kitanda) (km 396.0).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 383)**

313. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 17,036.30** zinazojumuisha **Shilingi milioni 540.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 16,496.30** fedha za nje kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Usesula – Komanga (km 115), Komanga – Kasinde (km 120), Kasinde – Mpanda (km 118) na Tabora – Sikonge (km 30). Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mpanda Airport – Kasimba Jct (km 3) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235)**

314. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10,220.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Sanzate – Natta (km 40), kuanza ujenzi wa sehemu za Waso – Loliondo (km 10), Engaruka - Ngaresero (km 39), Mto wa Mbu – Selela (km 23), Selela – Engaruka (km 27) na Monduli – Engaruka (km 115): sehemu ya Ngarashi - Enguik (km 11) pamoja na kuendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Natta – Mugumu (km 45). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Makutano – Sanzate (km 50) na Waso – Sale Jct (km 49).

**Barabara ya Ibanda – Itungi Port (km 26)**

315. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,020.00** kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa barabara za Ibanda – Itungi (km 26) na ujenzi wa sehemu ya Iponjola – Kiwira Port (km 6). Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi mpakani Kasumulu/Songwe (Kasumulu/Songwe– Tanzania/Malawi Border OSBP), pamoja na kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema Beach (km 39.1) na barabara ya Uyole – Kasumulu (sehemu ya Ilima Escarpment, km 3).

**Barabara ya Nzega – Tabora (km 289.7)**

316. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,220.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Puge – Ziba – Choma (km 109): sehemu za Ziba – Choma (km 1), Ziba – Nkinga (km 5) na Puge – Ndala (km 5). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Nzega – Puge (km 58.6) na Puge – Tabora (km 56.1).

**Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 803.6)**

317. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 26,240.34** zinazojumuisha **Shilingi milioni 13,890.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 12,350.34** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Mpanda – Mishamo – Uvinza: sehemu ya Vikonge – Luhafwe (km 25), Kibaoni – Mlele Jct (km 50), Luhafwe – Mishamo Jct (km 37.7), Mlele Junction – Sitalike (km 23.5), Kagwira – Ikola – Karema Port Lot 1: Kagwira – Kasekese (km 52.7) na Lot 2: Kasekese – Karema Port (km 59.3). Mradi huu utahusisha pia kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Mishamo – Uvinza (km 100), Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.31) na Lyazumbi – Kabwe (km 65). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa sehemu za Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Sitalike – Mpanda (km 36) na Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 37.65).

**Barabara ya Nyanguge – Musoma/Usagara – Kisesa Bypass (km 202.25)**

318. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,530.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa sehemu ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4) na kuanza ujenzi wa barabara ya Airport - Kayenze - Nyanguge (Airport Bypass) (km 46): sehemu ya Airport Jct – Igombe (km 10). Kazi nyingine ni kulipa sehemu ya madeni ya Makandarasi wa barabara za Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5), barabara ya kuelekea Uwanja wa Ndege wa Mwanza (km 12) na Usagara – Kisesa (Mwanza Bypass km 16.35).

**Barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 152.8)**

319. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,010.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Handeni – Kang'ata (km 30) na kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Magole – Turiani (km 48.80).

**Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini DSM na Barabara Unganishi**

320. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 510.00** kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo (Ubungo Interchange) pamoja na kuendelea na maandalizi ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, Fire pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct).

**Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 181)**

321. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 30.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Mwigumbi – Maswa (km 50.3), Maswa – Bariadi (km 49.7) na barabara ya Mchepuo wa Maswa (Maswa Bypass; km 11).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Sehemu ya Ipole – Rungwa (km 172)**

322. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,800.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25)**

323. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 33,230.80** zinazojumuisha **Shilingi milioni 5,520.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 27,710.80** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Kanyani Jct – Mvugwe (km 70.5), Mvugwe – Nduta Jct. (km 59.35), Nduta Jct. – Kibondo Jct. – Kabingo (km 62.5), Nduta Jct – Kibondo (km 25.9) na Kibondo – Mabamba (km 48). Kazi nyingine ni kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Kidahwe – Kasulu (km 63) na Nyakanazi – Kakonko (km 50).

**Barabara ya Kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mafia (Mafia Airport Access Road (km 16)**

324. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Kilindoni – Ras Mkumbi (km 54.4)

**Daraja la Kigamboni (Nyerere) na Barabara Unganishi**

325. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,030.00** kwa ajili ya mchango wa Serikali kwenye ujenzi wa Daraja la Nyerere, kuanza ujenzi wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (Kibada – Mwasonga – Songani Jct Section (km 41). Kazi nyingine ni kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Daraja la Nyerere – Vijibweni (km 1.5) na Tungi – Kibada (km 3.8).

**Barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 215.8)**

326. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,300.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7): sehemu ya Kanazi (Kyetema) – Kalebe Bridge (km 10) pamoja na upanuzi wa barabara ya Bukoba – Bukoba Port (km 5). Kazi nyingine ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za Bukoba Mjini – Busimbe – Maruku – Kanyangereko – Ngongo (km 19.1) na Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 136).

**Fedha za Matengenezo na Ukarabati wa Barabara**

327. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 599,756.47** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2024/25 kwa ajili ya mradi huu. Kazi zitakazofanyika ni matengenezo na ukarabati wa barabara, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira, matengenezo na ukarabati wa vivuko pamoja na kujenga uwezo

wa Wizara na Taasisi zinazosimamia masuala ya barabara na vivuko. Fedha hizi zinasimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

**Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu ya Ukanda wa Kati**

328. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 330.00** kwa ajili ya maandalizi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa maeneo ya kujenga njia za magari mazito kwenye miinuko na kujenga maegesho ya dharura katika Barabara Kuu ya Ukanda wa Kati. Aidha, ujenzi wa mradi huu utajumuishwa kwenye Usanifu wa Kina kabla ya kufanya ukarabati wa barabara za Ukanda wa Kati zilizopangwa kufanyiwa Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina ambazo ni Morogoro – Dodoma (km 260), Singida – Shelui (km 110) na Shelui – Nzega (km 110) ambazo usanifu wa kina unaendelea.

**Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**

329. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7); sehemu ya Kimara – Kibaha Mizani (km 19.2) na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji.

**Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119)**

330. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 800.00** kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**

331. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu za Bunju – Kibamba – Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma – Kigamboni (km 61) na Mbezi

Mwisho (Kwa Msuguri) – Kifuru – Banana – Kipara – Kigamboni (km 49).

**Barabara ya Kagoma – Lusahunga (km 172.50)**

332. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Muleba – Kanyambogo – Rubya (km 18.5).

**Barabara ya Singida – Shelui (km 110)**

333. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,900.00** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kuanza ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Singida – Shelui (km 110) pamoja na kuanza ujenzi wa barabara ya Singida Urban - Ilongero - Haydom (km 93): Sehemu ya Singida Urban (Igauri) – Ilongero (km 11) na upanuzi wa barabara eneo la Mlima Sekenke (km 6). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ulemo – Kinampanda – Gumanga (Singida) – Mkalama (km 46).

**Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road)**

334. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,054.15** zinazojumuisha **Shilingi milioni 2,010.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 44.15** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza upanuzi wa sehemu ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8) kutoka njia mbili kuwa njia sita. Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa daraja la Gerezani.

**Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 234.8)**

335. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,510.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ukarabati wa sehemu za Mafinga – Igawa (km 137.9) na kuendelea na upanuzi wa barabara eneo la Mlima Kitonga (km 10). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152) pamoja na

kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Morogoro – Iringa sehemu ya Tumbaku Jct – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi (km 158.45).

**Barabara ya Korogwe – Mkumbara – Same (km 239.5)**

336. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 6,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi (km 97); sehemu ya Ndungu – Mkomazi (km 36) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Same – Kisiwani – Mroyo (km 56.83). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa sehemu za Same – Himo (km 76) na Mombo – Lushoto (km 32) pamoja na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5).

**Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Manyoni (km 479.9)**

337. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 8,980.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Itigi Mjini (km 10), Noranga – Itigi – Mkiwa (km 56.6); sehemu ya Noranga – Itigi (Mlongoji): km 25), Itigi (Mlongoji) – Mkiwa (km 31.6) pamoja na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mbalizi – Makongolosi (km 56), Makongolosi – Rungwa – Noranga; sehemu ya Makongolosi – Rungwa (km 256). Kazi nyingine ni kulipa sehemu ya madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa sehemu za Mbeya – Lwanjilo (km 36), Lwanjilo – Chunya (km 36) na Chunya – Makongolosi (km 39).

**Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211)**

338. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,010.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha zege wa sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nkomang'ombe – Mchuchuma (km 7) na sehemu ya tatu ya Mawengi - Ludewa – Manda (km 111) kwa kiwango cha lami. Aidha, fedha hizi zitatumika kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Lusitu – Mawengi (km 50).

**Ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (Tanzanite)**

339. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (km 1.03) na barabara unganishi zenye jumla ya urefu wa kilometa 5.2.

**Handeni – Kibirashi – Kibaya – Njoro – Goima – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 424.24)**

340. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,050.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kwa sehemu za Handeni – Mafuleta (km 20) na Mafuleta – Kileguru (km 30). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kileguru – Kibirashi – Kibaya – Singida (km 374.24) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makambako – Songea na Barabara ya Mchepuo ya Songea (Songea Bypass) (km 295)**

341. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 18,323.95** zinazojumuisha **Shilingi milioni 3,000.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 15,323.95** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea sehemu ya Lutukila – Songea (km 95.18), ujenzi wa barabara ya Mchepuo wa Songea (Songea Bypass: km 11) pamoja na kuanza ujenzi wa barabara ya Ramadhani – Iyayi - Ilembula Hospital (km 75); Sehemu ya Ramadhani – Itulike (km 10). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Makambako – Lutikila (km 184).

**Barabara ya Dodoma – Iringa (km 267.1)**

342. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,810.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass km 7.3), kuimarisha matabaka ya barabara ya Iringa – Dodoma (km 20), kulipa madeni ya Mkandarasi wa ujenzi wa Mizani kwenye barabara ya Iringa – Dodoma na kuanza ujenzi wa barabara ya

Iringa – Pawaga (km 71.9); Sehemu ya Pawaga Jct – Ikonongo (km 5) na Itunundu – Ilolo mpya (km 20).

**Barabara ya Dodoma – Babati (km 263.4)**

343. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,930.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Babati (Babati Bypass km 15.5) pamoja na Miteremko ya Magara (Magara Escarpment) (km 3). Mradi huu utahusisha pia kuanza ujenzi wa barabara ya Dareda – Dongobesh (km 60): sehemu ya Dareda Mjini – Dareda Mission (km 8) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Dodoma – Mayamaya (km 43.65), Mayamaya – Mela (km 99.35) na Mela – Bonga (km 88.8).

**Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 343.2)**

344. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,689.09** zinazojumuisha **Shilingi milioni 1,040.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,649.09** fedha za nje kwa ajili ya madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Tunduru – Matemanga (km 59), Matemanga – Kilimasera (km 68.2), Kilimasera – Namtumbo (km 60) na Mbinga – Mbamba Bay (km 66). Aidha, mradi huu unahusisha kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi – Tunduru (km 300).

**Ujenzi wa Barabara za Chuo cha Uongozi (Uongozi Institute)**

345. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 220.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za ndani ya eneo la Chuo cha Uongozi Bagamoyo (km 8.8).

**Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma na Mbeya *Bypass* (km 266.9)**

346. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,450.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa sehemu ya Uyole – Ifisi – Songwe Airport (km 36), ujenzi wa barabara za Uyole – Songwe (Mbeya Bypass: km 48.90) na Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) kwa kiwango cha lami. Aidha, mradi huu utahusisha kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Iwambi – Mbalizi Bypass (km 6.5).

**Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT Phase I – V: km 69.8)**

347. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 90,353.13** zinazojumuisha **Shilingi milioni 2,960.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 87,393.13** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu na Nne. Aidha, fedha hizi zitatumika kuendelea na maboresho ya miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka iliyojengwa katika Awamu ya Kwanza, kuanza ujenzi wa daraja la Jangwani pamoja na kuanza ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano. Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili.

**Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT)**

348. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT) Mkoani Morogoro na majengo ya ICoT tawi la Mbeya.

**Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania**

349. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 7,155.21** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala ya Barabara (TANROADS) pamoja na kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

**Udhibiti Uzito wa Magari, Masuala ya Usalama Barabarani na Mazingira**

350. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi wa **Usalama Barabarani** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,202.955** kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa kituo cha mizani cha Buhigwe katika barabara kuu ya Kasulu-Manyovu; Ujenzi wa kituo cha mizani cha Kidyama katika barabara kuu ya Kasulu- Kibondo na Ujenzi wa kituo cha mizani cha Marolegwa katika barabara kuu ya Kibondo - Kakonko. Kazi nyingine ni kujenga mizani 16 ya kisasa inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo. Vilevile, fedha za mradi huu zitatumika kuwezesha utengenezaji na usimikaji wa mfumo wa usimamizi wa mizani kwenye mizani 56; Kuwezesha huduma ya ushauri kwa mapitio ya Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani na kuwezesha mikutano ya wadau ili kukusanya maoni ya mapitio ya Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani. Kazi nyingine ni kuwezesha ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Pamoja - One Stop Inspection Stations (OSIS) vya Idofi (Njombe), Iboya (Songwe), Himo (Kilimanjaro) na Segera (Tanga) pamoja na kutoa mafunzo ya udhibiti uzito wa magari kwa Wahandisi 20 na Mafundi Sanifu 20.

351. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa Kujenga **Uwezo wa Taasisi Katika Masuala ya Usalama Barabarani na Mazingira** umetengewa **Shilingi milioni 21.077** kwa ajili ya kuwezesha huduma za ukaguzi wa barabara (Road safety audits) kwa baadhi ya barabara za mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Mbeya, Songwe, Manyara, Singida, Arusha na Tanga. Kazi nyingine ni kuweka alama na michoro ya usalama barabarani pamoja na kuboresha maeneo hatarishi (Blackspot Areas Treatment) yalipo katika barabara kuu na za mikoa, Kutoa elimu ya usalama barabarani kwa wananchi wanaopitiwa na ujenzi wa miradi ya barabara, kufanya uchapishaji wa vitabu vya Kanuni za Usalama Barabarani (The Highway Code) na mwongozo wa Madereva wanafunzi (Learner’s Driver Manual) na pia kushiriki mikutano mbalimbali inayohusu masuala ya usalama barabarani katika Sekta ya Ujenzi.

352. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Menejimenti ya Usimamizi wa Mazingira** umetengewa **Shilingi milioni 146.114** kwa ajili ya kuandaa mkakati wa kukabili majanga kwa Sekta ya Ujenzi; kufanya mapitio ya miongozo ya tathmini na usimamizi wa mazingira ya Sekta ya Ujenzi na kuandaa mpango kazi wa mazingira kisekta wa miaka mitano (Sector Environmental Action Plan, 2025-2030). Kazi nyingine ni kuwezesha mafunzo kwa Wahandisi na Mafundi Sanifu kuhusu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

353. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25 mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 24,868.75** kwa ajili ya kazi zifuatazo:

354. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Maegesho ya Vivuko na Mifumo,** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,506.17** kwa ajili ya kulipa fidia kwa wakazi wa Kigamboni watakaopisha eneo la upanuzi wa maegesho Kigamboni; ujenzi na ukarabati wa maegesho 12 (Magogoni – Kigamboni, Bugolora - Ukara, Iramba - Majita, Nyakarilo - Kome, Ilagala - Kajeje, Rusumo - Nyakiziba, Musoma - Kinesi, Kasharu - Buganguzi, Kisorya - Rugezi, Kahunda - Maisome, Bukimwi na Rugasa). Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, majengo ya abiria na uzio kwenye vituo 18 vya vivuko ambavyo ni; Ilagala - Kajeje, Iramba - Majita, Kinesi, Ilunda - Luchelele, Kasharu - Bungaguzi, Rusumo - Nyakiziba, Buyagu - Mbalika, Mlimba - Malinyi, Kilambo, Ijinga - Kahangala, Bwiro - Bukondo, Nkome - Kikumbaitale, Kahunda - Maisome, Msanga Mkuu - Msemo, Kisorya - Rugezi, Bezi - Bukimwi, Nyakarilo - Kome na Bugolora – Ukara.

355. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine ni ujenzi wa maegesho mapya ya vivuko vya Kayenze - Kanyinya, Muleba – Ikuza mkoani Kagera, Ijinga - Kahangala (Magu), Bwiro – Bukondo (Ukerewe) mkoani Mwanza, Buyagu-Mbalika, IlundaLuchelele, Kilambo-Namoto, Utete-Mkongo na Kamanga- Kirumba Mwaloni, Chato, Muharamba, Kikumbaitale, Zumacheli na Nkome katika

kituo cha Chato – Nkome; kusimika Mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa vivuko na Mifumo ya Tiketi katika vituo 22; kufanya matengenezo kinga ya maegesho ya vivuko vyote pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya miradi hiyo.

356. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Ujenzi wa Vivuko Vipya** umetengewa **Shilingi milioni 10,826.76** kwa ajili ya ununuzi wa vivuko vipya vya Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangala, Bwiro – Bukondo, Nyakarilo – Kome, Nyamisati – Mafia na Buyagu – Mbalika. Kazi nyingine ni ununuzi wa boti mbili ndogo (sea taxi ferries) zitakazotoa huduma katika kituo cha Magogoni - Kigamboni, ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA, kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Maboresho ya Utendaji Kazi wa TEMESA (TEMESA Transformation Strategy), huduma za ushauri pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo.

357. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ***Ukarabati wa Vivuko*** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 11,535.82** kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa vivuko MV Mara, MV Ujenzi, MV Kome II, MV Misungwi, MV Nyerere, MV Kyanyabasa, MV Kitunda, MV Lindi, MV Kazi, MV Magogoni, MV Kigamboni, MV Mwanza, MV Ukara I, MV Ukara II, MV Sabasaba, MV Pangani II pamoja na ukarabati wa MV Kilombero II kabla ya kukihamishia eneo la Mlimba – Malinyi.

Vilevile, kazi nyingine ni ukarabati wa boti ya uokozi ya MV SAR III, ukarabati wa kivuko MV Malagarasi na MV Mafanikio pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya miradi hiyo.

**Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

358. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, jumla ya **Shilingi milioni 28,236.46** zimetengwa kwa ajili ya mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 21,672.58** ni kwa ajili ya miradi ya nyumba na majengo ya Serikali, **Shilingi milioni 4,015.46** ni kwa ajili ya miradi ya karakana za TEMESA na TBA na **Shilingi 2,548.42** ni kwa ajili ya kusimika Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Matengenezo ya Magari, Umeme na Elektroniki pamoja na

ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali. Kazi zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:

359. ***Mheshimiwa Spika,*** **Ujenzi wa Nyumba za Viongozi wa Serikali** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 50.00** kwa ajili ya Awamu ya II ya ujenzi wa nyumba 20 za Viongozi Dodoma. Aidha, Awamu ya II ya mradi wa **Ujenzi wa nyumba 150 za Watumishi wa Umma** jijini Dodoma imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00**.

360. ***Mheshimiwa Spika,*** **Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wizara za Ujenzi na Uchukuzi (awamu ya II)** katika eneo la Mtumba jijini Dodoma umetengewa **Shilingi milioni 500.00.**

361. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,500.00** zimetengwa kwa ajili ya **Ujenzi wa jengo la makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma katika eneo la Temeke Kota.** Aidha, mradi wa **Ujenzi wa jengo la makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma katika eneo la Magomeni Kota Wilaya ya Kinondoni** umetengewa **Shilingi milioni 4,000.00** na **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya **ujenzi wa jengo la Makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma katika eneo la Ghana Kota (Block II)** katika Mkoa wa Mwanza**.**

362. ***Mheshimiwa Spika,*** **ujenzi wa jengo la Makazi kwa ajili ya watumishi wa Umma katika eneo la Kaloleni Kota (Block II)** katika Mkoa wa Arusha umetengewa **Shilingi milioni 500.00.** Aidha, kiasi cha **Shilingi milioni 500.00** kimetengwa kwa ajili ya **Ununuzi wa nyumba (Chimala Apartments) za Watumishi wa Umma, jijini Dar es Salaam.**

363. ***Mheshimiwa Spika,*** **Ukarabati wa Nyumba** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10,172.58.** Kazi zitakazofanyika ni ukarabati wa nyumba 40 za viongozi Dodoma na nyumba 30 mikoa mingine pamoja na matengenezo kinga katika nyumba za makazi ya Magomeni Kota. Kazi nyingine ni ukarabati wa nyumba nyingine 66 zilizokuwa zinamilikiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) zilizohamishiwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) pamoja na

ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI zilizohamishiwa TBA katika mikoa 20.

364. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, kazi za **Kujenga Uwezo wa Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi na Huduma za Ushauri** zimetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,385.42** kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kupitia Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB). Kazi nyingine ni huduma za ushauri katika ujenzi wa jengo la Wizara za Ujenzi na Uchukuzi (awamu II) katika eneo la Mtumba Jijini Dodoma pamoja na kuendelea na kazi ya utungaji wa Sheria ya Majengo, kanuni pamoja na miongozo ya viwango msawazo (standard specifications).

365. ***Mheshimiwa Spika,*** **ujenzi na ukarabati wa Karakana za TEMESA na TBA** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,015.46.** Kazi zitakazohusika ni ukarabati wa karakana 14 za TEMESA katika Mikoa ya Tabora, Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya, M.T Depot - Dar es Salaam, Kigoma, Mara, Ruvuma, Pwani, Dodoma, Tanga, Kagera na Lindi. Aidha, fedha hizi zitatumika kufanya ukarabati wa karakana ya mitambo (heavy plant) ya TEMESA iliyopo Morogoro inayotumika kutengeneza mitambo ya barabara ambayo baadae itatumika kama karakana ya Mkoa wa Morogoro. Vilevile, zitatumika kuendelea na ujenzi wa karakana za TEMESA katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe, Katavi na karakana mpya ya kisasa Jijini Dodoma pamoja na kugharamia ushauri na usimamizi wa miradi ya Karakana za TEMESA.

Kazi nyingine ni ukarabati wa karakana sita (6) za TBA katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Morogoro, Tabora, Dar es Salaam na Mbeya.

366. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, kazi ya **Kusanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Matengenezo ya Magari, Umeme na Elektroniki** imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 770.00**. Aidha, jumla ya **Shilingi milioni 343.00** zimetengwa kwa ajili ya Ufuatiliaji na

tathmini kwenye miradi ya ujenzi na ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali pamoja na wahitimu wa Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi.

**Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Viwanja vya Ndege**

367. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 109,718.35.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 45,843.35** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 63,875.00** ni fedha za nje. Miradi ifuatayo imepangwa kutekelezwa:

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**

368. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,488.43** zinazojumuisha **Shilingi milioni 7,498.62** fedha za ndani na **Shilingi milioni 5,989.81** fedha za nje. Fedha hizi ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria pamoja na miundombinu yake (ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani). Kazi nyingine ni ujenzi wa uzio wa usalama, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

369. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,561.34.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 1,571.53** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 5,989.81** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria na miundombinu yake, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe**

370. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 6,728.83** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Washauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi za za ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege pamoja na eneo la usalama (Runway End Safety Area-RESA), Usimikaji wa taa za usalama na taa za kuongozea ndege (AGL) na umaliziaji wa jengo la abiria.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

371. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 6,255.06** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi za upanuzi na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maungio ya ndege, maegesho ya ndege, jengo la kuongozea ndege, jengo la mizigo pamoja na ujenzi wa mifumo ya maji safi na majitaka.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

372. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,561.32** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi zilizokamilika ambazo ni ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake, maegesho ya ndege, kusimika taa za kuongozea ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari pamoja na uzio wa usalama.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga**

373. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 6,788.41** zinazojumuisha **Shilingi milioni 798.60** fedha za ndani na **Shilingi milioni 5,989.81** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu. Kazi zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Kazi nyingine ni usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege na ujenzi wa uzio wa usalama.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga**

374. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 6,788.41** zinazojumuisha **Shilingi milioni 798.60** fedha za ndani na **Shilingi milioni 5,989.81** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kazi zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa. Aidha, kazi nyingine ni usimikaji wa mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ujenzi wa uzio wa usalama.

**Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

375. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 26,974.37** zinazojumuisha **Shilingi milioni 18,268.68** fedha za ndani na **Shilingi milioni 8,705.69** fedha za nje kutoka Benki ya Dunia. Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Iringa, Musoma, ujenzi wa uzio wa usalama kwenye kiwanja cha ndege cha Geita pamoja na kulipa madeni ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Songea. Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Lake Manyara, Iringa (awamu ya pili) na Tanga.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato**

376. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 33,527.22** zinazojumuisha **Shilingi milioni 2,317.15** fedha za ndani na **Shilingi milioni 31,210.07** fedha za nje kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Kimataifa cha Msalato mkoani Dodoma.

**Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)**

377. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 44.96** fedha za ndani kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi za ujenzi wa jengo la tatu la abiria.

**Mradi wa Kujenga Uwezo (Institutional Capacity Building)**

378. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 246.37** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu kwa lengo la kujenga uwezo wa watumishi wa Sekta ya Ujenzi kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi vya ofisi kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi.

**Fedha za Mfuko wa Barabara**

379. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi katika mwaka wa fedha 2024/25 ni jumla ya **Shilingi 599,756,467,800.00.** Kati ya fedha hizo, TANROADS imetengewa **Shilingi 534,662,653,430.00** kwa ajili ya kazi za matengenezo na ukarabati wa barabara kuu na za mikoa na Wizara ya Ujenzi imetengewa **Shilingi 59,406,961,492.00** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara za mikoa, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo. Aidha, **Shilingi 5,686,852,878.00** zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

380. ***Mheshimiwa Spika,*** mgawanyo wa **Shilingi 59,406,961,492.00** zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ni kama ifuatavyo: **Shilingi 15,820,073,000.00,** ni kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara zenye urefu wa kilometa **8,451.32** na **Shilingi 30,731,230,000.00** zimetengwa kwa ajili ya miradi ya barabara za mikoa itakayohusisha ukarabati wa jumla ya kilometa **325** kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa kilometa **38** kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja/makalavati **37** katika mikoa mbalimbali nchini. Aidha, **Shilingi 4,281,315,083.5** ni kwa ajili ya manunuzi na ukarabati wa vivuko pamoja na ujenzi wa maegesho na miundombinu ya vivuko; **Shilingi 3,570,357,225.9** ni kwa ajili ya

miradi ya usalama Barabarani na Mazingira na **Shilingi 5,003,995,182.6** ni kwa ajili ya kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara pamoja na kujenga uwezo wa watumishi.

*Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 3** na **4.***

381. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi 534,662,653,430.00** fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zimetengwa kwa ajili ya TANROADS zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu, barabara za mikoa, madaraja na uendeshaji wa mizani.

*Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5, 5A - 5D.***

**F.3 MPANGO WA KAZI ZA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25**

**Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)**

382. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wakala wa Barabara Tanzania umepanga kujenga barabara kuu zenye urefu wa **kilometa 385** kwa kiwango cha lami, ukarabati wa **kilometa 35** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa **madaraja 17,** ukarabati wa **daraja 1,** kufanya maandalizi ya ujenzi wa **madaraja 9** na kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa **madaraja mawili (2)** katika barabara kuu na baadhi ya barabara za Mikoa.

383. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya barabara za mikoa iliyopangwa kutekelezwa na Wakala ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 98.** Kati ya hizo, **kilometa 60** zitajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 38** zitajengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara. Vile vile, Wakala umepanga kufanya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara zenye urefu wa **kilometa**

**925**. Kati ya hizo, **kilometa 600** zitakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 325** zitakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, Wakala umepanga kujenga na kufanya ukarabati wa madaraja/ makalavati **107,** ambapo kati ya hayo, madaraja/ makalavati **70** yatatumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **37** yatatumia fedha za Mfuko wa Barabara.

384. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizopangwa ni kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za Mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa **kilometa 35,095.63,** matengenezo ya muda maalum **kilometa 3,206.63,** matengenezo ya sehemu korofi **kilometa 383.84** pamoja na matengenezo ya madaraja **2,904**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

385. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakala utaendelea na majukumu ya kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege. Miradi iliyopangwa kutekelezwa imeainishwa katika **Aya 457 – 470.**

**Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)**

386. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) utaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutumia fedha za ruzuku ya Serikali pamoja na mapato ya ndani ya Wakala. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kutoa huduma za ushauri kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali, kujenga majengo ya Washitiri mbalimbali; kuuza na kupangisha nyumba zinazojengwa na TBA kwa Watumishi wa Umma na kupangisha baadhi ya majengo ya Serikali kwa wasio watumishi wa Umma ili kuongeza uwezo wa Wakala kujiendesha.

387. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa kutumia ***fedha za ruzuku*** imeoneshwa katika **Aya 357- 364**.

388. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi itakayotekelezwa kwa kutumia ***mapato ya ndani ya Wakala*** ni ujenzi wa nyumba 72 za watumishi wa Umma mikoani; upatikanaji wa Hati Miliki za viwanja vya TBA; ujenzi wa jengo la Ofisi za TBA Geita na TBA Makao Makuu Dodoma; ujenzi wa jengo la ghorofa kwa Watumishi wa Umma eneo la Canadian Village Dar es Salaam na ujenzi wa jengo la ghorofa la Watumishi wa Umma eneo la Misheni Kota Geita, Ghana Kota (Block I) jijini Mwanza na Kaloleni Kota (Block I) Jijini Arusha.

389. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine ni ukarabati wa karakana 2 katika Mikoa ya Ruvuma na Rukwa; ukarabati wa majengo ya ofisi 20 za TBA mikoani; ukarabati wa majengo katika maeneo mbalimbali nchini; ujenzi wa maabara ya upimaji/majaribio ya malighafi za ujenzi Jijini Dodoma pamoja na ununuzi wa mitambo saba (7) ya ujenzi.

390. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umepanga kutekeleza miradi **274** ya ***Washitiri***. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: miradi **22** ni ya Buni- Jenga (Design and Build) ambapo hadi sasa miradi sita (6) inaendelea kutekelezwa.

391. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakala utaendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika ***Mji wa Serikali*** eneo la Mtumba Dodoma ikiwemo ujenzi wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, Wakala utatekeleza miradi **17** ya Ushauri Elekezi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi za Serikali.

392. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakala umepanga kutekeleza miradi **176** ya ***Ushauri (Consultancy***) ambapo kati ya hiyo 59 inaendelea. Aidha, Wakala umepanga kutekeleza miradi **72** ya ***Ujenzi*** ambapo miradi **15** inaendelea na miradi minne **(4)** ya ***Usimamizi (Project Management)*** ambapo kati ya hiyo miradi miwili (2) inaendelea.

**Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA)**

393. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wakala umepanga kuendelea na usimamizi na uendeshaji wa vivuko vya Serikali, kutoa huduma ya ukodishaji wa magari na mitambo ya ujenzi wa barabara pamoja na kufanya matengenezo ya magari, usimikaji wa mifumo ya umeme, majokofu, viyoyozi na elektroniki.

394. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya Ruzuku itakayotekelezwa na Wakala katika mwaka wa fedha 2024/25 inayohusisha ***maegesho ya vivuko, Ukarabati wa Vivuko, Ujenzi wa Vivuko Vipya*** na ***Ujenzi na Ukarabati wa Karakana*** ni kama inavyoonekana kwenye **Aya 352 – 356** na **Aya 365**.

395. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Wakala umepanga kuendelea na usimamizi na uendeshaji wa vivuko vya Serikali vipatavyo **32** ambavyo vinatarajiwa kutoa huduma kwa abiria **37,014,334** magari **1,366,053** na tani za mizigo **549** kwa mwaka. Wakala umepanga kufanya matengenezo ya magari **34,499**, matengenezo na usimikaji wa mifumo **263** ya umeme, **644** ya majokofu na viyoyozi na mifumo **14** ya elektroniki. Vilevile, Wakala umepanga kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo **90** ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu na kusimamia mifumo hiyo inayofikia **50.** Wakala pia utaendelea kutoa huduma ya ukodishaji wa mitambo ya magari na mitambo ya ujenzi wa barabara.

**Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB)**

396. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Mfuko wa Barabara unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 856,794,954,000** kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara za kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) ambazo husimamiwa na Wizara ya Ujenzi pamoja na barabara za Wilaya ambazo husimamiwa na Ofisi ya Rais –TAMISEMI. Mgawanyo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

Wizara ya Ujenzi **Shilingi 59,406,961,492.00**; TANROADS **Shilingi 534,662,653,430.00**; Ofisi ya Rais – TAMISEMI **Shilingi**

**25,460,126,354.00;** TARURA Shilingi **229,141,137,184.00**; na Bodi ya Mfuko wa Barabara **Shilingi 8,124,075,540.00**.

397. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Bodi imepanga kuendelea kufuatilia matumizi ya fedha zinazopelekwa kwa wakala za barabara (TANROADS na TARURA) ili kuhakikisha kuwa zinatumika kwa madhumuni yaliyowekwa. Aidha, Bodi itaendelea kufanya kaguzi za ubora wa kazi za barabara katika mikoa yote nchini ili kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inakidhi thamani ya fedha zilizotumika (value for money), na kuhakikisha mipango ya matengenezo ya barabara inazingatia mabadiliko ya tabia nchi ili kupunguza kiwango na athari za mabadiliko hayo katika kazi za barabara. Vilevile, Bodi itafanya mapitio ya sheria, kanuni na miongozo kwa lengo la kuongeza ufanisi wa makusanyo yanayotokana na matumizi ya hifadhi za barabara. Aidha, Bodi itakamilisha tathmini ya mtandao wa barabara (road inventory and condition survey). Takwimu zitakazokusanywa zitasaidia kuandaa mkakati endelevu wa matengenezo ya barabara.

398. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imepanga kuendelea kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali ili kupata vyanzo vipya vya mapato na teknolojia ya gharama nafuu ya matengenezo ya barabara. Lengo ni kukabiliana na changamoto ya uhaba wa fedha za matengenezo ya barabara. Aidha, katika jitihada ya kupunguza changamoto za kupata fedha za kutosha kwa mara moja ili kugharamia matengenezo maalum ya barabara, Bodi inafanya utafiti wa uwezekano wa kupata fedha kutoka kwenye soko la mitaji na dhamana kupitia hatifungani ili kugharamia matengenezo maalum ya barabara.

**Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB)**

399. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) imeweka malengo ya kusajili Wahandisi **3,200**, Mafundi Sanifu **300**, Kampuni za Ushauri wa Kihandisi **16** na maabara za kupima ubora wa vifaa tano (5). Vilevile, Bodi imepanga kusimamia utekelezaji wa mpango wa

mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi Wahitimu **3,651** ambapo Wahandisi Wahitimu watakaokuwa wanaendelea na mafunzo ni **2,451** na Wahandisi wapya **1,200**.

400. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi vilevile imepanga kuendelea kufanya kaguzi za shughuli za kihandisi nchini ili kuhakikisha kuwa shughuli zote za kihandisi zinafanywa na wahandisi waliosajiliwa na kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi. Bodi pia itaendelea na jukumu lake la kutembelea na kukagua miradi yote ya ujenzi ya kimkakati pamoja na barabara za Halmashauri pamoja na kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi watalaam na washauri. Aidha, Bodi itaendeleza jitihada za kuwashawishi wahandisi wataalam ili waanzishe kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani kwa lengo la kusogeza huduma karibu na watumiaji.

**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB)**

401. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2024/25, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi imepanga kusajili Wataalamu **180** na wataalamu wa kati **250** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Ubunifu wa Ndani ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Usanifu Teknolojia ya Majengo, Utathmini Majengo, Usimamizi Ujenzi na Usimamizi wa Miradi. Aidha, Bodi imepanga kusajili kampuni **32** za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi. Bodi pia imepanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **4,259** katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara pamoja na kusajili miradi ya ujenzi **1,775.**

402. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Bodi imepanga kuwajengea uwezo wahitimu **250** wa fani hizo kupitia mpango maalumu wa Mafunzo kwa Vitendo (Enhanced Articled Pupilage Programme - EAPP). Aidha, katika kutekeleza programu za kujengea uwezo wataalam wa fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Ubunifu wa Ndani ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo,

Usanifu Teknolojia ya Majengo, Utathmini Majengo, Usimamizi Ujenzi na Usimamizi Miradi, Bodi imepanga kuendesha

mitihani ya kitaalamu kwa wahitimu katika fani za Ubunifu majengo na Ukadiriaji majenzi. Bodi pia imepanga kutembelea vyuo vikuu 5 ili kuwahamasisha kuanzisha fani za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi ili kukuza namba ya wataalamu hawa nchini. Aidha, Bodi pia itafanya mikutano 5 na wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari pamoja na kuendesha mashindano ya insha kwa lengo la kuhamasisha wanafunzi hao kusoma masomo ya sayansi na hatimaye kusomea taaluma za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi na taaluma nyingine zinazoshabihiana nazo.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB)**

403. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Bodi imepanga kusajili jumla ya Makandarasi wapya **1,400** na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi **3,450.** Aidha, Bodi itaendesha kozi sita (**6)** za mafunzo katika vituo vitano **(5)** katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Pia Bodi itaendesha warsha moja **(1)** ya mafunzo ya ushirikiano wa ubia (Joint Venture) katika mkoa wa Mwanza.

Aidha, Bodi itaendelea na jitihada za kuuendeleza Mfuko maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia Makandarasi wa ndani (Contractor's Assistance Fund – CAF) pamoja na kuendelea kuhamasisha Makandarasi wa ndani kujiunga pamoja ili kuomba zabuni kwa mfumo wa ubia.

**Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC)**

404. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Baraza limepanga kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ujenzi nchini; kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa Maendeleo wa Sekta ya Ujenzi pamoja na kuandaa jukwaa la Sekta ya Ujenzi na Wiki ya Huduma za Ujenzi. Vilevile, Baraza litaendelea kushiriki katika utungwaji wa Sheria ya Majengo (Building Act), Taratibu za Majengo (Building Codes) na Viwango Msawazo vya ujenzi wa majengo na samani za Serikali. Baraza pia litaendelea kutoa ushauri wa kiufundi na kitaalam kwa wadau wa Sekta ya ujenzi; kuendelea kuchapisha taarifa ya utendaji wa Sekta ya Ujenzi;

kuratibu utatuzi wa migogoro inayotokea katika miradi ya ujenzi pamoja na kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha Sekta ya Ujenzi nchini.

405. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kutoa huduma za ukaguzi wa kiufundi katika miradi ya ujenzi kwa wadau wa Sekta ya Ujenzi na kuendesha kozi 12 za mafunzo ya kujenga uwezo wa wadau wa Sekta ya Ujenzi nchini. Aidha, Baraza limepanga kukusanya na kuchapisha takwimu za mwenendo wa bei za bidhaa na huduma za ujenzi kwa mwaka, kuandaa miongozo na taarifa za Sekta ya Ujenzi na kuandaa mfumo wa kuchakata taarifa na kutoa gharama za ujenzi na matengenezo ya barabara.

**Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji Tanzania (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre – TANT2)**

406. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo hiki kilianzishwa kwa lengo la kuimarisha/kuboresha sekta za ujenzi na uchukuzi kwa kutumia mbinu ya ukusanyaji na usambazaji wa teknolojia stahiki, maarifa na mbinu mpya katika Sekta hizi.

407. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Kituo kimepanga kuendelea kusambaza teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi hapa nchini. Aidha, kituo kitaendelea kuandaa, kuchapisha na kusambaza majarida yake yanayoandaliwa mara nne (4) kwa mwaka yanayohusu teknolojia, maarifa na taarifa mbalimbali muhimu katika Sekta za Ujenzi na Uchukuzi. Vilevile, kituo kitaendelea kupokea na kusambaza majarida kutoka kwa wadau mbalimbali yanayohusu teknolojia, maarifa na taarifa muhimu katika Sekta za Ujenzi na Uchukuzi.

408. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizopangwa ni kuandaa na kuendesha mafunzo kwa wadau yanayolenga kutatua changamoto zinazoikabili Sekta za Ujenzi na Uchukuzi; kuratibu shughuli mbalimbali za uanzishwaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT); kushiriki katika kuandaa na kufanyika

kwa Mkutano wa Vituo vya usambazaji wa Teknolojia Afrika (yaani 10th T2 Centre Conference) unaofanyika kila mwaka; na kuendesha makongamano ya Watalaam wa taasisi mbalimbali zinazohusika na miundombinu na usafirishaji ili kujadili na kutafuta majibu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta za Ujenzi na Uchukuzi. Pia kituo kitashiriki katika kufanya tafiti za matumizi ya teknolojia mpya mbalimbali katika ujenzi wa barabara ndani na nje ya nchi. Vilevile, kituo kitashiriki katika Kamati za Kujenga Uwezo za SADC chini ya ASANRA, Shirikisho la Barabara Duniani (PIARC) na International Road Federation (IRF) katika kubadilishana Tekinolojia na maarifa mapya.

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT)**

409. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25 Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi Kampasi ya Morogoro imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: - Kudahili wanafunzi wapya 150 katika ngazi ya cheti (NTA level 4) na kutoa mafunzo kwa wanafunzi 209 wanaoendelea na masomo ya stashahada katika fani za uhandisi Ujenzi, Umeme na Mitambo. Kudahili wanafunzi wapya 200 na kuendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 364 wanaoendelea na masomo katika Elimu ya ufundi stadi (VET).

Taasisi vilevile imepanga kuendelea kutoa kozi fupi kwa washiriki 400 katika fani za umeme wa magari, Maopareta wa Mitambo ya kazi za ujenzi, matumizi ya "Software" katika kufanya kazi za kihandisi, kozi kuhusu matengenezo ya madaraja, kozi ya udereva wa awali na udereva wa magari ya abiria na kufanya tathmini ya mafunzo kwa vitendo yanayofanyika viwandani na wanafunzi wa kozi ndefu za Stashahada ('NTA level 4' na 'NTA level 5') pamoja na wanafunzi wa kozi za VET.

410. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi pia itaendelea na usimamizi wa ujenzi wa jengo jipya la Utawala na Taaluma la Taasisi pamoja na kutangaza shughuli za Taasisi kupitia maonesho katika semina/warsha /mikutano mitano (5) ya bodi za kitaaluma.

## F. 4 MASUALA MTAMBUKA

### Matumizi ya Teknolojia Mpya

411. ***Mheshimiwa Spika,*** TANROADS kupitia Kitengo chake cha Utafiti na Maendeleo itaendelea kufanya tafiti mbalimbali kwa kushirikiana na *Council for Scientific and Industrial Research* (CSIR) ya Afrika Kusini katika kubaini teknolojia mpya, nafuu na zenye tija katika miradi ya ujenzi. Lengo ni kupunguza gharama za ujenzi na matengenezo ya barabara.

412. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25 Wizara imejipanga kuongeza matumizi ya Teknolojia Mpya/Mbadala ili kupunguza gharama za ujenzi na matengenezo ya barabara. Teknolojia ya *armaseal* itatumika katika barabara ya Mtwara – Mnivata, Mkoani Mtwara (km 50). Teknolojia ya *ecoroads* (chemical stabilizers) imepangwa kutumika kwenye barabara ya Nangurukuru – Liwale, Mkoani Lindi (km 50). Aidha, kwa kutumia fedha za matengenezo ya barabara, kilometa 100 zitafanyiwa matengenezo kwa kutumia teknolojia mpya/mbadala.

### Ushirikishwaji wa Makundi Maalum katika Kazi za Barabara

413. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ya kuwajengea uwezo makundi maalum ya wanawake na vijana ili kuongeza ushiriki wao katika kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara nchini. Katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara imepanga kutoa mafunzo kwa Makandarasi Wanawake juu ya namna ya kuomba na kujaza zabuni kwa ufanisi; kutoa mafunzo kwa Wanawake na Vikundi vya Wanawake juu ya kufanya matengenezo na ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvu Kazi ikiwa ni pamoja na kuwasaidia kusajili Kampuni zao za ujenzi pamoja baada ya mafunzo. Kazi nyingine ni kufuatilia kwa karibu kazi za barabara zinazofanywa na Makandarasi Wanawake. Aidha, Wizara itaendelea kutenga miradi maalum (Matengenezo/ Maendeleo) ya kuwajengea uwezo Wanawake ili kuweza kukuza ushiriki wao na kukuza Kampuni za Wanawake wazawa.

414. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara kupitia ERB, CRB na AQRB itaandaa mpango mahsusi wa kuwajengea uwezo vijana kwa nyenzo na ujuzi ili waanzishe kampuni za ujenzi na ushauri elekezi zitakazoshiriki katika ujenzi wa miundombinu. Wizara ina mpango unaofanana na programu ya *Building Better Tommorow (BBT)* kiuhandisi ambao utawajengea vijana kesho iliyo bora kwa kutenga miradi ambayo itawaongezea uzoefu katika kazi zao.

Nitoe rai kwa makundi ya vijana na wanawake katika fani ya ufundi sanifu kurasimisha na kuingiza sokoni kazi zao ili kuchangamkia fursa hii adhimu inayotolewa na Wizara. Wizara inaahidi kuwasimamia kwa kuzingatia taaluma zenu na kuwalea hadi kuwa kampuni kubwa zenye uwezo wa kushindana katika soko.

**Mapambano dhidi ya VVU na Magonjwa Yasiyoambukiza**

415. ***Mheshimiwa Spika,*** elimu kuhusu kujikinga na maambukizi ya VVU na magonjwa yasiyoambukiza kama vile kisukari, shinikizo la damu na figo itaendelea kutolewa kwa watumishi wa Wizara. Vilevile, Wizara itaendelea kuhimiza watumishi kufanya mazoezi ya viungo pamoja na kushiriki katika mabonanza na michezo ikiwa ni njia mojawapo ya kuboresha afya zao. Aidha, Wizara itaendelea kuwahudumia watumishi waliotoa taarifa ya kuathirika na virusi vya UKIMWI kwa kuwapatia posho ya chakula ili waweze kupata lishe bora.

**Mapambano dhidi ya Rushwa**

416. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukuza uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali katika mapambano dhidi ya Rushwa ikiwa ni pamoja na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara itaanza utekelezaji wa mikakati iliyomo katika Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (2023 – 2030) sambamba na kuendelea kutoa mafunzo yanayohusu

maadili na kuzuia vitendo vya rushwa kupitia mikusanyiko mbalimbali ya watumishi. Lengo ni kuimarisha utoaji wa huduma na ustawi wa wananchi.

## G. SHUKRANI

417. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa majukumu yangu umekuwa rahisi kutokana na ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwa viongozi wenzangu katika Wizara. Nawashukuru sana Mheshimiwa Mhandisi **Godfrey Msongwe Kasekenya (Mb.),** Naibu Waziri, Balozi Mhandisi **Aisha Salim Amour,** Katibu Mkuu pamoja na Ndugu **Ludovick James Nduhiye,** Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipoishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa weledi na kujituma katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Asanteni sana.

418. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kumshukuru kwa dhati mke wangu mpendwa Jennifer a.k.a Mama Alaska, pamoja na watoto wangu, Santo, Solana, Sankara na Samora kwa namna wanavyonitia moyo na kuniombea ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Nawashukuru pia wananchi wa Jimbo langu la Karagwe kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika uwakilishi wangu pamoja na kutekeleza majukumu niliyokasimiwa. Ninawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuhakikisha Jimbo letu linapata maendeleo tuyatakayo.

419. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia hadhira hii, naomba kuwatambua na kuwashukuru Washirika mbalimbali wa Maendeleo pamoja na wadau wote ambao wameshirikiana nasi kwa namna moja au nyingine katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Wizara. Kipekee nawashukuru wafuatao: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan International Cooperation Agency (JICA), OPEC Fund, Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Kuwait Fund, Barick, EACOP, Sekretarieti ya Jumuiya ya

Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Japan, China, Norway, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PSSSF, Taasisi za fedha za CRDB, NMB, NBC na TCB na Asasi mbalimbali zisizokuwa za Serikali; Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wengi. Itoshe tu kusema kwamba, asanteni sana.

420. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara **(www.mow.go.tz)**.

**H. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2024/25**

421. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,769,296,152,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 81,407,438,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Taasisi na **Shilingi 1,687,888,714,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 76,588,233,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 4,819,205,000.00** ni za Matumizi Mengineyo.

Bajeti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inajumuisha fedha za ndani **Shilingi 1,141,803,989,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 546,084,725,000.00.** Fedha za ndani zinajumuisha **Shilingi 599,756,467,800.00** kutoka Mfuko wa Barabara na **Shilingi 542,047,521,200.00** ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

422. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na Hotuba hii, nimeambatisha mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2024/25 **(Kiambatisho Na. 1 – 5)**. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

Haya, ahsanteni sana, sasa namwita Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, aje awasilishe maoni ya Kamati.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Bunge Fungu 98 - Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ni Utangulizi na inaeleza kuhusu Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake; sehemu ya pili inatoa Uchambuzi na Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; sehemu ya tatu ni Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; sehemu ya nne ni Maoni na Ushauri wa Kamati na mwisho ni Hitimisho.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2).

Mheshimiwa Spika, Makusanyo ya Maduhuli, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Ujenzi iliidhinishiwa na kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 70,000,000/=. Hadi kufikia Februari, 2024 makusanyo ya maduhuli yalikuwa ni jumla ya shilingi 142,368,000 sawa na 203% ya malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa makusanyo hayo ndani ya Wizara katika uchambuzi wake Kamati imebaini kwamba, baadhi ya taasisi chini ya Wizara ya Ujenzi zinakabiliwa na changamoto na kutopata fedha zitokanazo na huduma wanazotoa kwa taasisi nyingine za Serikali na hivyo kuathiri mwenendo wa makusanyo. Kwa mfano, Kamati imebaini kwamba, Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)*, hadi wakati inafanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya 2023/2024 madeni ambayo yamehakikiwa na kuwasilishwa kwa taasisi nyingine za Serikali yanafikia shilingi 39,463,035,862.33.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* ilikuwa inazidai taasisi za Serikali shilingi 2,250,954,983.82 ambazo hadi kufikia Desemba, 2023 ni shilingi 85,122,000.00 tu zilikuwa zimelipwa. Kwa maoni ya Kamati, taasisi za Serikali kutolipa madeni kunakwamisha makusanyo ya taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara iliidhinishiwa shilingi 48,395,392,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2024, Wizara pamoja na taasisi zake zilikuwa zimepokea jumla ya shilingi 37,471,146,758.48, sawa na asilimia 77.43 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi 35,440,580,641.90 ni mishahara na shilingi 2,030,566,116.58 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kama ambavyo Kielelezo Na.1 kinafafanua.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na mapokezi ya jumla ya fedha za matumizi ya kawaida. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kwa wakati fedha za matumizi mengineyo *(OC)* ili kuwezesha ufanisi na utekelezaji wa shughuli za kila siku za Wizara.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilitengewa shilingi 1,417,143,257,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,081,966,569,000/= ni fedha za ndani na shilingi 335,176,688,000/= ni fedha za nje. Hadi kufikia Februari, 2024, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 1,227,379,265,664.1 sawa na 86%. Kati ya fedha hizo, shilingi 892,202,577,664.12 ni fedha za ndani na shilingi 335,176,688,000 ni fedha za nje. Kielelezo Na. 2 kinatoa mchanganuo wa mwenendo wa mapokezi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa mapokezi ya fedha za miradi ya maendeleo na inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi kati ya tarehe 12 na 17 Machi, 2024 katika Mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza. Ziara hiyo ilifanywa ili kutimiza masharti kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) kutathmini hali ya mapokezi ya fedha, hatua ya utekelezaji pamoja na kubainisha changamoto za utekelezaji wake. Maelezo ya kina ya ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo inapatikana Ukurasa wa 9 – 19 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo; mradi Na.4188 - Ujenzi wa Barabara (Noranga – Itigi). Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kipande cha Noranga – Itigi *(Lot 7A)* chenye urefu wa kilometa 25 ni sehemu ya Mradi mkubwa wa Barabara ya Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa yenye jumla ya kilometa 413. Kipande hiki kilianza kujengwa tarehe 16 Septemba, 2022 kwa lengo la

kukamilika tarehe Mosi Julai, 2024, baada ya tarehe ya awali ya kukamilika 16 Machi, 2024 kupita.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* kwa gharama ya shilingi 29,770,297,741. Hadi wakati Kamati inatembelea eneo la Mradi kwa ukaguzi, maendeleo yalikuwa 74.4% ukilinganisha na malengo ya kufikia 97.24%.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji ni sababu zipi zilizosababisha Mradi kuchelewa kukamilika kwa wakati. Serikali ilitoa maelezo kwamba, utekelezaji wa mradi ulikabiliwa na changamoto ya mvua kubwa za *El-Nino* zilizonyesha Novemba, 2023. Aidha, uwepo wa nguzo za umeme za *TANESCO* kwenye hifadhi ya barabara umechangia kuchelewa kwa mradi kwa sababu nguzo hizo zilitakiwa kuhamishwa na TANESCO kwa gharama ya shilingi bilioni 1.2.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwamba, wakati wa maandalizi ya miradi, ifanye upembuzi wa kina kwa kushirikiana na taasisi za Serikali zinazohusika ili kuepukana na changamoto za kuongezeka kwa gharama za miradi kwa mabadiliko ya usanifu kwa uwepo wa miundombinu iliyowekwa na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi Kivuko pamoja na Maegesho ya Kivuko cha Buyagu – Mbalika, Mwanza, mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)* na unahusisha shughuli za ujenzi wa Kivuko Kipya cha Buyagu – Mbalika, pamoja na ujenzi wa maegesho yake. Gharama za ujenzi wa kivuko kipya peke yake ni shilingi 3,817,064,000 ambapo mkandarasi ni *Songoro Marine Transport Ltd* ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi ulianza tarehe 23 Aprili, 2023 na unatarajiwa kukamilika tarehe 4 Julai, 2024 ikiwa ni miezi minne (4) zaidi ya tarehe ya awali ya kukamilika mradi ambayo ilipaswa kuwa tarehe 28 Februari, 2024. Hadi wakati Kamati inafanya ukaguzi wa mradi huo, utekelezaji wake ulikuwa umefikia 45.9%. Aidha, Mkandarasi alikuwa ameshawasilisha hati

za madai zenye thamani ya shilingi 2,290,238,400 na malipo yaliyokuwa yamefanyika yalikuwa ni shilingi 1,107,054,755 sawa na 48.34% ya madai yaliyowasilishwa, na asilimia 29 ya gharama yote ya mradi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa. Moja kati ya changamoto hizo, ni Serikali kutokupeleka fedha za kutosha na hivyo wakandarasi kucheleweshwa malipo. Kamati inashauri kwamba, Serikali itoe fedha za ujenzi wa Kivuko cha Bulyagu – Mbalika na kumlipa mkandarasi kwa wakati ili kivuko hicho kianze kutoa huduma katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, Changamoto za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Pamoja na mapokezi ya kuridhisha ya fedha za maendeleo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali za utekelezaji wake zikiwemo zifuatazo:-

(i) Uharibifu wa miundombinu ya barabara kutokana na mvua kubwa; na

(ii) Malimbikizo ya madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri katika miradi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, tumeshuhudia mvua kubwa za *El Nino* ambazo kwa sehemu kubwa zimeharibu miundombinu ya barabara na madaraja nchini. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Serikali kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati imebaini kwamba, uwezo mdogo wa Mfuko wa Barabara kugharamia matengenezo ya barabara, unaathiri jitihada hizo kwa sababu matengenezo hayafanyiki kwa wakati na kwa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Spika, aidha, hadi wakati Kamati inakamilisha tathmini ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa *EPC + F* ilikuwa haijaanza kutekelezwa kwa kuwa hakuna fedha iliyotolewa za kutekelezwa kwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka Wa Fedha 2024/2025. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,708,958,532,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 80,907,438,000 ni Matumizi ya Kawaida, na shilingi 1,628,051,094,000 ni Fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa wastani wa 22.13% ukilinganisha na bajeti ya shilingi 1,465,538,649,000 iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. Kielelezo Na.3 kinafafanua kwa muhtasari ulinganisho kati ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Bajeti ya Mwaka huu wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 80,907,438,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 76,588,233,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 4,319,205,000 ni kwa ajili ya matumizi mengine *(OC)*.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa ujumla wake imeongezeka kwa shilingi 32,512,046,000 sawa na 67.18% ukilinganisha na shilingi 48,395,392,000 kati ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ambavyo Kielelezo Na. 4 kinaonesha.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,628,051,094,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya Fedha hizo, shilingi 1,081,966,369,000 ni fedha za ndani na shilingi 546,084,725,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa wastani wa 14.88% ukilinganisha na Bajeti ya Shilingi 1,417,143,257,000 katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, sawa na ongezeko hilo linalojionesha katika Kielelezo Na.5.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, pamoja na kwamba Bajeti ya Maendeleo kwa ujumla wake imeongezeka Serikali haijaongeza kabisa fedha za ndani katika bajeti hiyo. Kwa kutotenga fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya Wizara ya Ujenzi, Serikali haioneshi nia ya dhati ya kutekeleza miradi hasa kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya miradi kama vile ya ujenzi wa barabara na madaraja nchini.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne, maoni ya jumla. Kamati inaipongeza Serikali ambayo kwa ufanisi mkubwa imeendelea kutoa fedha za utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Fungu Na. 98 – Wizara ya Ujenzi, hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo na kwa kuthamini mtaji wa fedha za maendeleo unaotokana na kodi za wananchi, Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu na kuwepo kwa thamani ya fedha; na

(ii) Serikali kulipa madai ya wakandarasi kwa wakati wa madeni yaliyopo ili kuwezesha miradi kutekelezwa kwa wakati na kupunguza kudaiwa riba na adhabu na kujenga imani mbele ya macho ya tasnia ya wakandarasi na wazabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo ya Serikali *(TBA);* Kamati inaishauri Serikali kubuni mfumo mpya na rahisi utakaoiwezesha *TBA* kukusanya madeni na iwapo taasisi za Serikali na wapangaji wengine watachelewa kulipa, mfumo huo uweze kutoza riba ya ucheleweshaji. Aidha, kwa taasisi za Serikali ambazo zinalipia watumishi wake nyumba na hawajalipa, basi *TBA* ichukue hatua stahiki ikiwemo kuwaondoa wadaiwa hao kwa kuwa mahitaji ya nyumba kwa Watumishi wa Serikali bado ni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kulipa madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri; Kamati imebaini kwamba Serikali imekuwa ikisuasua katika kulipa madai na madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri katika miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa barabara na ujenzi wa vivuko. Kwa Serikali kutolipa madeni hayo, kwanza kuna kwamisha jitihada za kuwawezesha kiuchumi wananchi ambao wanapata changamoto ya marejesho ya mikopo katika taasisi za kifedha, lakini pia kunaathiri mzunguko wa fedha nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizo Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati madhubuti na wa kudumu ili kulipa madeni kwa wakati lakini pia kuwajengea uwezo wakandarasi wa ndani ili watekeleze miradi mingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, fidia kwa wananchi, Kamati imebaini kwamba, baadhi ya wananchi katika maeneo mbalimbali nchini ambao waliachia maeneo yao ili kupisha miradi inayosimamiwa na Wizara ya Ujenzi bado hawajalipwa fidia. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, wananchi wote wanaodai fidia, walipwe stahiki zao kwa mujibu wa sheria na iwapo Serikali haina uwezo wa kulipa fidia katika maeneo waliyotwaa, maeneo hayo yarejeshwe kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara kwa utaratibu wa *EPC + Fedha;* kwa kuwa Kamati imebaini kwamba miradi iliyopaswa kutekelezwa kwa utaratibu wa *EPC + F* haijatekelezwa kabisa, Serikali ifanye tathmini kuhusu utaratibu huo kuona iwapo una tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maboresho ya utendaji wa *TEMESA;* Kwa kuwa Kamati imebaini kwamba, pamoja na kwamba Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)* inatoa huduma na matengenezo ya magari ya Serikali, Wakala inakosa ufanisi kwa sababu ya kuwepo kwa changamoto ya madai ya madeni. Kamati inashauri kwamba Serikali ibuni Mfumo wa Kielektroniki ambao utaweka utaratibu kwamba, baada ya gari la umma kubainika kuwa na tatizo la kiufundi taarifa zote zitumwe katika taasisi husika na

gharama za matengenezo yake na gari hiyo lisitengenezwe hadi hapo taasisi husika itakapokuwa imekamilisha malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka *(BRT);* Kamati inapongeza jitihada za Ujenzi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka *(BRT)* Jijini Dar es Salaam. Pamoja na hayo, Serikali inashauriwa kuhakiki mradi huo na kuuboresha miundombinu inayozunguka mradi huo hasa mifereji ya maji ili kuepuka changamoto zinazowakabili watumiaji wa barabara wakati ujenzi huo unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutunisha Mfuko wa Barabara; Kamati imebaini kwamba uwezo wa Mfuko wa Barabara kukarabati barabara nchini ni mdogo ukilinganisha na mahitaji halisi kama ambavyo taarifa hiyo imefafanua hapo awali. Aidha, kwa kuwa mahitaji ya ukarabati wa barabara nchini yanaongezeka, Kamati inashauri Serikali itafute vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitawezesha Mfuko wa Barabara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya mwisho, shukrani; kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, namshukuru Naibu Spika kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha kwa ufanisi Vikao vya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu pamoja na Makamu wangu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendeleza, kuisimamia Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako Tukufu. Naomba niwatambue kwa majina yao kuingia katika Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama wanavyoonekana katika Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge, kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Msongwe Kasekenya, Mbunge. Aidha, niwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Balozi Mhandisi Aisha Amour. Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya Ujenzi inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 98 - WIZARA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**

1.1 **Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Fungu 98 –

Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

a) **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi na inaeleza kuhusu Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

b) **Sehemu ya Pili** inatoa Uchambuzi na Tathimini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

c) **Sehemu ya Tatu** ni Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

d) **Sehemu ya Nne** ni Maoni na Ushauri wa Kamati; na

e) **Sehemu ya Tano** ni Hitimisho.

### 1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti mbalimbali yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilifanya yafuatayo: -

a) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 (Kanuni ya 117 (1));

b) Kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

c) Kupokea na kufanya uchambuzi wa Randama ya Wizara (Kanuni ya 115 (1)); na

d) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SEHEMU YA PILI**

2.0 **UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

2.1 **Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 63 (3) (b)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inalipa Bunge madaraka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti.[1] Aidha, Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti kwa Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi za Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni.[2] Kwa muktadha huo, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa **Fungu 98 - Wizara ya Ujenzi** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa mujibu wa **Kanuni ya 117 (2)**.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

[1] Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977

[2] Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023

a) Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli;

b) Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida; na

c) Utekelezaji wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

2.2 **Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Ujenzi iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 70,000,000**. Hadi kufikia Februari, 2024 makusanyo ya maduhuli yalikuwa ni jumla ya **Sh. 142,368,000** sawa na **asilimia 203** ya malengo waliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya vyanzo vya makusanyo ya Wizara ni kazi za usajili wa magari mapya pamoja na uthamini wa magari chakavu. Kamati ilibaini kwamba makusanyo yalivuka lengo kwa sababu ya manunuzi yasiyotarajiwa ya magari na pikipiki kwa Fedha za Kupambana na UVIKO - 19 ambapo, magari mengi yalinunuliwa na kusajiliwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Januari 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa makusanyo hayo ndani ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kwamba, baadhi ya taasisi chini ya Wizara ya Ujenzi zinakabiliwa na changamoto ya kutopata fedha zitokanazo na huduma wanazotoa kwa taasisi nyingine za Serikali na hivyo kuathiri mwenendo wa makusanyo. Kwa mfano, Kamati imebaini kwamba, Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) hadi wakati inafanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya 2023/2024 madeni ambayo yamehakikiwa na kuwasilishwa kwa taasisi nyingine za Serikali yanafika **Sh. 39,463,035,862.33**. Kwa upande mwingine, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilikuwa inazidai taasisi za Serikali **Sh. 2,250,954,983.82** ambapo hadi kufikia Desemba, 2023 ni **Sh. 85,122,000** tu zilikuwa zimelipwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maoni ya Kamati, taasisi za Serikali kutolipa madeni kunakwamisha makusanyo ya taasisi hizo.

### 2.3 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara iliidhinishiwa **Sh. 48,395,392,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Sh. 43,958,274,000** ni Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na **Sh. 4,437,118,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024, Wizara pamoja na taasisi zake zilikuwa zimepokea **Sh. 37,471,146,758.48**, sawa na **asilimia 77.43** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Sh. 35,440,580,641.90** ni Mishahara **Sh. 2,030,566,116.58** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo kama ambavyo **Kielelezo Na. 1** kinafafanua.

**KIELELEZO NA. 1 – MCHANGANUO WA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KUFIKIA FEBRUARI, 2024**

| MATUMIZI YA KAWAIDA | BAJETI YA 2023/2024 (TZS) | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 (TZS) | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA (P.E) | 43,958,274,000 | 35,440,580,641.90 | 80.62% |
| MATUMIZI MENGINEYO (O.C.) | 4,437,118,000 | 2,030,566,116.58 | 45.76% |
| **JUMLA** | **48,395,392,000** | **37,471,146,758.48** | **77.43%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na mapokezi ya jumla ya Fedha za Matumizi ya Kawaida. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kwa wakati Fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.) ili kuwezesha ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za kila siku za Wizara.

## 2.4 Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilitengewa **Sh. 1,417,143,257,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh.1,081,966,569,000** ni Fedha za Ndani na **Sh. 335,176,688,000** ni Fedha za Nje. Fedha za Ndani zilijumuisha **Sh. 482,210,099,000** ambazo ni Fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **Sh. 599,756,470,000** ni Fedha za Mfuko wa Barabara.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2024, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Sh. 1,227,379,265,664.1** sawa na **asilimia 86**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 892,202,577,664.12** ni Fedha za Ndani na **Sh. 335,176,688,000** ni Fedha za Nje. **Kielelezo Na. 2** kinatoa mchanganuo wa mwenendo wa mapokezi ya Fedha za Maendeleo.

**KIELELEZO NA. 2 – MCHANGANUO WA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KUFIKIA FEBRUARI, 2024**

| FEDHA ZA MAENDELEO | BAJETI YA 2023/2024 (TZS) | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 (TZS) | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| FEDHA ZA NDANI | 1,081,966,569,000 | 892,202,577,664.12 | 82.46% |
| FEDHA ZA NJE | 335,176,688,000 | 335,176,688,000 | 100% |
| **JUMLA** | **1,417,143,257,000** | **1,227,379,265,664.1** | **86%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi*

**Mheshimiwa Spika**, katika mapokezi ya Fedha za Ndani, Kamati imebaini kwamba Mfuko wa Barabara ulipokea **Sh. 459,613,828,432.38** sawa na **asilimia 76.63** ya **Sh. 599,756,470,000** zilizoidhinishwa kwa Mfuko huo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024.[3]

[3] Randama ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ya Fungu 98 – Wizara ua Ujenz, Uk. 16

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo, na inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa zilitekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo yafuatayo: -

a) Wizara kuanza kutumia Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Kazi pamoja na Miradi ya Maendeleo;

b) Ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja;

c) Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT);

d) Ujenzi, upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege;

e) Miradi ya Usalama Barabarani inayojumuisha shughuli za ujenzi wa mizani, na kufunga mifumo ya kupima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo;

f) Kununua na kujenga vivuko vipya, kukarabati vivuko vya zamani pamoja na kujenga maegesho ya vivuko; na

g) Ujenzi, ukarabati na usimamizi wa nyumba na majengo ya Serikali.

### 2.5 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, ili kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi kati ya tarehe 12 na 17 Machi, 2024 katika mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza. Ziara hiyo ilifanywa ili kutimiza masharti kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) kutathmini hali ya mapokezi ya fedha, hatua ya utekelezaji pamoja na kubainisha changamoto za utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

2.5.1 **Mradi Na. 4188 - Ujenzi wa Barabara (Noranga - Itigi)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kipande cha **Noranga – Itigi (Lot 7A)** chenye urefu wa **Kilometa 25** ni Sehemu ya Mradi Mkubwa wa Barabara ya **Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa** yenye jumla ya **Kilometa 413**. Kipande hiki kilianza kujengwa tarehe 16 Septemba, 2022 kwa lengo la kukamilika tarehe 01 Julai, 2024 baada ya tarehe ya awali ya kukamilika 16 Machi, 2024 kupita.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa gharama ya **Sh. 29,770,297,741**. Mkandarasi wa Mradi ni Kampuni ya M/S China Henan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO) na Mshauri Elekezi ni M/S SABA Engineering PLC ya Ethiopia ikisaidiana na Kampuni ya M/S KAPSEL (T) Ltd ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inatembelea eneo la Mradi kwa ukaguzi, maendeleo yalikuwa **asilimia 74.4** ukilinganisha na malengo ya kufikia **asilimia ya 97.24**. Aidha, Kamati ilitaarifiwa kwamba, tayari Mkandarasi wa Mradi alikuwa amelipwa **Sh. 7,703,257,211.58** na malipo ambayo hayajalipwa ni **Sh. 8,911,234,348.72**, wakati Mhandisi Mshauri anadai **Sh. 500,136,300** kati ya **Sh. 1,693,240,000** za kazi ya ushauri elekezi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji ni sababu zipi zilizosababisha Mradi kuchelewa kukamilika kwa wakati. Serikali ilitoa maelezo kwamba, utekelezaji wa mradi ulikabiliwa na changamoto ya mvua kubwa za El Nino zilizonyesha Novemba, 2023. Aidha, uwepo wa nguzo za umeme za TANESCO kwenye hifadhi ya barabara umechangia kuchelewa kwa mradi kwa sababu nguzo hizo zilitakiwa kuhamishwa na TANESCO kwa gharama ya **Sh. Bilioni 1.2**.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto hizo, Kamati imetaarifiwa kwamba, Serikali inaendelea na tathmini na uhakiki

wa gharama na muda utakaotumika kuhamisha nguzo husika. Aidha, Serikali iko katika mchakato wa kumuongezea muda Mkandarasi ili kukamilisha kazi zilizobaki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kwamba, wakati wa Maandalizi ya Miradi, ifanye upembuzi wa kina *(scoping)* kwa kushirikiana na taasisi za Serikali zinazohusika ili kuepukana na changamoto za kuongezeka kwa gharama za miradi kwa mabadiliko ya usanifu kwa uwepo wa miundombinu iliyowekwa na taasisi nyingine. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutoa fedha za utekelezaji wa mradi wa **Barabara ya Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa** ili ukamilike mapema kwa kuzingatia umuhimu wa kuunganisha mikoa inayopitiwa na mradi huo.

2.5.2 **Mradi Na. 4159 – Ukarabati na Uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa gharama ya **Sh. 24,626,767,735.34** (Bila VAT) ambapo ulianza tarehe 01 Aprili, 2023 na unatarajiwa kukamilika tarehe 11 Oktoba, 2024 kwa kuwa lengo la awali la kukamilika tarehe 31 Machi, 2024 halikufikiwa. Mkandarasi wa Mradi ni M/S Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd, na Mhandisi Mshauri ni kampuni ya M/S Khatib & Alami Consulting Engineers – Offshore S.A.L. kutoka Lebanoni.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inatembelea Mradi huo, utekelezaji wake ulikuwa **asilimia 38** ukilinganisha na mpango kazi *(schedule of work)* wa kufikia **asilimia 43.6**. Aidha, Mkandarasi alikuwa tayari amelipwa malipo ya awali kiasi cha **Sh. 4,054,825,943.40** sawa na **asilimia 15** ya jumla ya gharama kimkataba *(total contract sum)*.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulikabiliwa na changamoto mbalimbali zilizosababisha utekelezaji wake kuchelewa. Changamoto hizo ni pamoja na mvua kubwa zilizonyesha kati ya Novemba, 2023 na Februari, 2024. Aidha, uhamishaji wa

miundombinu ya maji, umeme na mawasiliano kupisha mradi ulichelewa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwamba, wakati wa kuingia mikataba na wakandarasi, iepuke kukubali mabadiliko ya gharama za mradi kutokana na sababu za hali ya hewa ikiwemo mvua kwa sababu, majira ya mvua katika nchi yetu yanajulikana.

2.5.3 **Mradi Na. 4222 – Ujenzi wa Kiwanja wa Ndege cha Shinyanga**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa gharama ya **Sh. 49,179,439,663**. Mkandarasi wa Mradi ni M/S China Henan International Cooperation Group Limited kutoka nchi ya China, na Mshauri Elekezi ni kampuni ya M/S SMEC International (PTY) Limited ya Australia ikishirikiana na SMEC (T) Limited.

**Mheshimiwa Spika**, mradi ulianza kutekelezwa tarehe 05 Aprili, 2023 kwa lengo la kukamilika ifikapo tarehe 04 Oktoba, 2024. Hadi wakati Kamati inatembelea ili kukagua mradi huo, utekelezaji wake ulikuwa ni **asilimia 10.4** ukilinganisha na malengo ya kufikia **asilimia 35.8.** Aidha, Kamati ilibaini kwamba, Mkandarasi alikuwa amelipwa **Sh. 7,930,184,645.66** kama malipo ya awali sawa na **asilimia 15** ya Mkataba. Vilevile, Mkandarasi alikuwa amewasilisha hati ya madai ya malipo ya **Sh. 2,698,485,934.53** ambayo TANROADS ilikuwa haijalipa bado.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto za uchelewashaji wa malipo kwa Mkandarasi, changamoto nyingine ni pamoja na kuchelewa kwa uhamishaji wa miundombinu ya maji na umeme katika eneo la mradi pamoja na mvua kubwa zilizonyesha kati ya Novemba 2023 na Januari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kumlipa Mkandarasi kwa wakati, na kumsimamia ili kiwanja hicho cha ndege kikamilike mapema na kuanza kutoa huduma kwa wakazi wa Shinyanga na mikoa ya jirani.

2.5.4 **Ujenzi wa Jengo la Makazi kwa Watumishi wa Umma, Eneo la Ghana, Mwanza, Block I**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kwa gharama ya **Sh. 6,192,260,778** ambapo ulianza tarehe 20 Januari, 2023 na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 20 Julai, 2024. Hadi wakati Kamati inatembela mradi, ulikuwa umepokea **Sh. 2,123.159,500** sawa na **asilimia 34.28**. Aidha, utekelezaji wa mradi huo ulikuwa umefikia **asilimia 50**.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa inayoukabili mradi huu ni kutopatikana kwa wakati kwa fedha ili kuendana na kasi ya utekelezaji wake. Kamati inashauri kwamba, Serikali iiwezeshe TBA kupata fedha za kukamilisha mradi huu.

2.5.5 **Mradi wa Ujenzi Kivuko pamoja na Maegesho ya Kivuko cha Buyagu – Mbalika, Mwanza**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) na unahusisha shughuli za ujenzi wa Kivuko Kipya cha Buyagu – Mbalika, pamoja na ujenzi wa maegesho yake. Gharama za ujenzi wa kivuko kipya peke yake ni **Sh. 3,817,064,000** ambapo Mkandarasi ni *Songoro Marine Transport Ltd* ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi ulianza tarehe 23 Aprili, 2023 na unatarajiwa kukamilika tarehe 04 Julai, 2024 ikiwa ni miezi minne (4) zaidi ya tarehe ya awali ya kukamilika mradi ambayo ilipaswa kuwa tarehe 28 Februari, 2024. Hadi wakati Kamati inafanya ukaguzi wa mradi huo, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 45.9**. Aidha, Mkandarasi alikuwa ameshawasilisha hati za madai zenye thamani ya **Sh. 2,290,238,400** na malipo yaliyokuwa yamefanyika yalikuwa ni **Sh. 1,107,054,755** sawa na **asilimia 48.34** ya madai yaliyowasilishwa, na **asilimia 29** ya gharama yote ya mradi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mradi wa Maegesho ya Buyagu – Mbalika, mradi unahusisha ujenzi wa maegesho upande

wa Buyagu kwa gharama ya **Sh. 402,736,080** na ujenzi wa maegesho upande wa Mbalika kwa gharama ya **Sh. 574,510,800**. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba ujenzi wa maegesho hayo ulikuwa bado haujaanza, isipokuwa kazi zilizofanyika ni usanifu na taratibu za manunuzi tu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa. Moja kati ya changamoto hizo, ni Serikali kutopeleka fedha za kutosha na hivyo wakandarasi kucheleweshewa malipo. Changamoto nyingine ni ubovu wa barabara inayounganisha maeneo ambapo maegesho yatajengwa na maeneo mengine ya Wilaya za Sengerema na Misungwi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba, Serikali itoe fedha za ujenzi wa **Kivuko cha Bulyagu – Mbalika** na kumlipa mkandarasi kwa wakati ili kivuko hicho kianze kutoa huduma katika Ziwa Victoria. Aidha, Serikali ijenge barabara ili kuwezesha wananchi wa maeneo ya kanda ya ziwa kufika katika maegesho ya kivuko hicho kwa urahisi.

2.5.6 **Mradi Na. 4015 - Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa gharama ya **Sh. 592,608,692,836**, ambapo Mkandarasi ni China Civil Engineering Construction Corporation akishirikiana na China Railway 15 *Bureau Group Corporation (CCECC – CR15G JV)*.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 25 Februari, 2020 kwa lengo la kukamilika tarehe 24 Februari 2024. Hata hivyo, kutokana changamoto mbalimbali, mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Desemba, 2024. Changamoto hizo ni pamoja na kuongezeka kwa kina cha maji ya Ziwa Victoria kulikosababishwa na mvua kubwa na hatimaye kubadilika kwa usanifu wa daraja. Changamoto nyingine ni mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 uliosababisha shughuli nyingi za kiuchumi kudorora.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inatembelea mradi, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 85**, na tayari Mkandarasi alikuwa amelipwa **Sh. Bilioni 441.309** sawa na **asilimia 74.5**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ambayo mradi umefikia. Hata hivyo, ni vyema Serikali ikaongeza jitihada za kusimamia mradi huo ili ukamilike ndani ya muda wa nyongeza na kwa ubora unaostahili.

### 2.6 Changamoto za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mapokezi ya kuridhisha ya Fedha za Maendeleo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali za utekelezaji wake zikiwemo zifuatazo: -

a) Uharibifu wa miundombinu ya barabara kutokana na mvua kubwa;

b) Malimbikizo ya madeni ya wakandarasi na wahandishi washauri katika miradi ya barabara; na

c) Uwezo mdogo wa Mfuko wa Barabara kugharamia matengenezo ya barabara kwa kuwa Mfuko huo unaweza kugharamia **asilimia 40.8** tu ya mahitaji halisi.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, tumeshuhudia mvua kubwa za El Nino ambazo kwa sehemu kubwa zimeharibu miundombinu ya barabara na madaraja nchini. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Serikali kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati imebaini kwamba, uwezo mdogo wa Mfuko wa Barabara kugharamia matengenezo ya barabara, unaathiri jitihada hizo kwa sababu matengenezo hayafanyiki kwa wakati na kwa kiwango kinachostahili.

**Mheshimiwa Spika**, aidha hadi wakati Kamati inakamilisha tathmini ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa EPC + F ilikuwa haijaanza

kutekelezwa kwa kuwa hakuna fedha iliyotolewa za kutekeleza miradi hiyo.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**3.1 Umbile la Bajeti**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 1,708,958,532,000**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 80,907,438,000** ni Matumizi ya Kawaida, na **Sh. 1,628,051,094,000** ni Fedha za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, fedha inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 22.13** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 1,465,538,649,000** iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. **Kielelezo Na. 3** kinafafanua kwa muhtasari ulinganisho kati ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**KIELELEZO NA. 3 – ULINGANISHO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| BAJETI | MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | TOFAUTI (ASILIMIA) |
|---|---|---|---|
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 48,395,392,000 | 80,907,438,000 | +67.18% |
| FEDHA ZA MAENDELEO | 1,417,143,257,000 | 1,628,051,094,000 | +14.88% |
| **JUMLA** | **1,465,538,649,000** | **1,708,958,532,000** | **+22.13%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi*

3.2 **Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Sh. 162,400,000** ambayo ni ongezeko **asilimia 132** ikilinganishwa

na malengo ya makusanyo ya **Sh. 70,000,000** katika Mwaka wa Fedha unaoisha. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio yake ya makusanyo kwa kuwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha, makusanyo yalivuka malengo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutathmini uwezo wake na hatimaye kubuni namna bora ya kukusanya kulingana na vyanzo vya mapato.

3.3 **Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/205, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 80,907,438,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Sh. 76,588,233,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 4,319,205,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C).

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa ujumla wake imeongezeka kwa **Sh. 32,512,046,000** sawa **asilimia 67.18** ukilinganisha na **Sh. 48,395,392,000** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ambavyo **Kielelezo Na. 4** kinaonesha.

**KIELELEZO NA. 4** – ULINGANISHO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025

| MATUMIZI YA KAWAIDA | MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | TOFAUTI (ASILIMIA) |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA (P.E.) | 43,958,274,000 | 76,588,233,000 | +74.23% |
| MATUMIZI MENGINEYO | 4,437,118,000 | 4,319,205,000 | -2.66% |
| **JUMLA** | **48,395,392,000** | **80,907,438,000** | **+67.18%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi*

**Mheshimiwa Spika**, katika Fedha za Matumizi ya Kawaida, Mishahara imeongezeka kwa **asilimia 74.23** wakati Fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.) imepungua kwa **asilimia 2.66**. Kamati ilitaarifiwa kwamba, ongezeko la Mishahara (P.E.) linatokana na ajira mpya, upandishaji wa vyeo, nafasi za uteuzi, mabadiliko ya

kada za watumishi, pamoja na mabadiliko ya muundo wa baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza jitihada hizi za Serikali. Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba, ongezeko la Bajeti ya Mishahara linapaswa kwenda sambamba na ongezeko la Matumizi Mengineyo (O.C.) ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

### 3.4 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 1,628,051,094,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, **Sh. 1,081,966,369,000** ni Fedha za Ndani, na **Sh. 546,084,725,000** ni Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 14.88** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 1,417,143,257,000** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hilo linajionyesha katika **Kielelezo Na. 5**.

**KIELELEZO NA. 5 – ULINGANISHO WA BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025**

| BAJETI YA MAENDELEO | MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | TOFAUTI (ASILIMIA) |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | 1,081,966,569,000 | 1,081,966,369,000 | 0% |
| **FEDHA ZA NJE** | 335,176,688,000 | 546,084,725,000 | +62.92% |
| **JUMLA** | **1,417,143,257,000** | **1,628,051,094,000** | **+14.88%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, pamoja na kwamba Bajeti ya Maendeleo kwa ujumla wake imeongezeka katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali haijaongeza kabisa

Fedha za Ndani katika Bajeti hiyo. Kwa kutotenga fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya Wizara ya Ujenzi, Serikali haionyeshi nia ya dhati ya kutekeleza miradi hasa kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya miradi kama vile ya ujenzi wa barabara na madaraja nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya Kamati kuanza uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, ilibainisha mahitaji ya miradi ya ujenzi wa barabara nchini na kufanya kikao na Waziri wa Fedha ili kuitaka Serikali kutenga walau **Sh. Trilioni 5** Mwaka wa Fedha 2024/2025 ili kugharamia miradi hiyo. Kwa kuzingatia Bajeti iliyowasilishwa, Kamati haijaridhishwa na mwelekeo wa kibajeti kwa kuwa fedha zilizotengwa haziwezi kukidhi mahitaji yaliyopo.

**SEHEMU YA NNE**

4.0 **MAONI NA USHAURI**

4.1 **Maoni ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali ambayo kwa ufanisi mkubwa imeendelea kutoa fedha za kutekeleza majukumu mbalimbali ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi, hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha miaka mitatu, Kamati imeshuhudia sehemu kubwa ya bajeti ya Sekta ya Ujenzi imekuwa ikitolewa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, na kwa kuthamini mtaji wa fedha za maendeleo unaotokana na kodi za wananchi, Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo: -

a) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika utendaji kazi utakaochochea kuboresha huduma za Sekta ya Ujenzi nchini, kwa kuwa sekta hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi;

b) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika kukusanya maduhuli kutokana na vyanzo vilivyopo, na kubaini vyanzo vipya ambavyo vitaongeza wigo wa makusanyo hayo.

Sambamba na hilo, Serikali ihakikishe kwamba, huduma zitolewazo na taasisi zake, zinakuwa bora ili kukidhi matarajio ya wadau muhimu wa Sekta ya Ujenzi;

c) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu *(sustainability)* na kuwepo kwa thamani ya fedha *(value for money)*;

d) Wizara ya Fedha kutenga Kifungu Maalum ili iweze kukata Fedha za Matumizi ya Kawaida (O.C.) za Wizara mbalimbali kulingana na madai ya TBA, TEMESA na taasisi zingine za Serikali zinazotoa huduma kwa taasisi za Serikali ili kutozalisha madeni na kuzidumaza taasisi hizo; na

e) Serikali kulipa madai ya wakandarasi kwa wakati na madeni yaliyopo ili kuwezesha miradi kutekelezwa kwa wakati kupunguza kudaiwa riba na adhabu na kujenga imani mbele ya macho ya tasnia ya wakandarasi na wazabuni.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati inaishauri Wizara kuzisimamia taasisi zake kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake yote kwa ufanisi. Kamati inaamini kwamba, iwapo kutakuwepo na usimamizi madhubuti, taasisi hizo zitaweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na wakati huo huo zitaongeza tija na hatimaye kuboresha huduma za Ujenzi na kuongeza mapato ya Serikali.

### 4.2 Maoni Mahsusi

#### 4.2.1 Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali, kufanya tathmini juu ya uwezo wa Wakala huu kujiendesha bila kutegemea ruzuku ya Serikali. Moja kati ya jitihada za msingi kufanyika, ni kuipa TBA mtaji wa kutosha, angalau **Sh. Bilioni 50** ili Wakala huo uanze kufanya uwekezaji mkubwa zaidi ambao

utazalisha faida, na pia kushirikiana na Sekta Binafsi. Aidha, Wakala uruhusiwe kujenga, kuuza na kupangisha nyumba zake kibiashara ili ipate mtaji wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kubuni Mfumo mpya na rahisi utakaoiwezesha TBA kukusanya madeni, na iwapo taasisi za Serikali na wapangaji wengine watachelewa kulipa, mfumo huo uweze kutoza riba ya ucheleweshaji. Aidha, kwa taasisi za Serikali ambazo zinalipia Watumishi wake nyumba, na hawajalipa, basi TBA ichukue hatua stahiki ikiwemo kuwaondoa wadaiwa hao kwa kuwa mahitaji ya nyumba kwa Watumishi wa Serikali bado ni makubwa.

4.2.2 **Matumizi ya Hifadhi ya Barabara**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, kwa mujibu wa sheria za nchi, hifadhi ya barabara za TANROADS inaweza kutumika kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo sio za kudumu. Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

a) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria zilizopo kuhusu fursa ya matumizi sahihi ya hifadhi ya barabara kwa shughuli za kiuchumi;

b) Kubainisha maeneo yenye mvuto wa kibiashara na kuyatangaza kwa umma ili yatumike kwa masharti maalum; na

c) Kuweka mifumo thabiti ya kukusanya fedha zitokanazo na matumizi ya hifadhi hiyo kwa viwango shindani kibiashara.

**4.2.3 Serikali Kulipa Madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, Serikali imekuwa ikisua sua katika kulipa madai na madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri katika miradi mbalimbali

ikiwemo ujenzi wa barabara, ujenzi wa vivuko. Kwa Serikali kutolipa madeni hayo, kwanza kunakwamisha jitihada za kuwawezesha kiuchumi wananchi ambao wanapata changamoto ya marejesho ya mikopo katika taasisi za kifedha, lakini pia kunaathiri mzunguko wa fedha nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sababu hizo, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati madhubuti na wa kudumu ili kulipa madeni kwa wakati lakini pia kuwajengea uwezo wakandarasi wa ndani ili watekeleze miradi mingi zaidi.

**4.2.4 Fidia kwa Wananchi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, baadhi ya wananchi katika maeneo mbalimbali nchini ambao waliachia maeneo yao ili kupisha miradi inayosimamiwa na Wizara ya Ujenzi bado hawajalipwa fidia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, wananchi wote wanaodai fidia, walipwe stahiki zao kwa mujibu wa sheria na iwapo Serikali haina uwezo wa kulipa fidia katika maeneo waliyotwaa, maeneo hayo yarejeshwe kwa wananchi.

**4.2.5 Mkakati wa Kuondoa Matuta Ambayo si ya Lazima**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, Serikali katika kudhibiti mwendokasi wa madereva imeweka matuta katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, Serikali ifanye tathmini ili kubainisha maeneo ambayo hakuna umuhimu wa kuwepo matuta na iwapo maeneo hayo yana matuta, basi yaondolewe. Ushauri huu umejengwa katika misingi kwamba, uwepo wa matuta una athari hasi za kiuchumi kwa watumiaji wa magari. Hata hivyo, kwa yale maeneo ambayo kuna ulazima wa matuta kuwepo, matuta hayo yawe na viwango stahiki na vinavyolingana nchi nzima.

**4.2.6 Mkakati wa Kujenga Mizani Inayopima Magari Yakiwa Katika Mwendo**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuendelea kukabiliana na changamoto ya uzito wa magari uliopitiliza na ambao unaharibu barabara nchini, Kamati inashauri kwamba, pamoja na vituo vya mizani vilivyopo, Serikali pia ijenge Mizani inayopima magari yakiwa katika mwendo. Hatua hii itaongeza jitihada za Serikali kudhibiti uzito wa magari maeneo mengi zaidi nchini.

**4.2.7 Ujenzi wa barabara za mwendo wa haraka *(Express Ways)***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kushauri kwamba, ili kukabiliana na changamoto za msongamano wa magari hususan katika barabara zinazoingia miji mikubwa nchini, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ibuni miradi ya ujenzi ya barabara za mwendo wa haraka *(express ways)*. Aidha, Serikali inashauriwa kujenga barabara hizo kwa kushirikiana na sekta binafsi (PPP) na kuweka tozo za matumizi yake *(road tolls)*.

**4.2.8 Ujenzi wa Barabara kwa Utaratibu wa EPC + F**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Kamati imebaini kwamba miradi iliyopaswa kutekelezwa kwa utaratibu wa EPC + F haijatekelezwa kabisa, Serikali ifanye tathmini kuhusu utaratibu huo kuona iwapo una tija.

**4.2.9 Maboresho ya Utendaji wa TEMESA**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kamati imebaini kwamba, pamoja na kwamba Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) inatoa huduma za matengenezo ya magari ya Serikali, wakala huo unakosa ufanisi kwa sababu ya kuwepo kwa changamoto ya madai na madeni. Kwa muktadha huo, Kamati inashauri kwamba, Serikali ibuni Mfumo wa Kielektroniki ambao utaweka utaratibu kwamba, baada ya gari la umma kubainika kuwa na tatizo la kiufundi *(diagnosis)*, taarifa zake zitumwe katika taasisi husika na gharama za matengenezo yake, na gari hiyo

isitengenezwe hadi hapo taasisi husika itakuwa imekamilisha malipo.

#### 4.2.10 Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Ujenzi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Jijini Dar es Salaam. Pamoja na hayo, Serikali inashauriwa kuharakisha mradi huo na kuboresha miundombinu inayozunguka mradi huo hasa mifereji ya maji ili kuepuka changamoto zinazowakabili watumiaji wa barabara wakati ujenzi huo unaendelea.

#### 4.2.11 Kutunisha Mfuko wa Barabara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, uwezo wa Mfuko wa Barabara kukarabati barabara nchini ni mdogo ukilinganisha na mahitaji halisi kama ambavyo taarifa hii imefafanua hapo awali. Aidha, kwa kuwa mahitaji ya ukarabati wa barabara nchini yanaongezeka, Kamati inashauri Serikali itafute vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitawezesha Mfuko wa Barabara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, namshukuru Naibu Spika, kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha kwa ufanisi Vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako tukufu. Kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. | **Makamu** |
| 3. | Mhe. Kapt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb. | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb. | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako Mb. | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Livingstone Jpseph Lusinde, Mb. | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb. | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Mwatumu Dau Haji, Mb. | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Ujenzi, Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, (Mb) kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhe. Mhandisi Godfrey Msongwe Kasekenya (Mb).

Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa

Wizara hiyo, Balozi Mhandisi Aisha Amour. Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya Ujenzi na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

5.2 **Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu**
29 Mei, 2024

**SPIKA:** Mwenyekiti, ahsante sana kwa mawasilisho hayo ya maoni ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina hapa ya Wabunge walioomba kuchangia hoja hii. Majina ni mengi kuliko muda tulionao na hata wengine kwa kesho pia muda bado unahitajika mrefu zaidi kuliko idadi ya Wabunge walioomba kuchangia. Kwa hivyo tutapunguza dakika kidogo ili kila Mbunge anayehitaji kuchangia kwenye hoja hii apate nafasi, Wabunge mtachangia kwa dakika nane badala ya dakika kumi.

Tutaanza na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia asubuhi ya leo kwenye mada muhimu kabisa ya maendeleo ya Taifa leo. Kwanza kabisa nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Kamati kwa uchambuzi mzuri wa bajeti yetu na kipekee sana kwa uzalendo ambao Mheshimiwa Waziri anauonesha kwa maslahi mapana ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Mheshimiwa Rais kutengeneza Wizara mbili kutoka kwenye Wizara iliyokuwa ya Uchukuzi na Ujenzi na hivi kufanya Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Ujenzi maana ya kuwa na hizi Wizara mbili ililenga kuleta ufanisi wa sekta hizo mbili ya uchukuzi na sekta ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kumteua Mheshimiwa Bashungwa Innocent kuwa Waziri wa sekta hii kumelenga kuongeza ufanisi zaidi. Kwa sababu Waziri huyu ni moja kati ya Mawaziri wengi wazalendo wa kweli wa nchi yetu. Sisi Wanamadaba na Wanaruvuma kwa ujumla wetu tulipoona uteuzi huu tulirejesha matumaini na imani yetu kubwa kwamba changamoto kubwa za barabara ambazo tunazo ndani ya Mkoa wa Ruvuma sasa zitapata ufumbuzi, kwa maana zitawekewa kipaumbele na hatimaye zitajengwa kwa ubora. Kwa hiyo, matumaini hayo bado tunayo na ndiyo maana asubuhi hii nimesimama kwa sababu ninaamini kwamba haya tunayo ikumbusha Serikali itayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bashungwa amepata fursa ya kutembelea Jimbo langu la Madaba, amesimama Lilondo, amezungumza na Wajasiriamali na Wananchi wa Madaba, amesikia changamoto za barabara ya Makambako kuelekea Songea yenye urefu wa kilometa 296. Barabara hii imezungumzwa kwa miaka mingi sana. Ilijengwa na uongozi wa Awamu ya Pili ya Nchi yetu. Barabara imebomoka vibaya, barabara ina makorongo, barabara inahatarisha watumiaji wa magari na watumiaji wa miguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumelizungumza sana humu Bungeni na pengine watu wengi wamechoka kulizungumza na wengine

humu ndani wamechoka kulisikiliza, lakini sijachoka kwa sababu nyuma yangu wapo Watanzania, wapo Wanamadaba, wapo Wanaruvuma ambao wanaitegemea barabara hii kwa ajili ya uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukipita Barabara ya Makambako – Songea kikubwa utakachopishana nacho ni malori yenye ujazo mzito sana, ujazo mkubwa sana wa makaa ya mawe. Nilisema ramani ya nchi yetu imebadilika, sasa malighafi nyingi kwa maana ya viwandani hasa makaa ya mawe yanatoka Mkoa wa Ruvuma. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Tanzania lakini kwa uchumi wa Wanaruvuma. Wanaruvuma tutasubiri hadi lini barabara hii ijengwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa majuzi barabara inayotoka Dar es Salaam kuelekea Mikoa ya Lindi na Mtwara ilijifunga lakini barabara iliyowasaidia watu wa Mkoa wa Lindi na Mtwara ni Barabara ya Makambo – Songea. Barabara hii pia inahusu ulinzi wa nchi yetu, mnajua Mikoa ya Kusini tunapakana na nchi mbili muhimu sana ya Msumbiji na Malawi. Tunahitaji barabara bora, barabara imara na barabara nzuri ambayo itachangia uchumi na ulinzi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pembezoni mwa barabara hii wapo wananchi wengi ambao nyumba zao zimewekwa *X* muda mrefu wameahidiwa watalipwa fidia wengine mpaka wamemaliza uhai wao hawajaona hiyo fidia. Kamati imesema hapa tunachelewa sana kuwalipa fidia wananchi ambao wapo pembezoni mwa miradi ambayo tunaijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipojenga barabara hii tutakuwa hatujawasaidia Wanaruvuma, barabara hii ina kipande cha *by pass* pale Songea Mjini, kinaanzia maeneo ya Songea Mjini lakini kinakuja Msamala, kinatokea Msamala na kinakuja na eneo ambalo tulisema tutalijenga mpaka hapa Lutukira kilometa 120 mpaka leo miaka mitatu tunazungumza hapa Bungeni, tumeambiwa fedha ipo lakini eneo hili halijengwi. Mheshimiwa Waziri ninaomba utakaposimama tafadhali naomba ulisemee, useme *commitment* ya Serikali kuhusu Barabara ya Makambako –

Songea, kuhusu kuwalipa fidia Watanzania wa Madaba, vijiji vyote ambao wanapitiwa na mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tuna barabara muhimu sana ya uchumi wa nchi yetu ambayo inatoka Mkiu kuelekea Madaba ni kilometa chache tu, lakini mradi huu ndiyo unaotupeleka kule ambako tunaenda kuchimba chuma, kule ambako kuna makaa ya mawe. Tunavyoongea Liganga na Mchuchuma barabara ambayo itatumika ni hii ya Madaba – Mkiu. Barabara hii miaka mingi ipo kwenye Ilani ya Chama chetu Cha Mapinduzi. Mheshimiwa Bashungwa ninamwamini sana, yeye ni mmoja kati ya Mawaziri wazalendo sana nao wajua mimi, ninaamini *this time* barabara hii itapata fedha na itajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nisingependa nikukwaze naomba nihimishe hotuba yangu kwa kurejea shukrani zangu kwa Serikali na imani yangu kwa Serikali hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipatia muda, lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu na naomba nimpongeze sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyochapa kazi kuwatumikia Watanzania. Vilevile, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Waziri Bashungwa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yake yote ambayo wamekuwa na kipindi kigumu sana, lakini wamefanya kazi kwa jitihada sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nitachangia vipengele vitatu. Kwanza nitaongelea mafanikio ya Rais Samia Suluhu Hassan upande wa miundombinu kwa kipindi cha miaka mitatu. Pia nitazungumzia maafa, athari za mvua ya *El-Nino* kwenye miundombinu ya nchi hii, lakini nitamalizia kuongelea Barabara ya Mkomazi – Kisiwani - Same. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze mchango kwa kuzungumzia mafanikio ya Awamu ya Sita. Rais Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani tarehe 19/03/2021, kipindi alipoingia mtandao wa barabara za lami ulikuwa kilometa 10,830.2 kufikia Machi, 2024 mtandao wa lami umeongezeka na kufikia kilometa 12,028.7 sawa na ongezeko la kilometa 1,198.5. Hiki ni kiwango kikubwa sana, ikumbukwe kwamba hapa Afrika Mashariki kuna nchi ambazo zina chini ya kilometa 600 kwa nchi nzima. Kwa hiyo, tujue kwamba Rais amefanya kazi kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madaraja mapya nane yamekamilika kujengwa. Kuna Daraja la Wami – Pwani, Msingi – Singida, Gerezani – Dar es salaam, Tanzanite – Dar es Salaam, Kiegea – Morogoro, Mpwapwa – Dodoma, Ruhuhu – Ruvuma na Kitengule – Kagera. Upande wa mafanikio upande wa viwanja vya ndege, Viwanja vya Ndege vilivyokamilika kuna Geita, Mwanza, Songwe Mtwara na Songea. Haya ni mafaniko makubwa kwa kipindi cha miaka mitatu na haya ni kwa uchache wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije niongelee maafa ambayo yamelikuta Taifa letu. Nitoe pole za dhati tena kwa unyenyevu sana kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nitoe pole kwa wananchi wote wa Tanzania, kwa sababu kama ni maafa kipindi hiki kweli tumepatikana sana, lakini tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa yote ndugu zangu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiri Serikali ilipambana sana kujenga barabara, Serikali ilipambana sana kujenga madaraja, lakini athari za mvua ya *Eli Nino* kwenye miundombinu ya barabara na madaraja, lazima tukubali kwamba ni kubwa sana. Sasa tuangalie takribani mikoa yote ya nchi yetu ya Tanzania iliguswa ni kweli kuna Mikoa ambayo iliguswa zaidi. Tukienda Manyara, madaraja, barabara lakini na wananchi wengi tuliwapoteza. Naomba kwa dhati kabisa nitoe pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara lakini na wananchi wa Manyara na Hanang. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2024, Serikali ilikuwa inahitaji takribani shilingi bilioni 986 ili iweze kurejesha

miundombinu yote hiyo irudi kama awali. Vilevile, kuna Kimbunga Hidaya na chenyewe katika Mkoa wa Lindi ambacho hapa Serikali inahitaji takribani shilingi bilioni 84.15, ni kiasi gani Watanzania waone kwamba kipindi hiki tumepata tabu, lakini tuone pia kwamba Serikali imekutwa na matatizo makubwa kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali kwamba, imeweza kutanguliza bilioni 66 kwa ajili ya kurekebisha hizi barabara. Mimi kama Mbunge wa Same Mashariki niishukuru Serikali kwamba, katika bilioni 66 na mimi nimepata bilioni 1.68 za kurekebisha Barabara yangu ya Mwembe - Mbaga mpaka Ndungu naishukuru Serikali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie Barabara yangu ya Mkomazi – Kisiwani Same. Kwanza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi mpokee shukrani kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Same Mashariki lakini nianzie Kata ya Mkomazi, nije Kata ya Bendera, nije Kata ya Kihurio, Kalema, Ndungu, Maore, Kisiwani mpaka Same, wote wanaishukuru Serikali sana kwa kuamua kwamba, sasa hii barabara inawekwa lami yote kwa sababu malalamiko yameanza mwaka 2000 nilipoingia Bungeni hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie wananchi wangu wanisikilize vizuri, naondoka Bungeni Jumamosi hii, kwenda kuwaeleza kwa nini kilomita tano pale Mroyo zinasusua? Mimi ndiye ninayefahamu kwa nini zinasuasua, nipo Kamati ya Miundombinu, wananchi watulie, Jumamosi naingia Jimboni nitawaeleza na watanielewa, wasisikilize mtu mwingine, mimi ndiye Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumpongeza Rais, Waziri, Katibu Mkuu na wote ambao wapo kwenye Wizara ya Ujenzi, tunawashukuru sana kwa sababu wameonesha jitihada na kupambana sana, kuokoa maisha ya barabara na wananchi katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, ajiandae.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Awali ya yote napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anapambana kwa ajili ya nchi yetu na kazi nyingi ambazo anafanya kwa maono makubwa na dhamira ya dhati ambayo anayo kwetu wananchi wa Iringa na Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na kikosi kizima cha Wizara ya Ujenzi kwa namna ambavyo wanapambana. Sote tumeona jinsi ambavyo mvua zimeharibu miundombinu kwa mwaka huu, lakini tumeona wamehangaika usiku na mchana kuhakikisha kwamba, huduma zinarejea kwa wananchi. Kwa hiyo, tunawapongeza sana na tunawatia moyo kwamba tunayo imani na tunayo matarajio makubwa na nyinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Iringa tumepokea miradi mingi ya maendeleo katika Wizara ya Ujenzi. Barabara ya Ipogolo – Kilolo kilomita 63 tumepokea, zimetolewa bilioni 63 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo na Mkandarasi tayari yupo kazini na kazi inaendelea kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Mlima Kitonga; kutokana na maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam, barabara ya Mlima Kitonga ilikuwa haipitiki, magari ya mizigo yalikuwa ni mengi na kulikuwa kuna msongamano mkubwa, barabara tulikuwa tunashuka kwa nusu saa, lakini tulikuwa tunatumia zaidi ya masaa manne hadi matano kushuka na kupanda kwenye Mlima Kitonga. Tunaishukuru Serikali imetupatia bilioni 6.5 kwa ajili ya kufanya marekebisho kwenye kona kali katika Mlima Kitonga.

Upembuzi yakinifu unaendelea ili tuweze kupata barabara bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali pia imetupatia Barabara ya Iringa- Pawaga kilomita 20 na kwa sasa wapo katika mchakato wa kutafuta mkandarasi ili ujenzi uanze katika barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo makubwa na mazuri ambayo yanafanyika, lakini Mkoa wa Iringa tuna changamoto. Barabara ya Ihemi – Usukami. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, barabara hiyo haipitiki ina mashimo, wananchi wanalalamika, kwa hiyo tunaomba Waziri atusaidie atufanyie marekebisho ya kawaida ili wananchi waweze kupita na waweze kupata huduma zao za kila siku.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye ziara Mkoa wa Iringa alitupatia ahadi ya kutujengea Barabara ya lami Kinanyambo A – Madibila kilomita 10. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakaposimama tunaomba atuambie amefikia wapi katika kufanyia kazi ahadi ya Mheshimiwa Rais ili wananchi wa Jimbo la Mufindi Kaskazini waweze kusikia na waweze kupata matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri tunajua kwamba wanafanya kazi kubwa na tuna imani kubwa, lakini kuna vitu vinakatisha tamaa. Mnamo mwaka 2022 tulisaini mkataba wa barabara ya Mafinga - Mgololo na mkandarasi alikabidhiwa *site,* wote tulifurahi na tukawa na amani kwamba tunaenda kupata barabara hiyo. Sasa ni mwaka mmoja hamna kitu chochote kinaendelea barabara ni mbaya haipitiki, wananchi wanateseka, yaani Mheshimiwa Waziri sijui nimwambieje! Ile barabara ya Mufindi ndiyo tunaitegemea kwa ajili ya uchumi wetu Wilaya ya Mufindi, sasa hivi wananchi wanateseka mizigo haipitiki, kwa hiyo tunaomba akisimama atuambie ni lini atamlipa mkandarasi *advance payment* ili aweze kuendelea na kazi katika barabara hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto katika Wizara ya Ujenzi na changamoto yenyewe ni madeni ya wakandarasi ambayo yanapelekea riba kwa Serikali. Haya madeni ya wakandarasi yanaongezeka mwaka hadi mwaka, wanaolipwa haya madeni ni wakandarasi wa nje. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 tumelipa riba ya bilioni 36.8, Mwaka wa Fedha 2022/2023 tumelipa riba ya bilioni 44.4, Mheshimiwa Waziri watuambie wenyewe wanafikiria nini, kwamba ni kawaida, mazoea au wanaona kwamba ni kitu cha kawaida na ni sawa, hawajui kama tuna uhitaji wa hizo fedha na tuna matatizo mengi tunahitaji hizo fedha kwa ajili ya kutatua matatizo ya Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba na bajeti hii muhimu sana kwa maendeleo na kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya, miradi yote mikubwa ambayo Mheshimiwa Rais aliikuta wakati anaingia haijasimama na inaendelea vizuri. Kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais, Serikali na Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye zoezi la kurejesha miundombinu kwa sababu ya athari za mafuriko ambazo zilitokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, mimi kama Timotheo Mnzava sina ugomvi na ndugu yangu Innocent Bashungwa. Mimi kama Mbunge wa Korogwe Vijijini, sina ugomvi na Waziri wa Ujenzi, nataka nimfahamishe wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini na wananchi wa Jimbo la Bumbuli wana ugomvi na Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ugomvi wenyewe unatoka wapi? Tunayo Barabara ya kutoka Soni kwenda Bumbuli - Dindira - Korogwe, barabara ya kilomita 74 kwa mara ya kwanza ilitamkwa na kuahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010, ukisoma ukurasa wa 76 unakutana na ahadi ya ujenzi wa hii barabara kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuliihuisha mwaka 2015 kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ukurasa wa 49, tumeweka ahadi ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hatukuishia hapo, kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 tumeisema tena na Chama Cha Mapinduzi kiliahidi kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, nina Vitabu vya Bajeti ya Wizara hii kwa miaka mitano iliyopita. Bajeti ya mwaka 2019/2020, Serikali ilituahidi kwamba inatenga fedha kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya lami. Bajeti ya mwaka 2020/2021, Serikali iliahidi humu Bungeni kwamba, kuhusu hii Barabara ya Soni – Bumbuli kwa mwaka huu mradi umetengewa jumla ya shilingi milioni 840 kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi wa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2021/2022, Serikali ikaliambia Bunge kwamba, kuhusu Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe katika huu mwaka wa fedha wametenga shilingi milioni 924 kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Bajeti ya Mwaka 2022/2023, Serikali ikaliambia Bunge kwamba, kwenye hii barabara wametenga bilioni moja kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Bajeti inayoisha mwezi wa Sita mwaka huu, bajeti ya mwaka 2023/2024, Serikali ilituambia humu ndani na ikawaahidi wananchi wa Jimbo la Korogwe kwamba, barabara hii naomba niinukuu hotuba ya Waziri wa wakati huo.

*"Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe kilomita*

*74, ipo katika hatua za mwisho. Zabuni kwa ajili ya kazi ya ujenzi zinatarajiwa kutangazwa kabla ya mwezi Julai, 2023".*

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa ni hotuba ya Waziri. Haikuishia hapo kwenye hii bajeti hapa alikuwa anaeleza utekelezaji wa Bajeti ya 2022/2023. Kwenye bajeti hiyo ya mwaka 2023/2024 Mheshimiwa Waziri alisema: *"Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya shilingi 3,500,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami".*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimesema nimeangalia bajeti ya miaka mitano? Mheshimiwa Waziri nimesoma hotuba ya Waziri aliyoiwasilisha leo na nasema kabisa katika Mawaziri wanyenyekevu na wasikivu sina shaka kabisa na Mheshimiwa Bashungwa, lakini inawezekana Wizarani na kwenye taasisi zako kuna shida. Mheshimiwa Waziri nimesoma hapa kitabu chake na amesema vizuri kwamba: *"Mradi wa Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe kilomita 74. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya shilingi 3,200,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Sehemu ya Soni – Bumbuli – Funta kilomita 30 na Kwameta - Kwashemshi kilomita 10. Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Old Korogwe – Kwamndolwa – Magoma - Mashoa – Bombo Mtoni"*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa hata hiki kilichoandikwa humu sina imani nacho, kama kwa miaka mitano tunaambiwa fedha imetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi. Miaka mitano imekwisha hakuna hata nusu kilomita ya lami ambayo imejengwa. Leo kwenye kitabu hiki Mheshimiwa Waziri anasema ametenga tena fedha na anaanza kilomita 30 upande wa Bumbuli, kilomita 10 upande wa Korogwe, sina shida na hilo, lakini najua mpaka kupata kibali cha kutangaza kazi ni mchakato mrefu. Hizi kilomita 10 wanazosema hofu yangu mimi nimeambiwa jana na watu wake wakati nafuatilia kwamba eti, wameshapata kibali cha kutangaza hizi kilomita 30, lakini hizi kilomita 10 ndiyo wanaanza mchakato, mchakato huu utaisha lini?

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Korogwe na Bumbuli ni wamoja, yapo mambo ambayo tulikaa na Mheshimiwa Waziri,

mimi yeye na Mheshimiwa Mbunge wa Bumbuli tukakubaliana, lakini inavyoonekana wataalam wake hawataki kukubali kile sisi na yeye tulichokubaliana. Sasa, kama Waziri tunakubaliana na yeye jambo, wataalam wake hawako tayari, inanipa mashaka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kabisa katika bajeti ambayo sitaunga mkono mpaka nipate majibu ya jambo hili ni bajeti hii. Sitangazi kuunga mkono bajeti hii mpaka nimsikie Waziri anasema nini juu ya barabara hii, watu wa Korogwe na Bumbuli wameteseka muda mrefu, ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi, chama kikiahidi kazi yenu Serikali ni kwenda kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, nipate majibu ya jambo hili limekaaje, linakwendaje na hatma yake ni nini, vinginevyo kwenye bajeti hii sitaunga mkono kwa maslahi mapana ya wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo Mheshimiwa Halima James Mdee, ajiandae.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Bashungwa. Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kipenzi cha Watanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuweza kutupatia shilingi 153,500,000,000 kwa ajili ya kujenga Barabara ya kutoka Lusahunga – Rusumo yenye urefu wa kilomita 92 kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Ngara na Biharamulo kwa ndugu yangu Chiwelesa tumekuwa tukitegemea sana barabara hii kwenye uzalishaji, usafirishaji wa bidhaa na wananchi kutoka kwenye Wilaya zetu zilizopo pembezoni mwa nchi, kuja Makao Makuu ya Nchi, Dkt. Samia Suluhu Hassan

ameonesha mapenzi makubwa kwetu, sisi wananchi wa Kagera, Ngara na Biharamulo, kwa kweli tunamshukuru mama yetu kwa kuidhinisha fedha hizi na mkandarasi yupo *site* na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kabla sijaendelea nimpe maua yake Waziri wa Ujenzi, kaka yangu Mheshimiwa Innocent Bashungwa, ndugu zangu nyote ni mashuhuda wakati wa kipindi cha mvua za *El-Nino,* wameshuhudia namna ambavyo Bashungwa anachakarika anakimbia huku na kule, tumemwona kwenye mitumbwi na yeye kama vile tayari ni Mkandarasi, anajenga barabara. Mheshimiwa Bashungwa utendaji kazi wake tumeuona, hauna mashaka, kwa kweli tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie katika kipindi hiki cha mvua nyingi zilizopita amejitengenezea umaarufu na utendaji kazi wake tumeushuhudia, hongera sana kwake, asirudi nyuma aendelee, sisi tupo pamoja na yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nina mambo ya kuzungumzia, ninayo barabara ambayo iliingizwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi mwaka 2015, barabara yenyewe inaitwa Murugarama – Rulenge – Kumbuga – Murusagamba – Tembo Nickel. Barabara hii imeingizwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi mwaka 2015. Mwaka 2021 kwenye hotuba ya Waziri hapa Bungeni nilitengewa shilingi 1,500,000,000. Mwaka 2022 shilingi 3,000,000,000, mwaka 2023 shilingi 3,000,000,000. Sasa hivi tena nimetengewa shilingi 3,000,000,000 lakini barabara haijaanza kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilio walichonacho wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Mnzava Korogwe huko ndicho kilio walichonacho wananchi wa Tarafa za Rulenge na Murusagamba huko Wilayani Ngara.

Mheshimiwa Spika, alikuja Naibu Waziri Mheshimiwa Kasekenya tukawaahidi wananchi kwamba mwaka unaofuatia tunakwenda kuanza kujenga hiyo barabara. Unajua hizi ahadi

ambazo hazitekelezeki kuna muda tukikutana na Kasekenya mlangoni anatamani kunikimbia ajifiche, kwa sababu ni ahadi sugu za muda mrefu, zimeshamkaa mpaka moyoni, amezoea matatizo kiasi ambacho akikutana na Wabunge anatamani kutukimbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachokitaka tunaomba utusaidie hii Wizara ya Ujenzi wanatakiwa kutimiza ahadi ambazo zipo kwenye Ilani hazijatekelezwa za muda mrefu. Wabunge tunaumia tunapoona kwamba, tumeahidi wananchi ahadi hazitekelezwi kwa wakati. Niseme kabisa Kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa kama hutasema neno lolote kwenye hii barabara ambalo ni ahadi ya muda mrefu na ni siasa kubwa sana kwa Ngara, nami sitangazi kuunga mkono hii bajeti mpaka nisikie ni lini mkandarasi ataanza ujenzi wa hii barabara kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bashungwa kuna suala la fidia, wananchi wamefanyiwa tathmini pale muda mrefu sana. Nimekuwa nikifuatilia kutoka mwaka jana lakini fidia haijalipwa mpaka dakika hii. Kutoka Nyakahura wananchi wa Mheshimiwa Ezra Chiwelesa na wao wanalamika wakiona gari ya Mheshimiwa Ruhoro *V8* inapeperusha bendera wananiuliza na mimi fidia yetu lini? Tunaomba Mheshimiwa Bashungwa hawa wananchi walipwe fidia, vilevile tunaomba wananchi wa Ngara walipwe fidia na hii barabara ianze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kuna tatizo *TEMESA*. *TEMESA* wameanza kujenga kivuko cha kutoka Kanyinya kwenda Mayenzi kutokea mwaka 2021. Kivuko chenyewe wanachokijenga thamani yake haizidi milioni 200. Kila mwaka wana visingizio, tena wanapoona mvua imenyesha wanasingizia kumejaa maji hawataki kwenda *site*. Nimeenda *TEMESA* kuwafuata mimi mwenyewe zaidi ya mara 15, Wakurugenzi *TEMESA* wamebadilika hawatekelezi, wameleta vifaa pale wamevitelekeza *site*.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Bashungwa sema neno kwenye Kivuko cha Kanyinya kwenda Mayenzi, kwa sababu wananchi wamesubiria sana na ni muda mrefu, ahadi hizi Mheshimiwa Bashungwa zinatakiwa zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, wakati nasubiri Mheshimiwa Waziri atatamka nini kwenye barabara hii ya muda mrefu, maeneo mengine naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi na mimi kuchangia katika Wizara yetu ya Ujenzi. Kwa nafasi ya pekee nimpongeze sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri ambayo inafanyika katika ujenzi wa miundombinu ya barabara zetu na ile yote ambayo inasimamiwa na Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa nimpongeze Ndugu yangu na jirani yangu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa kazi nzuri anayoifanya akisaidiwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Injinia Godfrey Kasekenya pia na Katibu Mkuu wetu Balozi Aisha Amour na Naibu Katibu Mkuu Ndugu yetu Ludovick Nduhiye, pia Bodi ya Barabara ambayo inaongozwa na Injinia mzoefu wa barabara, Injinia Joseph Nyamhanga kwa kazi nzuri wanayoifanya kuisimamia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mahususi ninampongeza sana Mheshimiwa Bashungwa, lakini ninawapa pole kwa majanga ya barabara kipindi cha mvua. Alisimama kidete usiku na mchana, hakulala ndani na sisi tulikuwa tunashangaa. Wakati ule wengine asubuhi tunakuta barabara imeoshwa, kesho tunakuta barabara imerudi. Tunakupongeza sana kwa hiyo nguvu akisaidiana na Naibu Waziri, lakini na watendaji wote wa Wizara kwa umahiri walioonesha katika kipindi cha majanga kwani waliweza kukabili na tukarudi katika hali ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Missenyi wanaendelea kuipongeza Wizara hii katika maeneo ya barabara zote zinazosimamiwa na *TANROADS*. Tunazo takribani barabara saba ambazo kwa kweli zimeendelea kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara na zinapitika, japo kuna baadhi ambazo zina

changamoto na hiyo nitakuja kuisema hapa ili tuweze kupata ufumbuzi. Tunatoa shukrani za dhati kwa sababu barabara hizo zimekuwa katika kiwango kizuri na ninampongeza sana *Engineer* wetu wa Mkoa, *Engineer* Nturi pamoja na wasaidizi wake ndani ya mkoa wetu. Wanafanya kazi nzuri na tunasikilizana tunashauriana na ndiyo maana mambo mengi yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Wilaya ya Missenyi pamoja na changamoto zilizopo, lakini tunashukuru kidogo tunachokipata na kuomba zaidi. Tunayo Barabara ya kutoka Katoma – Gera – Kanyigo – Kashenye – Bukwali. Hii ni barabara ambayo inatuunganisha na nchi ya jirani ya Uganda. Hii barabara kila mara nikisimama hapa nimekuwa nikiiongelea. Barabara hiyo nimekuwa nikisema mpaka leo miaka 10 imefikiwa kiwango cha kilometa saba za ujenzi wa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni shida kutengeneza barabara hiyo kwa mita 200, 300, 400 au 500, lakini kwa kilio cha muda mrefu ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Wizara hii. Kwa sasa wameanza kufanya usanifu wa barabara hiyo. Mwanzo wa usanifu ukikamilika maana yake tunategemea iingizwe kwenye bajeti, basi kipande kilichobaki takribani kilometa 29 – 30 ziweze kuingizwa kwenye bajeti na barabara hiyo ijengwe kwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizo ni pongezi kubwa kwa Wanamissenyi hasa hizo kata ambazo zinapitiwa na barabara hiyo. Ninaomba Mheshimiwa Waziri *spirit* hiyo sasa iendelee ili Wanakagera, Wanakanyigo, Wanakashenye, barabara hiyo ambayo imekuwa ikijengwa kwa muda mrefu ifikie mwisho na barabara ianze kutumika lakini pia ituunganishe na nchi yetu ya jirani ya Uganda.

Mheshimiwa Spika, tuna barabara nyingine ambayo ni Barabara ya Mtukula kwenda Minziro. Hii ni ahadi ya viongozi, imeahidiwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano na tunaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia, Awamu ya Sita. Baada ya kuingia madarakani wameanza kuifumua hii barabara. Kwa sasa imeshafumuliwa kwa kiwango cha kilometa

sita. Barabara yenyewe ni kilometa 15 na hii barabara ni ya usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tukiangalia eneo letu la Minziro, maana yake ni eneo ambalo kwa kweli lilikuwa limefungwa. Kufungua Barabara hii inaiwezesha Minziro na Mtukula sasa kuwa na mawasiliano ya kiuchumi. Kwa hiyo ninaomba katika eneo hili, kwa bajeti ambayo haijatengwa kilometa saba zilizobaki, Mheshimiwa Waziri hapa ni eneo dogo sana lililobaki. Huwezi ukala ng'ombe mzima ukashindwa mkia. Hii barabara ikamilike ili sasa tuingie kwenye kiwango cha pili. Kwa sababu ahadi ni lami, lakini tumeshaifumua kiwango cha changarawe ambapo wananchi wa Mtukula na Minziro wanashukuru sana. Basi tuweze kumalizia katika eneo hilo ili sasa ahadi ya Waheshimiwa Viongozi wetu iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru pia,Serikali kwa Barabara ya *Bunazi Junction* na kwenda *Kagera Sugar* mpaka Daraja la Kitengule. Barabara hiyo ni kilometa 25. Tunaishukuru Serikali yetu kwa upendo mkubwa, barabara hiyo mkataba wa shilingi bilioni 54.9 umesainiwa na barabara hiyo itakuwa ni mkombozi, lakini itahuisha Mji wa Bunazi kwa sababu watumishi wengi ambao wana kipato cha *Kagera Sugar* wanaishi kule kwa sababu ya kuogopa zile kilometa 25 za vumbi.

Mheshimiwa Spika, ikishajengwa kwa kiwango cha lami itasaidia hata kukuza Mji wetu wa Bunazi ambao ni Makao Makuu ya Wilaya. Katika eneo hilo ninakuomba sana sana Mheshimiwa Waziri, kuanzia mwezi Septemba tangu mkataba umesainiwa, mkandarasi ameoneshwa *site,* lakini ameomba *advance payment*; leo ni miezi nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo ambalo kwa kweli ninaomba kwa msisitizo mkubwa. Mkandarasi alipwe hiyo *advance* hii barabara ianze kutengenezwa na wananchi waendelee kuwa na imani na Serikali yetu kama ambavyo inaendelea kufanya kazi nzuri katika eneo hili. Kwa sababu miezi nane mtu anasubiri *advance*, kwa kweli ni kipindi ambacho ni kirefu. Ninaomba kwa usikivu wako na uzalendo wako na utendaji kazi chini ya Serikali

yetu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ninaamini ndani ya muda mfupi kabla mwezi Juni haujakwisha, basi mkandarasi atapata *advance* ili barabara yetu ianze kujengwa na iweze kuhuisha maendeleo na uchumi wa Mji wa Bunazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maeno hayo tunaona katika maeneo ya Barabara yetu ya Minziro, ipo inatengenezwa katika kiwango cha moramu, lakini barabara hiyo imekuwa na changamoto sana. Leo ukiangalia mawasiliano kati ya Makao Makuu ya Wilaya kwenda Minziro yamekatika. Katika kipindi chote barabara ile imejaa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli mkandarasi yuko *site* lakini hawezi kufanya kazi katika eneo hilo. Mheshimiwa Waziri, kwa kazi kama tumeona unaweza kukabiliana na majanga katika maeneo mengine, ninaomba na eneo hili. Kwanza tunatakiwa kuongezewa bajeti katika eneo hilo. Barabara yetu ya kutoka Kasambia kwenda Minziro iweze kuongezewa bajeti inyanyuliwe tuta la juu, iwekewe *culvert* za kutosha, lakini pia ipanuliwe kwa sababu wananchi wetu wanalalamika ukipishana gari moja na nyingine haziwezi kupishana. Ninaamini kwa usimamizi wako katika maeneo hayo tutaweza kufikia vizuri na barabara hii itaweza kurekebishwa na wananchi wetu wa Minziro waweze kupita kwa amani.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana, katika Wilaya ya Missenyi katika miji yetu yote midogo iliyopo, tukiangalia Kyaka, Bunazi ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya na Mtukula, hakuna sehemu yoyote ambayo barabara ni nzuri lakini hakuna taa. Mheshimiwa Waziri, kwa wema wako tulishakuletea maombi na ukasema unayafanyia kazi. Basi ninaomba katika eneo la Mtukula angalau katika mzunguko wa kilometa 2.1.

Mheshimiwa Spika, tulishakaa na Meneja wetu wa *TANROADS, Engineer* Nturi, tukaona kwamba tuna mahitaji ya taa 70. Tumeenda Bunazi katika mzunguko wa kilometa 2.4 tunahitaji taa 80 na Kyaka tunahitaji taa 60 katika eneo la mzunguko wa kilometa 1.8. Kwa hiyo, ninakuomba sana katika maeneo hayo ambayo tumeshayapitia. Sisi Wanamissenyi ambao ni lango la

kutoka nchi ya jirani, basi hata wananchi wakiingia katika eneo hilo waweze kuona kwamba hii tunaingia Tanzania ambayo barabara zetu ni njema, ni nzuri na zimeboreshwa sasa ziendelee kuboreshwa ili kuleta taswira nzuri ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kushukuru katika Barabara yetu ya *TANROADS* ambayo inaunganisha Kyaka – Katoro – Ibwera – Kietema kwa ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza. Tunamshukuru Mheshimiwa Bashungwa, hii barabara ameenda ameikabidhi. Sasa hivi wameanzia kilometa 10 kuanzia upande wa Bukoba Vijijini. Kwa hiyo, tunaendelea kushukuru. Basi tunaomba mkandarasi aendelee na huku upande wa Missenyi itufungue, ikinifungua na mimi. Mheshimiwa Bashungwa anajua kwamba hata Wanakaragwe watakuwa wamefunguliwa ili basi tuweze wakati mwingine wakati tunaenda katika shughuli za kuhemea, tupite katika maeneo ya barabara hiyo na watu wa Karagwe na Missenyi waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima James Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Ninamshauri Mheshimiwa Bashungwa; yeye ni kijana, siku nyingine akiwa anaandika hotuba ajaribu kuepuka ku-*copy* na ku-*paste*. Kuna barabara nyingi sana ameziandika hapo, lakini nyingine zilishakamilika. Kwa hiyo, haina haja ya kutaja sana. Kikubwa ni kuangalia changamoto zilizopo halafu tunaendelea kutoka pale. Hilo la kwanza; muepuke ku-*copyi* na ku-*paste* kwa ku-*assume* kwamba Wabunge hatusomi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, bajeti yake ni shilingi trilioni 1.7 na Bajeti ya Maendeleo trilioni 1.6. Mpaka Machi, ana madeni, madai na fidia shilingi bilioni 913. Katika shilingi trilioni 1.6 za fedha za maendeleo, shilingi trilioni moja ni fedha za ndani na zile shilingi bilioni kama 500 ni fedha za nje. Katika shilingi trilioni moja

ambayo ni ya ndani ni ya uhakika, tunadaiwa shilingi bilioni 913. Tunatokaje hapo? Tunatarajia Bunge liweze kujua tunatokaje hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, riba; amezungumza mdogo wangu ametolea mifano miaka ya fedha iliyopita ambayo tayari zimeshalipwa zaidi ya shilingi bilioni 60. Riba shilingi bilioni 79.5 na riba mara nyingi inatokana na uzembe wa kwetu halafu tuna Wabunge hapa wanaomba kilometa moja, kilometa mbili, wanajadili kilometa saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi shilingi bilioni 150 za kipindi cha miaka mitatu zingejenga kilometa ngapi? Zingejenga kilometa ngapi? Hivi ni kiwango gani ambacho mimi na wewe tunajua? Miradi mingi ya kimkakati nchi hii inajengwa kutokana na mikopo. Kama tunapata fedha za mikopo kwa nini hatutumii kila shilingi vizuri? Kuna shida kubwa kwenye Wizara yako. Sisi tunaompenda tunataka akafumue Wizara aweze kusaidia nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukizungumza riba hapa kwa miaka 10, 15 iliyopita ni *disaster*. Sasa, ninataka aniambie, ana shilingi trilioni moja, ana madeni shilingi bililioni 913, kwenye hotuba yake hakuna popote ametueleza shilingi bilioni 913 itatoka wapi. Riba zita-*generate* na ku-*generate* na ku-*generate*. Mzunguko wa umasikini; hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ninaomba atusaidie kuhusiana na hii kitu ya *EPC + F*. Mtangulizi wake alipigiwa makofi sana mwaka jana kama siyo mwaka juzi. Akatuambia kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi hii tutajenga kilometa 2,035 kwa mkupuo. Tukapiga makofi tukasherehekea, tukasema dunia imekwisha na matatizo yamekwisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, leo, niwakumbushe tena akasema, ngoja ninukuu wasije wakanikamata. Akasema, wakati wanasaini mkataba na *TANROADS* tarehe 16/06/2023 akasema, "kwanza barabara zitatoa ajira 20,300". Pili, Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* akasema, "kuna wakandarasi 129 wameonesha nia. Kati ya hao, wakandarasi wanne wamekidhi vigezo vilivyowekwa." Mwenyekiti

wa Kamati Rafiki yangu Mheshimiwa Kakoso hapa akasema kwamba, "Tanzania inaandika historia ya kujenga barabara kilometa 2,035 kwa pamoja." Halafu akasema, "Hapo awali tulikuwa tunajenga 200 tu mpaka 250 kwa mwaka." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukapiga makofi maisha yakaendelea, mikataba imesainiwa, wakandarasi wako huko. Tunaomba leo watuambie *EPC + F*. Leo ninasoma hotuba yake mdogo wangu, tumekulia wote Kibangu. Yeye ni mdogo wangu ninampenda ndiyo maana ninasema. Serikali, tunaambiwa ukurasa wa 36 *EPC + F*, tunazungumzia mikoa 13. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa Serikali inaendelea na mazungumzo na wafadhili ili kupata fedha za utekelezaji wa miradi hiyo. Ninapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwa dhamira, Serikali itatekeleza miradi hii, wapi na wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa alituambia hapa Bungeni vizuri, akaenda akasaini mikataba vizuri, tena na kampuni za Kichina. Kuna sijui *China Civil Engineering*, *Sinohydro*, *China Overseas Engineering*, *China Railway*; shilingi trilioni 3.7. Tulitarajia leo wanakuja wanatuambia Wabunge tunaomba msamaha. Tulikuwa hatujajipanga, tulikurupuka tukalidanganya Bunge. Tunaenda hivi, wanakuja wanaandika kasentensi kamoja wanajua tumeshasahau maisha yameendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuendesha nchi hivi. Sina shida na wewe nina shida na Serikali hii ambayo kwa pamoja inashindwa kudadavua mambo na kuamua. Kwa sababu tungedadavua mambo na kuleta jambo mezani maana yake tumeshalipika. Hatuwezi kuendesha nchi kwa mazoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TANROADS*; ukisoma taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ama za Kaguzi mbalimbali za Kitaalam, nitanukuu maeneo machache. "*TANROAD* iliingia gharama ya shilingi bilioni 130.5 katika miradi sita." Kwa sababu gani? "Kuna mapungufu

makubwa katika upembuzi yakinifu, dosari katika usanifu, katika usimamizi wa mikataba, kuchelewesha malipo shilingi bilioni 130.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulifanyika Ukaguzi wa Kiufundi na Udhibiti Ubora, ulihusisha miradi nane kati ya mwaka 2009 – 2022. Kati ya miradi nane ya Barabara zilizokaguliwa, miradi saba ilikuwa na upungufu wa usanifu. Tunaambiwa, “Kutokana na hali hiyo, barabara sita kati ya nane ya miradi hiyo zilizokaguliwa zilipata madhara makubwa, hivyo kuharibika kabla ya uhai wake”. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Kilango anatuambia mafuriko na changamoto, tunahitaji shilingi bilioni 900. *I can assure you*; kwa sababu ya ujenzi wa kiwango cha chini ndiyo maana tunadai shilingi bilioni 900. Barabara zingejengwa kwa usanifu wa kina na umakini na uimara, hata mvua ingenyesha kwa kiwango gani *damage* ingekuwa ndogo sana. Tuna shida kubwa *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kwenye eneo la ukaguzi wa ujenzi wa barabara, *TANROADS* na *TARURA* walitumia ziada ya shilingi bilioni 66. Gharama kubwa ilitokana na mabadiliko makubwa ya miundombinu wakati wa utekelezaji. Upembuzi, usanifu ulifanyika kwa kiwango duni; *billions of moneys*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa kiufundi kwenye ujenzi wa barabara Sura ya 14. Tunaambiwa ulihusu barabara tano za *TANROADS*, barabara tano za *TARURA*, ulihusisha miradi ya ujenzi iliyokamilika na inayotarajiwa kukamilika kwa miaka sita ya fedha (mwaka 2016/2017 - 2021/2022). Kwa sababu ya usanifu duni, ilisababisha gharama za ziada za shilingi bilioni 64. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TANROADS* na *TARURA*, usanifu duni. Wabunge hapa wanakaa wanalia, mdogo wangu Mheshimiwa Mnzava pale, miaka 13 anapigwa *sound* ya barabara tu. Upembuzi yakinifu usanifu wa kina, upembuzi yakinifu, ukija kupata barabara ndiyo inajengwa kwa kiwango cha chini. Hii

nchi inayoishi kwa mikopo hamuwezi kuwa *irresponsible* kwa kiwango hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Kiufundi kuhusu udhibiti wa barabara; tathmini ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, ya pili? Niseme tu;

**SPIKA:** Dakika moja malizia.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, kuna hii nyingine inahusu *TANROADS*, shilingi bilioni 182. Tunaambiwa katika barabara zile zote za thamani ya shilingi bilioni 182 ni barabara moja tu ilikuwa imefanyiwa upembuzi yakinifu kwa kina. Halafu tuna watu hapa anaitwa Afisa nani Mtaalamu nani; *we have to change*. Kwa hiyo, Mheshimiwa amekabidhiwa hii Wizara, nilitamani sana tuwe tuna uwezo na uwezo tunao wa kurudi nyuma kwa hao Mawaziri wanaotupiga *sound*, wako hapa wanapelekwa Wizara nyingine, wanatukwepa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, lazima tufike sehemu tusifanye kazi kwa mazoea. Anayesifiwa tumsifie, anayehujumu uchumi twende naye sambamba *bumper to bumper*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi na Mheshimiwa Amina Ali Mzee ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Ujenzi ambayo ndiyo Wizara ya muhimu sana hasa kwa Mkoa wetu wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya, hasa ukiangalia Mkoa wetu wa Dar es Salaam kuna miradi mikubwa ambayo inaendelea. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee kabisa ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Bashungwa kwa wepesi wake wa kazi kubwa ambayo anaifanya, ukizingatia mvua ambazo zimenyesha kipindi hiki. Amekuwa akienda sehemu mbalimbali kuhakikisha kwamba anaweza kurudisha mawasiliano na wananchi wanaweza kupita. Ninampongeza sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara ya Ujenzi kwa kazi kubwa ambayo inaifanya na kwa wepesi ambao wameufanya kwa kipindi hiki ambacho tumeweza kupata madhara makubwa kutokana na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, ninapenda kuishukuru Serikali kwa barabara ambazo zinajengwa katika Jimbo langu la Segerea, ukianza na Barabara ya Bonyokwa – Kimara na Barabara ya Pugu – Kifuru. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri lakini pia ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba tunapata pesa kujenga hizi Barabara ambazo tumekuwa tukiziongelea hapa kwa kipindi cha muda wa miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo kuna mambo machache ambayo nilitaka niyaongee kuhusiana na Jimbo langu la Segerea. Tuna barabara moja ambayo inaitwa Barabara ya Tabata. Barabara ya Tabata ni barabara kubwa na ndiyo barabara ambayo imekuwa ikitumika na maeneo mengi kwa sababu watu wanaotoka Mbezi na Ubungo wanapitia Barabara ya Tabata, lakini pia kwa kuwa na wingi wa watu wanaoishi Jimbo la Segerea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara yetu ya Tabata kwa sasa hivi imekuwa ni barabara nyembamba. Pamoja na kuwa barabara nyembamba nilikuwa nawaomba sana wataalam wetu wa

*TANROADS;* kuna mashimo ambayo wanakwenda kuyaweka. Barabara ni nyembamba halafu pia watu wanakwenda kuchimba mashimo. Mashimo hayo wanaita ni kuziba viraka, lakini wanavyoyachimba yanakaa kwa muda mrefu. Kwa hiyo asubuhi watu wanapokwenda kazini wanakwenda kusubiriana kwenye foleni ili waweze kupishana kwenye mashimo. Kwa hiyo nilikuwa ninaomba Wizara ya Ujenzi, *TANROADS* Dar es Salaam, kama watakuwa bado hawapo tayari kuziba yale mashimo au kuchimba, basi wasubiri kwanza mpaka wanapokuwa tayari ili waweze kuchimba mashimo kuwafanyia wepesi wananchi ili waweze kupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Barabara ya Tabata kama unataka kwenda mjini asubuhi inabidi uamke saa kumi ya usiku kwa sababu foleni ni kubwa na mashimo ni mengi. Ukiachana na mashimo kuna vifusi ambavyo vimewekwa vinakaa muda mrefu havijawezwa kusambazwa. Vifusi hivyo pia vinasababisha ajali za bodaboda na magari. Kama tunavyojua hakuna mtu ambaye anaweza akapitisha gari lake kwenye shimo, kwa hiyo inabidi akae foleni akisubiri ili mwingine aweze kupita ndipo na yeye aweze kupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwamba barabara yenyewe ni nyembamba, kwa hiyo ukisema kwamba uendelee kusubiri, kutokana na muda unaotumika kwenye foleni ndiyo maana watu wanafika ofisini saa tano na wengine wanafika saa nne. Ukizingatia kwamba Mkoa wa Dar es Salaam unaendeshwa na wafanyabiashara pamoja na wafanyakazi, wote wanatakiwa waende kazini kwa wakati ili hata Serikali iweze kupata kodi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni kuhusiana na Wizara ya Ujenzi kwenda kuweka alama ya *X* kwenye nyumba za wakazi wa Tabata. Wameweka alama ya *X* kama miaka miwili iliyopita na hadi sasa hivi wananchi hawajui ni lini Wizara itakwenda kuongea nao kuwaambia kama wana mpango wa kujenga au wameahirisha au inakuwaje. Maana tangu wameweka alama ya *X* hakuna mtu ambaye amekuja kuongea na wale wananchi, kwamba sisi tumewapa muda fulani tutakuja kuongea nanyi ili tujue fidia inakuwaje, ili

sasa wananchi nao wakae kwa mtazamo kwamba wanatarajia kuondoka wakati wowote. Tangu Wizara imeweka alama ya *X* haijawahi kusema kitu chochote.

Mheshimiwa Spika, hili jambo la fidia limekuwa ni jambo gumu sana hasa kwenye Jimbo langu la Segerea ambako kuna watu wengine wanadai fidia. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri anisaidie kuhusiana na jambo la watu wa Tabata, hili jambo lisiwakute kama jambo ambalo liliwakuta watu wa Kipawa. Ninaomba sana kama inawezekana hawa watu wakafutiwe hizo alama za *X* na waambiwe kuwa waendelee na shughuli zao. Ikiwa Serikali inahitaji kuchukua hilo eneo basi wawaambie ili waanze kufanya mjadala na hao wananchi kujua watalipwa fidia kiasi gani na watalipwa lini ili waweze kufahamu kuwa wanaondoka. Ikiwa Serikali haipo tayari basi ninaomba kwa sasa Serikali iwaache wananchi ili waendelee kukaa kwa ajili ya kufanya mambo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuongelea ni kuhusiana na Barabara ya Bonyokwa *External*. Barabara hii ina kilometa mbili. Barabara hii ni muhimu sana. Ninafahamu kuwa wametupatia Barabara hii ya Bonyokwa Kimara yenye kilometa 6.2; lakini barabara hii ambayo ninaiongelea sasa hivi ninaomba nayo waiweke kwenye mpango wa kujengwa kwa sababu ni barabara muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, kwamba *TARURA* wanajenga mita moja moja. Kwa hiyo tunaomba hii barabara ambayo ipo; nafikiri bado ipo *TARURA;* waichukue na kuipeleka *TANROADS* ili iweze kujengwa na kuwawezesha wananchi wa Jimbo la Segerea au Mkoa wa Dar es Salaam kupata sehemu ambazo wanaweza kutokea. Ukiangalia Mkoa wa Dar es Salaam barabara nyingi zinaharibika kwa sababu ya mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii barabara ambayo ninaiongelea ikitengenezwa wananchi wa Bonyokwa watapitia Bonyokwa *External* na wananchi wa Kimara na Mbezi watapitia kwenye barabara hii. Kwa hiyo tunaomba sana tuangaliwe ili barabara hii pia itengenezwe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nilikuwa ninaomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja malizia, muda wako umekwisha.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninaomba, bajeti ya kwetu Mkoa wa Dar es Salaam wametupatia shilingi bilioni 1.7 ukilinganisha na mikoa mingine. Mkoa wetu ni mkubwa na ni mkoa wa kibiashara, hivyo tunaomba tuongezewe bajeti hiyo kwa kuwa bajeti ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Ali Mzee na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ili leo niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka 2024/2025. Bajeti hii inaombewa fedha shilingi trilioni 1.7.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anaifanya ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inapambwa na miundombinu thabiti ya barabara. Sambamba na hilo nimpongeze pia Waziri mwenye dhamana ambaye anafanya kazi vizuri sana. Ninaamini kabisa, kwa kuwa yeye ni kijana Wizara hii imepata mtu ambaye anafanya kazi ipasavyo, ni mwepesi na anakwenda pembe zote za nchi yetu ya Tanzania, akisaidiwa na Naibu Waziri wake kaka yetu Kasekenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze pia mpango wa Serikali wa kujenga barabara kwa mtindo wa *PPP (Public Private Partnership)* na pia *EPC+F (Engineering Procurement Construction + Financing)*. Mpango huu kama utakwenda vizuri nchi yetu

itafunguka vizuri kabisa na changamoto hii ya miundombinu ya barabara itapungua kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende kwenye mchango wangu. Kuna Barabara ya Makambako - Songea, barabara hii inahitaji kufanyiwa ukarabati. Ameiongelea hapa Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, lakini nasema kuna umuhimu wa kuendelea kuisemea; na atakapokuja Mbunge mwingine yoyote anayetoka Mkoa wa Ruvuma ataisemea hii barabara. Kwa hiyo tunaomba sana, tumeelezwa mwaka jana kuwa barabara hii yenye urefu wa kilometa 297, kilometa 100 zinazotoka Songea mpaka kufika pale eneo la Madaba itaanza kufanyiwa ukarabati, lakini mpaka sasa hivi bado barabara hii haijapelekewa fedha ili ianze ukarabati huo. Barabara hii imechimbika sana; yaani kuna mashimo mengine ukisimama yanakufikia kiunoni, kwa hiyo ni hatari, ni hatarishi. Hata wewe mwenyewe itakuweka katika hali ambayo siyo salama pindi unapoenda Mkoa wa Ruvuma kukagua barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana barabara hii iweze kuanza ukarabati mara moja kwa kuwa barabara hii imezongwa na malori mengi, magari ni mengi na kwamba makaa ya mawe ndiyo ambayo yanafanya hii barabara iwe *busy*. Kwa hiyo kutokana na uzito wa mizigo inayobebwa na yale malori kwa kweli mpaka sasa hivi barabara hii siyo himilivu. Kila baada ya mita 200 kuna mashimo, mita 200 mashimo, mita 200 mashimo, kwa hiyo hamna ladha ya barabara ya lami tena, hii ni shida. Kwa hiyo tunaomba tafadhali sana afanye juu chini kuhakikisha kwamba anapeleka fedha kule ili barabara hii ianze kufanyiwa ukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie pia Barabara ya Kitai - Luanda yenye urefu wa kilometa 40 ambako ndiko yanatoka makaa ya mawe. Barabara hii ni barabara ambayo sasa hivi ina mwaka wa tatu tangu ujenzi umeanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Mpaka sasa hivi barabara hii imefikia 26% tu. Fedha iliyopelekwa kati ya shilingi bilioni 60, imepelekwa fedha shilingi bilioni 11.5. Kwa hiyo mkandarasi bado ana-*suffer,* hawezi kwenda *speed* kwa barabara hii. Niombe sana kwamba

tunapozungumzia suala la miundombinu ya barabara katika nchi yetu tuwe *serious.* Wizara ya Fedha watoe fedha, wapeleke huko kwenye hiyo Wizara ya Ujenzi ili ujenzi huu uendelee kufanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine tutakuwa tunamlalamikia Waziri mwenye dhamana, lakini yeye si ndiye mwenye *mandate* ya kuleta fedha kwenye ile Wizara, Wizara ya Fedha ndiyo ambao wana-*mandate* ya kupeleka fedha hii kwenye Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo wapeleke fedha yote hii inayoombwa sasa hivi, trilioni 1.7 waone kama Bashungwa hatafanya *wonders* kwenye hizo barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa Bashungwa yupo vizuri na anafanya kazi vizuri na ana kiu ya kuhakikisha kwamba nchi yote inafunguka. Nilimwambia shikamoo Bashungwa baada ya kumwona yupo kule kwenye lile Daraja la Mitomoni amepanda juu ya pikipiki. Kwa kweli lile daraja ambalo mwaka juzi nililia hapa nikapiga na magoti Bashungwa kafika pale. Kwa hiyo ni matumaini yangu lile daraja sasa hivi linaenda kujengwa. Sasa isiwe ni *story*, anatenga fedha na fedha hazipelekwi. Tunalia na Wizara ya Fedha pelekeni fedha huko kwenye Wizara ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ya *bypass* ambayo ipo katika Manispaa ya Songea yenye urefu wa kilometa 14.5. Barabara hii inatoka Mletele eneo linaitwa Changarawe inaelekea Namanditi. Barabara hii imekuwa ikipigiwa *story* nyingi, haipelekewi fedha; ipelekwe fedha kwa sababu adha iliyopo katika Manispaa ya Songea haitafsiriki. Fikiria hayo malori yanayochimba mashimo kwenye barabara ya Makambako Songea, basi yale malori yote yanapita katikati ya mji. Ni tafrani, hali imekuwa ni mbaya, ajali zimekuwa ni nyingi; tunaomba barabara ya mchepuko. Mheshimiwa Bashungwa hebu agawe hiyo fedha, afumbe macho agawe hiyo fedha iende ikatengeneze hiyo barabara ya mchepuko pale katika Manispaa ya Songea, kilometa 14.5, najua ipo ndani ya uwezo wake. Ninaamini kabisa atafanya hivyo ili wananchi wa Mkoa wa Ruvuma waendelee kumwombea kwa kuwa wanaendelea

kupiga magoti kwa ajili yake na Mungu aendelee kumwona zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Likuyufusi - Mkenda ni maneno ambayo nimekuwa nikizungumza kila siku, ni barabara ambayo nimekuwa nikiimba. Hata nikienda jimboni kule katika Mkoa wangu wa Ruvuma ninaitwa Likuyufusi - Mkenda na siitwi jina lingine. Hii ni barabara yenye urefu wa kilometa 124 inayotoka Songea Mjini kwenda mahali ambapo ni mpakani mwa Tanzania na Mozambique. Inaunganisha Nchi ya Mozambique na Tanzania, kwa hiyo ni barabara ya kimkakati...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ukiwasha *microphone* yako, unanichanganya. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, sekunde 30 malizia.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, naomba basi nimalizie maana umenipa tishio. Kwa hiyo naomba, kwenye hii barabara Serikali imesema inatoa fedha shilingi milioni 60 ya kujenga barabara kutoka Songea Mjini kwenda mpaka pale Mkayukayu. Hata hizo kilometa 60 zenyewe hazijaanza.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kuwa barabara hii wenzetu wa Mozambique wanaitumia kuvusha magari yao na mizigo yao mbalimbali kutoka Bandari ya Dar es Salaam, kwa hiyo hii ni barabara ya kimkakati. Barabara hii ikishaanza kujengwa kwa kiwango cha lami itakuza uchumi, italeta ajira na wananchi ... *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ... ambao wapo pembezoni mwa hiyo barabara wataendelea kustawi; na ukizungumzia suala la uchumi unazungumzia wanawake ndio ambao wanachangia pato la Taifa kwa 80%...

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa ...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ... kwa hiyo wanawake hawa wanashindwa kuendeleza shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Ali Mzee, atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay na Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo ajiandae.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi hii, nami nishukuru kwa nafasi ya kuchangia ya Wizara ya Ujenzi. Nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kuendelea kutoa fedha nyingi ndani ya Sekta hii ya Ujenzi. Tunaona mtandao mkubwa wa barabara ndani ya nchi hii; Mheshimiwa Rais anatoa fedha nyingi ili mtandao uendelee kuenea na kuendeleza demokrasia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwa kuendelea kuwapa wakandarasi vijana na wanawake ambao wanamaliza chuoni pale *high court* kuwajengea uwezo wa miaka mitatu ili waweze kujiajiri katika kazi mbalimbali za barabara ambazo zinaendelea ndani ya nchi hii, niipongeze sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kuchangia kuhusu kuwawezesha Shirika la *TBA*. Serikali ilitazame kwa jicho la huruma Shirika hili la *TBA*. Shirika letu la *TBA* linajitahidi sana kuhakikisha kwamba linajenga nyumba kwa ajili ya wananchi na watumishi wanaoishi ndani ya Dodoma hii na maeneo mengine ya Taifa hili. Serikali itazame basi haja, kama Kamati ilivyoshauri, kuomba shilingi bilioni 50 ili shirika hili nao wapatiwe ili waweze kujiendesha kibiashara na waweze kuzalisha faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taasisi nyingi za Serikali zinadaiwa na Shirika hili la *TBA*, taasisi hizi zinalikwamisha shirika letu kujiendesha kwa faida na kibiashara. Wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi ambao pia wanadaiwa na shirika hili.

Nitoe wito kwa wananchi na taasisi za Serikali, zilipe madeni ambayo wanadaiwa na *TBA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee na mchango wangu kwa taasisi ya *TEMESA*. Tunaelewa kuwa taasisi nyingi za Serikali pamoja na Wizara wanapeleka magari yao ya halmashauri *TEMESA;* lakini wakishapeleka huko *TEMESA* wanaigeuza shamba la bibi. Wakishapeleka magari yao na yakishakuwa yamefika na kwamba wamepewa huduma, wakishamaliza kupewa huduma tu wanaondoka na magari yao, lakini taasisi yetu ya *TEMESA* hailipwi. Ninaomba taasisi za Serikali zilipe madeni yao wanayodaiwa na *TEMESA*. Tunajua kwamba *TEMESA* inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa vifaa kama vile vipuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali basi ione haja ya kuweza kuwapatia mtaji *TEMESA* ili waweze kununua *spare* wenyewe bila kutegemea *spare* kutoka kwa wafanyabiashara, maana sasa hivi wanachukua *spare* kutoka kwa wafanyabiashara. Wafanyabiashara hawa wakishawapa *spare* inawezekana hizo *spare* wanawapa nzima, inawezekana hizo *spare fake*, kwa hiyo wakija kutengeneza baada ya siku kadhaa gari za Serikali zinaharibika. Kwa hiyo tunaiomba Serikali iwape mtaji *TEMESA* ili waweze kujiendesha na wao kwa ajili ya kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, tumeona taarifa ya Kamati pia inaeleza juu ya wananchi wengi ambao wanadai fidia. Serikali yetu Tukufu, Mheshimiwa Waziri kijana, Naibu wake Waziri pamoja na Katibu Mkuu wetu mwanamke Mheshimiwa Aisha, tuchukue basi hatua na jitihada za haraka kuhakikisha kwamba wananchi wetu waliopisha maeneo kwa ajili ya ujenzi wa barabara nao wanalipwa fidia ili nao waweze kupisha maendeleo ya nchi yetu na ujenzi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi zaidi, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, atafuatiwa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo na Mheshimiwa Ghati Chomete, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi. Kwanza, nianze kumshukuru Mungu, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye kimsingi mwaka jana kama unakumbuka tuliomba Barabara hii ya Haydom – Mbulu - Karatu ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, nimeona hapa leo kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Bashungwa, barabara zipo nyingi, nimeona pia Barabara ya Dareda - Dongobesh kilomita 60, nimeona Barabara ya Haydom - Mogitu kilomita 68, nimeona pia Barabara hii ya Haydom - Labay.

Mheshimiwa Spika, ninataka niseme kitu kimoja leo hapa, Pamoja na yote yaliyotokea na nimekubali kwamba, ninampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kukubali barabara ijengwe. Hasa kinachotokea baada ya Mheshimiwa Rais, kukubali barabara ijengwe hawa ndugu zangu Mheshimiwa Waziri na Naibu nafikiri Katibu Mkuu, mimi sina shida nao. Waziri ni *gentlemen* mwenzangu anajua habari hili, ni rafiki yangu sana na sina mgogoro na yeye, lakini nina mgogoro na Wizara ya Ujenzi. Sasa, kwa sababu tumeshaahidi nisitake kurudi nyuma Ilani ya 2020 inasema hapa barabara imeahidiwa inatakiwa ijengwe kiwango cha lami, ya mwaka 2015 miongo mitano mfululizo inasema barabara ijengwe, sina shida.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, kakubali barabara imesainiwa sina tatizo, wakandarasi wamekuwa wapo *site* sina shida. Sasa Mheshimiwa Waziri lini anatoa pesa ili wale Wakandarasi hiyo kazi iendelee? Atakumbuka yeye mwenyewe alikuwa hapo mwaka jana, kipindi cha Kamati ya Matumizi na nadhani baadaye itabidi tuongee kwenye Bunge letu hili, maana katika Kamati ya Matumizi unashika shilingi, baada ya kushika shilingi hapo, unaenda wapi tena? Maana yake ukishika shilingi basi unamrudishia jamaa akafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, wanasema na sisi hapa tunapitisha bajeti hapa ikajenge barabara. Ile Garbabi kweli kule imeanza, lakini kule siyo kwangu hii ya kwangu ya Haydom - Mbulu. Sasa, kwa sababu imeshawekwa mkandarasi na yupo pale. Yule mkandarasi apewe hapewi hela, kwa hiyo, hajengi amekaa anasubiri tu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana mpaka mwaka huu, rafiki yangu Mheshimiwa Bashungwa, yaliyofanyika yanakumbukwa, sitaki kuendelea kutaka kusema yale waliyoahidi, maana hapa ananiangalia kwa jicho la tafadhali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa ndugu yangu hebu aniambie nafanyaje sasa? Maana sasa yeye anamdanganya na Mheshimiwa Spika wetu na sasa hivi anamdanganya Mheshimiwa Rais wetu. Mimi kuliko Mheshimiwa Rais, adanganywe *brother* aonekane mwongo, ninahakikisha wewe utaonekana mwongo humu ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba nikukumbushe tu kidogo hebu sikiliza Kamati ya Matumizi.

*(Hapa Mhe. Flatei G. Massay alilisikilizisha Bunge Sauti iliyorekodiwa kutoka kwenye simu yake kuhusu majadiliano ya Kamati ya Matumizi ya mwaka wa fedha uliopita)*

Majadiliano hayo yaliyorekodiwa ni kama ifuatavyo:-

"***MHE. FLATEI G. MASSAY:*** *Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha iliyowekwa hapa ni ndogo sana. Sasa ninataka ufafanuzi hapo wanapokwenda kufanya matumizi kupitia hii hela ya bilioni nane itaenda kufanya kazi gani?*

**MWENYEKITI:** *Hiki Kifungu hapa kiliandikwa 4114 kwa maana ya 4,114 Karatu, Mbulu, Haydom,* Sabiti, Lalago, Maswa. *Mmetenga bilioni nane inaenda kufanya nini? Kujenga kiwango cha lami, kuweka changarawe au kujenga daraja? (Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** *Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kutoka Labay mpaka Haydom section yenye urefu kilomita 25. Bilioni nane ukiweka, kwa sababu ukija ukichukua advance payment ya barabara hii pengine ni bilioni mbili ama bilioni tatu tu. Kwa vile hiyo pesa tutalipa advance payment na itakayobaki tutaweza kulipa certificate nyingine, kwa sababu barabara yenyewe inaweza kuchukua miaka miwili kujenga. Hatuhitaji kuweka pesa zote wakati huu. Naomba kuwasilisha. (Makofi)*

***MWENYEKITI:*** *Haya. Mheshimiwa Flatei, ameelewa kwamba, ni kiwango cha lami."* Mwisho wa majadiliano yaliyorekodiwa.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, unasikia wewe mwenye umesema nimeelewa kiwango cha lami. Sasa leo hakuna kiwango cha lami, nisaidie tunafanyaje? Shilingi tumeshika, umeniambia nimeelewa na nimekubali. Sasa hapa tunadanganywa au tunapigwa chenga? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini sasa kiwango cha lami kimeshaonekana, tumepitisha bajeti ya matumizi tayari. Ngoma imekwenda kuanza leo mwaka mzima Mkandarasi yupo *site* anakaa yupo mle bwana Mchina, anakaa, vifaa sasa anaviondoa kimoja baada ya kingine. Sasa nisaidie tunafanyaje kutoka hapa? Ili wasitudanganye hawa ndugu zangu, tujenge barabara na matumzi yawe sahihi.

Mheshimiwa Spika, hili tatizo ni kubwa sana inawezekana huyu Waziri ametangulia amesema, lakini Mheshimiwa Bashungwa anakwenda, tatizo ni nini ambapo fedha sasa hazipelekwi? Bilioni nane tu hebu kumbuka barabara imesema ina kwenda kujengwa Mkandarasi yupo *site*. Mimi nimfanye nini yule Mkandarasi? Niende nikamwambie bwana eeh sepa, ondoka, anazungumza Kichina hata Kiswahili hajui *ching ching* tutamalizana pale!

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu ndugu yangu amemweka pale aweke hizi pesa basi au atuambie pesa amepeleka wapi? Ni shida hii, shida kubwa zaidi tumefika mpaka

hapa. Mheshimiwa Rais amekubali yupo vizuri hakuna Mheshimiwa Rais anayesikia kama mama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mungu amsaidie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hapa chini yake kuna shida, tubadilishe namna ya kuwahukumu hawa kuwasimamia. Hii habari ya kushika shilingi hapana siyo sawasawa, tuisimamie bajeti hii isipite wakajipange warudi hapa tukatengeneze, tukiwapitishia watazoea. Hata wewe unadanganywa hebu angalia hapa huu ni ushahidi, kama ushahidi unataka mwingine nitaleta hapa. Ushahidi ninao sema tu sitaki kufungua, maana teknolojia hapa hazioani. Ingekuwa inawezekana ku-*display* pale ninge-*display*.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni shida na shida hii nafikiri kama haipo kwenye Sheria basi ni chenga chenga humu humu. Tumetoka kwenye upembuzi yakinifu tumemaliza, tumekuja *details design* tumemaliza, tumekwenda kwenye kusaini tumemaliza. Sasa jamaa wanakaa wanakaa, sarakasi leo hakuna umesema mwenyewe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sarakasi siyo kwamba, nimeishia hapa nina uwezo mwingine maana sarakasi uzuri wake ni jambo unalolifanya kupitia ufahamu wa kawaida. Sasa wakati ule nilipanda hapa, sasa hivi sitaki kupanda kwa sababu nafahamu Sheria zinazoendesha Bunge hili. Hasa kwa Sheria hili mimi leo sitaunga bajeti hii mkono. Nitakuwa wa kwanza, kwa sababu mimi sidanganywi pekee yangu, wewe ukidanganywa, hapa tukipigwa chenga na wananchi wanadanganywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukienda Mbulu hakuna gari unaweza kupanda zaidi ya *cruiser* na ukifika Babati nenda pale ni ma-*cruiser* utasikia Mbulu *cruiser, cruiser, cruiser* hakuna gari inakwenda. Sasa maana yake nini wananchi wapande *cruiser* tu? Waheshimiwa Wabunge, mnielewe siyo kwamba, tunapanda *cruiser,* kwa sababu mengine labda hatuwezi kununua au namna gani vipi? Ni kwamba *Hiace* haifiki, mabasi hayafiki.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya barabara ikiwekewa mkandarasi haijawekwa bajeti ya *maintenance*. Kwa hiyo, imeachwa vilevile, mwaka jana mpaka mwaka huu. Hebu fikiri bajeti ya mwaka jana imeachwa hivyo barabara hiyo haijawekewa chochote haina kitu kinaitwa *maintenance route* ile ya kujengwa kila mwaka kukwanguliwa unapitaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitoka huku unalala kabisa rrrrrreeee mpaka Babati pale. Nikiingia Mbulu hrrrrrrrrrr nitawezaje sasa maisha haya? Basi kama wameshindwa kujenga kwa kutumia lami wale Wakandarasi wapo kule si waweke hata pesa ya kukwangua pale wananchi wapite kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu dunia imeanza sisi hatujawahi kuona lami na lami hii ina umuhimu ukiangalia kwa Mikoa hii ya kwetu. Mikoa minne; Mkoa wa Arusha maana yake unatoka Karatu kuja Mbulu ni Mkoa huo, maana yake Mbulu ipo Manyara. Kutoka Mbulu hiyo unapita Mbulu Mjini unakuja Dongobesh unakuja Haydom. Unaenda Singida Mkoa mwingine, unaenda Simiyu Mkoammwingine na unaenda Shinyanga. Kwa hiyo, inaunganisha Mikoa hiyo niliyoisema ni mingi sana.

Mheshimiwa Spika, hasa Waziri atajua lini hawa jamaa wanatakiwa kupelekewa pesa? Siyo kwamba, fedha hamna ingekuwa hamna bora. 82% amepewa kwenye bajeti zimekwenda, kwa nini, hakuleta hata bilioni nane hiyo huku?

**SPIKA:** Haya, Ahsante sana. Kengele ya pili, imeshagonga.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, tutakutana kwenye shilingi kwa leo Mheshimiwa Bashungwa atanisamehe. Mimi sina nia mbaya na wewe, sina nia mbaya na Wizara ila hali barabara ni mbaya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Haya, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ghati Chomete, Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, ajiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru, kwa kunipa nafasi. Pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutuletea fedha nyingi za maendeleo. Pia, nimshukuru mdogo wangu Mheshimiwa Bashungwa kwa kazi anayoifanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuzungumza mambo ya Kijimbo, ninaomba nizungumze mambo ya ujumla, ambayo naamini yataenda kuleta tija katika maeneo yetu mengi hasa yale maeneo ya Dar es Salaam. Lipo tatizo kati ya hizi Taasisi mbili zinazohusika na ujenzi wa barabara kwa maana ya *TANROAD* ambayo ipo chini ya Wizara ya Ujenzi na *TARURA* ambayo ipo chini ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, *TANROAD* wanafanya kazi nzuri ya kujenga barabara, lakini barabara ile mwisho wa siku inakuwa na mifereji. Wakati wanajenga barabara ile mifereji lazima maji yanayokusanywa katika ile mifereji yaelekezwe katika barabara za *TARURA* kwa ajili ya kwenda kwenye mito mbalimbali inayopokea maji haya.

Mheshimiwa Spika, hakuna *coordination* nzuri kati ya *TANROAD* na *TARURA* katika kupokea maji yanayotoka katika barabara za *TANROAD*. Mafuriko zaidi ya 70% na nyumba zilizoharibika katika Mkoa wa Dar es Salaam zimetokana na tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano mdogo kuna Mfereji wa Kwa Shego ambao umetokana na barabara iliyotoka Charambe kwenda Mbande barabara hii ni ya *TANROAD*, *TANROAD* wamekusanya maji ya barabara ya kilomita zaidi ya saba, wameyapeleka kwa wananchi. Matokeo yake wananchi wa Kingugi katika Kata ya Kilungule na katika Kata ya Kiburugwa wananchi zaidi ya 50 wamepoteza nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyumba hizi hazipo katika maeneo hatarishi isipokuwa maji ambayo yamesababishwa na *TANROAD* yameshindwa kupokelewa na watu wa *TARURA*. Vilevile, eneo la Kata ya Mbagala Kuu eneo la Upugani katika Mtaa wa Mbagala

Kuu Kaskazini, kuna ile Barabara ya Mbagala Kuu inayotokea Kijichi ni barabara ya *TANROAD* wametengeneza vizuri wameweka mifereji, lakini maji wameelekeza katika maeneo ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kutokana na mvua hizi zilizonyesha maeneo mengi ya Upugani katika Kata ya Mbagala Kuu yameathirika sana na hatimaye makazi ya watu yamekuwa hatarini. Eneo la Bamia pale Chamazi barabara hii ya Chamazi kwenda Mbande eneo lile barabara yote ile hamna sehemu ya kupeleka maji. Maji wameyaeleza kwa wananchi matokeo yake Wakazi wa Bamia wote wameathirika kutokana na mvua hizi zinazonyesha.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine eneo la Mikwambe, Kata ya Twangoma barabara inayotoka Kigamboni kwenda Kongowe barabara ile hakuna sehemu ya maji yale ya *TANROAD* kwenda katika maeneo ambayo ni sahihi maji yote yameyaacha njiani matokeo yake yameenda kuathiri makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza Mwenyekiti wangu wa UWT Kata ile ambaye ni Mpiga Kura wangu ameathirika na nyumba yake imebomoka kutokana na maji yanatokana na *TANROAD*. Kwa Mbiku, Kata ya Charambe barabara ile ya Charambe kuelekea Chamazi hii barabara kubwa hamna sehemu ya maji kuyapeleka, maji yote yamekuwa yanaenda katika makazi ya watu na hatimaye makazi ya watu yamekuwa yanaathirika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hapa rai yangu tuweke muunganiko wakati tunataka tujenge hizi barabara Serikali mshirikiane kati ya *TANROAD* na *TARURA* Wizara ya Ujenzi na Wizara ya TAMISEMI kuhakikisha hali hii tunaiweka sawa. Sisi kama Waheshimiwa Wabunge, tunawauliza TAMISEMI hatima ya hawa wananchi, lakini ukweli ni wao *TANROAD* ndio wamesababisha madhara haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Waziri Mheshimiwa Bashungwa barabara yangu ile Msongola - Mbande tayari

mkandarasi yupo *site,* nimshukuru sana na wananchi wanampongeza sana na wanampa hongera. Vilevile, nimeona tangazo la Barabara ya Kokoto - Kongowe limetangazwa. Naamini baada ya kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Mbagala hasa barabara hii ambayo imekuwa ikisababisha vifo kwa muda mrefu sasa inaenda kupata mwarobaini.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa ninapata wasiwasi na maneno ya ndugu yangu Mheshimiwa Flatei Massay, kwamba, imeandikwa tu au itatekelezwa? Sasa kwa kuwa yeye ni Mwanasheria hebu huko tunapokwenda atutafutie utaratibu mwingine ambao barabara imewekwa mwaka jana haikutekelezwa, mwaka unaofuta tuweke kwenye Kanuni zetu badala ya kushika shilingi, tufanye kitu gani kingine? Kwa sababu mwisho wetu sisi tutaishia kwenye kushika shilingi, lakini mwaka wa kwanza tumeona vitabu vya bajeti vimetolewa pale vya miaka minne barabara hiyo hiyo. Je, baada ya mwaka wa kwanza, kushika shilingi, mwaka wa pili kinachofuata nini? Yeye ni Mwanasheria atatusaidia sana katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hiyo barabara kuna watu wamewekewa *X* kwa ajili ya kupigiwa fidia Mheshimiwa Waziri atueleze barabara ya Kokoto - Kongowe wale watu fidia inakuwaje na lini watalipwa barabara imetangazwa? Lini watalipwa, barabara imetangazwa?

Mheshimiwa Spika, barabara ile ya Rangi Tatu kwenda Mbande barabara ile kwa kweli sasa hivi imezidiwa na kumekuwa na msongamano mkubwa sana. Tumwombe sana Mheshimiwa Waziri, atafute kila namna tunapozungumza kufungua msongamano Dar es Salaam, tuyaangalie na Majimbo haya ya Dar es Salaam yalivyokuwa na wingi wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninateta hapa Mheshimiwa Askofu Gwajima, tukasema TAMISEMI kwenye kugawa madarasa, vituo vya afya na zahanati wanagawa kutokana na uwiano wa Majimbo. Hawaangalii kulingana wingi wa watu wanaangalia kulinga na majimbo. Sasa na hizi barabara kwa nini tusiangalie kugawana kilomita hizi kulingana na majimbo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Dar es Salaam tunapozungumza hapa tukipewa kilomita 60 au 70 Dar es Salaam nzima za *TANROAD*, tayari tunakuwa hatuna tatizo tena la barabara. Hapa tunaona tunapitisha kilomita 168, kilomita 200. Ninajua hiyo ni kengele ya mwisho na mimi ni muumini wa muda, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la mwongozo wa namna gani tufanye baada ya bajeti kuwekwa kwenye vitabu mara tatu. Lazima aseme kitu kulinga na sheria ambazo amezisoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, atafuatiwa na Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kunipa nafasi ya kuchangia, pia, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa na nzuri sana anazozifanya katika nchi yetu na hasa katika Wizara hii ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine, nimpongeze Waziri wa Ujenzi ndugu yangu Mheshimiwa Innocent Bashungwa, kwa kazi kubwa na nzuri anazoendelea kuzifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Wizara hii ya Ujenzi yeye pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Eng. Godfrey Kasekenya, lakini pia, Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi wakiongozwa na dada yangu Mheshimiwa *Engineer* Aisha, hongereni sana, tunashukuru sana kwa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu tumezunguka tumetembelea miradi mingi ambayo imetekelezwa na Wizara hii.

Ni pamoja na madaraja ambayo ametoka kuyasema mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango mengi katika nchi hii ambayo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetekeleza na yote yamekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu nikiwepo na mimi nilitembelea katika Mji wa Mwanza, tulitembelea Daraja la Kigongo Busisi, daraja lile ambalo lilianzishwa mwaka 2020 na lilitegemewa kuwahi kukamilika. Kwa vikwazo au vigezo ambavyo vilisababisha mradi ule kuchelewa, kwa umahiri mkubwa na uhodari mkubwa wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo daraja lile lipo 85%. Tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi kubwa, tunaiomba Serikali…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chomete, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, ninataka kumpa taarifa tu Mchangiaji, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sisi watu wa Mkoa, Mwanza na hasa katika Jimbo la Misungwi na Sengerema, daraja lipo 89% kwa leo na tumebakiza nguzo mbili tu daraja lile liweze kuungana. Unaweza ukachunga mbuzi kutoka Busisi na ukazipeleka Sengerema, ukazipeleka Misungwi. Ahsante sana mama Mheshimiwa Dkt. Samia. Endelea Mchangiaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, muda wako unalindwa Mheshimiwa Chomete; hebu nisaidie yeye alikuwa anasema nini Mheshimiwa Mbunge? Alikuwa anasema daraja halijajengwa, halipo ama?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, alisema limejengwa lipo 85% ila sasa hivi linakimbilia 89%.

**SPIKA:** Kwa hiyo unampa taarifa kwamba limefika 89% kutoka 85%?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, 89% tumebakiza nguzo mbili tu daraja likamilike. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya asante sana. Mheshimiwa Chomete unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya shemeji yangu Mheshimiwa Tabasam ila kwa sababu mimi nilienda kutembelea pale na nikakuta hizo 85% nimesema kile nilichokikuta, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba ninaomba kwa asilimia zilizobaki lile daraja liweze kumalizika kwa haraka ili wananchi wa Kanda ya Ziwa waweze kunufaika na lile daraja, kwa sababu nina imani litakapomalizika Watanzania wakiwemo Wananchi wa Kanda ya Ziwa wataenda kufaidika kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo niongelee kuhusu wakandarasi. Ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu benki ziweze kutoa *invoice discount* kwa wakandarasi wetu wa ndani. Wamefanya hivyo kwa kuwaongezea pia wakandarasi wetu wa ndani nguvu, uhodari, umahiri na kwa kujiamini waweze kufanya kazi vizuri na wakandarasi wetu wa ndani wanapopewa kazi wataweza kwenda kutoa ajira kwa vijana wetu wale ambao hawana ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo wanapopata kazi wakandarasi wetu wa ndani wataweza kuongeza uchumi wa nchi yetu kwa sababu hata zile pesa ambazo zinazunguka ndani ya nchi pia zinaiongezea nchi yetu uchumi. Ombi langu ni kuwaomba Serikali wawalipe kwa wakati wakandarasi wetu wa ndani watakapowachelewesha wanaendelea kuwadidimiza. Serikali wawalipe wakandarasi wa ndani mapema ili kusudi na wenyewe waweze kukidhi mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kusema kwamba katika Mkoa wetu wa Mara tumepata miradi ya barabara kwa kiwango cha lami na hapa niende nikampongeze sana Meneja wetu wa *TANROADS* katika Mkoa wa Mara Kaka yangu Vedastus Malimbe. Amekuwa ni meneja mzuri, mchapakazi na anayesimamia Miradi ya *TANROADS* vizuri. Hapa hata Wabunge wa Mkoa wa Mara watani-*support* kwa sababu meneja yule anachapa kazi. Mheshimiwa Waziri nikwambie, katika mameneja wote ulionao katika nchi hii nadhani Meneja wa Mkoa wa Mara anaweza kuwa anaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni yeye pamoja na watendaji wote wa *TANROADS* katika Mkoa wa Mara. Nasema hivyo kwa sababu tumekuwa na Barabara ya Sanzati – Nata kilometa 40. Ile barabara ina miaka zaidi ya 10 haijakamilika, lakini kwa umahiri mzuri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan barabara mpaka sasa hivi ipo 45%. Mkandarasi anadai pesa shilingi bilioni tano. Ninachokiomba, naomba mkandarasi yule aweze kulipwa ile pesa ili kusudi Mama Samia aweze kuweka historia katika Mkoa wa Mara kwa kufungua barabara iliyokaa zaidi ya miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na barabara hiyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupa Barabara ya Mogabili mpaka Nyamongo kilometa 25. Ile barabara mpaka sasa hivi mkandarasi anadai shilingi bilioni sita na pointi na anadai hizo pesa haendelei na mradi mpaka sasa hivi. Mradi ule umesimama, mvua zikinyesha ni changamoto kubwa sana. Akinamama wa kule wanafanya biashara ndogo ndogo, wakipita kwenye ile barabara ina utelezi. Mheshimiwa Bashugwa ulifika, ulijionea nadhani hata wewe mwenyewe na gari yako ilikwama. Tunaomba Waziri apeleke pesa ili mkandarasi yule aliyepo pale amalize ule mradi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kuipongeza Serikali yangu, tumepata Mradi wa Kiwanja wa cha Ndege unaosimamiwa na *TANROADS.* Ule mradi umesimamiwa vizuri sana mpaka sasa upo 55% ila mkandarasi anadai na sisi tunatamani uwanja ule uishe wananchi wa Mkoa wa Mara waweze kupata nafuu ya usafiri

kutoka Mara na maeneo mengine. Pia, mpaka sasa hivi mkandarasi anadai zaidi ya bilioni tatu na pointi, alipwe. Sambamba na huo uwanja kuna wananchi wa pale walipisha maeneo, Mheshimiwa Waziri wananchi wanadai. Walikubali kupisha ili kusudi maendeleo yapatikane katika mkoa wetu, lakini mpaka sasa hivi wanadai zaidi ya shilingi bilioni 3.9. Wawalipe wale wananchi, wanaipenda Serikali yao. Tusilete ugomvi kati ya wananchi na Serikali. Shilingi bilioni tatu ni kidogo sana kwa Serikali yetu, twende tukawalipe wale wananchi ili kusudi na wao waweze kufurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika barabara hizo ambazo zipo sisi Mkoa wa Mara tulipata barabara kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024. Tulipata barabara ya Musoma mpaka Busekera, mkandarasi hajawahi kufika na tulipata barabara ya Utegi mpaka Kirogo mkandarasi hajawahi kufika. Sisi Wabunge tumeenda kwenye mikutano tumewaambia wananchi kwamba kwenye Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia hii barabara itajengwa kwa kiwango cha lami. Mwaka mzima hakuna kinachoendelea mkandarasi hajafika *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba na ninachoiomba Serikali yangu iende ikapeleke fedha ili kusudi miradi ya barabara iliyopo Mkoa wa Mara iweze kutekelezeka kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma tutamalizia na Mheshimiwa Michael Costantine Mwakamo.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Nianze mchango wangu kwanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara kwani wakati tuliopata changamoto ya maporomoko ya Mlima Hanang barabara ya Babati - Singida ilifunga na waliifungua kwa wakati lakini pia niliiomba Wizara wakati wanafanya ukarabati wa

miundombinu watuwekee taa za kutosha Mji wa Katesh na taa zimewekwa. Ninashukuru sana kwa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa miundombinu pia unaoendelea pale Mji wa Katesh tunashukuru sana, lakini niiombe tu kwamba kuna eneo la Endasak tuliomba taa, tuliahidiwa taa 49 zile taa zimekuwa chache sana watu wanagombania naomba eneo hili mwongeze taa. Vilevile eneo la Endagaw naomba mwongeze taa, eneo la Nangwa pale mji umechangamka sana umekuwa mkubwa tuweke taa kwenye eneo hilo, lakini eneo la Mogitu pia tuweke taa kwa sababu shughuli za binadamu pale zimekuwa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nishukuru sana, Mheshimiwa Waziri na hasa *Engineer* Masele, *Engineer* wetu wa Mkoa amekuwa akinisaidia wakati anafanya ukarabati wa Nangwa – Gisambalang - Kondoa amekuwa akisaidia kuunganisha lile eneo la Changanyikeni ambalo lipo pembeni kidogo. Kila mara anapofanya ukarabati pale amekuwa akitusaidia, tunamshukuru sana kwa kazi hiyo nzuri na ushirikiano ambao amekuwa akitupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru vile vile kwa Barabara ya Nangwa - Gisambalang - Kondoa kuanza kufanyiwa mchakato wa kuwekewa lami kwani kwa sasa mchakato umeanza wa kuitangaza hiyo barabara ili mchakato wa kuiweka lami uanze. Tuliiomba na Mheshimiwa Rais alituahidi na Waziri akitekeleza ile ahadi maana yake atakuwa ameturahisishia sana sisi Wanahanang sisi Wanamanyara wakati tukitaka kuja Dodoma. Ukitoka Dodoma mpaka Kondoa ni kilometa 143, kutoka Kondoa mpaka Katesh kilometa 79. Ukizunguka kupitia Babati unatembea zaidi ya kilometa 100 ambayo siyo lazima uiongeze na unaingia gharama. Waziri atakuwa ametusaidia sana na wananchi wetu watafanya shughuli za maendeleo kwa urahisi. Tunaomba upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara hiyo ufanyike kwa kasi ili hatimaye barabara hiyo iweze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, muda mrefu tukilalamika kuna Daraja la Munguri linalounganisha Kondoa na Hanang na inategemewa na

wananchi wetu. Lilichukuliwa na mafuriko ya mwaka 2019. Nimeuliza maswali mengi sana juu ya daraja hilo, ninaomba lile daraja lijengwe. Lile daraja ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa Kondoa na wananchi wa Hanang, wananchi wa Mkoa wa Dodoma na wananchi wa Mkoa wa Manyara. Ninaomba kwenye eneo hilo watusaidie.

Mheshimiwa Spika, tuna Barabara yetu ya Hydom - Mogitu, Hydom – Katesh, Mheshimiwa Waziri hii barabara nimeongea na wewe mara nyingi. Kwenye hotuba yake nimejaribu kufuatilia imetaja maeneo mengi, mwaka jana tulisema tutafanya maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami. Kazi ambayo imekwishafanyika ni usanifu wa kina ambapo zimetumika shilingi milioni 745; na kandarasi ilikuwa iishe tarehe 17 Februari, 2014. Ninaamini maandalizi kwa maana ya kufanyiwa *design* ile barabara imekamilika. Mwaka huu ukiangalia kwenye kasma 4,114 imetengewa shilingi milioni 500. Sasa najiuliza kwa sababu tunaandaa hii barabara kujenga kwa kiwango cha lami, shilingi milioni 500 inakwenda kufanya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, barabara ni kilometa 70 wakati mwingine wanasema kilometa 68. Je, shilingi milioni 500 inaenda kufanya kazi gani? Mheshimiwa Waziri mimi na wewe tumeongea hapo tukajadili maeneo ambayo ni korofi nikakwambia Mlima Chavda pale magari kila siku yanateleza. Wananchi wanahangaika kulima kila siku wanamwaga ngano pale, lakini Eneo la Mogitu pale njiapanda ya Dawar lile tuta la barabara ambalo wamejenga sasa hivi imemeza mashamba ya wananchi zaidi ya ekari 600, pale pamekuwa ni bwawa sasa hivi. Wananchi hawana pa kulima na ukijaribu kuwabana watu wa *TANROADS* ili angalau watengeneze mifereji ili yale mashamba yaweze kuokolewa, changamoto ni rasilimali fedha ili angalau mitaro ile iweze kutengenezwa na wananchi waweze kuyatumia mashamba yao. Sasa pale pamekuwa ni kama bwawa.

Mheshimiwa Spika, hebu sasa ninaomba; tumeongea mimi na wewe na tumekubaliana kwamba baada ya bajeti yako tutaenda Hanang. Utaona maeneo hayo mawili korofi halafu utasema neno ili mimi niunge mkono bajeti yako. Utakaposema

neno kwamba pale unakwenda kufanya nini lakini hii shilingi milioni 500 kwa barabara ya karibu kilometa 70 inaenda kufanya kazi gani na barabara hii imeahidiwa tangu mwaka 2010? Wananchi wamekuwa wakiisubiri, shughuli nyingi za kilimo zinafanyika ukanda wa juu na kule ndiyo tuna mashamba makubwa ya ngano. Nchi yetu ina nakisi ya ngano zaidi ya…

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, Taarifa

**SPIKA:** Mheshimiwa Hhayuma kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Flatei Massay.

**TAARIFA**

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa mchango mzuri sana Mheshimiwa Hhayuma maana ni jirani yangu kabisa. Barabara anayoisema ndiyo inafika kwangu, nikwambie hata akija Waziri alishakuja kwangu haitasaidia kitu, bora aweke hela barabara ijengwe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hhyuma unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana taarifa hiyo naipokea. Mheshimiwa Waziri suala la kuja Hanang ni muhimu ili tujadiliane kwa pamoja yale mazingira yalivyo, aje na wataalam wa kutosha ili kwa pamoja tuamue nini cha kufanya pale. Suala la kuweka fedha shilingi milioni 500, yeye aniambie inaenda kufanya kazi gani kwenye barabara ya kilometa 70?

Mheshimiwa Spika, nimepitia pitia kwenye hotuba yako ukurasa wa 452 umeweka shilingi milioni 280, imeandikwa kwa Kiingereza *visibility study and detail design of Katesh - Hydom*. Si tumeshamaliza kufanya hiyo? Hiyo hela tena ni ya nini? Tunaomba fedha ziwekwe kwa pamoja kwa ajili ya kuanza ujenzi, wananchi wanataka barabara, hawataki maneno.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya kwenye ujenzi wa barabara nikisema barabara ya Hydom - Katesh, barabara ya

Nangwa - Gisambalang –Kondoa barabara zote hizi zinafanyiwa upembuzi na usanifu. Halafu zinafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, lakini barabara nyingine ni *design and construct*. Kwa nini barabara za Hanang haziwekwi kwenye *design and construct?* Kwa nini tunatenganisha? Halafu barabara nyingine unaona *EPC+Finance*. Hawa Watanzania kwa nini tunawaweka kwenye makundi ili barabara zijengwe kwa wakati wananchi wapate huduma?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninakushukuru kwa nafasi nitaunga mkono pale ambapo nitakuwa nimepata ufafanuzi mzuri kutoka kwa Waziri. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa namna ambavyo amenipatia nafasi ya kuchangia. Nianze moja kwa moja kwa kumshukuru Waziri kwa namna ambavyo anaendelea na utekelezaji wa majukumu lakini tunafahamu hili jahazi alilokabidhiwa kama kila mmoja atasema atasikiliza kwanza baada ya kauli yako ndiyo aunge mkono hoja inawezekana tukawa wote, lakini kwa kweli sisi wengine tunatanguliza kusema tunaunga mkono hoja ili tukupe nguvu ya kupokea haya mambo na kuendelea kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru Serikali tumesikia hotuba ya Waziri, mimi huu mwaka wa nne sasa nikizungumza Barabara ya Makofia – Mlandizi - Mzenga - Vikumbulu barabara yenye urefu wa kilometa 153. Leo nimemsikiliza Waziri nianze kusema nakupongeza sana, nakushukuru sana wewe, watendaji wa Wizara na namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kilio hiki na maneno ya watu wa Kibaha ambao nimetumia kinywa changu kuwasilisha kwenu. Nimeona wameweka kwenye bajeti wanaizungumzia Makofia - Mlandizi kilometa 36 ipo kwenye utaratibu wa kutafutiwa pesa, lakini wakati huo huo wametenga shilingi milioni 600 kama sehemu ya awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenzangu aliyemaliza kuchangia shilingi milioni 500 inafanya nini, lakini sehemu iliyo sifuri siyo sawa na sehemu iliyo na moja. Ninaamini katika utaratibu wa maandalizi ya bajeti unapowekewa pesa kidogo inakuwa ni sehemu ya kushika au kutengeneza kifungu pale kwa maana ya kwamba wakati wowote ikipatikana ya ziada inakwenda kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kukuomba Mheshimiwa Waziri kwamba ile 600 ambayo inaonekana pale Makofia - Mlandizi iwe sehemu ya kuleta chachu ya kuitafuta hiyo nyingine kujazia tuweze kutengeneza barabara hiyo. Vilevile nilikuwa naendelea kuzungumza kwamba nimeona kipande cha pili cha Barabara ya Makofia – Mlandizi - Vikumbulu kinaanzia Mlandizi kuelekea pale Mzenga na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru nimeona kwenye zile barabara za haraka zinazounganishwa na *SGR* barabara hii imewekwa na niseme namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Nilikuwa nazungumza na Meneja wa Mkoa pale amenithibitishia kwamba kipande cha Mlandizi kwenda *Ruvu Station* kwenye Reli ya *SGR* kimetangazwa. Kwa sababu kimetangazwa, basi ni imani yangu kwamba tunakwenda kwenye kuitekeleza. Kwa hiyo nikuombe na niiombe Serikali kwa kweli kupanga ni jambo moja, kupewa pesa Wizara na kwenda kutekeleza ni jambo la pili. Kwa hiyo tuiombe sana Wizara ya Fedha hapa iweze kuwapatia fedha za kutosha na kwa wakati ili hizi kazi ambazo wameziainisha na zenye umuhimu wake ziweze kwenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeona kwamba wameweza kufanya maandalizi ya kutaka kwenda kwenye utaratibu wa ulipaji wa fidia na wameanza kuweka malengo ya utengenezaji wa hizi barabara, lakini Mheshimiwa Waziri fahamu kwamba hatua ya kwenda kuitengeneza barabara inapitiwa na hatua ya awali ya kufanya michakato ile ya awali ya upembuzi yakinifu na kulipa fidia. Hii barabara ninayoisema wakati wote mpaka sasa haijawa na fidia. Kwa hiyo nikuombe sana Waziri pamoja na kuieweka kipande cha Ruvu - Mlandizi kwenda kule Ruvu, basi hebu atakaponyanyuka watakapokuwa wanahitimisha hotuba

yake, hebu atoe neno basi ili watu wamfahamu, watu wa Jimbo la Kibaha, watu wa Jimbo la Bagamoyo, watu wa Jimbo la Kisarawe pamoja na watu wa Jimbo la Kibaha Mjini. Hili neno fidia tumefikia hatua gani? Ni kweli tulikuwa tunaona wataalam wanapita, wamefanya ukaguzi, wameweza kupita kuwasainisha watu fomu lakini wananchi wanataka kujua kwamba fidia Barabara ya Makofia - Mlandizi, Mlandizi – Mzega - Vikumbulu imefikia hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunafahamu zipo hatua za kufikia kulipwa. Sasa namwomba sana, sana ndugu yangu utakapofika wakati akisimama hebu toa neno watu wapate kujua, pamoja na kuweka kwenye utaratibu wa matengenezo fidia imefika hatua gani? Bado *document* zipo mkoani au zipo kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali au zipo wapi? Zipo Wizara ya fedha? Nini tatizo na wakati gani atalipwa ili tuweze kwenda kutengeneza barabara hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo niiombe sana, sana Wizara na niiombe sana, sana Serikali kwamba tunajua Wabunge wote humu ndani wanalalamikia barabara. Wanafahamu kabisa kwamba barabara ni moja ya njia ya kitega uchumi. Nawashukuru sana Serikali kwa sababu jimbo langu limekaa katika maeneo ya kimkakati. Ukiitaja barabara ya mwendokasi inayotoka Dar es Saalam, inayotoka Mailimoja kupita pale kwenda Chalinze mpaka Morogoro unanikuta mimi, ukipata barabara ya Mailimoja kuja kwenda Chalinze mpaka Morogoro Jimbo la Kibaha Vijijini lipo. Kwa hiyo tunashukuru kwa hii mipango.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ielekeze fedha kwenye hii miradi kwa sababu ni Imani yangu mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kibaha kwamba endapo tutakuwa tumetekeleza miradi hii tutakuwa tumetekeleza tendo la kukuza uchumi wa wananchi. Kwa sababu barabara hizi zitakapokuwa zimekamilika wananchi watakaokuwa wamepitiwa na barabara hizi wataongeza kipato chao kwa shughuli mbalimbali za kuendesha biashara katika maeneo yale na ni imani yangu kwamba tutakuwa na suala la uchumi kwa wananchi wa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana siku ya leo. Mchana tutakapokutana hapa Wabunge wafuatao tutaanza nao kwenye michango na kisha wengine wataendelea kuitwa kadri muda utakavyokuwa unaruhusu. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao na wengine wataendea kuitwa kadiri muda utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao waliingia baada ya tangazo letu la wageni la awali kupita. Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni Waziri wa Ujenzi Ndugu Mecky Chawi, Rais wa Chama cha Wabunifu Majengo, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni Waziri wa Ujenzi. Wapo Wakuu wa Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara; Wapo Mameneja wa Mikoa wa *TANROADS* na *TEMESA*; Makatibu 13 wa Mikoa wa Jumuiya ya Vijana wa Chama Cha Mapinduzi; Kamati ya Siasa kutoka Wilaya ya Karagwe ikiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya; Chama cha Umoja wa Makandarasi na Watoa huduma Shirikishi Tanzania; Chama cha Wakadiriaji Majenzi Tanzania; Chama cha Wabunifu Majengo Tanzania; na Chama cha Madereva wa Serikali Tanzania. *(Makofi)*

Wapo wageni kutoka Mkoa wa Lindi ambao ni Mkoa Ulioathirika zaidi na Mafuriko na Kimbunga Hidaya; Waandishi wa Habari Mbalimbali kutoka Jijini Dar es Salaam; na Washirika wa Maendeleo na Taasisi za Fedha. *(Makofi)*

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya, Naibu Waziri wa Ujenzi, Wanafunzi kutoka Chuo cha Ufundi Arusha. *(Makofi)*

Wapo wageni 100 wa Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, ambao wengine tulikuwa tumewatangaza asubuhi, lakini wengine waliingia baada ya wengine kuwa wameshatangazwa.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Joseph Kamonga ambaye ni mpiga kura wake kutoka Ludewa Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Tunza Malapo ambaye ni Mdogo wake. *(Makofi)*

Wapo wageni nane wa Mheshimiwa Michael Kembaki ambao ni marafiki zake kutoka Jimbo la Tarime Mjini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wageni 11 wa Kikundi cha Sala kutoka Parokia ya Kiwanja cha Ndege Jijini Dodoma.  Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni leo.

*(Saa 7.22 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano kwenye bajeti iliyo mbele yetu, tutaanza na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, atafuatiwa na Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo ajiandae.

Simwoni Mheshimiwa Francis, Mheshimiwa Santiel yupo? Mheshimiwa Santiel, simwoni. Mheshimiwa Mwakamo? Mheshimiwa Mwakamo tayari, Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele. *(Makofi)*

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Wizara hii ya Ujenzi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa zawadi ya uzima, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka nguvu kubwa ya kuifungua Barabara ya Somanga – Lindi, tunamshukuru sana sisi wananchi wa Lindi na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Waziri Bashungwa na timu yake yote, Mheshimiwa Waziri huyu Bashungwa ni mchapakazi, ana upendo, anajituma, mzalendo, mpambanaji na ni mweledi wa kazi. Wananchi wa Lindi tumemuona Mheshimiwa Waziri Bashungwa alipokwenda Liwale mwezi Machi kuanzia tarehe 4-6 akasimamia Barabara ile ya Nangurukuru – Liwale, kuna sehemu ilikuwa na shida, Liwale ilijifunga na Nachingwea – Liwale ilijifunga lakini Mheshimiwa Bashungwa alisimamia, hakika Wanaliwale tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pia akaenda Somanga, amekaa kule kuanzia tarehe 4-10 lakini tarehe zingine kama za nyongeza mwenyewe anakumbuka, siku hizo zote siku nne mpaka tano usiku na mchana amefanya kazi, anasimamia ile kazi ya kurudisha yale Madaraja ya Somanga – Mtama, Mikereng'ende – Matandu na barabara ikafunguka. Tunashukuru sana, aliungana na timu ya Mkoa kule ikiongozwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Mama Zainab Telack na timu yake, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa na kazi ikafanyika. Mheshimiwa Waziri, wananchi

wa Lindi na Watanzania kwa ujumla tunashukuru sana. Siyo wananchi wa Lindi tu au Wanamtwara tunaokwenda kule, hata Watanzania wote walikwama kwenda Mikoa ya Lindi na Mtwara, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo, pale walipotengeneza yale madaraja, mimi mwenyewe nimepita, nimeenda kwenye Mwenge, lakini pia nilienda kuwafariji waliopata mafuriko, ikinyesha mvua tu kazi yote ile inakwenda. Tumwombe Mwenyezi Mungu mvua kubwa tena isinyeshe mpaka Mheshimiwa Bashungwa akajenge tena madaraja yale yenye uimara mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia itakapokuja kujengwa barabara ile, nimemsikia Mheshimiwa Waziri akisema kwamba tayari anataka kuifungua ile barabara, unataka ijengwe upya ile ya Somanga kwenda Lindi, barabara ile tunaomba wakandarasi wawe imara na wa ukweli na wa viwango, kwa sababu ile barabara ukiiangalia na ukalinganisha na barabara inayotoka Mbwemkuru kwenda Mingoyo ni tofauti na Barabara inayotoka Somanga kuja Mbwemkuru, ile Barabara ya Mbwemkuru kwenda Mnazi Mmoja ama Mingoyo ni barabara imara sana ilijengwa kwa uimara wake sana. Mheshimiwa Waziri na Injinia wake wanaifahamu, lakini hii Barabara ya kutoka Somanga kwenda mpaka Mbwemkuru hali siyo nzuri na ndiyo maana mvua ilivyofika ikazoa yale madaraja yale na ingeendelea madaraja zaidi ya hayo yangekwenda na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale, kilometa 175 *EPC+F*. Nimeona hapa kwamba azma ya Serikali inaenda kujenga ile, tunaomba tafadhali ijengwe kwa sababu yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri ameshuhudia Liwale kutoka Nachingwea ukienda Liwale amefika. Ukitoka Nangurukuru kufika Liwale, Waziri amefika. Hakuna barabara nyingine inayotoka Liwale kwa kutoka kwingine, ina maana ukishakwama Liwale hizi barabara mbili zikishajifunga hamna tena Liwale. Hakuna huduma za jamii, hakuna huduma za afya, hakuna chakula, hakuna mafuta *diesel*, *petrol* wala nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameshuhudia wiki tatu zile watu walivyopata shida kule Liwale, lakini naamini kabisa Serikali ya Dkt. Samia Suluhu inaenda kufungua zile barabara kwa njia ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Nanganga – Ruangwa. Nimeona katika barabara zile ambazo Waziri amezitaja katika vipaumbele anasema tuzipitishe kwa sababu zimeshafikisha kama 70% na kuendelea, mojawapo ni ile ya Nanganga kwenda Ruangwa, tunaomba ikaishe kwa sababu ile barabara ikinyeshewa mvua tena, kazi yote ile aliyoifanya inaenda kwisha, itaharibika bila mchezo kabisa bila kufikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya Nachingwea kuja Nanganga, ile barabara ina vijito vijito tu, hakuna mito mikubwa ya kuhitaji madaraja makubwa, kwa hiyo ujenzi wake hauna gharama sana. Ile barabara ingekuwa tayari imeshajengwa kwa njia ya lami, wakati ule Nachingwea tulivyojifunga ikawa haipitiki, Ruangwa hakupitiki na Liwale hakupitiki, kama ile barabara ingekuwa ina lami, tayari watu wa Nachingwea na Ruangwa wangezunguka hivi wakaja kupita njia ile na tayari wameunganisha ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tumtie moyo Mheshimiwa Waziri ili bajeti ipite, nawaomba sana ipite. Hebu tumuunge mkono, hebu mwoneni kwanza alivyomnyenyekevu, anavyojituma na alivyo mzalendo, hebu tumtie moyo tuipitishe bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Naunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii adhimu ili nipate kuchangia bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio makubwa ambayo taasisi yetu ya usimamizi wa barabara – *TANROADS* imeyapata, lakini zipo changamoto nyingi sana ambazo lazima tufanye mapinduzi kwenye taasisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia namna ambavyo taasisi hii ya *TANROADS* pamoja na Wizara wameshindwa kwa karibu miaka 20 kujenga Barabara ya Korogwe – Handeni – Kilosa – Mikumi. Barabara B127, barabara ya kitaifa, barabara inayounganisha Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *TANROADS* pamoja na Wizara wameshindwa kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Handeni – Kibilashi – Kiteto – Kondoa – Singida, barabara yenye takwa la kisera ya nchi hii, kuunganisha Mikoa ya Tanga na Manyara. Mimi nafikiri na ninaamini kwamba tatizo lipo katika muundo wa taasisi hii ya usimamizi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo hivi sasa *TANROADS* ni wakala, pamoja na mambo mengine inasimamiwa na sheria kama tatu. Sheria ya kwanza ni Sheria ya Wakala za Serikali *(Executive Agencies,* Sura 245) ambayo inaweka misingi ya ufanyajikazi na usimamizi wa *TANROADS* lakini ina-*establish* mamlaka za usimamizi, inamtaja Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, inataja Bodi ya Ushauri kwa Mheshimiwa Waziri na inataja Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara, sheria hiyo ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya pili ni Sheria ya Barabara *(Roads Act)* Na. 13 ya mwaka 2007 na yenyewe hivyo hivyo inaweka misingi ya usimamizi wa shughuli za Wakala wa Barabara na inataja mamlaka za usimamizi. Inataja Wizara ya Ujenzi, Bodi ya Barabara za Mikoa na inataja Bodi za Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS Board)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya tatu ni Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta *(Roads and Fuels Stores Act,* Sura 220). Sheria hii inaweka utaratibu wa namna ya kukusanya ushuru kwenye magari yanayotumia barabara za umma na inaanzisha

vyombo viwili. Inaanzisha Mfuko wa Barabara na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sheria zinatupa *structure* ambayo ni *very complicated* na ambayo kimsingi inaweka urasimu, ndiyo maana kuna ucheleweshwaji mkubwa sana wa fedha za miradi na kuna kutokuwa na vyanzo mbadala vya uhakika kwa ajili ya ku-*finance* miradi, pia kunazalishwa riba kubwa sana zinazosababishwa na ucheleweshwaji wa malipo na kuna kucheleweshwa kwa miradi na kutekelezeka kwa miradi kwa gharama kubwa sana na mwisho wa siku hakuna ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mlolongo wa sheria nilioutaja na bodi mbalimbali ambazo zimeundwa na mamlaka tofauti, zipo Bodi za kuisimamia *TANROADS* ambazo zimeundwa na Waziri, zipo bodi ambazo zinaundwa na Mheshimiwa Waziri na ipo bodi inayoundwa na Mheshimiwa Rais, Mamlaka mbili zinaunda bodi za kusimamia chombo kimoja, hiyo ni *contradiction* ufanisi utakuwa mdogo na kutakuwa na urasimu kwenye maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kulishauri Bunge na kuiomba Serikali tukafanye mapinduzi, tuibadilishe *TANROADS* kutoka kuwa wakala na kuipa mamlaka kamili *(authority)*, tuipe mamlaka kamili kwani tukiipa mamlaka kamili zipo faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kama nilivyosema tutaondoa urasimu, tutaondoa ucheleweshwaji wa miradi, tutaondoa ucheleweshwaji wa fedha za miradi na tutawawezesha *TANROADS* kutafuta fedha wenyewe na kusimamia fedha zote ambazo zinatokana na vyanzo vya tozo za barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu huu wa *TANROADS* katika muundo ambao nashauri tubadilishe iwe mamlaka kamili, umetupelekea sisi wananchi wa Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Morogoro, hatujawahi kuunganishwa na barabara ya lami kama sera inavyotaka. Mkoa wa Morogoro una wakazi karibu milioni tatu na Tanga milioni mbili na kitu, unawanyimaje fursa wananchi hawa ya kuwaunganisha kwa barabara ya lami kwa miaka zaidi

ya 20? Barabara ambayo ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya 2005 - 2010, 2010 - 2015, 2015 – 2020 na 2020 - 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Serikali wanataka kukiambia nini Chama Cha Mapinduzi, kwamba wameshindwa kutekeleza ilani ambayo tumewapa kuitekeleza? Wanatuambia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kutaja barabara hapa, barabara ambazo zinaunganisha Wilaya na Wilaya za zaidi ya kilometa 50 hadi 60, inashindikana nini, barabara inayounganisha mkoa na mkoa, barabara hii ambayo imebeba uchumi mkubwa wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape taarifa tu barabara hii zamani ilikuwa inaitwa *The Sisal and Sugarcane Plantation Economy Great Road,* toka mwaka 1940 mpaka miaka ya 80, barabarahii imeubeba uchumi wa nchi yetu. Kwa nini barabara hii haijengwi kwa kiwango cha lami? Ni nani ananufaika na Handeni isipofunguka? Nani ananufaika na Tanga isipofunguka? Tanga tuna bandari. Nani ananufaika na Bandari ya Tanga isipofunguka kwa kutojenga hizi barabara mbili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwenye mshahara. Nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwenye mshahara kama safari hii hatutapata majibu kuhusu hili suala. Miaka karibu minne toka mwaka 2020, inatengwa kwenye bajeti haitangazwi, ni kitu gani hiki? Wananchi wa Tanga na wananchi wa Morogoro wamekuwa waaminifu kwa Chama Cha Mapinduzi. Siku zote tumepiga kura kukichagua chama kwa kura nyingi na wakati mwingine tunaongoza kitaifa. Kwa nini wanatufanyia hivi? Kwa nini wanatufanyia hivi? Kwa nini wanatufanyia hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasubiri kipengele cha shilingi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Reuben. Sasa namwita Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, atafuatiwa

na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami natumia nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia jioni ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu ya kwamba Wizara hii inayo majukumu mengi sana, lakini inayo kazi kubwa sana ya kuhakikisha mtandao wetu wa barabara na miradi mingine ambayo inaisimamia inapata fedha za kujengwa na kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii walau kwa sekunde chache pamoja na changamoto zilizopo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kuhakikisha kwamba pamoja na changamoto walizonazo barabara zinajengwa na panapotokea changamoto, basi changamoto hizi zinatatuliwa kwa kiwango kinachostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru sana Serikali na nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, chini ya msaidizi wake Mheshimiwa Bashugwa ambaye kiukweli amekuwa kiungo mchezaji wakati wote na kama ni mchezaji, basi amekuwa ni *super sub* kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwa Daraja la Busisi, ambalo leo tunapozungumza limefika takribani 88% kwa mujibu wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri hapa. Maana yake ni nini, Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia na *slogan* yake ya kazi iendelee, inadhihirika kwenye suala hili ambalo watu wote wanashuhudia na hata wanapopita kwenye ile njia mbadala kuna kazi kubwa sana imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuzungumzia barabara moja peke yake ukiacha zingine nyingi na hii ni kutokana na maelezo ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri namna ambavyo amejipanga kuboresha barabara za kwenye majiji. Hakuna namna tumeshachagua, tunayo majiji takribani saba

yenye sifa ya kuwa majiji, halmashauri nyingine yoyote ile ingeweza kuwa jiji kama sifa hizo zingefikiwa kama ambavyo leo Dodoma imekuwa Jiji na kufikia sifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara katika Jiji la Mwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuitambua tena, Barabara ya kutoka Mwanza Mjini kwenda Usagara, inayopita Kata za Igogo, Mkuyuni, Butimba, Mkolani, Nyegezi, Buhongwa mpaka inakwenda Usagara na inakwenda kuungana na Daraja la Busisi, barabara hii *design* yake imekamilika kujengwa mwaka 1994 ikiwa ina umri wa miaka 20 leo imefikia umri wa miaka 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna namna barabara hii inaweza kuacha kujengwa sasa na tena ijengwe kwa kiwango cha barabara nne cha zege la lami ya barabara bora kabisa. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri ameitaja kipekee kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Mwanza, kufanya upanuzi wa Barabara ya Mwanza - Usagara kwenye Daraja la JPM kwa njia nne yenye jumla ya kilometa 37 na ukasema unaanza na Mwanza – Usagara yenye kilometa 22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na sina shaka atakwenda kulisimamia hili na sisi tutamuunga mkono. Leo unapozungumza kukamilika kwa Daraja la Usagara, meli kubwa ya *MV* Mwanza, meli ya *MV* Umoja, kuboresha miundombinu ya bandari, kuboresha miundombinu mbalimbali kwenye mji na kujenga *SGR* kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na kutoka Isaka kuja Mwanza; Mheshimiwa Waziri hakuna namna Mji wa Mwanza unahitaji mtazamo wa peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiji hili ni kubwa na ndiyo kitovu cha Mkoa na Kanda ya Ziwa. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwa mpango huu mzuri alionao sina shaka na barabara hii na nimwombe hata kama itaanza kujengwa kwa hatua. Tumesema kilometa 22 hata kama zitaanza 10 kwa awamu ya kwanza watu wa Mwanza tutamshukuru kwa sababu tunakokwenda itatokea siku Mwanza imejifunga hakuna atakayetoka pale kati kati ya mji na hii haitakuwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayoifanya na kwa kutazama peke yake. Nilikuwa naangalia hata kule Mbeya na lenyewe ni jiji kubwa kule kwa Mheshimiwa Spika, mkandarasi tayari ana 14%. Hii ni hatua nzuri sana, tuongeze *speed* kwa ajili ya kuyaboresha haya majiji kwani ndiyo yanayoleta sura ya Tanzania na uboreshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili niwapongeze sana watu wa *TBA,* Mkurugenzi Ndugu Shabaha pamoja na wasaidizi wake akiwemo ndugu yangu Urio, Meneja wa pale Mwanza. Kazi waliyoianza sasa ni lazima mashirika haya yatoke kwenye kujenga makazi peke yake na sasa yaendelee na utaratibu wa ujenzi wa makazi biashara. Hii ndiyo itakuwa njia peke yake ya kuyafanya mashirika haya kwanza yaendelee kuwa bora; pili yaendelee kuwa imara na hata pengine yaendelee kuwa *sustainable* kwa sababu bila kufanya hivyo tutabaki na nyumba nyingi ambazo zitakuwa ni nyumba za makazi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana mpango mzuri; tuwasaidie Mheshimiwa Waziri na Wizara yake inaweza sana. Makazi ya walimu na wauguzi ni tatizo. Kupitia *TBA* wanaweza kufanya jambo kubwa ambalo litakuwa faida kwa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane kwamba pamoja na mambo mengine changamoto zilizopo kati ya *NMC*, TAMISEMI pamoja na *TBA* wenyewe Serikali ilishaamua kupitia *GN* zake kwamba maeneo mbalimbali yaliyotwaliwa na *TBA* yaendelee kuwa chini ya umiliki wa *TBA*. Hakuna sababu ya kugombania fito, nyumba ni moja tukubaliane mambo yaende na wakala afanye kazi yake inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo tutakuwa tunaisaidia sana Wizara na tutakuwa tunaboresha sana mazingira mbalimbali ambayo mwisho wa siku tutasaidia wananchi wetu, tutasaidia na mazingira ya kibiashara na mashirika haya yatakuwa na uwezo wa kujiendesha pasipo tu kutegemea kodi ya wapangaji wa kawaida bali kwenye mfumo wa kibiashara ambao sasa wanaanza kuelekea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana na nirudie tena kusema nampongeza sana Mheshimiwa Bashungwa na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, nikiwa nimebeba matumaini ya watu wa Mwanza na Nyamagana kwamba sasa Barabara ya kutoka Mwanza Mjini kwenda Usagara itajengwa kwa kiwango cha njia nne. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya na wafuatao wajiandae: Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza jioni ya leo kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwekeza fedha nyingi kwa ajili ya kuboresha na kuleta maendeleo katika miundombinu ya barabara na madaraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia katika taarifa iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri, miradi mingi imekamilika, ipo inayoendelea na mingine ambayo inatarajiwa kuanza kutekelezwa; nampongeza sana Mheshimiwa Rais. Pia, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kutatua changamoto zilizotokana na mafuriko yaliyotokana na mvua za *El-Nino* pamoja na Kimbunga Hidaya ambacho katika Wilaya yetu ya Kilwa ni miongoni mwa wilaya ambazo zimeathirika sana na janga hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika zile shilingi milioni 72 zimefanya kazi kubwa sana ya kutukwamua na kurudisha hali ya mawasiliano katika Barabara zetu za Dar es Salaam – Somanga kwenda Lindi na Mtwara; Barabara inayokwenda Liwale sasa hivi zinapitika na hata ile Barabara inayokwenda Kipatimu kwa taarifa ambazo ninazo hivi sasa tayari imeshatengenezwa umbali wa kilometa 20 na sasa inaendelea kukarabatiwa hadi kufikia Kipatimu na sasa wapo Namayuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri. Amefanya kazi kubwa sana kututoa katika hali ambayo kwa hakika tulikuwa tumekwama katika Wilaya ya Kilwa na wananchi wa Mikoa ya Kusini kwa ujumla na kutuleta katika hali ya sasa ya kupitika kwa barabara zetu. Nawapongeza watumishi wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, nawapongeza watumishi wa *TANROADS* na *TARURA* kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza *RC* wetu Mheshimiwa Zainab Telack, Mheshimiwa *DC* Bwana Mohamed Nyundo, Mwenyekiti wetu wa CCM wa Mkoa wa Lindi pamoja na Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Kilwa Ndugu Said Timami kwa kazi nzuri na kuungana vizuri na Serikali katika kuhakikisha kwamba Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa na kuhakikisha barabara hizo zinapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vile vile kupongeza kauli ambayo Mheshimiwa Waziri aliitoa ya kuridhia Barabara inayotoka Kipatimu kupitia Nandete kwenda mpaka Nyamwage iweze kupandishwa daraja na iweze kuhudumiwa na *TANROADS* hivi karibuni na kwamba umetuhakikishia fedha ipo. Naomba ushikilie hapo hapo kwa sababu barabara hii itakuwa mwarobaini pale inapotokea changamoto kwenye barabara kuu inayopita Somanga na Njia Nne, basi gari zinaweza zikazunguka kupitia Kipatimu zikatokea Nyamwage zikaendelea na safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwenye bajeti ya mwaka jana wananchi wa Liwale na Kilwa tuliahidiwa kwamba Barabara ya Nangurukuru - Liwale ingejengwa kwa kiwango cha kilometa 72 kwa kiwango cha lami. Katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri nimeona ameitaja kama barabara ambayo imekamilisha ile tunasema *feasibility study* kilometa 210 jambo ambalo lilizungumzwa hata mwaka jana na wakasema baada ya kukamilika *feasibility study,* kazi itakayofuata ni kujenga lami kilomita 72 kutokea Liwale lakini sijaiona ikizungumzwa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri atakapokuja ku-*wind up* atuambie lile tamko la mwaka jana la kujenga kilometa 72 limefikia wapi? Tupo kwenye manunuzi au tupo wapi au walisahau kuweka kwenye hotuba yake? Pia, katika barabara hiyo hiyo naomba nishauri kwamba tusilazimike, lazima tujenge kilometa 72 zote kwa mwendelezo kwa sababu barabara ile yeye alishuhudia mwenyewe kwa *chopper* na kwa mguu alipokwenda kuitembelea. Ilikuwa imekatikakatika katika maeneo mengi; zaidi ya maeneo 15 yalikuwa yamekatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba zile kilometa 72 zimegwemegwe kulingana na hali mbali ya vipande vya barabara vilivyopo katika barabara ile. Pia, ningependa nizungumzie Barabara ya Somanga – Masaninga. Barabara hii ilikamilika kujengwa na kuzinduliwa mwezi Disemba, 2004. Barabara hii ilijengwa na kampuni ya *CGC* kutoka China. Kwa uhai wake mpaka yalipokuja kutokea haya madhara ya mafuriko imedumu kwa miaka 19 na nusu. Je, hayo ndiyo yalikuwa matarajio yetu barabara hii idumu kwa miaka 19 na nusu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba barabara hii ilipojengwa ilijengwa kwa teknolojia ya kizamani ikasababisha sasa baada ya kuwa Mikoa ya Kusini imefunguka kwa kuwa na madini ya jasi ya kutengenezea *cement*, magari yale yameweza kukandamiza lile tuta hadi limetitia. Pia, barabara hii imetumia teknolojia ya kizamani kiasi kwamba imetumia ma-*culvert* ya bati badala ya ma-*culvert* ya zege au madaraja ya zege. Pia, barabara hii tuta lake lilishaharibika kabla ya kutokea hizi mvua za *El-Nino* kwa hiyo hizi zimekuja kumalizia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaishauri Serikali iandae mpango mzuri wa matengenezo ya hii barabara ili iweze kutumika kwa kiwango cha kudumu kwa muda mrefu zaidi ya miaka 19 kwa kunyanyua tuta upya kutoka Somanga hadi Masaninga.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpe taarifa mzungumzaji anachangia vizuri sana. Hii barabara ya Kibiti – Lindi Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, marehemu Dkt. John Pombe Magufuli alishasema kwamba imejengwa chini ya kiwango, kwa hiyo barabara nzima hii inatakiwa irudiwe upya ujenzi wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Ndulane kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuinua tuta ningeomba yale ma-*culvert* yote ya bati yaondolewe katika kipande cha Barabara cha Somanga – Masaninga. Pia ningeomba maeneo yaliyo jirani na madaraja tutakapokuwa tumejenga madaraja mapya yajengewe kuta za zege zilizo imara *(head walls)*.

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako umekwisha Mheshimiwa Francis, nimwite sasa Mheshimiwa Leah...

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimwite Mheshimiwa Leah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu. Mheshimiwa Stella Simon Fiyao na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay wajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa maoni yangu katika hoja iliyopo mbele yetu. Nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Bashungwa, Mheshimiwa Naibu Waziri wake Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya na

Katibu Mkuu *Engineer* Aisha pamoja na watumishi wote waliopo Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika mwaka huu kulikuwa na mvua nyingi sana katika nchi yetu, lakini nishukuru kwa Mkoa wa Simiyu katika Jimbo la Meatu tumeweza kuzipita hizi barabara kutokana na juhudi zilizofanywa na *Engineer* Mkumbo, Meneja wa *TANROADS,* Mkoa wa Simiyu kwa kushirikiana na wataalam walio chini yake. Pia, tumekuwa na bahati Mkoa wa Simiyu tulikuwa na *Engineer* Mkumbo aliyeenda Dar es Salaam na sasa hivi tena tuna *Engineer* Mkumbo. Kwa hiyo naamini kazi zao ni nzuri zilizotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi zilizofanywa nishukuru kwa Daraja lililojengwa katika Kijiji cha Mwanyagula lililogharimu shilingi milioni 309 katika *junction* ya Nkoma kwenda Makao. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Pia, nishukuru kwa kupokea fedha za dharura katika Jimbo la Meatu shilingi milioni 367 ambazo ziliwezesha kunyanyua tuta juu na kuweka changarawe na kutengeneza mifereji ya maji pamoja na kujenga ma-*culvert;* nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile imeimarika na kipande hiki cha barabara ni muhimu kwa uchumi wetu kwa sababu barabara hii inaenda kuingilia katika Daraja la Sibiti; nashukuru kwa kazi nzuri sana. Pamoja na kazi nzuri zilizofanywa za fedha za dharura nilitaka kuomba Wizara watusaidie tena katika fedha za dharura angalau tujenge daraja mojawapo katika ya Lyusa, Chobe au Mkoma kwa sababu bado yanaleta athari katika wafanyabiashara wetu na bado yanapoteza wananchi wakati wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ananisikia, Mheshimiwa Naibu Waziri ananisikia, Mkurugenzi wa matengenezo dada yangu Christina pia ananisikia. Nawaomba sana watupatie tena angalau daraja moja ili tuweze kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo letu, utekelezaji unaendelea vizuri wa Miradi ya *TANROADS* ikiwemo ujenzi wa Daraja la juu la Mto Itembe ambao umefikia 79%. Changamoto iliyopo mkandarasi amelipwa kwa 38% ambayo ni chini zaidi ukilinganisha na kazi aliyoifanya; anadai shilingi bilioni 2.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni hili limekuwa la zamani sana. Ni *certificate* mbili anadai na mkijua kwamba wakandarasi wetu wanakopa kwenye benki ambapo fedha hizi zinaongezeka riba. Naomba tuwasaidie basi ili waweze kumalizia kazi vizuri. Tulikuwa na kilometa moja ya lami, mkandarasi amemaliza, lakini toka aanze mpaka leo hajawahi kulipwa hata shilingi moja. Anadai shilingi milioni 706, naomba wamsaidie basi aweze kukamilisha kutuwekea taa 25 ili wanawake na vijana wa Meatu na Mwanuzi waweze kufanya biashara usiku na mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aweze pia kukamilisha mifereji ili kuwe kuna thamani ya kazi iliyofanyika. Ameshindwa kuendelea kwa sababu hajalipwa fedha yoyote. Mheshimiwa Waziri alipokuja kumkabidhi mkandarasi wa kujenga barabara ya kilometa 25 za lami katika maingilio ya Daraja la Sibiti alituahidi kilomita moja ya lami. Naomba na yenyewe aiweke tutaenda polepole hivyo hivyo angalau tuweze kupunguza vumbi pale mjini Mwanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze sasa niongee kwa upande wa Kitaifa na kimkoa. Kazi nzuri inafanywa na Mheshimiwa Rais wetu kwenye ya Daraja la Kigongo – Busisi almaarufu JP Magufuli ambalo sasa lipo 88% lenye urefu wa kilometa tatu; linategemewa kwisha Disemba, 2024. Nipongeze sana kwa kazi nzuri, kukamilika kwa daraja hili kutaboresha mawasiliano, kutaimaisha biashara na kutakuza uchumi kwa mikoa iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kutaimarisha ufanyaji wa biashara kwa sababu daraja hili wanatumia watu wa Mikoa ya Kagera, Geita na mikoa mingine pamoja na nchi jirani. Kwa hiyo tutapunguza muda tuliokuwa tunatumia kusubiria pale mpaka masaa mawili ambapo sasa tutapita kwa dakika tatu kwa

sababu pia tulikuwa tunavuka kwa dakika 30. Kukamilika kwa daraja hili kutapunguza gharama kwa mtu na gari ambapo walikuwa wanatozwa watu waliomo ndani pamoja na gari, lakini *ferry* zilizopo zitaenda kutumika katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, ili daraja hili liwe na tija zaidi kwa sababu pia wanasafirisha wafanyabiashara kutoka Rwanda na mikoa niliyoitaja kwenda nchi jirani ya Kenya, tuimarishe na tukamilishe Daraja la Mto Simiyu ambalo lipo 15%. Kwa sasa magari yanasubiriana wapite upande mmoja halafu wapite upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilishwa kwa Daraja la Simiyu ambapo litaisha mwakani naomba waongeze *speed,* kutaleta pia thamani ya utumiaji wa *SGR* yetu kwa sababu mizigo itatoka Mwanza na lengo ni kuongeza mzigo katika reli yetu ya *SGR* kwa kipande kile cha Mwanza. Mizigo itatoka pale Mwanza itakwenda Bandari ya Musoma baadaye itaenda *Port Bell* - Uganda ama itaenda katika Bandari ya Kisumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ipo haja ya kuimarisha daraja letu. Pia, barabara ya lami ya Nyanguge – Simiyu - Mara *border* ni barabara ya muda mrefu iliyojengwa 1982. Nimwombe Mheshimiwa Waziri waiweke katika mipango ya baadaye ya kujengwa upya tofauti na ilivyo sasa. Kama *SGR* itafunguka na Daraja la Magufuli litafunguka, ile barabara yetu imechoka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay na Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan wajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa

anayoendelea kuifanya; na hata taarifa au hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeeleza kwa mapana sana juu ya mafanikio ya Mheshimiwa Rais katika kipindi chake hiki cha Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vile vile kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote wanne, kwa maana ya Naibu Waziri, kaka yangu Mhandisi Kasekenya, Katibu Mkuu Balozi Mhandisi Aisha Salim Amor pamoja na Naibu Katibu Mkuu, kaka yangu Ludovick kwa kufanya kazi kubwa sana. Kwa kweli wanafanya kazi, hamna shaka kabisa. Ninaamini hata Waheshimiwa Wabunge wote tunakubaliana kwamba Mheshimiwa Waziri ana wasaidizi hao wanne ambao ni wataalam na ni wabobezi ndani ya eneo lake ambalo analisimamia kama kamisaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli ni Waziri ambaye kwa mkoa anaotokea, katika mazingira ya kawaida ya Watanzania wanavyojulikana anafanana sana na wajomba zangu wa Unyirambani kule Singida. Ninajua wanajulikana kwa sifa zipi, lakini yeye ni tofauti sana, yeye ni mtu rahim, ni mtu mwenye hofu ya Mungu, ni mtu mwenye upendo, ni mtu msikivu. Mheshimiwa Bashungwa yuko tofauti sana. Sitaki kwenda mbali inaweza kuwa kule si kwao, pole sana; lakini kwa kweli yeye ni kijana muungwana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu nilimwomba kuja jimboni, akiwa Waziri wa TAMISEMI, na akaja; na leo ahadi yake ya Barabara ya Makabe nzima kwenda Msumi mpaka Madale kilomita 11.2 alitoa agizo. Leo nataka nimwambie kwamba imekwishatangazwa na keshokutwa tarehe 31 ndiyo siku ya mwisho wa *submission,* barabara ile itajengwa; ni yeye. Leo amekuja Wizara ya Ujenzi amekuja tena jimboni. Kati ya barabara zenye kilio kikubwa kwangu kama Mbunge ni Barabara ya Victoria; kwa maana ya Mbezi kwa Yusufu kwenda Mpiji – Magohe kilomita 9.55 tayari amekwishazitangaza hapa ninavyozungumza, juzi tu ametangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimshukuru sana, yeye ni mtu muungwana. Ndiyo maana kuna Waheshimiwa Wabunge wanatamani aende kwa sababu akienda akisema jambo linakuwa. Haya makelele mengine ambayo anakutana nayo ni kwa sababu ya *collective responsibility* ambayo anayo kama Wizara; ameyakuta na yameganda. Ninampongeza sana, yale anayoahidi yeye analazimisha kuyasukuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nitangulie kuyasema hayo; lakini ni ukweli, kwa sababu ya muda wetu lazima wananchi wa Kibamba wasikie. Hapa tunawaambia tunapiga na siasa humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima watu wakubali, kwamba uchaguzi ambao watu waliufanya tarehe 28 Oktoba, 2020 ulikuwa ni uchaguzi sahihi wa kumpata mtoto wao, kijana wao Issa Bin Jumanne Mtemvu kuwa Mbunge wa Jimbo lile la Kibamba. Kiatu kimenitosha tofauti na aliyekuwepo miaka kumi iliyopita, yaani ni kuku na mwewe, yaani huwezi kuwalinganisha kabisa watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme mbele ya Bunge lako kuwa hapa ninao Waheshimiwa Wabunge zaidi ya 68 ambao ni wananchi wa Jimbo lile; hawatakiwi kutajwa kwa sababu wana maeneo yao wanayoyatawala. Ninaomba niseme kwa uchache, tunayo barabara au Mradi wa Barabara ya Goba – Matosa – Temboni, kilomita sita, amezisoma ndani ya taarifa yake. Kilomita moja tayari, na sasa hivi mkandarasi yuko kwenye kilomita ya tatu, yuko barabarani anajenga hiyo lami. Niliwahi kuwaambia hamjawahi kuona mnaona nyeusi sasa hivi ndani ya Jimbo la Kibamba. Pili, Kibamba shule – Mpiji Magohe kilomita 9.2 mpaka sasa mkandarasi yuko *site* na tunaendelea kwa kilomita ya tano sasa hivi, nami ndiko ninakoishi huko, kwenye hiyo barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikwambie Mbezi Makabe – Msakuzi – Mpiji Magohe, kilomita nane, hii ni barabara ya mkoa. Wamemaliza mita 500 na ninajua ndani ya mkoa wameingiza *almost* kilomita moja, sasa hivi wanaendelea nayo. Zuri zaidi ni kuhusu Barabara ya Kimara – Bonyokwa, nilisema

humu ndani. Hii ni barabara ya Waheshimiwa Wabunge watatu, dada yangu wa Segerea Mheshimiwa Profesa Kitila na mimi. Mimi niko Darajani Kimara pale, ndiye ninayeanza kwenye Tawi langu la CCM linaitwa *TANESCO,* tayari kilomita zote sita amezitoa na mkandarasi yuko *site*. Mimi nisemeje? Tayari mkandarasi yuko *site;* na ameeleza kwenye kitabu chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niwakumbushe tu, Barabara ya Makondeko – Kwembe kwenda Kisopwe inazungukia Mloganzila, kilomita 16, wameziacha. Juzi nimeeleza hapa kwenye swali langu la msingi lakini hizi wamezisahau na sasa hivi hawajaziingiza kabisa. Niwaombe sana waendelee kuikumbuka barabara hii ambayo ndiyo inayoingia kwa Mkuu wa Wilaya, kwa Mkurugenzi na kuelekea Kwembe Kati. Wananchi wengi wanakaa kule; zaidi ya wananchi 60,000 wanakaa kwenye hiyo barabara. Ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya leo, kwenye mwaka 2024/2025, kwenye bajeti tunayokwenda nayo; kwanza ninaiunga mkono mapema tu, nisije nikasahu hapo baadaye mambo yakaharibika. Hii bajeti ya maendeleo ya trilioni 1.7 humu ndani kwenye maendeleo kuna Barabara ya Mpiji – Magohe niliyoizungumza, amekwishaiingiza humu ndani. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, amekwenda na akapewa na zawadi ya mbuzi, mimi hata kuku kule sikuwahi kupewa. Ninaomba niseme hivi, yeye ni mtu muungwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengine huko kwao wanakokwenda wanakutana na changamoto, kama vile Mheshimiwa Flatei. Nimehuzunishwa sana na ile changamoto ya Mheshimiwa Flatei. Ninaomba, kwangu wametangaza, mkandarasi akishakwenda mimi nitabanana na yeye, nitabanana na mjomba wangu Waziri wa Fedha ili kuona kwamba fedha inatoka na inaelekea Mpiji Magohe ili hii barabara ya kilomita 9.55 iishe kama ambavyo inatakiwa. Barabara hii…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari! Ninakushukuru sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay na wajiandae Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan na Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hii Wizara muhimu, hasa kwa kuwa ninatambua mchango mkubwa wa Wizara hii katika maendeleo ya Taifa letu na hasa ukizingatia zaidi ya 90% ya watu na abiria wanatumia njia ya barabara. Kwa hiyo ni barabara muhimu na ni kitu muhimu sana kwa ajili maendeleo ya Taifa letu. Kwa hiyo ina mchango mkubwa sana katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Bashungwa pamoja na Naibu Waziri na timu yao nzima; ni kwa mara ya kwanza ninapongeza. Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, lakini hatukunyongi, tunakupa haki yako mapema ili usife kabla hujaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana kwa namna ambavyo wamekuwa na utayari sana wa kuwatumikia Watanzania. Ndiyo maana asilimia kubwa ya Waheshimiwa Wabunge wanasimama hapa wanazungumzia utayari wao, namna ambavyo wamekuwa tayari katika kutumikia nafasi walizopewa kwa uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua changamoto mbalimbali ambazo zimetokea katika maeneo yetu. Nchi nzima tumekumbwa na adha mbalimbali zilizosababishwa na mvua nyingi zilizonyesha katika maeneo mbalimbali kama vile kubomoka kwa madaraja na kuharibika kwa barabara. Katika maeneo mengi tumeona yeye na Naibu Waziri pamoja na timu

yao nzima namna ambavyo wamepambana na kushughulika na kuyatatua matatizo kwa wakati. Katika hili ninawapongeza sana, wanastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi kabisa, ninawapongeza pia kwenye *issue* ya kuhakikisha wanawakumbuka wakandarasi wazawa na kuwapa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo inaendelea kwenye nchi yetu. Ni jambo zuri sana na wamefanya kitu kikubwa. Ninasema katika kumbukumbu za wazalendo kwenye Taifa hili watakumbukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba wamewakumbuka wakandarasi wazawa katika utekelezaji wa majukumu, mimi Stella ninaona kuna changamoto kubwa sana ambayo wasipotupatia majibu ninaona namna wakandarasi wazawa wanavyokwenda kukutana na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote tunajua kwamba wakandarasi wetu wa ndani asilimia kubwa hawana mitaji. Wengi wanategemea wakope benki halafu waende wakatekeleze miradi ya maendeleo. Tukisoma kwenye taarifa na kwa namna mbalimbali ambavyo tumeendelea kupitia tunaona namna ambavyo kumekuwa kuna kusuasua katika ulipaji wa fedha za wakandarasi. Sasa ninaiona changamoto kubwa ambayo inakwenda kutokea huko mbele. Hao wakandarasi wazawa ni kweli wamekwenda kuwapa kipaumbele ili watekeleze miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa ndani ya Taifa letu; lakini hatimaye watakwenda kukwamishwa na upatikanaji wa fedha za kulipa kwa ajili ya miradi hiyo ambayo wanaitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja atuambie ana mkakati gani wa kuwafanya wakandarasi hao wasiende kukwama na hatimaye mali zao zisikamatwe na benki na wala wasipoteze sifa za kukopesheka kwenye benki mbalimbali ambazo zimekubali kuwaamini na kuwapa mikopo ili waweze kulitumikia Taifa lao kwa uaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakapokuja ni vyema akatuambia wao kama Wizara wamejipanga vipi katika kukabiliana na changamoto hiyo ya ucheleweshwaji wa malipo ya wakandarasi ili tusiende kuwakwamisha wakandarasi wetu wazawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu ufinyu wa bajeti. Kuna changamoto kubwa sana na sisi kama Kamati tumeendelea kushauri siku zote, kwamba, ili walau tuvuke tuwe na trilioni tano. Kwa sababu tunajua kwamba miradi mingi ipo na inaendelea kutekelezwa huko kwenye maeneo yetu na pia miradi mingi ni mipya inangojea kutangazwa ili iendelee kutekelezwa. Vilevile kuna miradi mingi ambayo ilikwishakamilika kabisa na wakandarasi bado wanadai fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kwenye *issue* ya bajeti, kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo tuna trilioni 1.7. Ni nini tunachokwenda kufanya ilhali tukiangalia tuna mlundikano wa madeni ya bilioni 915 ambazo tunadaiwa na wakandarasi? Ni kitu gani ambacho tunakwenda kukifanya ili tuhakikishe kwamba mahali hapa tunavuka? Kwa sababu hatimaye ninaona ongezeko kubwa la deni linakwenda kuonekana hapa. Riba za miradi iliyotekelezeka zitaongezeka, miradi mipya kuna wakati itasimama kwa sababu ya fedha. Bajeti tuliyonayo ni ndogo, haitoshi na ndiyo maana kama Kamati tumeendelea kushauri kwamba walau Serikali itutengee trilioni tano ili tuweze kuvuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumzia miradi ya barabara, Mfuko tu wa Barabara sasa hivi unatekeleza miradi kwa 40.8%. Maana yake ni kwamba miradi mingi inakwama na ndiyo maana barabara nyingi zinakufa kabla ya wakati kwa sababu hazirekebishwi pale zinapotokea changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona kabisa mzigo mkubwa ambao Wizara wanao huko mbele, lawama kubwa ambazo tutawatupieni. Mwisho wa siku tunaomba waje na majibu ni namna gani wamejipanga ili kukabiliana na changamoto ambayo tunaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu kulikuwa na mvua za kutosha na mwaka 2025 tunaouendea mvua hazijazuiliwa kunyesha, bado zitanyesha, bado changamoto iliyotokea sasa hivi inaweza kutokea hata mwaka ujao. Ni namna gani wamejipanga kukabiliana na hii changamoto ili hatimaye tuwaondoe wananchi wetu kwenye shida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ninalotaka kuzungumzia ni kuhusiana na habari ya malipo ya fidia ya wananchi waliopisha maeneo mbalimbali ya miradi ya barabara. Wananchi wangu wa Songwe ni miongoni mwa hao wananchi, vilevile Rukwa na maeneo mengine. Nchi nzima tunaona kuna deni la trilioni saba. Fedha hizi ni kwa ajili ya kuwalipa wananchi waliopisha miradi mbalimbali ya barabara. Hii haileti sura nzuri, wananchi wamekuwa na malalamiko makubwa, wengine wanasema Serikali tuambieni ili tuyaendeleze maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi fikiria umemsimamisha mwananchi kwa miaka 10 hadi 20 ambapo hawezi kuendeleza eneo lake, anafika mahali analiacha na Serikali hawajamlipa fidia na hatimaye tunazungumzia trilioni saba. Sasa, tusishangae kwamba miaka ijayo deni likawa ni mara mbili ya trilioni saba, kwa sababu tathmini waliyoifanya mwaka 2000, tathmini waliyoifanya mwaka 2005, waliyoifanya mwaka 2010 haitakuwa hivyo huko mbele tuendako. Tafsiri yake ni kwamba deni litakuwa kubwa zaidi ya trilioni saba tunayoizungumzia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali watoe majibu kwa wananchi. Ikiwa kuna maeneo wanaona kabisa hawatayahitaji hapo mbeleni wawaambie wananchi wayaendeleze. Wananchi waendelee kuyaendeleza maeneo yao ili wanufaike nayo. Hebu fikiria umemkalisha mwananchi miaka 20 hajaliendeleza eneo lake halafu hatimaye Serikali inakuja na majibu kwamba haiyahitaji hayo maeneo na haitayatumia tena, hivi hao wananchi waliowakalisha muda mrefu namna hiyo watawalipa riba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie yale maeneo yenye uhitaji muhimu na wawalipe wananchi fidia na yale

maeneo ambayo wanaona hayatahitajika kwa haraka wawaambieni wananchi wayaendeleze kwa sababu hatimaye wanawapa wananchi shida, kwa sababu hawataweza kuyaendeleza maeneo hayo, hawatawezi kujenga, hawatawezi kufanya chochote. Wamekaa wanasubiri Serikali ije iwalipe fidia na hatimaye tukiangalia kwenye bajeti tunaona Serikali haitavuka kwenye kuwalipa wananchi fidia kwenye hayo maeneo…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** … Serikali watoe majibu ya msingi ili wananchi waendeleze maeneo yao na wanufaike nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na kwa mara ya kwanza ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fiyao.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni ambao wametutembelea ndani ya ukumbi wetu. Kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Ali Mohamed, Viongozi wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Jimbo la Shaurimoyo kutoka Mjini Magharibi Zanzibar. Naona hawajaingia.

Tuna viongozi wanne wa Kamati ya Utekelezaji ya Umoja wa Vijana Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) kutoka Kata ya Kikuyu Kaskazini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wale watatu kumbe nao wapo, hebu ninaomba msimame tena. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Sasa nimwite Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba na Mheshimiwa Mary Francis Masanja wajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia

siku hii ya leo kuwa mahali hapa na kuweza kujadiliana mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. Aidha, nitoe pole nyingi kwa Watanzania wote waliopoteza ndugu zao katika kadhia mbalimbali mwaka huu kutokana na hali ya mvua nyingi zilizonyesha, lakini pia Mwenyezi Mungu awapokee katika ufalme wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa zinazofanyika katika majimbo yetu katika sekta mbalimbali, lakini pia na Serikali nzima ya Awamu ya Sita. Kazi nyingi zimefanyika. Pia nichukue nafasi hii kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri Bashungwa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwa kupongeza kazi nyingi zilizofanyika kwanza, baada ya hapo nitayasema yale yote yenye makengeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze hii Wizara, Mheshimiwa Waziri na timu yake; kwa sababu mimi kwenye Jimbo la Mbulu Mjini huwa niko kwenye mzunguko wa Bonde la Ufa, kwa mwaka huu ambao ulikuwa na mvua nyingi sana wameitendea haki Barabara ya Magala. Wananchi wangu wametembea mwaka mzima, wamesafiri na kila nilipompigia simu yeye ni mnyenyekevu sana; alipiga simu na alitoa maelekezo. Yote yale yalisaidia watu katika Jimbo la Mbulu Mjini kusafiri; kwa sababu Mlima Magala haupo popote Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mlima wenye kona mia kumi na tatu, mia ishirini ambapo kila Waziri aliyekwenda aliniambia hii ndiyo barabara yako? Hata Mheshimiwa Rais alipokuwa Makamu wa Rais alipokuja kuniombea kura alipopita Mlima Magala aliniuliza hii ndiyo barabara yako Mheshimiwa mgombea? Nikamwambia ndiyo Mheshimiwa Makamu wa Rais. Akasema sasa baada ya uchaguzi uje kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti kazi kubwa wameifanya hata bila kwenda kwake; na zaidi nikituma meseji huwa anawapelekea na

wao wanafanya kazi kubwa sana. Kwa hilo tu ninawashukuru, kwa sababu hata yeye alisafiri kwenye ule mlima. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri alikuja jimboni kwangu, alifanya ziara, alikwenda kijijini. Mbulu Mjini si mji, kuna kata za pembeni. Tulipokwenda aliniuliza, je, kule ni Babati nikamwambia ndiyo. Tulipokwenda kata nyingine akasema huku ni Monduli? Nikamwambia ndiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiografia ninapakana na majimbo manne na hayo majimbo manne ni pamoja na eneo la katikati la mji na kata za pembezoni. Ninazungumza hivyo kwa sababu eneo hilo la Mbulu Mjini ni eneo lenye milima na wakati wa mvua hali ya usafiri inakuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi kubwa waliyoifanya na vilevile kwa kazi kubwa inayofanyika Mlima Magala. Alipokuja nilimwambia atarudi bila kupita Mlima Magala kwa sababu watamficha akaniambia nimwambie ninataka kufanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika na juzi ameniambia kwamba ataunganisha viraka vyote vya Mlima Magala na kilomita zote nane zitakuwa za zege, kwa maana ya kuunganisha vile vipande. Hongera sana na timu yake. *TANROADS* Manyara wanaitendea haki nafasi yao kwa Barabara ya Magala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ambayo ninataka kuizungumza ni kuhusu hii bajeti yetu tunayoizungumza. Ninaomba niokoe muda. Kwanza tusimlaumu sana Waziri wa Ujenzi. Sisi tunatambua kabisa kwamba yeye anagawiwa fedha. Hali ya upatikanaji wa fedha ndiyo iliyotufikisha hapa. Ninachotaka kufahamu ni kwamba, kama mwaka jana tulisaini mkataba kule Jakaya Kikwete wa barabara zile saba kilomita 2,035, tukategemea kazi inaanza kwa wakati, yaliyojiri hadi leo, baada ya mwaka mmoja, hakuna hata barabara moja mkandarasi ameenda *site*. Maelezo haya ya Waziri, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, haya ameandikiwa, sio yake kwa sababu yeye ni mtu muungwana, asiyependa hila wala

asiyependa kuyaandika hayo. Kwamba Serikali itaendelea na mazungumzo, ule ukurasa wa 36, Serikali itaendelea na mazungumzo na wafadhili ili kupata fedha za kutekeleza miradi hiyo ya *EPC+ Finance* kuhakikisha kwamba Waheshimiwa Wabunge kuwa dhamira ya Serikali ya kutekeleza miradi hii iko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tulisaini mkataba baadaye tunakwenda kuzungumza na wafadhili na wananchi waliona ile mikataba hadharani tafsiri yake kwetu sisi ni nini na wananchi ambao wanasubiri zile barabara? Nimwombe Mheshimiwa Waziri akae na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, wakati atakapokuja pale aseme barabara hizo zitaanza kutekelezwa tarehe fulani kwa kila barabara hapa nchini. Hapo ndipo tutakapomwelewa na bajeti yake itakuwa imeng'ara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni barabara ya Mbulu – Garbabi, kipande cha kilometa 25, mkandarasi alikwishaondoka. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, awe msikivu kwetu. Yeye anakuja na *handbag* yenye sura nzuri ambayo imeandikwa Bajeti, lakini anatuingiza kichakani. Tumekuja tumesaini mkataba, kazi imeanza, tuna miaka miwili kule Garbabi hakuna hata kipande kimoja cha lami na mkandarasi ameondoka. Nimekwenda kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, nimemwomba sana, amenisihi sana, tunamheshimu lakini mbona tunakwenda vibaya? Mheshimiwa Waziri asicheke yaani hali ni mbaya kule na jimbo langu halikaliki, kwa kweli nimwambie kabisa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Bashungwa afanye ziara atembelee pale ili aone hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivunja nyumba za wananchi, yapata miaka miwili sasa, hakuna kilichofanyika, hakuna lami hata kilometa moja, mkandarasi alikwishaondoka, sasa watuambie anarudi lini, kazi hiyo inakamilika lini na iko nyuma ya wakati, sasa hivi iko 28%, tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inatuchanganya na inatuchonganisha sisi na wananchi, inamchonganisha Rais na

wananchi wake na hasa wananchi wenye kutegemea hiyo ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumza Barabara ya Karatu - Haydom – Mbulu – Sibiti, yaani hapo kwa Mkoa wa Arusha, Manyara, Singida na Simiyu, kila mwananchi anasubiri barabara hii itakuja lini? Kwa hiyo, tumewafurahisha wananchi, lakini matokeo hayajaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza kwamba, kama inawezekana sentensi hii waiondoe na watuambie wakandarasi wanakwenda kufanya kazi hii lini kwa sababu tulikwishasaini mkataba? Kwanza tunapata hasara kubwa sana kwa ajili ya miradi inayochelewa kama hii ambayo sasa hivi mkandarasi anaacha kazi anasubiri gharama za ucheleweshaji tu baada ya muda na baada ya mradi kukamilika inaweza kuwa ni mara mbili ya gharama halisi ya mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuzungumza ni eneo la Laban. Mheshimiwa Naibu Waziri Kasekenya na Mheshimiwa Mbarawa walikuja wakasema tunakwenda Haydom kusaini Mkataba, leo hii wanasema mkandarasi ataanza kazi baada ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara niliikataa hapa Bungeni nikasema, kwa hali ninayoiona Mbulu – Garibabi tusiende Haydom. Hebu tekelezeni hii ya Mbulu – Garibabi ikikamilika tekelezeni hii ya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issaay, malizia

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda wapi?

**MWENYEKITI:** Malizia dakika zako zimekwisha.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hii bajeti haina uhalisia na leo siungi mkono hoja mpaka nitakapoona matokeo mapya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ninamwita sasa Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, atafuatiwa na Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba na Mheshimiwa Mary Francis Masanja na Issa Ally Mchungahela wajiandae.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara ya Ujenzi. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya uhai na pumzi. Pia, napenda kumpongeza Rais wetu Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapa pole ndugu zangu wa Lindi (Jimbo la Mchinga, Lindi na Kilwa), kwa maafa makubwa na mafuriko makubwa waliyoyapata kutokana na Kimbunga cha Hidaya, nawapa pole sana na wale ndugu zetu wawili waliopoteza maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya nchi yetu inatekelezwa chini ya kiwango, viwango na ubora wa miradi yetu inayotekelezwa mingi iko chini, sielewi kwa nini. Kuna Barabara ya Kibiti – Lindi – Mingoyo, hii barabara tangu imetengeneza kipindi ambacho kabla haijakabidhiwa, barabara ilikuwa imekwishabomoka. barabara ina mashimo makubwa kabla haijakabidhiwa, viraka zaidi ya milioni 10. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninashangaa, mimi ni mtu wa manunuzi, nashangaa na mpaka leo ninashindwa kuelewa, *BOQ* zimeandaliwa, wanunuzi wapo, Ma-*engineers* wapo, wasimamizi wa miradi wapo, shida ni nini? Hivi hawa wakandarasi wanaotuletea barabara mbovu za chini ya kiwango kwa nini hawachukuliwi hatua? Fedha za nchi yetu wakati mwingine zinakwenda vibaya, Mkandarasi analipwa, lakini kiwango cha barabara ni kibovu (kiwango kiko chini kabisa). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafuriko ya Hidaya ile barabara hata kabla haijaanza kutumika ilikuwa ni mbovu. Sasa ilipokuja Hidaya ikatafuta sababu na sababu ikapatikana. Barabara imesombwa kweli kweli na madaraja katika sehemu nyingi sana. Hata hivyo, ukiiangalia barabara tangu mwanzo kabla ya mvua hii kunyesha mpaka imekuja *El-Nino* yenyewe na ikaja Hidaya, ile barabara inakatisha tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara inakatisha tamaa na inaweza kusababisha ajali na ajali nyingi zinatokea kwa sababu ya mashimo. Ile barabara ukienda yaani vile viraka vinatia kichefuchefu. Unajiuliza hii barabara ni ya *design* gani? Niombe Mheshimiwa Waziri na timu yake, wanapokwenda kurekebisha ile barabara sehemu zilizoharibika waiangalie na barabara yote, ile barabara ni mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale; Wabunge wengi wanaotoka Mikoa ya Lindi na Mtwara wanaposimama hapa hii barabara lazima waizungumzie. Barabara hii kila siku tunaililia, sawa, mwaka 2023 ilisainiwa kwa Mradi wa *EPC+F*. Nimwombe Mheshimiwa Waziri hebu tuangalie Mikoa ya Lindi na Mtwara, hatuna mtandao mkubwa wa barabara zaidi ya Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea. Tunashukuru barabara inaendelea vizuri na Mheshimiwa Waziri kazi yake inaonekana, niwape maua, wote wanafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale, barabara hii ni muhimu sana. Kule Masasi, Nachingwea na Liwale watu wanalima sana korosho, ufuta na mbaazi, barabara zile ndiyo zinazotegemewa peke yake. Niombe sana Mheshimiwa Waziri, najua na nimeangalia kwenye randama yake ukurasa wa 116 inaonesha barabara hii inajengwa kwa fedha za ndani, sijaona fedha za nje. Nimwombe sana Waziri wangu wajitahidi kutujengea barabara hii, ni barabara ya kimkakati na hatuna barabara nyingine, tangu wazazi wetu wamezaliwa mpaka sisi tumezaliwa na wengine wamekufa hatujawahi kuiona lami kwenye barabara zile. Tunaomba kidogo

watuangalie kwa jicho la huruma na sisi tujisikie sawa na wenzetu, tugawane keki ya Taifa hili wote kwa usawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na barabara hiyo, kuna wale watu waliopisha mradi wa barabara hiyo miaka minne. Waliambiwa wavunje nyumba zao, waliacha kuendeleza, wametoka kwenye zile nyumba na hawajui hatima yao. Hatima zao hazieleweki mpaka leo wapowapo tu, wanashindwa kufanya mambo yote ya maendeleo, barabara haijengwi na hawajui itakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Viwanja vya Ndege Lindi, Nachingwea na Kilwa, nimejaribu kuangalia humu sijaona. Kuna Mradi mkubwa wa *LNG* ambao unakuja kufanyika pale Lindi wa kuchakata gesi asilia.  Hivi kweli, nakumbuka kauli ya Mama yetu mpenzi Dkt. Samia Suluhu alisema kwamba, kwa sababu mradi mkubwa unakwenda Lindi, barabara na viwanja vya ndege vijiandae na vitengenezwe vizuri kwa ajili ya kupokea wageni. Inasikitisha, sijaona sehemu inayoonesha viwanja vile vinatengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kiwanja cha Nachingwea, wakati mwingine ndege inashindwa kutua kwa sababu ya vumbi. Ikitaka kutua vumbi ni kali sana ndege inaamua kuondoka kwenda kutua Mtwara. Sasa hii si ni hatari jamani? Pia, kuna wakati mwingine inatua kwa kulazimisha, tunaomba watufikirie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kiwanja cha ndege kwa hawa waliopigania uhuru wa nchi za jirani walikitumia, kina historia kubwa lakini nimepitia humu sijaona Kiwanja cha Ndege cha Lindi, Kilwa wala Nachingwea, naomba watusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara nyingine ya kutoka Njia Nne – Kipatimu kilometa 50, tunashukuru tumetengenezewa kilometa mbili bado kilometa 48. Tunaomba sana barabara hii ni ya kimkakati, tunaomba sana tusaidiwe tupate barabara hiyo. Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*windup* hapa tunaomba atusaidie atupatie na sisi tujisikie kama Watanzania wengine, tuone mitandao yetu ya barabara inafunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara nyingine ya kuunganisha Mkoa wa Lindi na Morogoro, hii Barabara ya kutoka Liwale kwenda Morogoro, tunaomba hiyo barabara itengenezwe. Barabara ile ikitengenezwa kama inavyoonesha ilani itasaidia sana kupunguza foleni kwenye barabara hii ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara tungeingia Morogoro, tunakwenda zetu Liwale tunaendelea na safari. Tusingekuwa na haja ya kwenda Dar es Salaam. Siyo kila mtu lazima apite Dar es Salaam, tungepita huku na mambo yote yangekwenda vizuri, tunaomba watufikirie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni fedha za matengenezo ya barabara, naona fedha hizi hazitengwi inavyotakiwa. Naomba hizo pesa za matengenezo ya barabara zitengwe ili hizi barabara zisizidi kuharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, naona muda wangu umekwisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, atafuatiwa na Mary Francis Masanja, wafuatao wajiandae, Issa Ally Mchungahela na Anna Richard Lupembe.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Kwa kweli cha kwanza ningeanza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo aliweza kununua mitambo ya kisasa ya *TMA* na kupelekea hata *TANROAD* kufanya kazi zao kwa ufasaha katika kipindi hiki ambacho *El-Nino* ilivyoweza kutokea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaza kwamba, Mheshimiwa Rais asingewekeza nguvu kubwa katika kununua mitambo ya kisasa ingekuwa ni ngumu sana kwa sisi kugundua kwamba kuna mvua kubwa na miundombinu isingekuwa imeimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais aliweza kutoa *Emergence Fund* bilioni sita za kwenda kutatua mitandao yote ya barabara ambayo ilikwama. Sisi Mkoa wa Shinyanga ni wanufaika namba moja ambao tulipata bilioni 1.9, kwa hiyo, utaona kwa namna moja au nyingine Mheshimiwa Rais amekuwa akikaa macho kuhakikisha Tanzania haisimami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyojua barabara ni siasa, barabara ndiyo uchumi wa nchi. Mheshimiwa Rais anapambana kwa namna ya hali ya juu. Kingine Mheshimiwa Rais kwa kipindi kifupi alichokuwepo pia ameweza kuhakikisha anatekeleza miradi yote aliyoikuta na tuna kauli mbiu yetu tunasema "Hakuna Kilichosimama", hakuna kijiji ambacho hakijafikiwa. Kwa kweli Mheshimiwa Rais ni mchapakazi na ili Mheshimiwa Rais kuonesha kwamba ana maono ya dhati na Wizara hii, akaivunja kutoka kwenye ujenzi na uchukuzi na kuweka Ujenzi isimame yenyewe na akaweka vijana wachapakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaona kwa namna moja kuna vijana na kuna yule mama ambaye ni Balozi (Balozi Aisha) na kuna *DG* mchapakazi. Wote hii timu iliyoweka wote ni timu sahihi ambayo mnaona kwa kipindi hiki barabara zinapitika, zote ni jitihada zao, hawakulala. Leo unaweza ukamwona Bashungwa huku, Kasekenya huku, *DG* kule lakini yote haya ni kwamba, vijana hawa Mheshimiwa Rais ana maono makubwa na amewaamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nipende kumpongeza Meneja wetu wa *TANRDOAD* wa Mkoa *Eng*. Joel, kwa kweli na yeye ameshirikiana vizuri kuhakikisha barabara zile zinapitika, madaraja yanaungana, njia hakuna hata moja tunayoweza tukasema tulikaa na hatukuweza kupita ili kuendelea na shughuli zetu za kiuchumi na pia hata DC wetu Mboni ambaye alikuwa Mbunge humu amefanya kazi kubwa sana katika Mkoa wetu wa Shinyanga, apokee maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kilichopita katika Bunge lililopita niliendelea kuongea kwamba *Road Fund* kwa mwaka

inahitaji trilioni moja. *Road Fund* kwa mwaka Serikali Kuu inaipelekea bilioni 600 ni kitu ambacho hakiwezekani, vyanzo ambavyo *Road Fund* inavyo vya kuweza kuihudumia hii mitandao mikubwa ya barabara kongwe ambazo ni 71 Tanzania nzima ni vichache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ifike mahali, tutailaumu sana Serikali, tutawalaumu sana hawa vijana wanaochapa kazi bila kufikiria kwamba Serikali imefika mahali imebanana, lazima tukubali hilo suala. Ukikaa kwenye Kamati ya Miundombinu utaelewa, hiki tunachokipata ni kidogo, kikiweza kugawanywa kitafika kwa kuchelewa. Kwa mwaka huu wa fedha ningemwomba Waziri wa Fedha aangalie chanzo kipya cha kuisaidia *Road Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukichukulia tu mfano wa hii barabara tunayopita Dodoma – Morogoro – Dar es Salaam, mashimo yalikuwepo, kila ikitengenezwa mashimo, ni viraka ni viraka, zile barabara mvua zikinyesha hazipitiki. Kwa hiyo, naomba *Road Fund* iangalie namna bora ya kuweza kupata trilioni moja kwa mwaka ili kutatua hizi changamoto za barabara ambazo ni kongwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ninaendelea kuongea ni kwamba, tumekuwa tukisaini barabara mpya kila kukicha, barabara kongwe hazipitiki, kwa hiyo, bado naendelea kusisitiza *Road Fund* iangalie chanzo kipya. Tumeona Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari waliweza kusema kwamba *line* ambazo ziko *active* mpaka sasa hivi ni milioni 72.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wakati wa kuona kama katika kupitia chanzo cha simu tunaweza labda tukapata kwa kila *line* shilingi 50 ili ziweze kuisaidia *Road Fund.* Kwa sababu hili inabidi tuongee ukweli kwamba tatizo la barabara ni tatizo la kiuzalendo, kwa hiyo, tunapoendelea mbele ni lazima tuangalie *Road Fund* tunaisaidiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia ni changamoto. Mpaka sasa hivi tunavyoongea Serikali inadaiwa trilioni saba.

Naweza nikawatolea tu mfano, katika Mkoa wangu wa Shinyanga kile Kiwanja cha Ndege cha Ibadakuli kilitathminiwa mwaka 2017, wananchi wamekuja kulipwa siku za hivi karibuni, mapunjo yamekuja kulipwa, kaya 80, zimekuja kulipwa mwaka huu mwezi Aprili, shilingi milioni 320.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria mwananchi anajitolea kutoa ardhi yake anaipisha Serikali kufanya mradi, Serikali inakuja kuchelewa kumlipa huyu mwananchi. Sisi tunapenda kuongea ukweli, wananchi wetu ni wa hali ya chini, kutafuta kiwanja kingine kule ni milioni moja, milioni moja ya mjini siyo milioni moja ya kijijini. Sasa ninaomba kuiambia Serikali, kama haina miradi ya haraka, hawana fedha za kutosha basi waache wananchi hawa wakae, kuliko unakuja unamwekea *X* mwananchi tena wa kijijini aondoke katika lile eneo apishe ndege, kuna wananchi wengine hata ndege hawapandi, unataka apishe lile eneo na unatumia miaka saba, nane kumlipa yule mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kwa namna moja au nyingine hii ni hasara kwa Serikali na ni hasara kwa mwananchi kwa sababu mnapolimbikiza gharama za fidia, zinapanda, kwa sababu gharama za vifaa zinapanda mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo, nashauri kwamba, kama Serikali inakuwa haijajipanga wasimwekee mwananchi *X*. Nawaombaeni sana sana waacheni wananchi wakae waendelee na shughuli zao, mtakapokuwa tayari nawaomba sana muweze kuwalipa fidia kwa wakati na kuweza kuwasaidia wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tumeongea hapa na Wabunge wengi wameongea, *issue* ya madeni ya wakandarasi ni changamoto. Sasa hivi hata tunapoelekea mabenki itakuwa ni shida, *invoice discount,* sijui hizi zote wanazoziongea, wanazozitoa ndani ya masaa 24, sidhani kama hela nyingi tunazoongelea bilioni 900 ziko nje, mwakani itakuwa karibu trilioni, Serikali haijaweza kulipa, bado madeni hayo yana riba. Tunaongelea sasa bilioni 44 ambazo ni riba, mtaona kwa jinsi gani au nyingine Serikali inaingia kwenye hasara… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nimwite Mheshimiwa Mary Francis Masanja, atafuatiwa na Issa Ally Mchungahela na wafuatao wajiandae: Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Zuberi Mohammed Kuchauka na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris,

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Kwanza kabisa nimpongeze kaka yangu Innocent Bashungwa, kwa kazi nzuri anazozifanya. Ninampongeza na nimesikia Wabunge wenzangu wanampongeza wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwa lugha yangu ya Kisukuma *"Ng'wana nogu akalyaga na akabhisile"* maana yake ni kwamba mtoto mnyenyekevu anakula na kile kilichojificha. Kaka yangu Bashungwa anafanya kazi kubwa sana, tumemshuhudia jinsi ambavyo hapa katikati *El-Nino* imepita, amekuwa akitembea huku na huku, anapanda hadi pikipiki lakini kazi yake imeonekana kwa macho yake na macho yetu pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Waziri, ndugu yangu Kasekenya, jembe la Wanaileje kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Kwa kweli kaka yangu anajitahidi sana na Mungu aendelee kumbariki sana. Tunaipongeza menejimenti ikiongozwa na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nimpongeze sana Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Mwanza Ndugu yangu Paschal Ambrose. Meneja huyu anasaidia sana kutekeleza Ilani ya CCM kwa takribani 99%. Tunampongeza sana kwa sababu ni mnyenyekevu lakini anajituma sana. Tunatambua kwamba majukumu ya Wizara hii ya Ujenzi ni pamoja na kusimamia ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja, lakini pia kusimamia wakandarasi na fani za wahandisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka niiongelee hii Barabara ya kutoka Shinyanga kuingia Mkoa wa Mwanza. Unapoanza tu kuuona Mkoa wa Mwanza kwa maana ya vijiji vinavyoanzia pale Mwasamba. Utambulisho wa kwanza ni ile Barabara ya kutoka Shinyanga kuelekea Mwanza, barabara hii haifai ikiwezekana ijengwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Rais miradi mingi imetekelezwa katika Mkoa huu wa Mwanza likiwemo Daraja la Kigongo - Busisi na kuna miradi mingi ambayo imetekelezwa kuna ujenzi wa meli, kuna Stendi ya Buzuruga, Nyamhongolo pamoja na Nyegezi. Haya yote ni maandalizi ya uchumi wa Kanda ya Ziwa ikiwemo Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayojitokeza ni Barabara hii inayotoka Shinyanga kuelekea Mwanza. Tumejiandaa vizuri, tumetekeleza vizuri, lakini mgeni au yeyote anapouanza Mkoa wa Mwanza kunakuwa na changamoto kubwa sana. Kwa hiyo ikiwezekana barabara hii aidha iweze kukarabatiwa vizuri au inaposhindikana basi ijengwe upya. Kwa kuwa Wizara hii inasimamia hawa wakandarasi, basi tujue kama wakandarasi hawana uwezo maana mimi toka ninakua ninaiona ile barabara inakarabatiwa tu hakuna siku imekamilika ikaonekana kwamba inafaa machoni na kwa matumizi ya magari na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii Barabara ya Sengerema - Nyehunge yenye kilometa 54. Tarehe 23 Aprili, 2023 barabara hii ilisainiwa. Wananchi wa Sengerema na Buchosa walihudhuria katika hafla hiyo na walishangilia sana na wakafurahi sana

kwamba sasa lami inapita Sengerema kuelekea Nyehunge mpaka itatokezea Geita. Cha kushangaza mpaka sasa nimesoma ripoti ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi, kwamba hata kuanza ile kazi bado hajaanza, sasa hivi ni mwaka mzima umepita wananchi wanasubiri wanaangalia lami yao hawaioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, namwomba Mheshimiwa Waziri, barabara hii ikiwezekana ianze mara moja kujengwa ili wananchi wanufaike na eneo hili, lakini pia kuna suala la fidia, ninaiomba Serikali iweze kuwalipa wananchi wa maeneo haya ambao wamekubali kupisha barabara hii ili waweze kuona thamani yao na mali zao zinalipwa kwa njia ya fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza sana Serikali kwa mradi huu wa upanuzi wa barabara kwa njia nne kutoka Mwanza Mjini - Usagara yenye kilometa 37 na tumeona katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba zimetengwa kilometa 22. Tunapoitengea fedha barabara hii, tunaishukuru Serikali, lakini barabara hii ni pacha na barabara inayotoka Mwanza Mjini kuelekea Nyanguge kwa njia nne. Tunaiomba Serikali itenge angalau hata kilometa 10 ili iweze kuokoa yale mazingira ya foleni kutoka Mwanza Mjini kuelekea Buzuruga kwenda mpaka Kisesa kutoboa mpaka Nyanguge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana sana ikiwezekana kidogo kitakachopatikana inapoanza Barabara hii ya Mwanza Mjini kuelekea Usagara basi na hii ya Mwanza Mjini kuelekea Igoma - Kisesa mpaka Nyanguge angalau hata kilometa 10 iweze kuanza, kwa sababu tutakuwa tumetengeneza upande mmoja lakini upande mwingine *jam* ya magari itakuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipogeza Serikali, Barabara ya *Airport* Igombe - Nyanguge wametenga kilometa 10 na tayari wameshaanza; mkandarasi yuko *site*. Ikiwezekana pia barabara hii ni ya thamani kubwa sana kwa sababu mtalii anapotoka *airport* kuelekea Serengeti, barabara hii ni ya muhimu sana itaokoa hata muda wa kupita mjini ili atafute mazingira ya

kwenda kufika Nyanguge na aelekee Serengeti lakini barabara hii ikiboreshwa itaokoa sana ile *movement* ya kuingia mjini na kutoka kuelekea Serengeti kwenda kutalii. Kwa hiyo tunaomba pia iongezewe fedha ili wananchi wa maeneo hayo na uchumi wa Wanakanda ya Ziwa upande huo, uweze kuimarika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niikumbushe Serikali kuna hii Barabara ya Hungumalwa - Ngudu kutokezea Magu. Barabara hii ni ya kilometa 71, tunashukuru imetengewa kilometa 10 lakini barabara hii imeahidiwa takribani Awamu Tatu, Nne zilizopita. Kila viongozi wanapofika katika maeneo haya wanaiahidi, ninaiomba sana Serikali iweze kuiangalia kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya mwisho ni Barabara ya Magu - Salama na Bariadi kupitia Ng'haya. Ninaomba sana Serikali maana majibu ya kwenye hotuba wamesema mpaka sasa wako kwenye taratibu za kumpata mhandisi mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana jicho la Serikali liangalie barabara hii. Naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa Innocent Kalogeris na Mheshimiwa Ally Makoa, wajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi, lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa uhai pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupambania. Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa sana, kwenye jimbo langu Mheshimiwa Rais nitaendelea kumsifia mara kwa mara kwa kazi kubwa aliyoifanya. Namshukuru kilometa 60 za kutoka Newala kuelekea Masasi kupitia Mitesa zilishaanza kufanyiwa kazi. Pia namshukuru kwa kilometa 42 kutoka Newala kwenda Mbuyuni ziko katika manunuzi. Namshukuru pia kwa kutuwezesha kupata daraja lenye ukubwa na urefu takribani mita 120 Daraja la Mbangala. Daraja hili limegharimu takribani shilingi 9,800,000,000 na sasa hivi liko katika kiwango cha 66%. Kwa kweli haya ni mambo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote ambayo Mheshimiwa ametusaidia kuyafikia bado sisi tuna mahitaji. Jimbo langu mahitaji yake ni tofauti na jimbo lingine. Kila jimbo lina mahitaji tofauti kama nilivyoanza kusema, sisi kule tulikuwa na jukumu kubwa moja, kipindi hicho kulikuwa na vita ambayo ilikuwa ikishughulika na mtu mmoja anaitwa Kaburu na Mreno. Tulikuwa tukifanya kazi hii ya kulinda, tuligeuka walinzi bila kujali umri maana yake ni kwamba hata watoto wa umri wa miaka 12 hivi na kuendelea badala ya kwenda shule tulikuwa tumegeuka kama walinzi. Kwa hiyo kwa sasa hivi naomba kazi ile tuliyoifanya wakati watani wenzetu katika majimbo mengine wao wakiendelea na shughuli zao, Serikali ione kwamba, sasa tunahitaji na sisi angalau kufidia kipande kile ambacho sisi hatukuweza kupata elimu, labda hatukuweza kupata uchumi na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ambayo naiombea ni barabara ya uchumi na yenyewe ni barabara ya mpakani. Kama ilivyokuwa mipaka mingi ni neema lakini tunaomba na sisi kwa barabara hii iwe neema ya mpakani. Hali kadhalika tumekuwa tukiomba barabara zingine ambazo zimeharibika kwa kipindi hiki cha mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na barabara takribani nyingi zimeathirika na mvua kama maeneo mengine ilivyokuwa japo wakandarasi wa *TARURA* wako *site*, lakini kuna baadhi ya barabara bado hazijapatiwa ufumbuzi. Tuliomba takribani shilingi

milioni 800 kwa ajili ya kurekebishia barabara hizi, lakini kwa bahati mbaya tulipata shilingi milioni 100 pekee. Mnaweza mkaona kwa kiasi gani tuna uhitaji wa barabara. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri sana kwenye barabara hizi ambazo tuliziombea pesa takribani shilingi milioni 800 *at least* atuletee ili tuweze kuzirekebisha ili wananchi wetu na wenyewe waweze kusafirisha mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja ambacho nataka kukizungumzia hapa cha msingi sana ni kuhusiana na Bajeti hii ya Ujenzi. Kwa kweli Bajeti hii ya Ujenzi haiko *realistic* kwa sababu ukiisoma hii bajeti unaweza ukakuta kwamba inakupotosha kabisa ukashindwa kuelewa kwamba hiki ni nini? Kwamba huu ni uhalisia au ni kitu tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika kiasi kilichotengwa cha shilingi trilioni 1.4 kilikusanywa au kilipokelewa zaidi kwenye ile bajeti zaidi ya takribani shilingi bilioni 1.9. Baada ya kupokelewa kiasi hicho utekelezaji wake tulikuwa tunategemea kwamba kwa kiwango kikubwa kile tulichokifanyia kama bajeti kingekwenda kuwa *affected* lakini haijawa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano barabara za matengenezo tukiangalia katika ile ripoti ya utekelezaji kuna takribani kilometa 34 ambazo ndizo zilitakiwa zijengwe, lakini katika kilometa hizo 34 zimejengwa kilometa 23,985 yaani kuna upungufu wa takribani kilometa 10,000. Hali kadhalika matengenezo ya muda maalum kilometa 3,612 zilitakiwa kujengwa, lakini kati ya hizo zimejengwa kilometa 2,160.46 pekee kwa maana kuna upungufu wa takribani kilometa 1,444.13. Matengenezo ya sehemu korofi kulikuwa na barabara zilizotakiwa kujengwa takribani kilometa 402.65 lakini katika utekelezaji zimejengwa takribani kilometa 287.83 pekee, kwa hiyo kuwa na upungufu wa kilometa 114. Hali kadhalika matengenezo ya madaraja. Kulikuwa na madaraja takribani 3,129 lakini katika madaraja hayo ni madaraja 2,011 pekee yaliyotengenezwa na hivyo kuwa na upungufu wa madaraja takribani 1,118.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia hali hiyo hapo kuna mambo mawili, aidha, bajeti hii iliyopangwa haiko *realistic* kwamba kiasi kilichotajwa katika kuchangia ujenzi wa barabara hii ni pungufu, ndipo pale nilipoona Wajumbe wa Kamati walio wengi wamesimama wakilalamika na kusema kwamba kiasi kinachohitajika ni takribani shilingi trilioni tano. Huu ndiyo ukweli kabisa tusianze kuendelea kujidanganya tukasema kwamba bajeti ya shilingi trilioni 1.4 itatosha, hii siyo kweli hatuwezi kujifurahisha kwani, tunamfurahisha nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lina madhara makubwa sana kwa sababu kuna madeni mengi yanakuja kujitengeneza kwa kutokulipa. Sasa haya madeni yakishakaa muda mrefu yanakuwa na changamoto kubwa. Mfano tukiangalia bajeti ya mwaka jana ambayo kulikuwa na takribani trilioni 5.8 za madeni, lakini katika deni lile trilioni 5.8 kulikuwa na trilioni 2.3 ni riba na hii riba inatokana na vitu vya namna hii kwamba kuna vitu vya kujizuia yaani kutokakukamilika… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mchungahela, muda wako umekwisha.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja lakini nikisisitiza kabisa kwamba tujitahidi kuweka bajeti ambayo ni *realistic* kuondoa changamoto zinazoweza kujitokeza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa Innocent Kalogeris, Mheshimiwa Ally Makoa, Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya na Mheshimiwa Abeid Ighondo, wajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi naomba nimshukuru Mungu ambaye

ameendelea kututunza na kutulinda kwa ajili ya afya tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya tunaona juhudi zake kwa ajili ya barabara zinayoendelea kujengwa katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na *Engineer* Martin wa Mkoa wetu wa Katavi kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya na watendaji wote ambao wanahusika na Mamlaka hii ya *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba niseme kuhusu fidia. Wabunge wengi wamesema kuhusu fidia, katika Jimbo langu la Nsimbo katika Kata ya Sitalike tukielekea Manispaa, *Mpanda Hotel,* Misunkumilo mpaka *Mpanda Girls*. Wananchi walipisha barabara ya lami toka mwaka 2012, lakini mpaka leo hawajawahi kulipwa fidia zao. Kuna wengine wameshafariki, kuna wengine wameshakuwa na hali ngumu, tunaomba Serikali wengi wamesema tuanze kujipanga vizuri tuhakikishe kama tunapisha barabara basi tufanye tathmini, tuwalipe wananchi haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wananchi wa Sitalike, Mpanda Hoteli, Misunkumilo wanaendelea kulalamika kwa ajili pesa zao zimekaa muda mrefu, wazazi wao wamefariki wamesubiri kifuta jasho chao mpaka leo hawajapata. Tunaomba Serikali kuhusu fidia tunajua fidia hii ni nchi nzima tujipange vizuri, tufanye tathmini, tuwalipe wananchi hawa kuhakikisha wamepata haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru na kupongeza wametujangea jengo zuri pale Mpanda Mjini *Airport* na karibu tutaanza kulitumia. Tunaomba tumshukuru sana Rais kwa kutuwekea mahali pazuri kwa ajili ya kupumzika kwa ajili ya kusubiri usafiri wa ndege, naomba nimpongeze sana Rais kwa ajili ya Mkoa wetu wa Katavi ametukumbuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Waziri sijaona hapa Barabara lami ya kutoka Kawajense ya, Ugalla - Kaliua - Kahama mpaka inaelekea Bukoba, hii barabara ni barabara ya uchumi. Ninaomba nishukuru Daraja la Ugalla mmeanza kulijenga, lakini kwenye bajeti hii hatujaipangia pesa Daraja la Ugalla. Sasa miradi yoyote ambayo tunaianza na kuiacha inakuja kutumia gharama kubwa sana huko mbeleni. Sasa Mheshimiwa Waziri hili daraja kwa sababu tayari ameshaanza kulijenga, nimeangalia hapa kwenye madaraja mbalimbali ambayo, ameyaandika Daraja la Ugalla hajaliandika hajalipangia fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri atambue anavyoliacha huko mbele ya safari atakuja kutumia gharama kubwa na hii Barabara ya Kawajense - Ugalla - Kaliua - Kahama iko mpaka kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kuanzia 2020/2021, 2021/2022 na 2023/2024 lakini hajaipangia pesa. Tunaomba hii barabara kwa sababu barabara hii ni ya uchumi ambayo itawaleta Watanzania wengi kwa ajili ya mwingiliano ili waweze kupata manufaa makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara za mzunguko katika mikoa mingi. Sasa hivi tumeanza barabara za mchepuko ambazo zinatusaidia kuunganisha Wilaya, Kata au Tarafa, hususan kwenye kata, kuna barabara ya mchepuko ya Magamba ambayo ni Manispaa, Kapalala, Mtapenda hadi Kasokola kuelekea Mpanda Ndogo, mpaka Wilaya ya Tanganyika. Ina maana unatoka Manispaa unainga Nsimbo unaelekea Wilaya ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni barabara ambayo ni muhimu sana kwa Mkoa wetu wa Katavi kwa sababu ni barabara ya mchepuko ambapo barabara nyingine yoyote ikipata majanga ya aina yoyote, hii barabara itasaidia wananchi wa Katavi Manispaa, Nsimbo na Tanganyika katika Wilaya ya Tanganyika Ndiyo maana hapa tuna barabara ya Dodoma ya mchepuko ambayo inatusaidia. Kwa hiyo, hata hizi barabara za mikoa katika maeneo yetu nazo zitatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii barabara ya Magamba – Kapalala – Mtapenda - Kasokola kuelekea Mpanda Ndogo Wilaya ya Tanganyika kuelekea Kigoma iwekwe hata kwenye bajeti inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna barabara nyingine ya mchepuko ambayo inatoka Kanoge kushuka mpaka Msaginya. Hii barabara ni ya mchepuko na inatusaidia sana kuja barabara kuu, maana barabara ya Kanoge na barabara hii hapa Msaginya inatoka kwenye barabara kuu. Najua Serikali inafanya kazi kubwa na ina mipango mizuri, lakini naomba barabara hizo za michepuko ziwekwe ili kuhakikisha tunapata unafuu ndani ya Mkoa wetu wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna Daraja la Stalike ambalo lipo katika barabara yetu ya Katavi ambayo inaingia kwenye mbuga za Wanyama. Safari hii nina madaraja mawili pale Stalike. Mheshimiwa Waziri mwenyewe ni shahidi kwamba Mkoa alisimama kupitia daraja hili, na hapa naomba kumshukuru kwa kutuma wataalam ambao walikuja katika Kata ya Stalike kuona lile daraja. Nafikiri Waziri mwenyewe amejihakikishia kwamba lile daraja linatakiwa liinuliwe, yaani lijengwe upya kwa sababu ya kiuchumi kwa nchi yetu. Tunaona Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendeleza kuhakikisha na kuleta watalii mbalimbali, na sisi kutokana na utalii ambao upo Mkoa wa Katavi, hili daraja ndiyo litafanya watalii wengi waweze kuingia na kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris ajiandae, atafutiwa na Mheshimiwa Ally Juma Makoa pamoja na Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama

jioni hii kuchangia Wizara hii ya ujenzi. Hapa nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Mtendaji Mkuu wa *TANROAD* pamoja na injinia wa matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *El-Nino* iliponikwamisha Liwale nikalazimika kuondoka kwa chopa, Mheshimiwa Waziri hakuniacha, alikuja na chopa akaniokoa; nilipokumbwa na Kimbunga Hidaya nikakwamia Lindi, Mheshimiwa Waziri alipoamua kuondoka na boti, hakuniacha tuliondoka pamoja, nakushukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba niwaase wenzangu ambao wanataka kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, hebu tumwachie hiyo Shilingi. Tunachozungumza hapa ni rasilimali fedha. Tunapozungumza rasilimali fedha, tunamgusa Waziri wa Fedha. Shida kubwa aliyonayo Mheshimiwa Bashungwa na timu yake ni rasilimali fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mama mwenye maono makubwa sana, ndiyo maana akaunda Wizara tatu, akaja na Wizara ya Mipango, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee na Waziri wa Mipango. Hizi vurugu na songombingo zote unazoziona hapa ni kwa sababu mama alishaziona mapema, kwamba tuna-*lose*, hatuna Wizara ya Mipango. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Mipango upo, naomba twende na mipango, na mipango yetu lazima iende na viapaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikubali na nitakuwa wa mwisho kukubali; Mbunge anapouliza ujenzi wa Barabara, Waziri akasema pesa zitakapopatikana ndiyo tutajenga, siyo kweli. Kwamba umuhimu wa hiyo barabara utakapoonekana tutajenga. Kama ni fedha, fedha zipo, tatizo letu ni kwenye mipango na ugawaji wa hii keki tunayoigawanya hii leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Kumi na Moja nilisema kuna Sera ya Taifa letu kuhusu ujenzi wa kuunganisha mikoa yote ya nchi hii kwa Barabara. Nikaomba tuunganishe Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Morogoro kwa barabara, sikusikilizwa. Kimbunga Hidaya kimekuja kunisaidia. Kimbunga Hidaya kilipokuja Lindi, *LATRA* wakatoa *route,* mtu atoke Nangurukuru aende Lindi, apite Ruvuma, apite Njombe, apite Iringa ndiyo aje Dodoma; atoke Nangurukuru aende Lindi, aende Ruvuma, aende Njombe, aende Iringa, aje Morogoro, aje Pwani ndiyo aende Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Nangurukuru kwenda Dar es Salaam ni kilomita 300. Shida tuliyonayo ni vipaumbele vyetu. Leo ile barabara ya Morogoro na Lindi ingeunganishwa, *route* fupi ilitakiwa iwe kutoka Lindi - Morogoro - Mikumi - Kilosa - Dodoma, *route* fupi kabisa; lakini kwa sababu tuliposhauri hatukusikilizwa, nami nikaomba kama hili jambo halitekelezeki, hii sera ya kuunganisha mikoa kwa barabara za lami, tuiondoe. Hilo ndiyo tatizo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema shida iliyopo pale ni rasilimali fedha, nina maana nenda kwenye vipaumbele vya nchi yetu. Leo kwenye *SGR* tumesaini vipande sita vya Dar es Salaam – Morogoro, Morogoro – Dodoma, Dodoma – Tabora, Tabora – Isaka, Isaka Mwanza na Mwanza – Kigoma, lakini wakati tunasaini hizo zote sita hata kile kipande cha kwanza hatujamaliza. Sasa unaposema una rasilimali fedha kidogo wakati umesaini kandarasi zote hizi, mimi sikubaliani na hilo. Shida ni kipaumbele. Ni kipi kipaumbele chetu? Kipi tuanze na kipi tuache? Kwa nini tusiende kidogo kidogo tukasaini *lot* moja moja wakati mipango mingine inatekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumekuja na *BRT.* Mpango wa *BRT* nimeambiwa kwamba utafanyika kwenye majiji yote, kwa maana ya mwendokasi, mnataka kupeleka kwenye majiji yote. Leo Dar es Salaam peke yake kuna *lots* kama nane. Kuna Mbagala – Kigamboni, Kariakoo – Gongo la Mboto, Nyerere – Segerea, Mwenge – Tegeta, Kawawa *Road* sijui Kinondoni na Kariakoo – Kimara zote hizi ni fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati ninyi mnatengeneza hizo *lots* za *BRT,* sisi Liwale hatujawahi kupata lami. Liwale hatuna lami. Ukiniambia barabara ya Nangurukuru mpaka ipatikane fedha, siyo kweli. Barabara ya Nangurukuru itajengwa pale mtakapoona kwamba ina umuhimu wa kujengwa kama fedha zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata mashaka sana juu ya ugawaji wa hizi fedha tulizonazo. Leo nazungumzia Kigoma na Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa. Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa sasa hivi inafikika kwa njia nne, unafika kwa meli, unafika kwa barabara, unafika kwa ndege na unafika kwa reli ile ya *MGR* na miaka mitano ijayo itafikika kwa njia tano *SGR* ikikamilika. Sisi Lindi tunafikika kwa njia moja tu ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Bahari, lakini hatuna meli; tuna uwanja wa ndege, lakini hatuna ndege; tunafikika kwa njia moja tu, njia ambayo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli amesema imejengwa kwa kiwango cha chini. Hiyo ndiyo barabara pekee tunayoitegemea sisi watu wa Kusini. Tunapokuja kuambiwa mpaka fedha zipatikane, tunapata shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo Barabara, kwa mfano nizungumzie barabara ya Nangurukuru – Liwale; hii barabara kule tumeshaipa jina kwamba ni barabara ya kuombea kura. Kwamba, ili watu wapate kura, watu wa Liwale unawaambia nini? Unawaambia mwaka huu nitahakikisha barabara hii inajengwa kilomita 72. Mwaka 2023 nikajimwambafai pale tukashangilia kilomita 72 itajengwa. Mpaka leo imekuwa hadithi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Waziri hana rasilimali fedha, naomba tuanze hata kama ni kilomita tano. Najua shida siyo yake, naomba tuanze. Waziri wa Mipango nakwambia, songombingo zote hizi Mama aliziona ndiyo maana akaunda hii Wizara. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu miaka miwili au mitatu ijayo haya mambo yanaenda kurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya kufanyia upembuzi yakinifu barabara nchi nzima, halafu unaenda kujenga daraja moja, haiwezi kuwa sawa. Kuna sababu gani? Kwa sababu upembuzi yakinifu hamfanyi bure, mnafanya kwa fedha. Sasa kama unafanya upembuzi yakinifu barabara 20, kwa nini usifanye barabara mbili halafu hizo fedha nyingine ukajenga barabara hizo ambazo ushafanya upembuzi yakinifu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mmojawapo ni barabara ya Nachingwea – Liwale mpaka Masasi, upembuzi yakinifu wa barabara hii uliisha mwaka 2014. Leo tunapozungumza nim waka 2024, barabara haijajengwa. Hivi kweli barabara ile itajengwa kwa kutumia upembuzi yakinifu wa mwaka 2014? Si itabidi ifanyiwe upya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo shida ni kwamba tunagawaje hizi fedha? Tuna vipaumbele gani? Tunagawaje hizi fedha? Tuna sababu gani ya kufanya upembuzi yakinifu barabara 60 hadi 70 kwenye nchi hii? Mnamfurahisha nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mtindo wa kuziweka barabara kwenye bajeti kwa sababu hatuwezi kupinga bajeti, lakini bajeti ikiisha hakuna fedha. Sasa kama *projection* mnayo, wachumi mpo, watu wa mipango mpo, na mnajua uwezo wetu wa kukusanya mwaka huu ni kiasi fulani, kwa nini mnaweka barabara nyingi? Mnamdanganya nani na mnatafuta nini? Haiwezi kuwa sawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Mheshimiwa Bashungwa sina deni naye, nina deni na hawa watu wawili; mtu wa fedha na mtu wa mipango, hebu twendeni tukapange mipango inayotekelezeka. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Juma Makoa,

Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Abeid Ighondo na Mheshimiwa George Joseph Kakunda wajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha nyingi kukamilisha miradi ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege ambavyo viko chini ya Wizara hii. Vilevile, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuona umuhimu wa kuigawa Wizara ambayo ilikuwa ni Uchukuzi na Ujenzi na sasa kuwa Wizara mbili tofauti ili kuweza kukamilisha hayo maono ambayo anayataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Waziri, wajina wangu Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu *Engineer* Aisha na Watendaji wote ambao wako chini ya taasisi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nitumie nafasi hii kumpongeza kwa umuhimu kwa namna moja au nyingine Meneja wangu wa *TANROADS,* mdogo wangu *Engineer* Razaq kwa kazi kubwa ambayo ameifanya hasa katika kipindi hiki cha mvua za *El-Nino* katika kurejesha mawasiliano. Mheshimiwa Waziri pokea maua yako na timu nzima ya *TANROADS,* hakika mnaitendea haki nafasi ambayo mmepewa na Mheshimiwa Rais katika kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini, Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki na Morogoro Mjini kwa ujenzi wa barabara ya Bigwa - Kisaki kwa kiwango cha lami, ambayo tayari imeshasainiwa na mkandarasi nina uhakika muda wowote ataingia kazini, hasa baada ya kupitisha bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Ubena Zomozi - Ngerengere ambayo nayo itajengwa kwa kiwango cha lami kilometa 11. Kuna kilometa 166 upembuzi yakinifu kutoka

Ngerengere - Mvuha tunakwenda Kisaki mpaka Matembele *Junction* kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kwa uhakika tuna kila sababu wananchi wa Morogoro kumpongeza Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kuliona hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Bigwa – Kisaki, Barabara ya Ubena Zomonzi kwenda mpaka Mvuha mpaka Kisaki ni barabara kubwa ya kimkakati ya kiuchumi kwa sababu inakwenda kwenye Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere na kwenye hifadhi kubwa ya Mwalimu Nyerere katika nchi yetu. Nina uhakika kama tutakamilisha kazi ya ujenzi wa barabara hizi mbili, tutahakikisha tunafanya utalii kwa nyanda ya kusini kuendelea kuimarika na kuongeza mapato makubwa Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu tu kwa Serikali, baada ya kukamilisha michakato yote, naamini sasa hivi mkandarasi ameshapeleka *performance guarantee* na ameshapeleka *advance guarantee,* basi tuangalie katika bajeti hii tukishakamilisha kupitisha ipatikane fedha na mkandarasi aende *site* mara moja kuweza kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi ambazo nimezitoa kwenye Wizara, nitumie nafasi hii kwa Mkoa wangu wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro ni Mkoa ambao kiuhalisia ni wa kimakakati na ndiyo tumeshautamka kwamba ni ghala la Taifa la chakula, lakini mvua za *El-Nino* zimeathiri maeneo makubwa katika Mkoa wa Morogoro. Kwa hiyo, tuliomba takribani shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kurejesha mawasiliano. Namwomba Mheshimiwa Waziri, najua kuna fedha zimeshapatikana, lakini ahakikishe kwamba kile kingine tulichomwomba kipelekwe kwa *TANROAD,* Mkoa wa Morogoro ili waweze kwenda kukamilisha ujenzi wa madaraja ya Mlimba, Ifakara kule Mahenge. Hata kwangu kwenye Jimbo langu tuna madaraja pale ya Kisaki mvua zilizopiga tulishindwa kuwa na mawasiliano. Mawasiliano yalikatika karibu masaa 40 au 60 hivi, wananchi walipata changamoto. Kwa hiyo, nadhani akitupatia fedha hizi zinaweza kwenda kurejesha mawasiliano na hali nzuri kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulipata bajeti ya shilingi bilioni 20.1 mwaka huu tunapongeza kwamba mkoa umeongezewa bajeti kwa *almost one billion,* tumekwenda kwenye *21.7 billion.* Ombi langu kwako Mheshimiwa Waziri, kwa umuhimu wa Mkoa wa Morogoro na mazingira yake, kwa sababu kuna mito mingi, hebu angalie mwakani tutenge kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi wa mbio za mwenye wakati tunakabidhi mwenge pale Mkoa wa Pwani alisema mbio zimekimbizwa katika mikoa aliyopita, lakini kwa Mkoa wa Morogoro ameuona ni Mkoa *special* na ingewezekana iwe Kanda Maalum kama vile Kanda za Kipolisi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kufanya tuweze kufanikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili lingine naunga mkono hoja na naendelea kuwaomba wenzangu ambao wanasema wanataka kukamata Shilingi ya Mheshimiwa Waziri, tumwachie Mheshimiwa Waziri Bashungwa shilingi yake akafanye kazi. Kubwa zaidi naomba kwa Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea kutoa michango yetu, tuielekeze Serikali ikaangalie namna gani itaongeza bajeti hii, kwa sababu kazi ya ujenzi wa barabara siyo kazi ambayo inaisha kwa mara moja, ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni imani yangu sisi tuna *expenditure budget,* hatuna *cash budget.* Imani yangu ni kwamba tutakapopitisha bajeti ya Serikali, kuna vyanzo vingine vya mapato vitapatikana, basi katika hivyo vyanzo vya mapato vitakavyoapatikana, naomba vielekezwe kwenye Wizara ya ujenzi, bajeti iongezeke ili hizi kelele ambazo tunazifanya ziondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni kwenye suala la *local content.* Naomba ni-*declare interest,* mimi ni mkandarasi. Naipongeza Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan lakini nakupongeza wewe Mheshimiwa Waziri Bashungwa na nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Tarehe 21 mwezi wa 11 mwaka 2023 tulifanya mkutano pale na sisi wakandarasi tulitoa hoja zetu, nimeona zimefanyiwa kazi, lakini

kuna hoja moja, suala la kodi siyo rafiki kwa mfanyabiashara hasa mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashungwa tulizungumza kwenye Kamati, lakini naomba nizungumze kwenye Bunge hili na bahati nzuri ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu yupo. Suala la *Withholding Tax* ni kodi ya wizi ambayo inamuumiza mkandarasi. Mfano, shilingi bilioni moja *profit margin* ya kazi hiyo huwezi kupata zaidi ya 10%. Maana yake nini? Mkandarasi atapata shilingi milioni 100 na kwa mujibu wa kodi, haki yake ni kulipa 30% ambayo ni shilingi milioni 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuchukua *five percent Withholding Tax* maana yake unachukua zaidi ya shilingi milioni 20 kwenye milioni 50. Kwa hiyo, ndani ya miaka mitatu au minne, mkandarasi huyu hawezi kwenda. Kwa hiyo, naomba, wakati mnaingia katika suala la kuona tunamsaidia vipi mkandarasi mzawa ili fedha hii nyingi ambayo tunaipeleka kujenga uchumi wa nchi za wenzetu nje ibaki nyumbani, hivyo mliangalie suala la kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko kwenye benki mmeweka vizuri, *performance security* mmeweka vizuri, *advance security* mmeweka vizuri lakini kwenye suala la kodi bado kuna changamoto. Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa namna moja au nyingine aone tunafanyaje ili kufanikisha jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwenye suala la Baraza la Ushauri la Wakandarasi. Hili ni Baraza muhimu kwa ajili ya kuweza kufanya kazi nzuri za ukandarasi kwenye nchi hii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba tuendelee kutenga fedha nyingi kwenye Baraza hili ili tuweze kupata makadirio sahihi ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nakuita sasa Mheshimiwa Ally Juma Makoa, utafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya neema ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyotuletea Watanzania na tunaona kazi zinafanyika na neema tunazifaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa *Eng.* Kasekenya ni watu wa kazi, naunga mkono bajeti yao. Naomba Wabunge wenzangu pia tushirikiane kuunga mkono bajeti hii ili wakafanye kazi kwa sababu ni watu wanaofanya kazi nzuri, wasikivu na wanatutembelea. Mimi niwashukuru sana wote wawili wamefika kwenye miradi yangu yote tatanishi. Hongereni, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kondoa Mjini tulikuwa na vipaumbele sita ambavyo tulikabidhi Wizara hii na tunatarajia baada ya miaka mitano ya awamu hii kabla hatujarudi tena awamu inayofuata katika Bunge hili wawe angalau wameshafika kwenye 80% kwenda 90%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ujenzi wa Daraja la Munguri B, na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamefika. Pia tunataka tujengewe daraja letu la *NMB* kwani limekuwa dogo sana ambapo kwa sasa kwa kweli gari hazipishani. Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wamefika na kuliona. Pia, kulikuwa na fidia ya Shule ya Msingi Ukuku ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amefika. Pia, tulikuwa na ujenzi wa barabara ya *TANROADS* kilometa 0.8 katikati ya mji, ambayo tulikuwa tunatakiwa tuwe nayo. Kipengele kingine cha sita ni taa za barabarani katika Mji wa Kondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapita haraka kutokana na muda. Suala la taa za barabarani tunaishukuru Wizara na tunamshukuru Mheshimiwa Rais, kwani kupitia Wizara hii, tayari tumeanza

kipande cha Bicha kwenda mpaka darajani pale *NMB,* lakini sasa ule mji tunataka tuung'arishe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri, amwelekeze *engineer*, mwelekeze *CEO* ndugu yangu Mohamed Besta amshirikishe Meneja wetu, *RM* wa Mkoa, *Engineer* Zuhura, wamalizie kile kipande cha kutoka darajani kwenda mpaka *Sunrise*. Maana yake ile ni barabara ambayo inatakiwa iwekwe taa maeneo yote katikati ya mji ili mji ule angalau tuupendezeshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba sasa ile fidia. Naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri jambo moja, nyuma yake hapo yuko Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda, hebu ampe kile kipande cha shule. Lile eneo ambalo walitakiwa walipe fidia ya shule kwa sababu Wizara ya Elimu wanajenda shule, ampasie ndugu yake pale watuwekee shilingi milioni 400 tuijenge ile shule tukitoe kile kipande cha shule kilichobaki baada ya barabara yetu ile kukata pale katikati ili ampunguzie mzigo, yeye aendelee na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini nina kijana wangu hapo, akielekezwa tu na Mheshimiwa Waziri wa Elimu, ndugu yangu Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, Mbunge wa Mafia, Naibu Waziri, watatekeleza jambo hili na watakupunguzia mzigo. Haya mambo mawili nilikuwa namshauri Mheshimiwa Waziri afanye hivyo ili kumpunguzia mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye daraja la *NMB*. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, baada yay eye na Mheshimiwa Naibu Waziri kufika, tayari nimeona wameliingiza kwenye mpango wa kufanyia *feasibility study*. Naomba ndugu zangu, lile daraja walifanye haraka, mapema, waweze kuokoa wananchi. Pale kunatokea ajali nyingi. Ni daraja la mwaka 1947 ambalo linasababisha ajali. Hebu wataalamu wafanye haraka kufanya hiyo *feasibility study*, tulipanue lile daraja liwe la njia mbili. Tunawashukuru sana kwa kutukubalia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili, nimepata tetesi kwamba hizi kilometa 0.8 katikati ya mji zitasubiri kukamilika kwa hii *feasibility study* ya daraja hili ndipo waanze kujenga. Jambo hili limekuwa la muda mrefu, bajeti ya kwanza tumezungumzia, bajeti ya pili, bajeti ya tatu na hii ni ya nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kipande cha kilometa 0.8 kutokea *NMB* kwenda *National Milling* hebu kama tunasubiri hili daraja likamilike ile *feasibility study*, basi waanzie kwa upande wa *National Milling* washuke chini wafike mpaka maeneo ya Migombani pale Pazo ili waendelee kusubiri hiyo *feasibility* ya daraja, wasiachie, lile linaleta uchafu pale mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine yana lami, sasa na hii inatakiwa iwekwe lami. Kwa hiyo, daraja lisisababishe kile kipande cha kilometa 0.8 kisubiri tena kwa sababu bajeti zinaisha na mwaka unaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka ni lile daraja la Mto Bubu. Lile tunatakiwa tulizungumzie sana. Hebu kwa sababu Mheshimiwa Waziri amefika mwenyewe na Naibu Waziri wamefika, naomba amwelekeze na *Engineer* Aisha Amour afike kwenye lile eneo ili aone jinsi akinamama wenzake wanavyopata taabu katika kuvuka maji kwenye lile daraja. Wanawake wanatoa nguo, wanavua nguo zao zinanyanyuliwa juu ili wavushwe maji. Kwa maana hiyo lile jambo ni kama la unyanyasaji vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lile daraja litengenezwe, maana nimeangalia hapa bado wanasema *feasibility study* inaendelea. Hivi itaendelea mpaka lini? Kwa sababu siasa na uchumi wa Jimbo la Kondoa Mjini zinategemea sana daraja hili. Ukienda kwenye mtaa wowote unafanya mkutano watu wanakuuliza juu ya daraja la Mto Bubu. Hebu hiyo *feasibility study* ikamilike ili lile daraja lianze kujengwa kuokoa maisha ya wananchi na hata shughuli za wananchi za kiuchumi ambazo zinafanyika kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri juu ya jambo hili kwa sababu amefika na Naibu Waziri pia, hebu na

Katibu Mkuu wa Wizara naye afike akaone ni namna gani wanawake wenzake wanavyopata taabu kuvushwa kwenye ule mto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaendelea kufanya *feasibility study* miaka yote, lile daraja tutachelewa kuanza kulijenga. Naomba sana hebu jambo hili litekelezwe ili tuanze kuleta *package* nyingine kwa ajili ya wananchi wa Kondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo naunga mkono hoja. Nawatakia kila la heri, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, na Mheshimiwa Joseph George Kakunda ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia. Awali ya yote nianze kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa anayoifanya katika kuendeleza nchi yetu katika nyanja mbalimbali ikiwemo hii ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na wote wanaowasaidia. Pia, nawapongeza kwa jitihada kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu, nilifarijika sana wakati Mheshimiwa Waziri ametembelea Mkoa wa Ruvuma akakubali kutembea kwa shida kuanzia Songea mpaka amefika Lituhi, akapita kule barabara za ufukoni mpaka amefika *Mbamba Bay*. Kesho yake akatoka tena Likuyufusi mpaka Mkenda kwa ajili ya kuona yale madaraja mawili: Daraja la Mitomoni na la Mkenda. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo hata Mheshimiwa Jenista naamini hawezi kuzungumza humu, lakini ni jambo ambalo analipigania usiku na mchana kuhusu Barabara ya Likuyufusi kwenda Mkenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwamba kipande cha barabara kutoka Rwanda kwenda mpaka Ndumbi ambacho ni mwendelezo wa Barabara ya Kitai – Lituhi nayo sasa inafikia hatua nzuri, imeshasainiwa na ninaamini itaenda kuanza kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza mambo yale yale ambayo wote tumezungumza, lakini hatutaacha kwa sababu ni kilio chetu. Nikiigusa pia barabara ya Makambako – Songea, hali halisi ni mbaya na ni tishio kubwa kwa uhai wa wananchi wanaotumia barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa namwona Prof. Mkandala akizungumzia *MV. Bukoba*, jinsi ushauri ulivyokuwa unatolewa halafu hatua zilikuwa zimechelewa kuchukuliwa tukafikia kupata maafa. Tusifikie huko. Naomba tusifikie huko. Barabara hiyo ni hatari, inahitaji sasa kurekebishwa. Naamini hata aliyejenga wakati ule, yule mkandarasi, *BAFOBIT*, ingekuwa hawa wa leo, ile barabara sasa hivi ingekuwa haionekani. Ila zamani watu walikuwa waaminifu, walikuwa wanajenga kiukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelalamikia hapa barabara nyingine ambazo zina hali mbaya zilitengenezwa vibaya, sijui nini. Kuna wakandarasi ambao hawajui kukataa kiwango cha Barabara. Ukimwambia unataka barabara yako kwa bei ya shilingi milioni tano, anakwambia naweza. Shilingi milioni 10, naweza, lakini atakutengenezea kitu cha ajabu. Ndiyo haya yanayotokea sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipoenda Liwale, yule mkandarasi alimwambia fani ya yule mkandarasi wake ni *philosophy,* akasema wewe ni Aristotle? Sasa nina wasiwasi utakuja kuitwa Aristotle kwa sababu unapewa majukumu makubwa, lakini fedha hupewi. Bajeti hii ni ndogo

sana. Ninashukuru tuko na Mheshimiwa Spika humu ndani, bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi ikaangaliwe upya. Haiwezekani. Ni ndogo sana, kwa sababu haya ni masula ya kiufundi, huwezi kufanya masuala haya kwa kutumia *philosophy* za Aristotle, hapana. Tuseme ukweli, kama kweli tuna nia ya kuisaidia nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malengo na mikakati yetu na vipaumbele, mimi naamini barabara ni kipaumbele. Kwa nini tunafanya mchezo? Tupunguze maeneo mengine ambayo siyo ya lazima kiasi hicho. Mbona tunashangaa sasa hivi Wizara nyingine bajeti zimepanda? Mambo yake wala siyo ya muhimu kiasi hicho, lakini bajeti zimepanda, tukafurahi. Kwanini tupunguze huku kwenye bajeti ya Ujenzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu tuna shida za muda mrefu, watu wana shida ya kuongeza vipato vyao. Sasa hivi tunasema wanahitaji bima za afya, wanahitaji mambo gani, yote haya ni maendeleo yao. Kwa nini tunafanya mchezo katika suala la msingi kama hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, hili siyo suala la kushika shilingi. Kamati yetu ya Bajeti haijatutendea haki katika suala hili. Haijatutendea haki kuleta bajeti ndogo kama hii wakati hawa watu wamekumbwa na Kimbunga Hidaya, hawa watu wana madeni na wana barabara chungu mbovu kama zilivyoorodheshwa humu za kujengwa halafu tunaletewa bajeti ya aina hii. Maana yake nini? Tukafumue kule tulikopitisha hizo bajeti tuongeze bajeti katika Wizara hii, kwa sababu wote tunajua umuhimu wa barabara katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vituo vya afya sasa hivi, mama kafanya kazi kubwa kila mahali, halafu mtu anajifungulia njiani kwa sababu ameshindwa kufika hospitali, barabara ni mbaya. Kwa sababu gani? Kituo cha afya kimeshajengwa vizuri, shule imeshajengwa vizuri, anashindwa kufika kwenye shule kwa sababu gani? Jamani hebu tuache mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mujibu wa Katiba, Kifungu 63, kiko wapi kile (wewe kifungu njoo). Vimejichanganya

hapa, lakini ni kifungu cha 63, utapata pale kuna sehemu inasema kwamba sisi wajibu wetu ni kujadili utekelezaji wa bajeti wa Wizara. Kwa hiyo, ni wajibu wetu, tusimsingizie Waziri. Hili ni wajibu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge tunao wajibu wa kusema huku haturidhiki, tupeleke huku. Leo siongei mengine kwa sababu hata nikilalamikia barabara ngapi, kama hatutampa fedha Waziri atakuwa Aristotle. Hatutaki awe Aristotle kwa sababu ni kijana mwenye utendaji mzuri na ninamfahamu vizuri, nimeishi naye, ni mwanangu, lazima tumsadie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja, nikiamini kwamba kuna mabadiliko yatafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita sasa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani atafuatiwa na Mheshimiwa George Joseph Kakunda, na Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye Wizara yetu hii muhimu ya ujenzi wa miundombinu ya barabara. Awali kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Bashungwa pamoja na Naibu wake. Kwa kweli, hawa Waheshimiwa wengi wamesema hapa jinsi walivyo *humble* na ambavyo ni wafuatiliaji wa kero tunazowawasilishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa ni shuhuda, tangu mwaka 2023 nilipoongea kwa lugha kali sana kuhusu Barabara yangu ya Singida – Igauri – Ilongero – Haydom nikaomba fedha ili hiyo barabara itekelezwe, ijengwe kwa kiwango cha lami kwa sababu ni ahadi ya Waheshimiwa Marais wote wa nchi hii, waliotangulia na hata aliyepo madarakani, leo hii ninashukuru sana kuiona barabara hii ikiwa imeandikwa kwenye kitabu hiki kwenye hotuba takatifu ya Mheshimiwa Waziri *page* 173. Naomba wananchi wa Singida Kaskazini wasikie, kwamba sasa

barabara yao ipo kwenye *plan* ya kwenda kuanza kutekelezwa, kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo sababu kubwa ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, Balozi Aisha, Katibu Mkuu pamoja na Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Singida ambao mara kadhaa nimekuwa nikiwapigia kelele nikiwasumbua hata usiku katika kuililia barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaombee kwa Mwenyezi Mungu awape maisha marefu, mazuri na pia mioyo yenu iendelee kukunjuka ili sasa nimwone mkandarasi *site,* nione vifaa vikiwa *site* na twende tukasaini mikataba sasa ili wananchi wa Singida Kaskazini waondokane na adha wanayoipata hivi sasa ya usumbufu wa zile rasta ya ile barabara. Huwa tunapata taabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilifika wakati wananchi wakakata tamaa wakaona tumedanganywa, lakini hapa naomba niwahabarishe wananchi wa Singida Kaskazini, nakuja na habari njema kwamba sasa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupa fedha kwa ajili ya kuhakikisha barabara hii inawekwa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nina maombi. Ametoka kuzungumza Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, mama yangu ambaye nampenda sana, naomba sana Waheshimiwa Wabunge mtakaofuata baada ya mimi kukaa, wote leo pamoja na kesho tuielekeze Serikali iongeze fedha kwenye Wizara hii ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anapambana sana, anajitahidi, anapenda kuona mambo yanatokea, lakini anakwamishwa na bajeti. Naomba sasa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Serikali, Kamati ya Bajeti chukueni jambo hili kwamba ni la dharura na limejitokeza, lina umuhimu, fedha ziongezeke kwenye Wizara ya Ujenzi ili tutekeleze miradi yetu ya barabara ziweze kupitika wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na barabara nzuri, hata uchumi wetu utakua, lakini tukiwa na barabara mbaya hata ufanye nini hatuwezi kusogea, tutakuwa tunapiga *mark time*. Hatuwezi kuwa na barabara za vumbi leo hii karne hii ya 21. Naomba sana tuhakikishe tunaongeza bajeti kwenye Wizara hii, kwani shilingi trilioni 1.7 ni ndogo kwenye eneo hili ambalo linagusa moja kwa moja maisha ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tulichukue hili kama *special case*, twende tuiongezee bajeti Wizara hii ili iweze kutuletea maendeleo na mabadiliko chanya tunayoyatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kengele sijui ni ya kwanza au ya mwisho?

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya kwanza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hilo nilitaka pia niseme kuhusu barabara hii ambayo tumepewa kilomita 11. Mheshimiwa Waziri, naomba hizi kilomita 11 ni sawa na mtu umeoga nusu; yaani umeingia bafuni umeoga kutoka kwenye miguu mpaka kiunoni, huku juu umeacha hujaoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sasa, mkandarasi atakapoingia *site* angalau tuongeze kidogo 10 nyingine ili ifike pale kwenye ile Hospitali ya St. Carolus ili wananchi wetu wanaokwenda kupata huduma kwenye ile Hospitali yetu ya St. Carolus pale Mtinko nao waweze kufaidika, wapate uwezo wa kwenda kupata huduma kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha naye ni wa kunyumba, namwomba sana aweke umakini hapa, ahakikishe kwamba fedha zinakwenda zote kadiri ambavyo tumezipanga kwenye bajeti hii. Ahakikishe kwamba katika kila mradi ambao tumeuweka zinakwenda ipasavyo ili wananchi wetu waondokane na hizi taabu wanazozipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo, upande wa barabara yangu hii siongei sana. Naomba kwa hili nipongeze mwakani nikija hapa baada ya kuona wakandarasi wako *site*. Nikimwona mkandarasi yuko *site,* basi hapo nitafurahi sana. Naomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama wakati wa kuhitimisha aniambie ni lini sasa mkandarasi ataonekana *site*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila atafuatia na Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi naanza kwa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwanza kwa kututeulia Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Kasekenya katika Wizara hii. Ndugu zangu hawa ni Mawaziri ambao ni wasikivu na wanamheshimu kila mtu, awe mkubwa au mdogo. Vilevile ni watu ambao wanafuatilia sana kazi zao. Nimemshuhudia Mheshimiwa Bashungwa akienda katika maeneo tata ambako barabara zimekatika, zimeharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwona Mheshimiwa Waziri amekwenda maeneo ya Ndanda kule Kusini na maeneo mengine mengi. Kwa kweli kazi yake anaifanya vizuri na Mheshimiwa Kasekenya anazifahamu barabara zote za nchi hii. Kwa hiyo, nawapongeza sana wote, pamoja na Mheshimiwa Rais, kwa kazi ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zile *4R* za Mheshimiwa Rais; *R* ya nne ni ya ujenzi wa nchi. Tunazitegemea sana hizi Wizara mbili katika ujenzi wa nchi; Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji pamoja na wananchi wanahitaji sana gharama nafuu za usafiri na usafirishaji, ndiyo maana leo hii Bunge lako Tukufu linajadili bajeti inayokaribia

shilingi trilioni 1.7. Juzi tumepitia Bajeti ya Uchukuzi ambayo ni ya shilingi trilioni 2.7. Maana yake ni kwamba hii sekta ya usafiri na usafirishaji tunaipitishia bajeti ya trilioni 4.4. Kwa kweli ukilinganisha katika bajeti yote, hiki ni kipaumbele cha juu kabisa cha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali na Mheshimiwa Rais kwa maamuzi ya kuleta hii, kwa sababu hata ukiangalia na kulinganisha na miaka ya nyuma, kidogo mwaka huu kuna ongezeko la bajeti kwenye sekta hii nzima ya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tu kwamba furaha ya Watanzania ina mafanikio zaidi kwa kukamilika kwa barabara 17 kwa kiwango cha lami katika nchi hii, ambazo zina urefu wa zaidi ya kilometa 12,000. Ukilinganisha na nchi nyingine za jirani, Tanzania tuna mafanikio makubwa sana kwenye ujenzi wa barabara za lami, kama mtafuatilia kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekamilisha kwa mfano, naweza nikazitaja Barabara, T1 Dar es Salaam – Tunduma, T2 Chalinze – Namanga, Kenya, T3 Morogoro – Rwanda kupitia Rusumo, T4 kutoka Kenya – Sirari inazunguka mpaka Mtukula, Uganda, T5 Iringa – Arusha, T6 Mtwara – Makambako, T7 Dar es Salaam – Lindi – Mingoyo, halafu kuna T10, T11, T13 – T26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni barabara 17 ambazo zimekamilika. Nchi hii ina sifa kubwa kwa ujenzi wa barabara za lami, hongera sana kwa ndugu zangu ambao wanatuongozea Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila palipo na mafanikio huwa hapakosi changamoto. Changamoto kubwa ambayo ninaiona katika Wizara hii ni kukosa fedha katika kipaumbele cha kumalizia baadhi ya barabara ambazo ni ndefu na ambazo zimeanza kujengwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema tu kwamba, kuna Barabara kama T18 Manyoni – Tabora – Kidahwe, najua wataikamilisha kwa sababu fedha zipo. Wamhimize tu mkandarasi

ili aweze kumalizia kile kipande cha kilometa chini ya 50 ambacho kinaendelea kutekelezwa kule kuelekea Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna T09 Bihalamuro – Kasulu – Uvinza – Mpanda – Sumbawanga – Tunduma; hivi vipande vya Kasulu – Uvinza – Mpanda vina *financing*, kwa hiyo, ni jambo la muhimu kukamilisha hatua ambazo zinaendelea ili iweze kukamilisha kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa sababu *financing* tayari ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *financing* ambayo ni changamoto ni hii Barabara ya kutoka Mwanza – Nzega – Tabora – Mbeya, kilometa 881. Hii najua wana changamoto, nami nawatia moyo, ninaamini tutafanikiwa kupata fedha kwa ajili ya barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipande cha Ipole – Rungwa kilometa 172, kuna kipande cha Rungwa – Makongorosi kilometa 181 na kuna kipande cha Rungwa – Itigi – Mkiwa kilometa 219. Hiki cha Rungwa – Mkiwa kimeanza kujengwa kwa kiwango fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli nawatia moyo, naomba endeleeni kufanya juhudi ili tuweze kupata fedha za ujenzi wa barabara hizi. Kumekuwa na *options* mbili ambazo zinazungumzwa. *Option* ya kwanza inayozungumzwa ni *EPC + F*. Hii kidogo ina shida kwenye kile kipande cha *F (Financing)*. Kupata wakandarasi unaweza ukawapata, lakini *financing* kukamilisha inaweza ikachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kama tutazungumza na *AfDB (African Development Bank)* ambao walitupa fedha za kujenga Barabara ya kutoka Tabora – Mpanda, ninaamini tunaweza tukafanikiwa kwa haraka zaidi na hii barabara yote ikakamilika ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri akubaliane nami kwamba ziara ya Mheshimiwa Rais juzi kule Ufaransa, ile ziara ilikuwa ni ya muhimu sana kwa sababu alikuwa na yule Rais wa *AfDB* kule, ninaamini wamezungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali, Mheshimiwa Bashungwa pamoja na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, wamwone Rais wa *AfDB* ili atupatie zile fedha kwa ajili ya kujenga hii Barabara ya kutoka Mwanza – Mbeya na vilevile kipande cha kutoka Rungwa – Mkiwa. Hii itakuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa nchi yetu. Barabara hii umuhimu wake ni kuunganisha mikoa mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia, kwamba tunaunganisha mikoa mitano; Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Songwe, Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Singida. Barabara hiyo moja. Kwa hiyo naomba sana hilo lizingatiwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula na mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Dorothy George Kilave ajiandae.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri hasa kwa ziara aliyofanya wakiambatana na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwenye Jimbo langu la Kyela na matunda yake Wanakyela wanayajua na wanayasubiri. Ahsanteni sana kwa kututembelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niliwahi kuuliza swali hapa juu ya mkandarasi ambaye alikuwa amepewa kujenga Barabara ya Ibanda – Kajunjumele – *Itungi Port,* juu ya uwezo wake; na nilijibiwa kwamba ana uwezo, lakini baadaye naishukuru Serikali kwamba ule wasiwasi wa wananchi wa Kyela ulikuwa ni kweli, kwamba mkandarasi hakuwa na uwezo mpaka ilipofikia sasa Serikali kuvunja mkataba, naishukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hilo naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa idhini ya kuvunja mkataba. Pia ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri wake

na Katibu Mkuu kwa kazi waliyoifanya ya kuhakikisha huyu mkandarasi anaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili, naomba sasa wananchi wa Kyela wa Kata ya Kajunjumele mpaka kufika Ibanda walipwe fedha zao za fidia wakati tunasubiri mkandarasi mwingine aingie pale. Inapovuka mwezi wa Saba, Mheshimiwa Waziri anajua, tunakwenda kufanya mchakato wa tathmini upya. Mimi ikivuka mwezi wa Saba, sitakubali wananchi walipwe ile fidia ya nyuma, itabidi tuanze mchakato upya. Namwomba Mheshimiwa Waziri huko tusifike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nimekuwa nikifuatilia hizi hotuba za Waheshimiwa Mawaziri wetu wa Ujenzi, kipindi hicho ilikuwa ni Ujenzi na Uchukuzi. Nimeziangalia hotuba tatu mfululizo, zote zinafanana. Nilichokuwa nafikiria ni kwamba, hotuba ya mwaka huu ingekuwa iko tofauti. Ni kwa nini ingekuwa tofauti? Nilijua Mheshimiwa Rais kuna chombo amekiunda kimeanza kufanya kazi. Chombo hiki ni Tume ya Mipango ikiwa chini ya Mheshimiwa Profesa Mkumbo. Je, Mheshimiwa Profesa Mkumbo hajaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Tanzania ya sasa tukaanza kuongelea mambo ya kugawana keki. Leo ni lazima tuangalie vipaumbele vya Taifa hili kwamba barabara zipi zitatufikisha wapi na zitaleta fedha kwa ajili ya ku-*finance* miradi mingine. Mimi nitakuwa tofauti sana kwenye mambo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya *TANZAM*, kila mtu anaielewa. Leo hii barabara imejaa malori, imejaa magari, uchumi unasimama. Bandari yetu ili ifanye kazi, lazima *TANZAM* ifanye kazi. Leo ukifika pale Mbeya, daladala, bajaji, baiskeli, mpaka pikipiki zimejaa. Unafikiri utajenga uchumi? Kwa nini tusipanue hizi barabara ambazo ni za muhimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma hapa ni shida. Sasa nataka kuuliza, vipaumbele vyetu na mipango yetu ikoje kwenye barabara? Kwa nini hatujaviweka

kwenye bajeti hii ili tuone kwamba Taifa sasa limeanza kuwa na maono? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Askofu Gwajima alikuwa anaimba kila siku juu ya mipango hapa. Mimi nilikuwa sijui ni kwa nini? Sasa nimejua ni kwa nini alikuwa anaimba. Naomba sana twende tukalifanyie kazi hili na Taifa letu litasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalalamika hapa juu ya viwango vya ujenzi wa barabara. Wanaotusumbua kwenye ujenzi wa barabara sio wakandarasi. Wakandarasi hawana kazi kwenye ujenzi wa Barabara. Walio na kazi kwenye ujenzi wa barabara ni wale wanao-*design* barabara na kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa, tumewapa watu wa-*design* barabara ile ya *BRT*, wanafika pale Jangwani wanapitisha pale chini, halafu tunawaangalia tu, mikataba yetu ikoje? Eti mafuriko yanapanda juu ya Barabara! Maji yanapanda juu ya barabara kwa sababu ya mafuriko. *Designer* aliyefanya kazi ile yuko wapi? Ni nani atalipa hizo gharama tulizojenga ile barabara? Hapa tuna udhaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema hapa, mikataba yetu haina meno ya chuma, ina meno ya plastiki. Naomba tuweke meno ya chuma kwenye mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ungefika Tabora, uwanja wa ndege wanakwambia tumeshindwa kumaliza kwa wakati na kuanza kwa wakati kwa sababu baada ya kuanza ujenzi, ile mezamaji *(water table)* iko juu, aliye-*design* aliiweka chini, huyo *designer* tunamfanya nini? Atalipa? Sasa naomba tulifuatilie hilo ili tufanye kazi zetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye ujenzi, kuna Barabara hii ya kutoka Dodoma – Iringa *chainage* 76 pale, wametupitisha nje takribani mwaka mzima. Wamekuja kuturuhusu, tumepita kwenye barabara siku mbili tu, inakuwa na mashimo; imejaa

mashimo. Hivi kweli tunalisaidia Taifa hili! Naomba Mheshimiwa Waziri achukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala ambalo tumelizungumza sana la *EPC+F*. Kwenye ukurasa wa 35 Mheshimiwa Waziri amesoma vizuri, lakini nikashangaa nilipopitia *literature* na *citation* nyingi nikaona kuna sifa mbili kuu za *EPC + F*. Sifa ya kwanza ni kwamba kunakuwa na *fixed price*, lakini sifa ya pili ni kwamba anaye-*finance* ni mkandarasi. Sasa kwa nini tunasema leo Serikali haina fedha ku-*finance* miradi hiyo? Kuna shida gani ilhali anayetakiwa ku-*finance* ni mkandarasi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama kuna sehemu tumeteleza, tuweke vizuri ili Bunge hili lielewe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ninaomba sana sasa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia, muda wako umekwisha.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba ni kwamba, watu wetu, wakandarasi wetu walipwe madeni yao. Tunaomba sasa Mheshimiwa Bashungwa asiwe mbuzi wa kafara. Bunge tusimweke Mheshimiwa Bashungwa kwenye matatizo. Wapo wanaoeleweka na twende tukatafute fedha na wanaotafuta fedha tunawajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ninamwita sasa Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nami ninaanza kwa kumshukuru Mungu kwa fursa ambayo nimeipata kuchangia katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa miradi yote ya kimkakati yakiwemo madaraja na barabara ambavyo ni viungo katika kukuza uchumi. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpongeza pia Mheshimiwa Waziri Bashungwa na timu yake kwa namna ambavyo anasimamia, na tumeona katika utendaji wake. Hata tulipopata hii zahama ya mvua tumemwona amekuwa tayari kulala hata katika maeneo ambayo siyo mazuri sana, lengo lake ni kuona kuwa miundombinu ile inarejea. Hongera sana kwa Mheshimiwa Bashungwa pamoja na timu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuzungumzia suala zima la ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Ujenzi ule una muda mrefu unajengwa na unapanuliwa na lengo ni kuufanya uwe uwanja wa Kimataifa. Ni kweli hatua nzuri zimefikiwa, tunaishukuru Serikali, ni juzi juzi tu hapa tumesaini mkataba wa ujenzi wa jengo la abiria. Katika upanuzi ule awali walifanya tathmini ya watu 1,429 na Mheshimiwa Rais akatenga kwa roho njema kabisa shilingi bilioni 19.2 ili waweze kurejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazungumzo, awali ilikuwa imebaki mita 700 kutoka kwenye *running way*, sasa kama ni la uchukuzi au ni la ujenzi, nadhani wote ni wale wale, lakini sasa hivi wamekwenda wamefikia watu 3,929 na eneo lote linachukuliwa. Ni wazi ile fedha iliyotengwa haitatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nawapa *assignment* Serikali, na nilisema kwamba tuangalie upya, kuna haja ya kuchukua eneo lote mpaka milimani, tukaiingiza hasara Serikali, au tuchukue lile eneo ambalo linahitajika kwa ajili ya upanuzi na kufanya ikubalike Kimataifa. Vinginevyo tunaiingizia Serikali hasara kwa kitu ambacho siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la barabara naishukuru sana Serikali, Barabara ya *Aiport* – Nyanguge kilometa 16 imekuwa ikiwekwa katika Ilani ya Chama ya Uchaguzi kwa vipindi vitatu mfululizo. Mwaka huu pia upembuzi yakinifu

umekamilika kwa kilometa zote 46. Naishukuru Serikali inaanza na kilometa 10. *Signing* ya mkataba tayari na mkandarasi mwezi wa wa Sita mwanzoni anakabidhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu kwa sababu upembuzi yakinifu umekamilika katika barabara hizo, ikiwemo pia na Barabara ya Salawi – Kahama yenye urefu wa kilometa 136, imejengwa kwa kilometa tatu sawa na asilimia tano toka sasa. Kuna Barabara ya Magu – *Bukwimba Station* – Hungumalwa, kwa Kwimba, ile wilaya haijaunganishwa na lami kabisa. Naomba hizi barabara pia zijengwe, kwani watakuwa wamesaidia maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mwanza – Nyanguge sawasawa na ya Mwanza – Shinyanga, tunaomba zijengwe upya na zijengwe kwa njia nne. Tunaomba tu, kama Serikali haina fedha za kutosha, tubinafsishe ili watu wajenge na watoze *road toll*, baada ya miaka inarudi Serikalini ili tupunguze gharama kubwa hii. Nchi nyingine wanafanya hivyo na barabara zinakuwa nzuri miaka yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani akipewa *private* kujenga, hawezi kujenga kwa kuharibu haribu kwa sababu anajua atahitaji kurejesha hela zake. Tuwape, tuweke *road tolls* ili tuweze kuwa na barabara nzuri na za kudumu. Mwanza inakua, barabara ni finyu, tunaomba sana barabara zipanuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba pia Mheshimiwa Waziri aangalie *TANROADS* Mwanza bajeti imekuwa inapungua tu. Walianza na shilingi bilioni 17 mwaka 2021/2022, ikaja shilingi bilioni 15, ikaja shilingi bilioni 14.4, sasa tena inarudi pale pale shilingi bilioni 14.4, lakini bado utengenezaji wa barabara hauendi kwa mpango mzuri kama ilivyo. Bajeti zinapopungua pia inakuwa siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kuipa shilingi trilioni 1.7 bado siyo sahihi. Tukumbuke hii ndiyo ina-*link* na wazalishaji hasa kwenye kilimo. Kilimo kapewa fedha nyingi; atazalisha, barabara mbovu, atasomba na mizigo yake? Tuweke *linkage* katika suala

zima la miundombinu ili hata kile kinachozalishwa kiweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kupitia *TBA* wanajenga majengo. Naomba kuuliza, kuna maeneo wamezungumza kujenga nyumba 20 za viongozi Dodoma kwa shilingi milioni 50. Shilingi milioni 50 maana yake kila nyumba ni shilingi 2,500,000/=. Ni nyumba ya aina gani hiyo? Aidha ni *typing error* au namna gani? Chini yake wakaweka tena nyumba 150 kwa shilingi 10,000,000/=, maana yake nyumba 50 kwa shilingi bilioni 150. Maana yake ni shilingi milioni 10 kila nyumba. Sasa nataka kujua, hiyo *variation* ikoje? Ni *typing error* au namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuwa na nyumba nyingi kwa sababu *TBA* wanajenga, na maeneo yote yenye nyumba ambazo ni chakavu watengeneze kama walivyofanya *Magomeni Quarters.* Magomeni *Quarters* sasa panapendeza. Mwanza tunazo *Pemba* na *Ghana Quarters*, tunashukuru wameshaanza. Tunaomba waendelee kubadilisha miji yetu ili watumishi waweze kupata nyumba nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukarabati wanaoufanya, kwa mfano wamesema Dodoma kukarabati nyumba 40, ukienda Nyumba Mia Tatu, nyumba zinasikitisha. Zinakarabatiwa, nyumba inayoangaliwa ni ya fulani lakini nyumba zote zile ni za Serikali. Nyingine zina *fence*, nyingine hazina *fence*. Haileti sura nzuri kwa wakaaji wa kule. Naomba sana kwenye maeneo ya nyumba, waone namna ya kuendelea nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vivuko, tunashukuru wanakwenda kujenga vivuko vipya, lakini naomba kuuliza, kuna vivuko vinakarabatiwa. Mfano *MV Kigamboni* kinakarabatiwa kwa shilingi 1,200,000,000, *MV Magogoni* shilingi 6,070,000,000. Sasa, hizi shilingi 6,000,000,000 ni za ukarabati au ni za kivuko kipya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna vivuko vingine kama vile *MV Misungwi* kinakarabatiwa kwa shilingi milioni 740, *MV Mwanza* shilingi milioni 174 na *MV Kome* shilingi milioni 340. Hizi zenye *billions*

ni kwa ajili ya ukarabati au ni ujenzi? Naomba waangalie kama iko sawa au haiko sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ukarabati wa vivuko ambao wanakwenda kuweka kwenye maeneo ya maegesho. Nashukuru sana kwa sababu kuna maeneo ambayo wanakwenda kujenga vivuko vipya na kurekebisha maegesho. Naomba sana, Kanda ya Ziwa Mkoa wa Mwanza una visiwa vingi na usafiri wao mkubwa wanaoutumia ni hivi vivuko. Sasa, kama hakuna maeneo ambayo yana vivuko vizuri vya kuweza kurahisisha usafiri, tutakuwa pia tunawaonea. Naomba sana hivi viweze kufanyiwa matengenezo mazuri na waweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wakandarasi ambao hawafanyi kazi yao vizuri, akiwemo yule mwenye Barabara ya Nyehunge kule Sengerema, ana miezi, tangu Aprili mwaka 2023 hadi leo bado anafanya maandalizi. Wanasubiri nini kuvunja mkataba wake? Kwa sababu hawezi. Naomba sana tutafute namna bora ya kuchukua wale wakandarasi ambao ni wazuri na ambao pia watatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kuona kwamba kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya kufanya mafunzo kwa wakadiriaji majenzi na wale wengine wanaojenga…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzunguzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Daktari…

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani twende kwa vijana wetu zaidi ili tuweze kuwapa kazi na kuwe na *internship* za kutosha, waingie kwenye hii miradi ambayo inajengwa ili waweze kupata ujuzi na hivyo tuwe na akiba ya vijana ambao wataweza kufanya kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni ya leo, Mheshimiwa Dorothy George Kilave. *(Makofi)*

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na kuwa mchangiaji wa mwisho. Nadhani nitapata nafasi zaidi kwa sababu ni dakika za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Rais wangu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Sisi Wanatemeke tunasema kwamba uso wa Temeke umependeza. Kwa nini ninasema hivyo? Mheshimiwa Rais wetu amejenga barabara za juu. Ukianza *TAZARA* utaona tunapita juu; ukipitia *TAZARA*, ukija Chang'ombe, pale Chang'ombe Mataa utaona tunapita juu; ukienda *BP*, kote tunapita juu; ukija *CBE* pia kuna daraja zuri sana ambalo limejengwa. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana pia Mawaziri wetu kwa jinsi ambavyo wanaendelea kufanya kazi za ziada. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu alikuwepo tangu mwanzo. Namshukuru sana kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya katika Jimbo letu la Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri ambapo Mheshimiwa Rais wetu ameweza kutoa fedha nyingi za zikajenga barabara hizi kubwa, lakini naomba kuongelea kuhusu *BRT* ambayo *TANROADS* ndiyo wanaosimamia. Barabara hizi ambazo zinajengwa ni nzuri sana, lakini tatizo ni pale ambapo vile vivuko au *culvert* wanazoziweka hazifai. Kwa nini? Kwa sababu, mara nyingi wanapoweka ni kwenye nafasi ndogo sana ambapo mvua zikinyesha au maji yakitoka mahali popote yanajaa katika zile barabara na hivyo yanatuama kwa muda mrefu na yanakwenda kukaa ndani ya barabara zile ambazo *TARURA* wanakuwa wamezijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyofahamika, *TARURA* inapata fedha ndogo sana, kwa hiyo barabara zetu zikikaa na

maji muda mrefu, *TARURA* nao wanakosa jinsi ya kuweza kuzifanyia kazi. Kwa hiyo, naomba sana *TARURA*, waende wakaangalie, hii Barabara hasa ambayo inatoka Chang'ombe – *VETA – DUCE* – JKT. Ukipita pale kona ya kwenda Uwanja wa Taifa utaona tayari imeshaharibika, ina bomba la maji ambalo lilipasuka, sina uhakika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba wanapoanza kujenga barabara hizi, basi wakutane na *TARURA* eneo husika pamoja na *DAWASA* au *TANESCO* pia ili wapate namna ya kufanya kwa sababu barabara hii bado haijapokelewa na bado haijaanza kufanya kazi. Wapitie wao wenyewe, wataona bomba kubwa la maji lililopasuka na kusababisha barabara sasa hivi kuchimbwa, na imewekwa maeneo ambayo hatuwezi kupita kwenda popote pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana, waangalie upya haya maeneo waone ni jinsi gani ambavyo wanaweza kufanya kazi na *TARURA*, *DAWASA* pamoja na *TANESCO* ili kazi nzuri ifanyike. Hata tunapoona fedha nyingi zinazotolewa kwa ajili ya barabara hizi, basi tuone na thamani ya ile fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kuangalia, kwamba hizi barabara ambazo *TANROADS* wanazijenga, mara nyingi *TANROADS* wanapoanza ujenzi, hasa kwenye Jimbo letu la Temeke, wanaelekeza magari yapite katika barabara za mitaa ambazo zimejengwa na *TARURA*. *TARURA* wana fedha kidogo na barabara zile zinajengwa kwa mkakati. Sasa, wanapoelekeza yale magari yapite kwenye zile barabara za mitaani ndani, wanakuwa hawawezi kuzifanyia kazi tena, wanaziacha kama zilivyo, zinakuwa zimeharibika na inakuwa tena sasa ni kazi ya *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana, watakapokuwa wanapitisha magari yale upande wa pili, ili *TANROADS* wafanye kazi, basi wawafanyie kazi nzuri ili *TARURA* nao barabara zile kama walikuwa wameshazijenga zibaki vilevile

zilivyo. Kila wakati wawe wanaziangalia ili *maintenance* iweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu pamoja na yote hayo, kwa barabara hizi zinazojengwa, naomba sana ile barabara ya kutoka *junction* ya kwenda Uwanja wa Taifa na ninasikia kuna *AFCON,* ile barabara natamani waipanue ili iwe barabara inayolingana na hizi nyingine kwa sababu sasa hivi tunakwenda kwenye michezo. Barabara ile imekuwa ni finyu kwa wanaokwenda kwenye michezo. Utaona barabara ile wamewaachia *TARURA* Wilaya ya Temeke ambao hawawezi kuimudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana waipokee barabara hii, tumeshaomba muda mrefu, kwamba hii barabara irudi *TANROADS,* lakini bado hawajatujibu. Naomba sana watujibu, waipokee barabara hii na kuitengeneza, barabara ambayo sisi tunasema ni ya Uwanja wa Taifa. Sasa kama ni ya Uwanja wa Taifa, kwa hali ya barabara ile sidhani kama ni barabara ya kitaifa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo pia ambapo katika Jimbo letu la Temeke waliatuambia tuache wazi kwa ajili ya kwamba *BRT* itapita eneo letu la Temeke, lakini mpaka sasa ni takribani miaka miwili hawajatuambia chochote, na *TARURA* wanashindwa kupanga fedha za kwenda kutengeneza ile barabara kwa kiasi kikubwa, wanaweka tu kiasi kidogo ili tuweze kuziba mashimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo ninaomba, Mheshimiwa Waziri atakaposimama hapa ku-*windup* atuambie, je, ile barabara itajengwa muda wa karibu au bado? Ili na sisi tujue *TARURA* tunaombaje fedha za kuweza kuitengeneza ile barabara kwa sababu ni barabara kubwa ambayo inakwenda kuunganisha kwenye malori yanayotoka bandarini. Hivyo ninaomba sana watafute namna ya kufanya ili wananchi wangu wa Temeke wajue sasa tunapata hii barabara ya *BRT* au tunaendelea na *TARURA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa sababu kazi anayoifanya Mama Samia ni kubwa sana, na tunaamini Waheshimiwa Mawaziri waliopo pamoja na Watendaji wao wataendelea kufanya kazi nzuri ambayo tunatamani Tanzania ipendeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na waliopangwa kuchangia siku ya leo wamekwisha. Kwa hiyo, ninaahirisha Bunge mpaka kesho siku ya Alhamisi, tarehe 30 mwezi Mei, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.47 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 30 Mei, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*